AFRICAN UNION
الاتحاد الأفريقي
UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE
UNIÃO AFRICANA
UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: 5517 700 Fax: 5517844
Website: www.au.int

**MKUTANO MKUU**
**Mkutano wa Thelathini na tisa wa Kawaida**
**14-15 Februari 2026**
**Addis Ababa (ETHIOPIA)**

**Assembly/AU/Dec.942-982(XXXIX)**
**Assembly/AU/Decl.1 - 10(XXXIX)**
**Assembly/AU/Res.1 - 2(XXXIX)**

# MAAMUZI, MATAMKO NA MAAZIMIO

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA MPITO YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU YANAYOHUSIANA NA KAULIMBIU YA AU YA MWAKA 2025: "HAKI KWA WAAFRIKA NA WATU WENYE ASILI YA AFRIKA KUPITIA MALIPO YA FIDIA"**
**EX.CL/1653(XLVIII)**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec. 884(XXXVII) wa Februari 2024 kuhusu Kujenga Umoja wa Kusaidia Kupigania Haki na Malipo ya Fidia kwa Waafrika (katika kutekeleza Uamuzi Assembly/AU/Dec. 847(XXXVI)),

2. **PIA UKIREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec. 903(XXXVIII) kuhusu Utekelezaji wa Mwongozo wa Kaulimbiu ya Mwaka 2025: *"Haki kwa Waafrika na Watu wenye Asili ya Afrika Kupitia malipo ya Fidia."* – DOC. EX.CL/1569(XLVI),

3. **UNAREJEA ZAIDI** Uamuzi EX.CL/Dec.1267(XLV) kuhusu Andiko Dhana la Kaulimbiu ya Mwaka 2025, *"Haki kwa Waafrika* na Watu wenye Asili ya Afrika Kupitia malipo ya Fidia." – Doc. EX.CL/1528(XLV), na EX.CL/Dec.1311(XLVII) wa Mkutano wa 47 wa Kawaida wa Baraza Kuu, tarehe 10-11 Julai 2025, mjini Malabo, Guinea ya Ikweta kuhusu Ripoti ya Maendeleo ya Utekelezaji wa Mwongozo wa Kaulimbiu ya AU ya Mwaka 2025: "Haki kwa Waafrika na Watu wenye Asili ya Afrika Kupitia malipo ya Fidia" – DOC. EX.CL/1622(XLVII);

4. **UNAKARIBISHA** Ripoti ya Maendeleo ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuhusu Uratibu wa Utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka 2025: “"Haki kwa Waafrika na Watu wenye Asili ya Afrika Kupitia malipo ya Fidia ″, na **UNATOA** shukrani kwa juhudi zilizofanywa na Kamisheni katika suala hilo;

5. **UNATOA** shukrani za dhati kwa Mheshimiwa John Dramani Mahama, Rais wa Jamhuri ya Ghana kwa mchango wake muhimu na na Malezi kama Kiongozi wa Umoja wa Afrika katika Kupigania Haki na Malipo ya Fidia kwa Waafrika. kwa mujibu wa Uamuzi Assembly/AU/Dec. 884(XXXVII)

6. **UNAIDHINISHA** maazimio ya mikutano ya utangulizi ya Kamati ya Wataalamu kuhusu Fidia ya Umoja wa Afrika (AU CER), na Kundi la Wataalamu wa Kisheria wa Umoja wa Afrika kuhusu Fidia (AU LER) iliyofanyika kuanzia tarehe 15-19 Disemba 2025 kama ilivyo katika Hati Na. XXX (iliyoambatishwa), na **UNAIAGIZA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuitisha mikutano yake ya kawaida kwa lengo la kuchangia zaidi katika ufafanuzi wa kina wa Muongo huo. **UNAZINGATIA** maoni yaliyotolewa katika mikutano yote miwili kwamba Programu ya Fidia kwa sasa haina ufadhili wa kutosha, na hivyo **UNAPENDEKEZA** kwamba programu na mikutano inayofuata ya fidia ifadhiliwe kikamilifu kama sehemu ya utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka ya Umoja wa Afrika ya mwaka 2025 _

7. **UNAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec. 903 (XXXVIII), ambao ulikaribisha ombi la Algeria la kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kimataifa kuhusu Uhalifu wa Ukoloni, kwa ushirikiano na Kamisheni ya Umoja wa Afrika na **KUKARIBISHA** kuitishwa kwa mkutano kuanzia tarehe 30 Novemba hadi 1 Desemba 2025 mjini Algiers chini ya kaulimbiu "Mkutano wa Kimataifa kuhusu Uhalifu wa Ukoloni Barani Afrika: Kuelekea Kurekebisha Udhalimu wa Kihistoria kwa kuharamisha Ukoloni" na **KUTOA SHUKRANI** kwa Mhe. Abdelmadjid Tebboune, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria.

8. **UNAIDHINISHA**[1] "Azimio la Algiers" (lililoambatishwa) kama mchango kwa juhudi za bara la Afrika za kuharamisha ukoloni na fidia, na **UNAITEUA** tarehe "30 Novemba" kama siku ya Kiafrika ya kuwaenzi mashahidi wa Kiafrika na waathirika wa biashara ya utumwa kuvuka bahari ya Atlantiki, ukoloni na ubaguzi wa rangi;

9. **UNAPONGEZA** kufanyika kwa Kongamano la 9 la Kimajumui lililofanyika Lomé, Togo, kuanzia tarehe 8 hadi 12 Desemba 2025 chini ya Kaulimbiu: "Kurudisha upya Umajui wa Kiafrika na Jukumu la Afrika katika Mageuzi ya Taasisi ya Kimataifa: Kutafuta Rasilimali na Kuchukua Hatua Mpya," kama ilivyoagizwa katika uamuzi Assembly/UA/Dec.913 (XXXVIII), na **UNAIDHINISHA** azimio lake la mwisho(limeambatishwa); na kutoa shukrani kwa Mhe. Faure Essozimna Gnassingbé, Rais wa Baraza la Jamhuri ya Togo kwa kufanikisha kongamano hilo.

10. **UNAKARIBISHA** matokeo ya awali ya juhudi za Nchi Wanachama na Kamisheni, ili kukuza hatua kwa hatua, kaulimbiu ya mwaka katika ushirikiano wa kidiplomasia wa Umoja wa Afrika na washirika husika wa kimataifa, na **UNATOA WITO** wa kuendelea kwa juhudi hizi katika utekelezaji wa Mwongozo wa Kaulimbiu ya Mwaka 2025, ambao vifungu vyake sasa vinapaswa pia kupanuliwa hadi Muongo Mmoja.

11. **UNATOA WITO** wa kuharakisha utekelezaji wa Mkataba wa Maelewano kuhusu "Kuongeza Ushirikishwaji na Watu wenye Asili ya Afrika" uliosainiwa Septemba 2024;

12. U**NAKARIBISHA** mafanikio makubwa ya mwaka 2025 ya kufanyika kwa Mkutano wa Pili wa Afrika-CARICOM, ulioitishwa Addis Ababa tarehe 7 Septemba 2025, ambao ulipitisha Azimio la Addis Ababa kuhusu "Ushirikiano wa Bara katika Kutafuta Haki ya Fidia kwa Waafrika na Watu wenye Asili ya Afrika kupitia Fidia",.

13. **UNAIDHINISHA** taarifa iliyoambatanishwa ambayo iliyopitishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali ambapo Wakuu wa Nchi na Serikali walitaka Mkutano wa tatu wa Afrika-CARICOM ufanyike tarehe 7 Septemba 2028, katika Nchi Mwanachama wa CARICOM, pamoja na kuimarisha uhusiano wa kitaasisi kati ya AUC na Sekretarieti za CARICOM, na kuendelea kuchunguza njia za ziada za ushirikiano, ikiwa ni pamoja na kuzingatia. kuanzisha ofisi ya uwakilishi ya AU mjini

Georgetown, Guyana, katika makao makuu ya CARICOM na uidhinishaji kwa Nchi zake zote Wanachama, na ofisi ya CARICOM mjini Addis Ababa katika makao makuu ya Umoja wa Afrika, na **UNAIOMBA** Kamisheni kuwasilisha ripoti kuhusu matokeo ya programu na bajeti.

[1] Pingamizi lililowekwa na Ufalme wa Morocco

**14.** **UNAPITISHA** Azimio la Addis Ababa kuhusu ushirikiano wa kimataifa katika kutafuta Haki ya Fidia kwa Waafrika na Watu wenye Asili ya Afrika kupitia Fidia ambalo linaelezea masuala ya marejeleo, masuala muhimu, matokeo pamoja na hati na mipango, ushirikiano ikiwa ni pamoja na mipango ya ufuatiliaji kwa kuendeleza harakati za pamoja za kutafuta haki ya fidia kwa Waafrika na watu wenye asili ya Afrika.

**15.** **UNASISITIZA** hitaji la kuendelea kuimarisha uratibu wa mfumo mzima wa AU, ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Makundi ya Afrika kwenye Umoja wa Mataifa mjini Geneva, New York na Paris katika utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka 2025, kama ilivyoanzishwa na Kamisheni ya Umoja wa Afrika;

**16.** **UNATOA WITO kwa** Vyombo vyote vya AU, Taasisi, na Ofisi Maalum za Kitaalamu pamoja na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda kuchangia katika juhudi hii iliyoratibiwa, ikiwa ni pamoja na kupitia taarifa za mara kwa mara za shughuli zao na **UNATOA WITO ZAIDI kwa** Kamisheni kufanya kazi kwa ushirikiano na Vituo vyote husika vya Taaluma za Kiafrika Barani ambavyo vinaweza kuchangia vyema katika kuendeleza haki na hatua za kudai malipo ya fidia;

**17.** **UNATAMBUA** mchango wa Nchi Wanachama ambazo zimeunga mkono kikamilifu utekelezaji wa Kaulimbiu ya mwaka 2025, ikiwa ni pamoja na kupitia uandaaji wa mikutano ya kisheria, mikutano yenye kaulimbiu mahususi, na majukwaa ya mazungumzo ya kisiasa ya ngazi ya juu, na **UNAZIHIMIZA** Nchi zote Wanachama kuunganisha zaidi ajenda ya bara ya haki na fidia wakati wa Muongo wa 2026-2035 katika sera zao za kitaifa, elimu, utamaduni, na mikataba ya kidiplomasia, kama kipengele kikuu cha Umajui wa Afrika na Ajenda 2063

**18.** **UNAIDHINISHA** kupanua Kaulimbiu ya Mwaka 2026-2035 Muongo wa Haki kwa Waafrika na Watu Wenye Asili ya Afrika Kupitia Fidia, na **KUZITAKA** Nchi Wanachama kuongeza jitihada zao katika kutekeleza Kaulimbiu ya Muongo wa Haki kwa Waafrika na Watu Wenye Asili ya Afrika Kupitia Fidia katika nchi zao husika;

**19.** **UNAZITAKA** Nchi Wanachama, katika kuendeleza jitihada zinazoendelea kutafuta uungwaji mkono wa kimataifa katika lengo la Umoja wa Afrika la kutafuta haki kwa Waafrika na Watu Wenye Asili ya Afrika kupitia fidia, ili kusaidia kikamilifu jitihada za AU kwa ajili ya Fidia, kupendekeza rasimu ya Azimio kwa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa ajili ya kutambuliwa kwa Biashara ya Watumwa Kuvuka

Bahari ya Atlantic kama uhalifu mkubwa zaidi dhidi ya binadamu, kwa mujibu wa Maamuzi ya Mkutano Mkuu Assembly/AU/Dec.884(XXXVII) na uamuzi Assembly/AU/Dec.934 (XXXVIII);

20. **UNATOA WITO PIA** kwa ajili ya raslimali fedha na raslimali watu zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Mkutano Mkuu na matokeo yanayohusiana na Kaulimbiu ya Muongo, na **UNAIELEKEZA** Kamisheni kuwasilisha ripoti inayoonesha raslimali za ziada zinazohitajika kwenye mikutano ya mapitio ya bajeti inayotarajiwa kufanyika siku za karibuni zaidi kwa ajili ya kujadiliwa na PRC;

21. **UNAIOMBA** Kamisheni, kwa uratibu wa karibu na Vyombo na taasisi husika za AU ikiwa ni pamoja na Ofisi za Uwakilishi mjini Geneva na New York, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Kaulimbiu ya Muongo;

22. **UNAIOMBA ZAIDI** Kamisheni kuwasilisha ripoti za maendeleo ya Utekelezaji wa Muongo huo kwenye mkutano ujao wa Baraza Kuu na kupitia baraza hilo kwenye Mkutano Mkuu.

# UAMUZI KUHUSU UTEUZI WA KINARA WA UMOJA WA AFRIKA KUHUSU HATUA ZA KIBINADAMU NA ULINZI WA WATU WALIO KWENYE MAZINGIRA HATARISHI

**Mkutano Mkuu,**

1. **UKIREJELEA** uamuzi wake Assembly/AU/Dec. 750(XXXIII) ukitangaza Kaulimbiu ya Umoja wa Afrika ya Mwaka 2019: "*Mwaka wa Wakimbizi, Wanaorejea Nyumbani na Wakimbizi wa Ndani: Kuelekea Suluhisho la Kudumu la Uhamiaji wa Kulazimishwa Afrika*";

2. **UKIREJELEA ZAIDI** Azimio Assembly/AU/Dec.1(XXXIII), ambalo linamtaka Kiongozi wa AU wa kaulimbiu ya mwaka 2019, **Mhe. Teodoro Obiang Nguema Mbasogo**, Rais wa Jamhuri ya Guinea ya Ikweta kuendelea kuunga mkono juhudi za AU katika kushughulikia changamoto za uhamiaji wa kulazimishwa;

3. **UKITAMBUA** uongozi wa mfano ulioonyeshwa na Mheshimiwa Teodoro Obiang Nguema Mbasogo, Rais wa Jamhuri ya Guinea ya Ikweta, kama Kiongozi wa Kaulimbiu ya Mwaka ya 2019 katika kuendeleza hatua za bara kushughulikia sababu za msingi na matokeo ya kibinadamu ya uhamiaji wa kulazimishwa;

4. **UKIZINGATIA** changamoto za kibinadamu zinazoendelea na zinazobadilika kote barani, ikiwa ni pamoja na idadi inayoongezeka ya wakimbizi, wanaorejea nyumbani, wakimbizi wa ndani ya nchi, na watu wengine wanaohitaji ulinzi na msaada;

5. **UKIZIONGOZWA na** dhamira ya Umoja wa Afrika ya kuimarisha utawala wa kibinadamu, kuimarisha utayari na hatua za kuchukua, na kukuza suluhu za kudumu kulingana na Mkataba wa Kampala, Mpango wa Sera ya Kibinadamu wa Afrika, na Ajenda 2063;

6. **UNAAZIMIA** kuhakikisha uongozi endelevu wa kisiasa na utetezi wa ngazi ya juu ili kutafuta rasilimali, kukuza hatua zilizoratibiwa, na kuinua vipaumbele vya kibinadamu katika ngazi za bara na kimataifa

**7. HIVYO UNAAMUA:**

i) **KUMTEUA** Mheshimiwa Teodoro Obiang Nguema Mbasogo, Rais wa Jamhuri ya Guinea ya Ikweta, kama Kinara wa Umoja wa Afrika katika kukabiliana na masuala ya kibinadamu na ulinzi wa watu walio katika mazingira hatarishi;

ii) **KUMTAKA** Kinara kutetea mshikamano ulioimarishwa wa bara, kikanda, na kimataifa, mshikamano wa kushirikishana mizigo, na ushirikiano katika kushughulikia migogoro ya kibinadamu barani Afrika, ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa ufadhili wa kibinadamu unaotarajiwa na endelevu;

iii) **KUMTAKA ZAIDI** Mhe. Rais kuhamasisha uendeshaji kamili wa Shirika la Huduma za Kibinadamu la Afrika;

iv) **UNAIELEKEZA** Kamisheni kutoa msaada wote muhimu wa kitaalamu na vifaa kwa Kinara katika utekelezaji wa majukumu yake, na kuwezesha uratibu wa Nchi Wanachama, Jumuiya za Kiuchumi za Kanda, vyombo vya Umoja wa Afrika, na washirika wa kibinadamu

v) **UNAIELEKEZA ZAIDI** Kamisheni kutoa ripoti mara kwa mara kwa Vyombo vya Sera kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa jukumu hili

# UAMUZI WA MKUTANO MKUU WA AU KUHUSU MKUTANO MAALUM WA AU WA KUTOKOMEZA UKIMWI IFIKAPO MWAKA 2030 NA KUSHUGHULIKIA VIFO VYA AKINA MAMA WAJAWAZITO NA WATOTO, MAGONJWA YA KUAMBUKIZA NA YASIYOAMBUKIZA YANAYOSAMBAA BARANI NA KUIMARISHA MIFUMO YA AFYA IFIKAPO MWAKA 2030

EX.CL/1656(XLVIII) i

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJELEA** uamuzi Assembly/Dec.852(XXXVI) na Assembly/AU/Dec.908(XXXVIII) kuhusu Mwongozo wa AU kuelekea mwaka 2030 na Zaidi: Kudumisha hatua dhidi ya UKIMWI, Kuhakikisha Uimarishaji wa Mifumo na Usalama wa Afya kwa Maendeleo ya Afrika na kufanya Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Kutokomeza UKIMWI ifikapo mwaka 2030 na Kushughulikia Vifo vya Akina Mama Wajawazito na Watoto Vinavyoweza Kuzuilika, Magonjwa ya Kuambukiza na Yasiyoambukiza Yaliyosambaa Barani, na Kuimarisha Mifumo ya Afya ifikapo mwaka 2030; na **UNAZINGATIA** kwamba Kamisheni haikuweza kuitisha Mkutano Maalum mwezi Desemba 2025, kutokana na kalenda ya AU iliyojaa, ikiwa ni pamoja na Mkutano wa AU-EU na Kongamano la 9 la Afrika.

2. **UNAAMUA** kwamba Mkutano Maalum uliokuwa umepangwa kufanyika mwaka 2025 utaitishwa kabla **ya mwaka 2027;** na **UNAIOMBA** Kamisheni kuchukua hatua zote muhimu ili kuhakikisha Mkutano huo unaandaliwa kwa wakati, kwa uratibu wa karibu na Nchi Wanachama na wabia.

3. **UNATOA WITO KWA** Nchi Wanachama kujitolea kutekeleza na kuingiza katika mipango ya ndani Mwongozo wa AU kuelekea 2030 na Zaidi: "Kudumisha Hatua dhidi ya UKIMWI, Kuhakikisha Uimarishaji wa Mifumo na Usalama wa Afya kwa ajili ya maendeleo ya Afrika" kama mpango mkuu wa sera wa kuendeleza usalama wa afya, kutokomeza UKIMWI, na kupunguza vifo vinavyoweza kuzuilika.

# UAMUZI
# KUHUSU RIPOTI YA MAENDELEO YA MWAKA 2025 YA KINARA WA AU WA UFADHILI WA NDANI WA AFYA KUHUSU UTEKELEZAJI WA AZIMIO LA MKUTANO WA UONGOZI WA AFRIKA KUHUSU KUWEKEZA KATIKA AFYA

**EX.CL/1656(XLVIII)ii**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJELEA** Ahadi ya Addis Ababa kuhusu Uwekezaji katika Afya (Azimio la ALM) na agizo la bara la kuimarisha mifumo endelevu ya ufadhili wa afya inayoongozwa na nchi.

2. **UNATAMBUA** shinikizo kubwa la kifedha linalozikabili Nchi Wanachama, kupungua kwa kasi kwa misaada ya afya kutoka nje, na umuhimu wa kujenga mifumo ya afya imara na inayojitegemea;

3. **UNAZINGATIA** maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ripoti ya Maendeleo ya Uwekezaji katika Afya ya Mkutano wa Uongozi wa Afrika (ALM) na mapendekezo yake.

4. **UNAMPONGEZA** Mhe.Rais Paul Kagame, Kinara wa Umoja wa Afrika kuhusu Ufadhili wa Ndani wa Afya kwa uongozi wake wa mfano ambao umekuwa chanzo cha mwongozo wa kimkakati na kasi ya kuendeleza ajenda ya ufadhili wa afya ya ndani ya Afrika hata katika muktadha wa shinikizo kubwa la kifedha linalozikabili Nchi Wanachama, kupungua kwa kasi kwa misaada ya afya ya nje, na umuhimu wa kujenga mifumo imara ya afya na inayojitegemea;

5. **UNAIPONGEZA ZAIDI** Kamisheni ya AU, AUDA-NEPAD, Jumuiya za Kiuchumi za Kanda na washirika kwa juhudi za pamoja mwaka 2025 kupitia utekelezaji wa Vituo vya Ufadhili wa Afya vya Kanda (RHFHs), upanuzi wa Mijadala ya Kitaifa ya Ufadhili wa Afya (NHFDs), kuanzishwa kwa Programu ya Uwekezaji na Ufadhili wa Sekta ya Afya ya Afrika (PIFAH); na kuanzishwa kwa kikosi kazi cha AU cha Ufadhili wa Afya;

6. **UNATHIBITISHA TENA** Ufadhili wa afya kama kipaumbele cha bara na unasisitiza Azimio la ALM kama mwelekeo wa kisiasa na kitaalamu unaoongoza mageuzi ya Afrika kuelekea ufadhili endelevu wa ndani wa afya unaoongozwa ndani ya nchi;

7. **UNAZIHIMIZA** Nchi Zote Wanachama kufanya Majadiliano ya Kitaifa ya Ufadhili wa Afya angalau mara moja kila baada ya miaka mitatu kama utaratibu mkuu wa uwajibikaji na mageuzi wa kutafsiri ahadi za ALM katika michakato ya bajeti ya

kitaifa, mikakati ya fedha, na hatua za wizara mbalimbali.

8. **UNATOA WITO kwa** Jumuiya za Kiuchumi za Kanda kuanzisha kikamilifu Vituo vyao vya Ufadhili wa Afya vya Kanda, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wanaojituma, bajeti, na mipango kazi ya miaka mingi, na kuhakikisha uhusiano wa kimfumo na vikosi kazi vya kitaalamu vya kitaifa vya ufadhili wa afya.

9. **UNATOA WITO ZAIDI** kwa Nchi Wanachama, Jumuiya za Kiuchumi za Kanda na washirika wa maendeleo kuisaidia Kamisheni na AUDA- NEPAD kitaalamu na kifedha kutekeleza kikamilifu Mpango wa AU wa mwaka 2030 na Zaidi na Kikosi Kazi cha Bara cha AU cha Ufadhili wa Afya.

10. **UNAIAGIZA** Kamisheni ya AU kwa kushirikiana na AUDA-NEPAD, Jumuiya za Kiuchumi za Kanda na Nchi Wanachama kukamilisha Mfumo wa Ufuatiliaji wa Maendeleo ya Ufadhili wa Afya na kuwasilisha toleo la mwisho kwenye Mkutano Ujao wa Kawaida wa STC kuhusu Uponyaji, Idadi ya Watu, Lishe na Udhibiti wa Dawa uliopangwa kufanyika mwaka 2026;

11. **UNAIELEKEZA ZAIDI** Kamisheni kuchukua jukumu la kuandaa Kadi ya Alama ya Afrika ya Ufadhili wa Ndani wa Afya kuhusiana na AIDS Watch Africa (AWA) au jukwaa lolote husika la AU;

12. **UNAIDHINISHA** Programu ya Uwekezaji na Ufadhili wa Sekta ya Afya Afrika (PIFAH) kama chombo cha uwekezaji barani cha kuchochea maendeleo ya soko la afya, na **UNATOA WITO** kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Afreximbank na washirika kushirikiana na AUDA-NEPAD katika kuanzisha kituo cha maandalizi ya mradi ili kuharakisha utayari wa mradi wa PIFAH;

13. **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kuimarisha utafutaji wa rasilimali za ndani na mifumo ya usimamizi wa fedha za umma, ikiwa ni pamoja na kupitisha manunuzi ya pamoja, ufuatiliaji wa matumizi ya kidijitali, utekelezaji bora wa bajeti, na uchunguzi wa kodi lengwa za afya au hati bunifu vya ufadhili;

14. **UNATOA WITO ZAIDI** kwa washirika:Taasisi za fedha za maendeleo, wawekezaji, na mashirika ya kitaalamu kuoanisha msaada na muundo wa ALM, kuelekeza misaada kupitia RHFH na PIFAH, na kukuza vipaumbele vya Afrika vya ufadhili na maendeleo ya soko.

# UAMUZI
# KUHUSU JUHUDI KUBWA ZA KUTOKOMEZA MALARIA
# EX.CL/1656(XLVIII)iii

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAPOKEA** “Ripoti ya Maendeleo ya Malaria Barani Afrika ya Mwaka 2025” iliyowasilishwa na Rais Kinara Duma Gideon Boko wa Jamhuri ya Botswana na Mwenyekiti wa Muungano wa Viongozi wa Afrika wa Kutokomeza Malaria (ALMA);

2. **UNAREJELEA** Azimio la Abuja kuhusu VVU/UKIMWI, Kifua kikuu na Magonjwa Mengine Yanayohusiana ya Kuambukiza (OAU/SPS/ABUJA/3); Mpango wa Kutokomeza UKIMWI, Kifua kikuu na Malaria Barani Afrika ifikapo mwaka 2030; Mpango wa Utekelezaji wa Afrika kuelekea mwaka 2030 na Kuendelea; Azimio kuhusu Kukabiliana na Vitisho na Kuimarisha Hatua za Pamoja kufikia Malengo ya mwaka 2030 (AFR/RC75/8); pamoja na maazimio ya awali (Decl.3(XXXVI), Decl.2(XXXVII)) na maamuzi (Dec.709(XXXI), Dec.725(XXXII), Dec.770(XXXIII), Dec.904(XXXVIII)) yanayozitaka Nchi Wanachama na washirika kuchukua hatua madhubuti kutokomeza malaria barani Afrika ifikapo mwaka 2030;

3. **UNAELEZEA WASIWASI WAKE** kwamba malaria bado ni chanzo kikuu cha maradhi na vifo, hususan miongoni mwa makundi yaliyo hatarini zaidi, na ni kikwazo katika kufikia malengo ya maendeleo ya afya, kijamii na kiuchumi yaliyoainishwa katika Mpango Unaochochea Kutokomeza UKIMWI, Kifua kikuu na Malaria Barani Afrika ifikapo mwaka 2030, Mkakati wa Afya wa Afrika 2016–2030, Mpango wa Utekelezaji wa Umoja wa Afrika kuelekea mwaka 2030 na Kuendelea, pamoja na Ajenda 2063: Afrika Tunayoitaka;

4. **UNATAMBUA** kuwa upatikanaji wa fedha za masuala ya afya ya umma duniani unaendelea kupungua, na kwamba kuna umuhimu kwa Nchi Wanachama kuharakisha utafutaji wa rasilimali za ndani ili kugharimia kikamilifu mipango mikakati ya kitaifa ya malaria.

5. **PIA, UNATAMBUA** kwamba kutokomeza malaria kunahitaji mikakati jumuishi na bunifu;

6. **UNAZITAKA** Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda kuchukua hatua kubwa na za dhati ili kufikia malengo yaliyowekwa katika Mpango Unaochochea kwa kufanya yafuatayo:

(i) kuimarisha uongozi wa kitaifa, uwajibikaji, na ushughulikiaji jumuishi wa kutokomeza malaria kupitia mkakati wa kujumuisha sekta mbalimbali, unaohusisha serikali nzima na jamii nzima, unaoratibiwa na Mabaraza ya Kitaifa ya Kutokomeza Malaria;

(ii) kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji, kuongeza matumizi ya takwimu katika kufanya maamuzi kwa kutumia nyenzo za kadi ya alama katika ngazi zote, na kushirikiana katika ufuatiliaji na kuchukua hatua dhidi ya mbu aina ya *An.stephensi* pamoja na tishio linaloongezeka la usugu wa mwili dhidi ya afua za malaria.

(iii) kutekeleza mkakati jumuishi unaounganisha huduma za afya ya msingi na magonjwa mengine yanayoenezwa na vimelea (kwa mfano, Magonjwa ya Kitropiki Yasiyopewa Kipaumbele);

(iv) kuongeza upatikanaji, kukubalika, na ubora wa afua zilizopo, pamoja na kubuni, kuendeleza na kusambaza nyenzo mpya zinazofaa kwa madhumuni husika ili kuharakisha mafanikio na kukabiliana na vitisho vya kibiolojia na vingine vinavyohatarisha utokomezaji wa malaria.

(v) kuwekeza katika utafiti na maendeleo pamoja na uzalishaji wa ndani wa bidhaa za malaria na bidhaa nyingine za afya, kwa kuhakikisha viwango vya juu vya ubora wa bidhaa, ithibati ya awali ya Shirika la Afya Duniani (WHO), pamoja na kutegemeana kunakovuka mipaka na baina ya kanda kwa ajili ya idhini ya ithibati na usajili wa bidhaa; na

(vi) kulinda upatikanaji uliopo wa fedha za malaria, kuongeza mgao wa fedha kwa ajili ya malaria katika bajeti za kitaifa, na kuhamasisha rasilimali mpya na bunifu, ikiwamo kutoka sekta binafsi kupitia Mabaraza na Mifuko ya Kutokomeza Malaria.

7. **PIA UNATOA WITO** kwa Muungano wa Viongozi wa Afrika wa Kutokomeza Malaria (ALMA) kuandaa na kutekeleza utaratibu wa ufuatiliaji na uwajibikaji kwa ajili ya kupiga hatua kubwa ya kutokomeza malaria.

# UAMUZI
# KUHUSU RIPOTI ZA KINARA WA LISHE WA UMOJA WA AFRIKA NA VIONGOZI WA AFRIKA WENYE DHAMANA YA LISHE (ALN)
# Doc. EX.CL/1656(XLVIII)iv

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJELEA** uamuzi (Assembly/AU/Dec.621(XXVIII) kuhusu uteuzi wa Kinara wa Lishe wa Afrika, Mfalme Letsie III wa Ufalme wa Lesotho, na kuongeza muda wake hadi 2026 (Assembly/AU/Dec.892(XXXVII) na uamuzi Assembly/AU/Dec. 681 (XXX) ulioidhinisha Mpango wa Viongozi wa Afrika wenye dhamana ya Lishe (ALN).

2. **UNAREJELEA ZAIDI** uamuzi (Assembly/AU/Dec.892(XXXVII) ulioidhinisha Azimio la Abidjan kuhusu kaulimbiu ya mwaka 2022 na Wito wa Kuchukua Hatua ya "Kuharakisha uwekezaji, utekelezaji na uratibu ili kuboresha lishe na usalama wa chakula barani Afrika", pamoja na mwendelezo wa shughuli za Mwaka wa Lishe hadi 2025 kupitia mpango wa utekelezaji wa 2023-2025 unaohusiana na kuendelea kwa changamoto nyingi zinazolikabili bara hili katika maeneo ya lishe na usalama wa chakula; na "Wito wa Kuchukua Hatua ya Kuhamasisha Ufadhili Bunifu kwa Ajili ya Mapambano Dhidi ya Utapiamlo" na "Wito wa Kuchukua Hatua kuhusu Lishe ya Vijana" uliopitishwa wakati wa Mazungumzo ya Ngazi ya Juu kuhusu Ufadhili wa Lishe yaliyoandaliwa na Kinara wa Lishe wa AU mwezi Machi 2023

3. **UNAPOKEA NA KUIDHINISHA:**

(i) Ripoti ya Kinara wa Lishe wa Umoja wa Afrika, Mfalme Letsie III wa Ufalme wa Lesotho, kwa kipindi cha 2024-2025 na mapendekezo yaliyomo;

(ii) Ripoti kuhusu shughuli na maendeleo ya Mpango wa Viongozi wa Afrika wa Lishe (2024-2025) na mapendekezo yaliyomo;

(iii) Hati ya matokeo (Taarifa ya Afrika N4G), ya mkutano wa pembezoni wa ngazi ya juu kuhusu kaulimbiu "Kutoka Sera hadi Utekelezaji: Kuelekea Msimamo wa Pamoja wa Kushughulikia Utapiamlo Barani Afrika" uliofanyika wakati wa Mkutano wa Kawaida wa 38 wa AU, mwezi Februari 2025, Addis Ababa, Ethiopia; na ilithibitisha tena Mkutano wa Lishe kwa Ukuaji (N4G) wa Machi 2025 mjini Paris, Ufaransa, ambao (a) unabainisha jukumu muhimu la lishe katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi; (b) unadhamiria kutekeleza mikakati ya lishe ya bara, kupitisha mkakati wa sekta tofauti za lishe kwa kuijumuisha katika sekta zote; na (c) kuwezesha ufadhili wenye kuchochea na bunifu kwa kutafuta rasilimali za ndani na kimataifa na kutumia mifumo bunifu ya ufadhili ili kutekeleza ahadi za lishe kwa ukuaji katika ngazi ya nchi; na

(iv) Taarifa ya Doha kuhusu Ufadhili wa Lishe yenye kichwa "Lishe kama Uwekezaji Makini Zaidi: Wito wa Afrika wa Ufadhili wenye kuchochea" ikiwakilisha msimamo mmoja wa Afrika kuhusu diplomasia ya ufadhili wa lishe na kutumika kama njia ya uzinduzi wa uhamasishaji unaoendelea wa ufadhili wa lishe.

4. **UNATAMBUA** kwamba kaulimbiu ya AU ya mwaka 2026 kuhusu maji na usafi wa mazingira inatoa fursa ya wakati mwafaka kusisitiza utegemezi kati ya maji, usafi wa mazingira na usafi (WASH), lishe, na ukuaji wa utotoni na maisha ya watoto ikisisitiza hitaji la hatua kali na zilizoratibiwa katika nyanja hizi.

5. **UNAPONGEZA** juhudi za Kinara na Viongozi wa Afrika wa Lishe (ALN) katika kuhamasisha kipaumbele cha lishe katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa, ambapo imekuwa muhimu katika kuhamasisha serikali na wafadhili kuongeza na kuendeleza uwekezaji kwa ufadhili bunifu wa lishe.

6. **UNAIDHINISHA** kuongeza muda kwa Mfalme Letsie III wa Ufalme wa Lesotho kama Kinara wa Lishe wa Umoja wa Afrika kwa muhula mwingine (2026-2028) ili kuendelea kuhamasisha Nchi Wanachama kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati wa Lishe wa Kikanda wa Afrika (2026-2035), Mpango wa Sera ya Lishe wa Sekta Mbalimbali kwa Afrika na Lengo la Ufadhili kwa Uwekezaji wa Lishe Afrika (ulio kwenye kiwango cha chini) pamoja na Ahadi chini ya Azimio la Kampala Baada ya Malabo

7. **UNAIAGIZA** Kamisheni kuandaa mpango kamili wa kazi wa kiwango cha juu kwa Kinara wa Lishe wa AU

8. **UNAZINGATIA KWA MASIKITIKO:**

(i) Kwamba utapiamlo bado ni changamoto kubwa kote Barani na kwamba data kutoka kwa Kadi ya Alama ya Uwajibikaji kuhusu Lishe ya Bara (CNAS) inaonyesha kwamba Nchi nyingi Wanachama zimepoteza mwelekeo na hazitaweza kufikia malengo mbalimbali ya lishe ifikapo mwaka 2025.

(ii) Kwamba hali hii inazidi kuwa mbaya kutokana na kupungua kwa kiwango cha fedha za ndani, kupungua kwa msaada wa maendeleo, mageuzi ya tabianchi, migogoro, shinikizo la mfumo wa chakula, na mifumo dhaifu ya afya, na kurudisha nyuma maendeleo yaliyopatikana kwa juhudi kubwa kuhusiana na mapambano dhidi ya utapiamlo, na hivyo kuathiri maisha ya watoto.

(iii) Kwamba nchi nyingi za Afrika zinawekeza chini ya asilimia moja ya bajeti zao katika lishe, na kuacha sekta hiyo ikiwa katika hatari ya kutegemea misaada ya nje; na kwamba kwa makadirio ya dola bilioni 34 za Marekani zinazohitajika katika muongo ujao ili kuchukua hatua zilizothibitishwa za lishe katika Afrika Kusini mwa

Jangwa la Sahara, kuna haja ya haraka ya kufikiria upya mifumo ya ufadhili wa lishe ambayo ni endelevu na himilivu.

**9. HIVYO, UNAZITAKA:**

(i) Nchi Wanachama wa AU kuharakisha maendeleo kuelekea kufikia malengo ya lishe kupitia sera na mipango yenye ushahidi na kupitisha mipango ya uwekezaji wa sekta mbalimbali na uwajibikaji katika sekta mbalimbali;

(ii) Nchi Wanachama wa AU kutekeleza sera na ahadi za kifedha zilizotolewa wakati wa Mkutano wa Lishe kwa Ukuaji (N4G) mwaka 2025; kuweka kipaumbele katika ufadhili wa ndani kwa ajili ya lishe katika sekta mbalimbali kwa kuendana na Malengo ya Ufadhili yaliyopendekezwa kwa ajili ya Uwekezaji wa Lishe barani Afrika (yanayoendelea kuendelezwa) na kuunganisha ufadhili wa lishe kupitia michakato husika ya kisheria;

(iii) Viongozi wa Afrika wa Lishe (ALN) na Kinara wa Lishe wa AU kusimamia diplomasia ya ufadhili wa lishe kupitia majukwaa/mipango (mazungumzo, matukio, taarifa, barua n.k.) kwa ajili ya kutafuta mtaji wa kuchochea kutoka Benki za Maendeleo ya Kimataifa, Wahisani, mitaji ya ndani, mifuko ya pensheni, na wafadhili wengine wasio wa kawaida; na

(iv) Kuitisha Mkutano wa Lishe wa Bara kila baada ya miaka 2-3 chini ya uongozi wa Kinara wa Lishe wa Umoja wa Afrika na Viongozi wa Afrika Lishe kufuatia kupitishwa kwa mpango wa Sera ya Lishe ya Sekta Mbalimbali kwa ajili ya Afrika na vyombo vya sera vya AU.

## UAMUZI
## KUHUSU RIPOTI YA MWAKA 2025 YA MAENDELEO YA SHIRIKA LA DAWA AFRIKA (AMA)
## Doc. EX.CL/1682(XLVIII)

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJELEA** uamuzi Assembly/AU/Dec.735(XXXIII) uliopitisha Mkataba wa Kuanzishwa kwa Shirika la Dawa Afrika (AMA), na uamuzi Assembly/AU/Dec.907(XXXVII) kuhusu uendeshaji wa AMA.

2. **UNAPOKEA** Ripoti ya Maendeleo kuhusu Uendeshaji wa Shirika la Dawa Afrika (AMA).

3. **UNAZIPONGEZA** Kamisheni, Sekretarieti ya AMA, Jamhuri ya Rwanda, Nchi Mwenyeji, AUDA-NEPAD, Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Afrika, Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs), Mashirika ya Afya ya Kikanda (RHOs), na wadau kwa maendeleo yaliyopatikana katika uanzishwaji na uendeshaji kamili wa AMA, ikiwamo kufanyika kwa Mkutano wa Pili wa Kawaida wa Nchi Wanachama (CoSP) mjini Kigali mwezi Juni 2025, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa kwanza, na kuanza kwa shughuli za AMA mjini Kigali, Jamhuri ya Rwanda.

4. **PIA UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Rwanda, kama Nchi Mwenyeji wa AMA, kwa msaada wake endelevu wa kisiasa, kidiplomasia, kifedha na kiutendaji katika kuanzishwa na uendeshaji wa Shirika.

5. **UNAKARIBISHA** kuanza majukumu rasmi kwa Mhe. Dkt. Delese Mimi Darko kama Mkurugenzi Mkuu wa kwanza wa AMA tarehe 13 Oktoba 2025, na kuhitimishwa rasmi kwa Sekretarieti ya Mpito ya AMA kama jambo linaloashiria kuanza kwa uendeshaji kamili wa Shirika.

6. **PIA UNAKARIBISHA** uteuzi wa mjumbe mpya wa Bodi ya Usimamizi ya AMA kutoka Kanda ya Afrika ya Kati wakati wa Mkutano Maalumu wa Bodi, na **UNATAMBUA** kuwa muundo wa sasa wa Bodi una uwakilishi kutoka Kanda za Afrika ya Kati, Kusini, Mashariki na Magharibi, pamoja na wawakilishi wa WAHO, ECCAS, CEN-SAD na AUC.

7. **UNATOA WITO** kwa Kanda ya Afrika Kaskazini kukamilisha majadiliano yake ya ndani na kuwasilisha mteule wake kwa AMA kwa ajili ya kujadiliwa na kuteuliwa kwenye Bodi ya Usimamizi, ili kukamilisha muundo wa kisheria wa Bodi na kuhakikisha uwakilishi kamilifu wa kikanda.

8. **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama ambazo bado hazijasaini au kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Shirika la Dawa Afrika kufanya hivyo haraka, na

**UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama zote kuchukua hatua zinazohitajika ili kuutumia Mkataba huo ndani ya nchi**,** ikiwamo kuteua wahusika wa kitaifa wa AMA na kuoanisha taratibu za kitaifa za udhibiti ili kurahisisha ushirikiano wenye ufanisi na Shirika.

9. **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama zote kutekeleza majukumu yao ya kifedha kwa AMA kwa wakati, ikiwamo malipo ya michango iliyokadiriwa mara mfumo wa michango utakapopitishwa**,** ili kuhakikisha uendelevu wa kifedha, uhuru na ufanisi wa Shirika.

10. **UNAZINGATIA** maendeleo ya maandalizi ya Mpango Mkakati wa AMA (2026–2029), muundo wa taasisi, na mpango uliopendekezwa wa michango ya kifedha na kiwango cha michango, na **UNAMUAGIZA** Mkurugenzi Mkuu wa AMA kuwasilisha Mpango Mkakati uliopitishwa pamoja na nyaraka muhimu za kitaasisi katika Mkutano ujao wa Kawaida wa Baraza Kuu kwa ajili ya taarifa.

11. **PIA UNAIAGIZA** AUDA-NEPAD, kama taasisi iliyokuwa mwenyeji na mtekelezaji wa Mpango wa Ulinganifu wa Udhibiti wa Dawa na Afrika na Mpango wa ufuatiliaji wa usalama wa bidhaa za afya Afrika tangu kuanzishwa kwake, kuhamishia rasmi kwa Shirika la Dawa Afrika nyaraka zote za kitaalamu, kisheria, za programu, za kitasisi na kifedha, mali, mifumo, ahadi zinazoendelea na shughuli zinazoungwa mkono na wadau zinazohusiana na AMRH na AU3S, ili kurahisisha uhamishaji wa wazi na kamili wa mipango hii kwenda AMA na kuhakikisha kuendelea, uendelevu na utekelezaji wenye ufanisi chini ya uongozi wa AMA, kwa mujibu wa Mkataba wa AMA.

12. **UNASISITIZA** kwamba, kwa mujibu wa Mkataba wa AMA, AMA ni Shirika maalumu la Umoja wa Afrika linalohusika na kuweka mfumo wa udhibiti wa bara la Afrika kwa bidhaa za afya**,** ikiwamo uoanishaji wa viwango na miongozo ya udhibiti, uratibu wa tathmini na ukaguzi wa pamoja, kuimarisha mifumo ya udhibiti, na kukuza kutegemeana na ulinganifu wa udhibiti miongoni mwa Mamlaka za Kitaifa na Kikanda za Udhibiti wa Dawa**.**

13. **PIA UNATHIBITISHA** kwamba, kwa mujibu wa uamuzi Assembly/AU/Dec.880(XXXVII), pamoja na mambo mengine Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Afrika kimepewa jukumu la kuongoza uratibu wa mfumo wa uzalishaji wa bidhaa za afya barani Afrika kupitia Jukwaa la Uoanishaji wa Uzalishaji wa Bidhaa za Afya Barani Afrika (PHAHM)**,** likiwemo jukumu la kupanga vipaumbele vya afya ya umma, kuunda soko, kukadiria mahitaji, mifumo ya ununuzi wa pamoja na ushirikiano wa kimkakati ili kupanua uzalishaji wa ndani wa bidhaa za matibabu**.**

**14.** **UNATHIBITISHA** kwamba hakuna mgongano wa kisheria au wa kitasisi kati ya Mkataba wa AMA na maamuzi Assembly/AU/Dec.880(XXXVII) na

Assembly/AU/Dec.924(XXXVIII), na kwamba majukumu ya AMA na Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Afrika katika eneo la uzalishaji wa bidhaa za afya barani Afrika yanakamilishana, ambapo Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Afrika kinaongoza katika mfumo wa uzalishaji, mahitaji na uratibu wa soko, na AMA inaweka mfumo wa udhibiti uliooanishwa, sayansi ya udhibiti na majukumu ya kuhakiki ubora.

15. **UNASISITIZA** kwamba shughuli zinazohusiana na viwango vya udhibiti, idhini ya masoko, ukaguzi wa uzalishaji bora (GMP), usimamizi wa majaribio ya kliniki na ufuatiliaji wa bidhaa za afya ni sehemu ya mamlaka ya kitaalamu na ya kawaida ya AMA na mtandao wa Mamlaka za Kitaifa na Kikanda za Udhibiti wa Dawa, na zinapaswa kutekelezwa kwa ushirikiano wa karibu na, inapofaa, chini ya uongozi wa AMA.

16. **UNAAMUA** kwamba Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Afrika katika kutekeleza PHAHM na mipango mingine inayohusiana na uzalishaji, itazingatia kupanga vipaumbele vya afya ya umma, uratibu wa viwanda na soko, kuunda mahitaji na ununuzi wa pamoja, na kitaitegemea AMA kwa ajili ya viwango vya udhibiti, sayansi ya udhibiti, tathmini za pamoja, ukaguzi na kujenga uwezo unaohusiana na udhibiti.

17. **UNAIHIMIZA** Bodi ya Usimamizi ya AMA na Bodi ya Usimamizi ya Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Afrika kufanya majadiliano ya pamoja mara kwa mara kuhusu masuala yanayohusiana na uzalishaji wa ndani wa bidhaa za afya, ikiwa ni pamoja na kabla ya mikutano mikubwa ya kikanda na kimataifa, ili kuhakikisha mshikamano wa nafasi na ujumbe wa Umoja wa Afrika kwa Nchi Wanachama na wabia.

18. **UNAWAKARIBISHA** wabia wa maendeleo, mashirika ya hisani na sekta binafsi kuendeleza na, pale inapowezekana, kuongeza msaada wao wa kitaalamu na kifedha kwa AMA, kwa kuzingatia vipaumbele vya Afrika na kwa namna inayounga mkono, lakini si mbadala wa michango ya Nchi Wanachama.

19. **UNATOA WITO** kwa wadau wa maendeleo, mashirika ya kimataifa, mashirika ya hisani na sekta binafsi kujumuisha msaada wao kwa uzalishaji wa ndani wa bidhaa za afya barani Afrika ndani ya majukumu yanayokamilishana ya AMA na Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Afrika, na kupeleka msaada unaohusiana na udhibiti kupitia mipang0 iliyokubaliwa na AMA, kwa uratibu na Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Afrika.

20. **UNAIAGIZA** Kamisheni, kwa kushauriana na Shirika la Dawa Afrika, kuzingatia uteuzi wa Kiongozi wa Kisiasa wa Ngazi ya Juu na uteuzi wa Mjumbe Maalum kwa Shirika la Dawa la Afrika, ili kusaidia uhamasishaji wa uridhiaji na kuingiza Mkataba wa AMA katika sheria za nchi kwa nchi zote wanachamaa,

kuhamasisha msaada wa kisiasa na kifedha, na utekelezaji wa ufanisi wa Maamuzi ya Wakuu wa Nchi na Serikali na Baraza Kuu yanayohusiana na Shirika**.**

21. **PIA UNAIAGIZA** AMA kuripoti katika Mkutano ujao wa Kawaida wa Baraza Kuu kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa uamuzi huu**,** ikiwa ni pamoja na uhamishaji rasmi na ujumuishaji wa Mpango wa Uoanishaji wa Udhibiti wa Dawa Afrika na Mpango wa Ufuatiliaji wa Usalama wa Bidhaa za Afya Afrika ndani ya AMA, pamoja na kuhamishwa kwa mali zote, mifumo, mikataba na rasilimali zinazohusika kwa Shirika.

# UAMUZI
# KUHUSU KUFANYIKA MKUTANO MAALUM WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI WA UMOJA WA AFRIKA KUHUSU KUIMARISHA MIFUMO YA KUZUIA NA KUTATUA MIGOGORO AFRIKA

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNATHIBITISHA** kanuni na malengo yaliyoainishwa katika Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika, pamoja na dhamira yake ya kukuza amani, usalama na utulivu barani Afrika, na **UNAREJELEA** jukumu kuu la Baraza la Amani na Usalama (PSC) katika kuzuia, kudhibiti na kutatua migogoro barani;

2. **UNATAMBUA** kuendelea na ugumu wa migogoro ya silaha katika maeneo mbalimbali ya Afrika, ongezeko la mapinduzi, kuenea kwa mageuzi ya serikali yasiyo ya kikatiba, na ugaidi wa kimataifa na msimamo mkali wa kikatili, ambao unazidi kuwa tishio;

3. **UNASISITIZA** haja ya kuimarisha na kuendesha Taasisi ya Amani na Usalama ya Afrika (APSA) kwa ukamilifu na ufanisi, sambamba na matarajio ya Ajenda ya Umoja wa Afrika ya 2063, hasa Azma ya 4: *"Afrika yenye amani na usalama* "; kutekeleza mradi mkubwa wa "***kusitisha mapigano***"

4. **UNAZINGATIA** pendekezo la kufanya, mwezi Mei 2026, katika jiji la Luanda, Jamhuri ya Angola, Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kuhusu Kuimarisha Mifumo ya Kuzuia na Kutatua Migogoro barani Afrika;

5. **UNAAMUA** kwamba Mkutano wa Luanda uwe mkutano wa mwelekeo wa kimkakati, ulioandaliwa maalumu kwa ajili ya kuzuia migogoro barani Afrika pekee, na si jukwaa la kutangaza, lenye matokeo halisi na yanayopimika na makataa.

6. **UNAKARIBISHA** dhamira ya Serikali ya Jamhuri ya Angola ya ushirikiano wa pande mbalimbali na kukuza amani, usalama, maendeleo endelevu na utawala wa kidemokrasia barani Afrika**;**

7. **UNAAMUA** kuandaa Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kuhusu kaulimbiu: *"Kuimarisha Mifumo ya Kuzuia na Kutatua Migogoro Barani Afrika"* ;

8. **UNAAMUA PIA** kwamba Mkutano huo Maalum utafanyika mwezi Mei 2026, katika jiji la Luanda, Jamhuri ya Angola, na **UNAIAGIZA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kwa uratibu wa karibu na Nchi mwenyeji na mipango husika ya kikanda, kuchukua hatua zote muhimu ili kuhakikisha maandalizi, upangaji na uendeshaji wake umefanikiwa**;**

9. **UNASISITIZA UMUHIMU** wa ushiriki wa Wakuu wote wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika katika Mkutano Maalumu na **UNAITAKA** Kamisheni na nchi mwenyeji kupanga mkutano katika namna ambayo itawapa Wakuu wa Nchi na Serikali wanaoshiriki fursa ya kujadili suala hilo kwa uwazi na kutoa mapendekezo ya mwisho;

10. **UNATOA WITO** wa ushiriki kikamilifu wa Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda na Mipango ya Kikanda (RECs/RMs), pamoja na vyombo vingine husika vya Umoja wa Afrika katika Mkutano wa Maalum.

.

# UAMUZI

## KUHUSU MKUTANO MKUU KUHUSU KAULIMBIU YA MWAKA 2026 "KUHAKIKISHA UPATIKANAJI ENDELEVU WA MAJI NA MIFUMO SALAMA YA USAFI ILI KUFIKIA MALENGO YA AJENDA 2063"

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAKURISISHA** uamuzi wa Mkutano Mkuu Assembly/AU/Des.912(XXXVIII) ambao ulipitisha Kaulimbiu ya Mwaka 2026

2. **UNAPOKEA** Andiko Dhana na Ripoti kuhusu Mpango wa Utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka 2026: "Kuhakikisha Upatikanaji Endelevu wa Maji na Mifumo Salama ya Usafi wa Mazingira ili Kufikia Malengo ya Ajenda 2063";

3. **UNAIDHINISHA** Mpango wa Utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka 2026, ikiwa ni pamoja na uzinduzi wa Dira ya Maji ya Afrika na Sera ya mwaka 2063. **UNAKARIBISHA** Uzinduzi rasmi wa Kiwango cha Juu wa Kaulimbiu hiyo uliopangwa kufanyika wakati wa kikao cha ufunguzi wa Mkutano wa 39 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali mwezi Februari 2026;

4. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama, Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs), na Washirika kushiriki kikamilifu katika uzinduzi huo na kuunga mkono utekelezaji wa Mpango wa Utekelezaji ili kuharakisha maendeleo kuelekea Ajenda ya 2063 na SDG 6;

5. **UNAITAKA** Kamisheni, kwa kushirikiana na Baraza la Mawaziri wa Afrika kuhusu Maji (AMCOW) na washirika, kutafuta rasilimali, kukuza uhamasishaji, na kuripoti kuhusu maendeleo ya utekelezaji kwa Vyombo husika vya Sera vya AU.

---

[2] Pingamizi lililowekwa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho ya Ethiopia kuhusiana na Dira na Sera ya Maji ya Afrika 2063

## UAMUZI
## KUHUSU KUIMARISHA MBINU ZA UTENDAJI KAZI ZA VYOMBO VYA SERA VYA UMOJA WA AFRIKA

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZINGATIA** Andiko Dhana kuhusu "kuimarisha mbinu za utendaji kazi za Vyombo vya Sera vya Umoja wa Afrika" kama lilivyoandaliwa na Jamhuri ya Angola kama mwenyekiti wa Umoja huo kwa mwaka 2025-2026; na

2. **UNAAMUA:**

**(i)** **KUSISITIZA** NA **KUTEKELEZA KIKAMILIFU** mamlaka yaliyowekwa na uamuzi Assembly/AU/Dec.582(XXV) na uamuzi Assembly/AU/Dec.635(XXVIII), kuhakikisha ajenda ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali inathibitishwa na kuwekewa mipaka kwa masuala yasiyozidi matatu (3) ya muhimu na ya kimkakati (k.m, Amani na Usalama, Utangamano wa Bara, Masuala ya Fedha) katika kila Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali.

**(ii)** **KWAMBA** kila moja ya masuala haya ya kimkakati hayatakuwa na zaidi ya vipengee viwili (2) katika kila mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali

**(iii)** **KUTUMIA** si zaidi ya siku mbili (2), ili kukuza ushiriki wa Nchi Wanachama zote katika ngazi ya juu iwezekanavyo na kuhakikisha ufanyaji maamuzi wenye ufanisi na unaolenga kwenye masuala ya kimkakati yaliyoamriwa.

**(iv)** **KUKASIMISHA** masuala yote yasiyo ya kimkakati au ya kitaalamu yanayotoka kwenye Vyombo vya Umoja wa Afrika na Nchi Wanachama na majukumu mengine yote ya kiuendeshaji yaliyotambuliwa kwa Baraza Kuu, huku yakikasimishwa zaidi kwa Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC) kadri inavyofaa. Zaidi ya hayo, **KUTHIBITISHA** ujumuishaji wa ripoti kutoka kwa Viongozi walioteuliwa kwenye ajenda ya Mkutano Mkuu, kuhakikisha vipengele vinavyohusiana tu moja kwa moja na Kaulimbiu ya Mwaka ndivyo vinavyochaguliwa kwa ajili ya kuwasilishwa, kwa kufuata kikamilifu uamuzi 819 wa Mkutano Mkuu na kwa hali ya dharura.

**(v)** **KUWEKA MAKATAA** kwa ajili ya kukamilisha mikutano yote ya Kamati Maalum ya kitaalamu (STC) ifikapo tarehe 31 Oktoba. Makataa haya ni ya lazima ili kuhakikisha Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC) ina muda wa kutosha wa kupitia kwa kina na kujadili kwa kina ripoti na rasimu zote za maamuzi kabla ya kufungwa kwa shughuli za mwaka za AU mwezi Desemba.

**(vi)** Kwamba hakuna mikutano ya kisheria ya Chombo chochote cha AU, au Taasisi yoyote ya AU isipokuwa PRC, PSC, itakayoandaliwa wakati wa mwezi wa Baraza Kuu, Mkutano Mkuu na Mkutano wa Uratibu wa Nusu Mwaka (Januari / Februari/Julai).

**(vii)** **KUZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuwakilishwa katika ngazi inayofaa katika vikao vya Vyombo vya Sera vya Umoja wa Afrika

**(viii)** **K**wamba ripoti ya Baraza Kuu kuanzia sasa itawasilishwa na Mwenyekiti wake kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali, sambamba na utaratibu uliopo ambapo Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC) inawasilisha ripoti yake kwa Baraza Kuu kupitia Mwenyekiti wake, na hivyo kuhakikisha mshikamano wa kitaasisi na kuimarisha uwazi, uhalali, na uwazi wa kazi ya Baraza huku ikiimarisha umiliki wa kisiasa wa mapendekezo yake kwa Mkutano Mkuu.

**(ix)** **KUTHIBITISHA** kwamba Wawakilishi wa Kudumu walioidhinishwa na Kamisheni ya Umoja wa Afrika watapewa ruhusa ya kuhudhuria ya kuhudhuria bila vikwazo kwenye vikao vyote vya Baraza Kuu, Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali, na mikutano yote isiyo ya kisheria ya Umoja wa Afrika. Ushiriki huo utaruhusiwa tu baada ya kuwasilishwa kwa beji rasmi ya uidhinishaji iliyotolewa na Kamisheni, bila kuhitaji beji yoyote ya ziada, ili kuhakikisha mwendelezo wa kitaasisi na uwepo wa ngazi ya juu wa mara kwa mara.[2]

**(x)** **KUAGIZA KUZIANGATIA KIKAMILIFU** Protokali inayohitaji Mkutano na Waandishi wa Habari mara tu baada ya kumalizika kwa kila Kikao cha Mkutano Mkuu. Hii ni muhimu ili kuhakikisha mwonekano wa haraka, wa wazi, na sahihi wa kazi na maamuzi ya AU kwa umma wa bara na kimataifa.

**(xi)** **KUTOA WITO KWA** Nchi Wanachama kuhamasisha kupitishwa na kutekelezwa kwa sera za kitaifa zinazoendana moja kwa moja na, na kuendeleza kikamilifu, malengo ya Kaulimbiu ya Mwaka, na hivyo kuongeza matokeo ya bara.

**(xii)** **KULIPA MAMLAKA** Baraza Kuu kufanya uchanganuzi wa kina wa uwezekano wa kufanyika na faida za kupitisha mpango ambao unawezesha Uenyekiti Ujao wa Mkutano Mkuu ambao unapendekeza kaulimbiu ya mwaka. Uchanganuzi unapaswa kutathmini haswa jinsi mbinu kama hiyo ingeunda hali zenye malengo zaidi, nyenzo, na zinazopimika kwa ajili ya kutathmini athari na utumiaji wa sera wakati wa kipindi cha Uenyekiti wa Mkutano Mkuu.

**(xiii)** **KUIAGIZA** Kamisheni ya AU kukamilisha mara moja Hadidu za Rejea (ToR) zilizo wazi, za uendeshaji, na zinazopatikana hadharani kwa ajili ya Jopo la Watu Mashuhuri wa Afrika, ambalo lazima liweke wazi vigezo vya tathmini ya wagombea. Zaidi ya hayo, ili kuhakikisha uwazi wa hali ya juu, ripoti ya mwisho ya Jopo hilo itatakiwa kujumuisha orodha ya majina yote yanayojadiliwa, pamoja na asilimia halisi iliyopatikana kwa kila mgombea wakati wa awamu ya kwanza ya mchakato wa tathmini.

**(xiv)** **KUHIMIZA** Nchi Wanachama kuweka kipaumbele na kutenga rasilimali zinazohitajika kwa ombi la Kamisheni ya AU la kuanzishwa kwa Kitengo maalum cha G20. Kitengo hiki kitakuwa na wafanyakazi maafisa waliojitolea pekee kwa kitengo G20 ili kuhakikisha mchango uliopangwa, wa haraka, na wenye athari wa Umoja wa Afrika ndani ya mfumo wa Kundi la G20, na:

**3. UNAKASIMISHA KWA PRC:**

**(i)** **MAMLAKA** Kurugenzi ya Usimamizi wa Mikutano na Machapisho (DCMP), ikiongozwa na Kamati Ndogo ya Programu na Mikutano, **KUBADILI** kalenda halisi ya Mkutano kuwa Kalenda moja, kamili, na isiyoweza kujadiliwa ya Mkutano wa Mwaka kwa mikutano yote ya kisheria ya Vyombo vya AU, ikiwa ni pamoja na PRC na Kamati zake Ndogo, inayojumuisha kipindi cha kuanzia Machi hadi Januari ya mwaka unaofuata na kuitekeleza kwa ukamilifu. Kalenda hii **ITAUNGANISHWA** na Programu za Kazi za kila mwaka zilizoandaliwa, kupitishwa, na kuwasilishwa na Kamati Ndogo husika za PRC.

**(ii)** **KUWEKA** ratiba inayoamuru kwamba Kikao cha Kawaida cha PRC kitaitishwa mara moja baada ya kumalizika kwa kila Mkutano wa wakuu wa Nchi na Serikali. Hii ni muhimu ili kuhakikisha ushiriki endelevu, wenye taarifa, na wa wakati unaofaa wa PRC na Kamati zake Ndogo katika ufuatiliaji wa maamuzi na mpango kazi wa mwaka mzima.

**(iii)** **KUWEKA RASMI** na **KUTEKELEZA** ratiba ifuatayo ya maandalizi kwa ajili ya Vikao vya Baraza Kuu na Mkutano Mkuu vya Februari: kazi ya maandalizi ya PRC, inayoanzi na Kamati zake Ndogo, itaanza Septemba na kumalizika ifikapo Desemba kila mwaka. Muda huu ni wa lazima ili kuhakikisha Ajenda za Muda mfupi na nyaraka zote zinazohusiana zinasambazwa kwa Nchi Wanachama angalau siku thelathini (30) kabla, kwa kufuata kabisa Kanuni za Uendeshaji za Vyombo vya Sera.

**(iv)** Katika maandalizi ya mkutano wa uratibu wa nusu mwaka mwezi Juni/Julai, kazi ya PRC, ukitanguliwa na Kamati zake Ndogo, inapaswa kuanza Mei**.**

**(v)** **KUFANYA MARA KWA MARA MIKUTANO YA KISHERIA** mwaka mzima ili kuchunguza na kuwasilisha ripoti zilizokamilishwa kutoka kwa Kamati zake Ndogo, vyombo vingine vya AU, na STC. Lengo dhahiri la vikao hivi ni kuthibitisha na kurahisisha rasimu ya ajenda ya Baraza Kuu.

**(vi)** **KUSIMAMIA KIKAMILIFU UWASILISHAJI NDANI YA MAKATAA**. Ripoti yoyote ambayo haitapokelewa na Sekretarieti angalau siku 3 za kazi kabla ya mkutano wa PRC, kikao cha mwisho cha maandalizi cha Baraza Kuu **HAITAJADILIWA** katika kikao hicho, bila kujali mada, na badala yake itaahirishwa hadi mkutano wa kisheria unaofuata wa PRC na Baraza Kuu.

(vii) **KUTENGA RASILIMALI MUHIMU NA ZA KUTOSHA ZA BAJETI** ili kuhakikisha urejeshaji endelevu wa mikutano ya ana kwa ana ya mara kwa mara ya Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC), huku kipaumbele kikitolewa kwa majadiliano ya ana kwa ana kwa ajili ya kuongeza ufanisi na ubora.

(viii) **KUIMARISHA NA KUAGIZA** usambazaji kwa wakati kwa nyaraka zote za kufanyia kazi angalau siku kumi (10) za kazi kabla ya mikutano yote ya kisheria na siku 5 za kazi kwa mikutano isiyo ya kisheria, kutekeleza kikamilifu Kanuni husika za Utaratibu ili kuwapa wajumbe muda wa kutosha kwa ajili ya mapitio ya kina, mashauriano muhimu ya kitaifa, na maandalizi kabla ya kikao.

(ix) **KUPANGA** mkutano wa kwanza wa robo mwaka wa Uongozi *(Bureau)* wa Mkutano Mkuu utakaofanyika sambamba na Mwenyekiti (CP) na Makamu Mwenyekiti (DCP) na wenyeviti wa Kamati Ndogo za PRC kabla ya kuanza kwa Vikao vya PRC, ili kuhakikisha uoanishaji wa kimkakati na maandalizi yaliyoratibiwa.

(x) Kuandaa vikao vya taarifa vya kila robo mwaka kwa ajili ya Makamishna kuipa taarifa fupi PRC kuhusu programu na shughuli zilizopangwa kwa mwaka.

(xi) **KUIAGIZA** Kamati ya Uandishi kukutana mara moja baada **ya** vikao vya Baraza Kuu na Mkutano Mkuu ili kukamilisha marekebisho muhimu ya kitaalamu na kisheria kwa rasimu ya Maamuzi yaliyopitishwa. Hii ni muhimu ili kuhakikisha Maamuzi ya mwisho yaliyosainiwa yanatolewa na kusambazwa kwa Nchi Wanachama ndani ya siku zisizozidi saba (10) baada ya kufungwa kwa mikutano.

(xii) **KUIAGIZA** Sekretarieti na Ofisi ya Mshauri wa Sheria (OLC) kushirikiana katika uandaaji na upitishaji wa Miongozo Sanifu (yenye violezo vya sampuli vilivyooanishwa) kwa ajili ya uandishi wa Maamuzi yote ya AU, hususan ili kuboresha usomaji wake, uwiano, na uthabiti wake wa kisheria, kwa kuzingatia kikamilifu Uamuzi EX.CL/Dec.1194 (XLII).

(xiii) **KUZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuimarisha na kuwezesha Jukumu la Wakuu wa Kanda kwa kutoa kipaumbele kwa wasilisho la misimamo ya pamoja ya kanda katika mikutano ya PRC. Zaidi ya hayo, **KUDHAMIRIA** kutekeleza ratiba ya mikutano iliyopangwa na kuandaliwa vizuri kwa vikao vyote, kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi 12:00 jioni, ili kuongeza ufanisi.

(xiv) **KUFANYA MKUTANO MARA KWA MARA** wa Uongozi wa PRC katika muundo uliopanuliwa ili kujumuisha Wakuu wa Kanda na Uongozi wa Kamisheni ya AU. Mfumo huu utatumika kuhakikisha ushirikiano imara zaidi, ushughulikiaji wa masuala uliooanishwa, na utekelezaji wa haraka wa Maamuzi. Kila mkutano wa PRC lazima utanguliwe na mkutano huu wa

Uongozi uliopanuliwa ukiwa na ushiriki kamili kutoka kwa Uongozi wa Kamisheni.

(xv) **KUANZISHA** Mfumo rasmi wa Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Maamuzi (ulioundwa na Troika ya PRC) ili kufuatilia kwa makini utekelezaji wa maamuzi yote yaliyopitishwa. Mfumo huu utapewa mamlaka ya kuwasilisha Ripoti ya Ufuatiliaji kamili na inayolenga matokeo kwa PRC wakati wa mkutano wake wa kisheria mara baada na kabla ya Baraza Kuu.

~~(xvi)~~ **KUPITISHA** utaratibu rahisi wa hitimisho ambapo Ripoti ya PRC na rasimu ya Maamuzi iliyoambatishwa vitawasilishwa na Mwenyekiti wa PRC kwa Baraza Kuu kwa ajili ya kupitishwa kama kifurushi kimoja cha jumla, bila mjadala, isipokuwa kwa wajumbe wanaotaka kutoa maoni mahususi, yaliyowasilishwa mapema, na muhimu ambayo hayafungui tena majadiliano kuhusu masuala muhimu~~.~~

(xvii) **KUHIMIZA** utekelezaji wa haraka wa Mahitimisho ya Dakar na **KUAGIZA** upangaji wa haraka wa ratiba ya Semina kuhusu Mbinu za Utendaji Kazi za PRC. Semina hii itafanyika katika Makao Makuu ya AU mjini Addis Ababa ili kuhakikisha ufanisi kwenye gharama na uratibu wa vifaa.

(xviii) **KUFANYA** Mapitio kuhusu Taratibu za Ushiriki wa AU katika G20, kama ilivyoainishwa katika Uamuzi Assembly/AU/Dec873(XXXVII). Mapitio hayo yatatoa mapendekezo halisi na ya kimkakati yatakayowasilishwa kwa Baraza Kuu na Mkutano Mkuu kwa lengo la kuongeza thamani ya uanachama wa G20 wa AU kwa Bara zima.

(xix) **KUITAKA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuchukua hatua muhimu kuelekea uandaaji, ukamilishaji, na upitishaji wa Mfumo wa Kisheria ulio wazi, thabiti, na unaofanya kazi unaosimamia mwenendo, wigo, na matokeo ya Mikutano Isiyo ya Kisheria ya Umoja wa Afrika, kuuwasilisha kwa PRC na Baraza Kuu kwa ajili ya kuidhinishwa, na baadaye kwa Mkutano Mkuu kwa ajili ya kupitishwa mwezi Januari 2027.

(xx) **KUITAKA** Kamisheni ya AU kupanga na kuandaa Semina ya Mwaka ya Ukaribisho na Maelekezo kwa ajili ya wanadiplomasia wote walioidhinishwa hivi karibuni. Semina hiyo lazima itoe maarifa kamili na ya kina kuhusu miundo ya AU, mbinu za utendaji kazi, na michakato ya kufanya maamuzi, pamoja na mgao maalum na unaolengwa wa bajeti kwa ajili ya kazi hii muhimu ya kitaasisi.

(xxi) **KUITAKA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuitisha, mara mbili kwa mwaka, mkutano kwa njia ya mtandao wa Makundi ya Afrika yaliyoko katika nchi zinazoandaa Ubia wa AU, kwa lengo la kuimarisha ushiriki na kuongeza uelewa wa kanuni na taratibu zinazosimamia mipango hii ya ushirikiano.

(xxii) **KUITAKA** Kamisheni iambatanishe kwenye rasimu zote athari za kifedha, kisheria na kimuundo za utekelezaji wake

4. **KUIOMBA** PRC, kwa kushirikiana na Kamisheni, wakati wa mkutano wao wa pamoja, kuzingatia uwezekano wa kukasimu kwa PRC jukumu la kuendesha uchaguzi wa wajumbe wa vyombo vya kitaalamu vya AU.

# UAMUZI KUHUSU
# KAULIMBIU YA UMOJA WA AFRIKA YA MWAKA 2027:

## “AU KUELEKEA MAADHIMISHO YAKE YA MIAKA 25: KUTUMIA UWEZO KAMILI WA SAATM NA TEKNOLOJIA MPYA KWA UTANGAMANO WA BARA”

**Mkutano Mkuu,**

**1. UNAKUMBUSHIA** kuanzishwa kwa Soko la Pamoja la Usafiri wa Anga la Afrika (SAATM), kama mradi mkuu wa Ajenda ya 2063, na ahadi za AU za kutumia teknolojia zinazoibuka kwa ajili ya ujumuishaji wa bara chini ya mikakati na mipango husika;

2. **UNASISITIZA** jukumu muhimu la utekelezaji wa SAATM ulioharakishwa, unaoungwa mkono na teknolojia zinazoibuka, ili kuendana kikamilifu na Mkataba wa Chicago na viwango vya kimataifa vya usafiri wa anga vinavyotumika;

3. **UNAKARIBISHA** Andiko Dhana, **UNAPITISHA** Kaulimbiu ya Mwaka 2027 kama “AU Kuelekea Maadhimisho yake ya Miaka 25: Kutumia Uwezo Kamili wa SAATM na Teknolojia Mpya kwa Ujumuishaji wa Bara”

4. **UNATOA WITO** kwamba fedha na rasilimali zinazohitajika zitengewe kwa ajili ya utekelezaji wa kaulimbiu hiyo;

5. **UNAIAGIZA** AUC, kwa kushirikiana na AFCAC, AfCFTA, AUDA-NEPAD, na wadau wengine, kutengeneza mwongozo, kwa uratibu na mamlaka za usafiri wa anga za Nchi Wanachama, na kuiwasilisha kweye Mkutano wa 49 wa Kawaida cha Baraza Kuu.

6. **UNAIAGIZA** AUC kwa ushirikiano wa karibu na AFCAC na AUDA-NEPAD, kufuatilia, na kuripoti kuhusu utekelezaji, ikifanya kazi kama chombo kuwezesha na kuratibu bila kuathiri mamlaka ya udhibiti ya kitaifa.

## UAMUZI
## KUHUSU KUUCHUKULIA UTUMWA, UHAMISHAJI NA UKOLONI KAMA UHALIFU DHIDI YA UBINADAMU NA MAUAJI YA KIMBARI DHIDI YA WATU WA AFRIKA

(Assembly/AU/25 (XXXVIII)

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZINGATIA** pendekezo lililotolewa na Jamhuri ya Togo kuhusu '*kuuchukulia utumwa, uhamishaji na ukoloni kama uhalifu dhidi ya ubinadamu na mauaji ya kimbari dhidi ya watu wa Afrika*' na **UNATAMBUA** umuhimu kaulimbiu hii kwa Bara la Afrika;

2. **UNAREJELEA** uamuzi Assembly/AU/Dec934(XXXVIII) kuhusu kuuchukulia utumwa, uhamishaji na ukoloni kama uhalifu dhidi ya ubinadamu na mauaji ya kimbari dhidi ya watu wa Afrika

3. **UNAREJELEA ZAIDI** Uamuzi kuhusu Kaulimbiu ya Mwaka 2025;

4. **UNAZINGATIA** na kuridhishwa na maendeleo yaliyopatikana katika Utekelezaji wa Uamuzi Assembly/AU/Dec.934(XXXVIII) na Nchi Wanachama, Kamisheni ya AU na Vyombo vya AU;

5. **UNAZINGATIA ZAIDI** hitimisho la kwanza la Utafiti wa AUCIL kuhusu matokeo ya uainishaji wa ukoloni kama uhalifu dhidi ya ubinadamu, na uainishaji wa vitendo fulani vilivyofanywa wakati wa utumwa, kufukuzwa, na ukoloni kama mauaji ya kimbari dhidi ya watu wa Afrika, na **UNAAOMBA** AUCIL iendelee na kazi hiyo;

6. **UNAAMUA** kuuchukulia 'utumwa, uhamishaji na ukoloni kama uhalifu dhidi ya ubinadamu na mauaji ya kimbari dhidi ya watu wa Afrika' na **UNAAMUA** kufanya kazi pamoja kwa mshikamano ili kutambuliwa hivyo katika ngazi ya kimataifa;

7. **UNAAMUA ZAIDI** kushughulikia suala hilo

## UAMUZI KUHUSU MAGEUZI YA TARATIBU ZA UENDESHAJI WA MKUTANO MKUU NA KATIBA YA KAMISHENI

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZINGATIA** marekebisho yaliyopendekezwa ya Katiba ya Kamisheni na Taratibu za Uendeshaji wa Mkutano Mkuu;

2. **UNAITAKA** PRC kujadili ripoti hii na kutoa mapendekezo kwa Mkutano wa 49 wa Kawaida cha Baraza Kuu mwezi Juni 2026;

# UAMUZI KUHUSU MATOKEO YA KONGAMANO LA 9 LA UANAMAJUMUI WA KIAFRIKA LILILOFANYIKA KUANZIA TAREHE 8 HADI 12 DESEMBA 2025 MJINI LOMÉ, TOGO

**Mkutano Mkuu**,

1. **UNAZINGATIA** ripoti ya Kongamano la 9 la Uanamajumui wa Kiafrika, lililofanyika kuanzia tarehe 8 hadi 12 Desemba 2025 mjini Lomé, katika Jamhuri ya Togo, kuhusu kaulimbiu "Uanamajumui mpya wa Kiafrika na jukumu la Afrika katika mageuzi ya taasisi za pande mbalimbali: kutafuta rasilimali na kujipanga upya kwa ajili ya kuchukua hatua";

2. **UNAREJELEA** uamuzi Assembly/AU/Dec. 913 (XXXVIII) uliopitishwa katika Kikao cha 38 cha Kawaida cha Mkutano huo ukiikabidhi Togo na Kamisheni jukumu la kuandaa Kongamano la 9 la Uanamajui wa Kiafrika na kuripoti kwenye Kongamano mwaka 2026;

3. **UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Togo na Kamisheni kwa kufanikiwa kuandaa Kongamano hili;

4. **UNAREJELEA** malengo na kanuni za Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika, pamoja na matarajio na vipaumbele vya Ajenda ya Umoja wa Afrika ya 2063;

5. **UNAREJELEA ZAIDI** Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu mageuzi ya taasisi za pande mbalimbali, kwa mujibu wa Makubaliano ya Ezulwini na Azimio la Sirte;

6. **UNATHIBITISHA** umuhimu wa Uanamajumui wa Kiafrika kama mfumo wa umoja, mshikamano, maendeleo na ushawishi wa kimkakati kwa Afrika na diaspora yake;

7. **UNAZINGATIA** mapendekezo yanayotokana na kazi ya Kongamano, haswa hitaji la kuimarisha ushirikiano wa bara na diaspora, kukuza uhuru wa kitamaduni, kiuchumi na kisiasa wa Afrika, na kuimarisha ushawishi wa Afrika katika vyombo vya kimataifa;

8. **UNAPITISHA** Azimio la Mwisho la Kongamano la 9 la Uanamajumui wa Kiafrika na Mpango wake Mkuu kama mfumo wa kimkakati wa Uanamajumui Mpya wa Kiafrika katika karne ya 21;

9. **UNAAMUA** kuanzisha mfumo wa kudumu wa ufuatiliaji na uratibu, unaohusisha Nchi Wanachama, Kamisheni ya AU na diaspora, ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa maamuzi na mapendekezo ya Kongamano;

10. **UNAAMUA** kuanzisha Kamati inayohusika na kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo na maamuzi ya Kongamano la la 9 la Afrika;

11. **UNAUNGA MKONO** kukuza elimu ya Kiafrika, uboreshaji wa lugha za Kiafrika, urejeshaji wa mali za kitamaduni na utekelezaji wa mifumo ya fidia na utambuzi wa uhalifu wa kihistoria;

12. **UNAHIMIZA** utafutaji wa rasilimali za Kiafrika, uboreshaji wa utaalamu na uongozi kutoka kwa watu wanaoishi nje ya nchi, pamoja na maendeleo ya ushirikiano wa kimkakati wa Kusini-Kusini na kati ya mabara na maeneo yenye watu wenye asili ya Afrika;

13. **UNASISITIZA** hitaji la mageuzi ya haki ya mfumo wa pande mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ili kuhakikisha uwakilishi mzuri na sawia wa Afrika;

14. **UNAIAGIZA** Jamhuri ya Togo kuwasilisha kwa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa azimio kuhusu kuanzishwa kwa siku ya kimataifa ya fidia na urejeshaji;

15. **UNAAMUA** kuandaa kila baada ya miaka mitano (05) Kongamano la Uanamajumui wa Kiafrika na kuunda uongozi wa kudumu ya Kongamano la Uanamajumui wa Kiafrika ambalo nchi na/au taasisi yake mwenyeji itaamuliwa baada ya mashauriano kati ya Mataifa na wadau mbalimbali;

**16.UNAYAALIKA** Mataifa ya Afrika yanayozikaribisha jamii na watu wenye asili ya Afrika kujumuisha mapendekezo ya Kongamano la 9 la Uanamajumui wa Kiafrika katika sera zao za kitaifa, kikanda na kidiplomasia.

# UAMUZI

## KUHUSU ENEO HURU LA BIASHARA BARANI AFRIKA (AfCFTA)

**EX.CL/1667(XLVIII)**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAELEZEA MASIKITIKO** kuhusu kutotekelezwa kwa aya ya 18 ya uamuzi wa Mkutano Mkuu Assembly/AU/Dec.911(XXXVIII) na **KUIELEKEZA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kutekeleza kikamilifu uamuzi kuhusu kurejeshwa kwa dola za Marekani milioni 2.9 kutoka kwenye salio la matumizi lililokubaliwa na Kikao cha 38 cha Kawaida cha Mkutano Mkuu; na **UNAIELEKEZA ZAIDI** Kamisheni kulipa kiasi kilichosalia cha dola za Marekani milioni 1.7 kama sehemu ya bajeti ya matumizi ya AU iliyopitishwa.

2. **UNAZINGATIA** Maelekezo ya Baraza la Mawaziri kuhusu Utekelezaji wa Kanuni za Muda za Asili ya bidhaa za nguo na mavazi yaliyopitishwa na Baraza la Mawaziri.

3. **UNALIELEKEZA** Baraza la Mawaziri kufanya mapitio ya taratibu za ushuru, kwa mujibu wa Vifungu vya 28 na 29 vya Mkataba unaoanzisha AfCFTA .

4. **UNAEILEKEZA** Sekretarieti kubuni na kutekeleza mfumo wa utambulisho wa kidijitali na wa ufuatiliaji wa bidhaa zinazoundwa chini ya kanuni za AfCFTA.

5. **UNALIELEKEZA PIA** Baraza la Mawaziri kukamilisha Mkataba wa Utambuzi wa Pamoja wa AfCFTA (MRA) na **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutenga rasilimali ili kuendeleza muafaka wa kanuni chini ya Mfumo wa Kanuni za Kitaalamu wa Bara la Afrika (ACTReF).

6. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuimarisha miundo ya kitaifa ya utatuzi wa vikwazo visivyokuwa vya ushuru (NTB) kwa ajili ya utatuzi bora wa NTB chini ya AfCFTA na **UNAIELEKEZA** Sekretarieti ya AfCFTA na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda kuimarisha ushirikiano na uratibu wao ili kutatua NTB kwa ufanisi.

7. **UNALIELEKEZA** Baraza la Mawaziri kuanzisha mchakato wa kuchagua nchi mwenyeji wa Mamlaka na Mahakama ya Ushindani ya AfCFTA na **UNAIELEKEZA ZAIDI** Sekretarieti kuandaa mpango wa biashara wa Mamlaka hiyo na Mahakama,

ukiwemo mwelekeo wa kimkakati, miundo na mifumo ya ufadhili ya muda mfupi, wa kati na wa muda mrefu na kuuwasilisha kwa Vyombo husika vya Sera vya AU.

8. **UNAIPONGEZA** Sekretarieti ya AfCFTA kwa kupata dola milioni 5 za Marekani za ufadhili wa nje ili kusaidia utekelezaji wa Protokali ya AfCFTA kuhusu Hakimiliki na **UNALIAGIZA** Baraza la Mawaziri kutoa mapendekezo kwa Mkutano Mkuu kuhusu kudumisha, kulinda na kutetea haki za kisheria za Wamiliki wa Hakimiliki wa Afrika

9. **UNAPITISHA** mapendekezo ya Baraza la Mawaziri kuteua watu wawili (2) walioteuliwa kujiunga na Chombo cha Rufaa.

| **Jina Kamili** | **Nchi** | **Kanda** |
|---|---|---|
| 1) Bw. Bett Jackson Kiprotich | Kenya | Mashariki |
| 2) Bw. Paul Kuruk | Ghana | Magharibi |

10. **UNAPITISHA:**

- Kanuni zilizokubaliwa katika Kiambatisho cha IV kuhusu Kanuni za Asili ya Bidhaa zilizoidhinishwa na Baraza la Mawaziri;
- Rasimu ya Ratiba ya Ahadi Maalum ya Ufalme wa Morocco;

11. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuanza kutekeleza Utambulisho wa Kidijitali wa AfCFTA na kutekeleza kwa haraka ahadi zao kuhusu miundombinu ya umma ya kidijitali, inayohusiana na utambulisho wa kidijitali, malipo ya kidijitali kwa biashara za kuvuka mipaka na ulinzi na uhamishaji wa data za kuvuka mipaka chini ya Protokali ya Biashara ya Kidijitali ili kuwezesha biashara jumuishi ndani ya Afrika na kurahisisha usafirishaji wa bidhaa, huduma, mtaji na wanabiashara chini ya AfCFTA.

12. **UNAIELEKEZA** Sekretarieti ya AfCFTA kutafuta na kuhamasisha rasilimali za kusaidia maendeleo ya miundombinu ya kidijitali na miundombinu ya umma ya kidijitali kwa ajili ya biashara ya kidijitali na **UNAWAOMBA** wabia wa maendeleo, kwa ushirikiano na Sekretarieti ya AfCFTA, kuingiza utekelezaji wa Protokali ya Biashara ya Kidijitali katika miradi na programu zao zilizopo na zijazo.

13. **UNAREJELEA** aya ya 13 ya uamuzi **Assembly/AU/Dec.911(XXXVIII)** wa Kikao cha 38 cha Kawaida cha Mkutano Mkuu na **UNAIELEKEZA** Sekretarieti ya AfCFTA na Afreximbank kuwasilisha ripoti kuhusu utekelezaji wa Mfuko wa Biashara ya Kidijitali chini ya Mfuko wa Marekebisho wa AfCFTA kwa Kikao cha 40 cha Kawaida cha

Mkutano Mkuu na kuharakisha mchakato wa kuajiri na kuajiri Mkuu wa Biashara ya Kidijitali.

14. **UNAZITAKA** Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda kuandaa mipango/shughuli za utekelezaji kutoka kwa mikakati yao ya kitaifa/kikanda ya utekelezaji wa AfCFTA na **UNAIELEKEZA** Sekretarieti ya AfCFTA kuzisaidia Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda katika mchakato huu ili kuendeleza utekelezaji madhubuti wa mikakati hiyo.

15. **UNAIELEKEZA** Sekretarieti ya AfCFTA kufuatilia na kutoa ripoti za mara kwa mara kuhusu athari za sera za biashara na kiuchumi za nchi ambazo ni wahusika wa tatu kwa biashara ndani ya Afrika na zilizo na madhara katika utekelezaji wa Mkataba wa AfCFTA.

16. **UNAMUOMBA** Kinara/Kiongozi wa AfCFTA, Mhe. Mahamadou Issoufou, kuwasilisha ripoti ya maendeleo kuhusu hali ya utekelezaji wa AfCFTA katika Mkutano wa 8 wa Uratibu wa Kati ya Mwaka utakaofanyika Juni 2026.

## UAMUZI WA KUPITISHA RASIMU YA HATI ZA KISHERIA

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAPOKEA** mapendekezo ya Baraza Kuu ya Rasimu kuhusu Hati za Kisheria kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa.

2. **UNAPITISHA** Rasimu ya Hati za Kisheria zifuatazo:

   (a) *Rasimu ya Katiba ya Taasisi ya Fedha ya Afrika*

   (b) *Rasimu ya Marekebisho ya Katiba ya Baraza la Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni la Umoja wa Afrika*

   (c) *Rasimu ya Viambatisho vya Protokali ya Makubaliano ya Kuanzisha Eneo Huru la Biashara Afrika Kuhusu Hakimiliki za Ubunifu*

      i. *Kiambatisho kuhusu Aina za Matumizi*
      ii. *Kiambatisho kuhusu Maarifa ya Jadi, Utamaduni wa Jadi na Rasilimali za Kijenetiki*
      iii. *Kiambatisho kuhusu Ulinzi wa Aina za Mimea*
      iv. *Kiambatisho kuhusu Hatimiliki*
      v. *Kiambatisho kuhusu Alama*
      vi. *Kiambatisho kuhusu Ubunifu Viwandani*
      vii. *Kiambatisho kuhusu Alama za Kijiografia*
      viii. *Kiambatisho kuhusu Hakimiliki na Haki Zinazohusiana nazo*
      ix.

3. **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kuridhia hati za kisheria ili kuhakikisha zinaanza kutumika haraka na kutekelezwa ipasavyo.

---

[4] Pingamizi liliwekwa na Jamhuri ya Afrika Kusini na Jamhuri ya Kiarabu ya Misri kuhusu Ibara ya 30

## UAMUZI KUHUSU USHIRIKIANO WA PANDE MBALIMBALI

**Mkutano Mkuu**,

### A. Kuhusu Ubia wa AU – EU

1. **UNAKARIBISHA** kufanyika kwa Mkutano wa 7 wa AU - EU na **UNATOA SHUKRANI** kwa Rais wa Jamhuri ya Angola, Mhe. João Manuel Goncalves Lourenco na kwa Serikali na watu wa Angola kwa mpangilio bora wa Mkutano wa 7 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU - EU;

2. **UNAPITISHA** Azimio la Mkutano wa 7 wa Umoja wa Afrika - Umoja wa Ulaya uliofanyika tarehe 24 - 25 Novemba 2025, mjini Luanda, Angola.

### B. Kuhusu Mkutano wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD)

3. **UNAKARIBISHA** kufanyika kwa Mkutano wa 9 wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD) na **UNATOA SHUKRANI** kwa Serikali na Watu wa Japani kwa mpangilio mzuri wa Mkutano wa 9 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa TICAD;

4. UNAPITISHA Azimio la Mkutano wa 9 wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD) uliofanyika tarehe 20 - 22 Agosti 2025, mjiniYokohama, Japani.

# UAMUZI
# KUHUSU "RAMANI YA AFRIKA DUNIANI" (SUALA LILILOPENDEKEZWA NA JAMHURI YA TOGO)
# Doc. EX.CL/1680(XLVIII)

**Mkutano Mkuu**,

1. **UNAREJELEA** uamuzi wa Assembly/AU/Des.903 (XXXVIII) kuhusu utekelezaji wa mwongozo wa kaulimbiu ya Mwaka 2025: "Haki kwa Waafrika na watu wenye asili ya Afrika kupitia fidia",;

2. **UNAREJELEA PIA** uamuzi wake kuhusu andika dhana ya Kaulimbiu ya Mwaka 2025, "Haki kwa Waafrika na watu wenye asili ya Afrika kupitia fidia",

3. **UNAZINGATIA** andiko dhana la mpango wa "Kusahihisha Ramani ya Afrika Duniani" na **UNAIPONGEZA** Togo kwa jitihada zake;

4. **UNATHIBITISHA** kwamba makadirio ya ramani ya Mercator yanapotosha ukubwa halisi wa bara la Afrika, yanaathiri mitazamo, na yanaathiri vibaya tathmini ya lengo la uwezo wa kiuchumi wa Afrika, **UNAZINGATIA** kwamba ardhi iliyo mbali na ikweta inaonekana kupotoshwa haswa, na kusababisha athari ya "kupungua" kwa Afrika na maeneo mengine;

5. **UNAFAHAMU** kwamba upotoshaji huu unachangia kupunguza ukubwa wa hali halisi ya kiuchumi na kijamii ya Afrika, mipango ya miundombinu, ustawi, na uwezo wa ukuaji, na **UNAZINGATIA KWA WASIWASI** na hali ya Upendeleo dhidi ya Kusini mwa Dunia, haswa katika maeneo ya rasilimali za mazingira, mipaka na usalama, miundombinu, jiografia ya siasa na jamii;

6. **UNAKARIBISHA** mpango wa mageuzi wenye asili wa Afrika wa Ajenda 2063, unaolenga kutumia ulinganifu wa faida za bara hilo zinazotokana ba idadi ya watu wake, historia, tamaduni, maliasili, na nafasi yake duniani, kwa lengo la kufikia mageuzi ya kijamii, kiuchumi, na kiteknolojia yanayozingatia usawa na watu, yanayofaa kuondoa umaskini;

7. **UNATAMBUA** kwamba umiliki wa simulizi na chapa ya Afrika ni mojawapo ya malengo ya Ajenda 2063 ambayo yanaakisi kwa usahihi uhalisia, matarajio, na vipaumbele vya bara, pamoja na nafasi yake duniani;

8. **UNATHIBITISHA** kwamba maadili ya Uanamajumui wa Afrika lazima yajumuishwe kikamilifu katika mitaala yote ya shule na kwamba urithi wa kitamaduni wa Afrika (urithi, ngano, lugha, sinema, muziki, michezo ya kuigiza, fasihi, sherehe, dini, na masuala ya kiroho) lazima yaimarishwe na kuthaminiwa;

9. **UNAREJELEA** azimio la Kongamano la 9 la Uanamajumui wa Afrika uliofanyika kuanzia tarehe 8 hadi 12 Desemba mjini Lomé, Togo, ambalo linahimiza Umoja wa Afrika, Nchi Wanachama, na mataifa yanayowahifadhi jamii za watu wenye asili ya Afrika kuwasilisha ombi rasmi kwa Umoja wa Mataifa na mashirika yake yenye uwezo wa kurekebisha uwakilishi usio sawa wa ramani za bara, hasa makadirio ya Mercator, kama kitendo cha haki cha utambuzi na fidia, muhimu katika kurejesha nafasi halisi ya Afrika duniani;

10. **UNASISITIZA** hitaji muhimu la kukuza na kuoanisha ufundishaji wa historia, jiografia, maadili ya Kiafrika, na Uafrika katika shule zote na taasisi za elimu, kama sehemu ya kukuza utambulisho wa Kiafrika na Mvuvumko wa Kiafrika, na kuiwezesha Afrika kuchukua nafasi yake halali katika mifumo ya kimataifa ya kisiasa, usalama, uchumi, na utawala wa kijamii;

11. **UNASISITIZA** kwamba uwakilishi huu wa ramani wenye upendeleo ni urithi wa kikoloni, unaolenga kupunguza umuhimu wa Afrika katika jukwaa la kimataifa;

12. **UNAPITISHA** makadirio sawa ya ramani ya Dunia ili kuwakilisha bara la Afrika kwa usahihi zaidi na kurekebisha uwakilishi wake kimataifa, na **KUZITAKA** Nchi Wanachama kurekebisha mitaala ya kitaifa kulingana na makadirio ya Ramani Sawa ya Dunia;

13. **UNAMTEUA** Kinara wa kutekeleza na kuhamasisha mpango huo na **UNAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kushirikiana na Kinara kuwasilisha ripoti za kila mwaka kuhusu hali ya utekelezaji wa mpango huo

# UAMUZI KUHUSU PROGRAMU KAMILI YA MAENDELEO YA KILIMO AFRIKA (CAADP) KAMA MWONGOZO WA PROGRAMU YA AJENDA YA 2063

**Mkutano Mkuu**,

**1. UKIREJELEA** kupitishwa kwa CAADP mwaka 2003 kupitia Azimio la Maputo kuhusu Kilimo na Usalama wa Chakula barani Afrika [Assembly/AU/Decl.7 (II)], ambalo lilizitaka Nchi Wanachama kutenga angalau asilimia 10 ya bajeti za kitaifa kwa kilimo na kufikia angalau asilimia 6 ya ukuaji wa kilimo kila mwaka, na hivyo kuweka msingi wa mfumo ulioratibiwa, wa bara zima wa mageuzi ya kilimo;

**2. UKITAMBUA** kwamba Azimio la Maputo liliweka kilimo katikati ya ajenda ya maendeleo ya Afrika kama kichocheo cha usalama wa chakula, kupunguza umaskini, ukuaji wa uchumi, upanuzi wa biashara, na maendeleo endelevu ya vijijini;

**3. UKIREJELEA ZAIDI** Azimio la Malabo kuhusu Ukuaji wa Kilimo na Mageuzi ya Haraka kwa Ustawi wa Pamoja na Maisha Bora Assembly/AU/Decl.1 (XXIII), Doc. Assembly/AU/2(XXIII) lililopitishwa mwaka 2014, ambalo lilithibitisha tena dhamira ya Nchi Wanachama kuhusiana na kanuni za CAADP na kuanzisha seti ya malengo yanayoweza kupimika kwa mwaka 2025, ikiwa ni pamoja na kutokomeza njaa, kupunguza umaskini kwa asilimia hamsini kupitia kilimo, kuimarisha uhimilivu, kukuza biashara ya ndani ya Afrika, na kuhakikisha uwajibikaji wa pande zote kupitia utaratibu wa Mapitio ya Miaka Miwili ya CAADP;

**4. UKIREJELEA** kwamba Azimio la Malabo liliwakilisha mageuzi makubwa kutoka kwa ahadi za sera hadi utekelezaji unaozingatia matokeo, kuweka mipango inayotegemea ushahidi kupitia Mipango ya Kitaifa na ya Kikanda ya Uwekezaji wa Kilimo (NAIPs na RAIPs), na kuzindua Mapitio ya Miaka Miwili na Kadi ya Alama ya Mageuzi ya Kilimo Afrika kama njia za kufuatilia maendeleo;

**5. UKIREJELEA PIA** kwamba Wakuu wa Nchi na Serikali mwaka 2025, walipitisha Azimio la CAADP la Kampala Ext./Assembly/Decl./3(XIX) kuhusu Kujenga Mifumo ya Kilimo Endelevu barani Afrika walithibitisha tena jukumu la kimkakati la CAADP kama mpango wa sera wa bara kwa ajili ya mageuzi ya mifumo ya chakula, uboreshaji wa kilimo, na maendeleo vijijini, huku wakilinganisha malengo yake na Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP) wa Ajenda 2063;

**6.UKITAMBUA** kwamba Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa CAADP wa Kampala (2026–2035) uliweka dira mpya ya kutumia mifumo ya kilimo na chakula kama injini za ukuaji endelevu, utengenezaji wa ajira, ujumuishaji wa biashara, uhimilivu dhidi ya tabianchi, na ujumuishaji wa kijamii, kwa malengo yanayoweza kupimika katika uzalishaji, uwekezaji, kupunguza hasara baada ya mavuno, na upanuzi wa biashara;

**7. UKITAMBUA** kwamba kwa zaidi ya miongo miwili, CAADP imebadilika kutoka ahadi ya bajeti na tija (Maputo) hadi mfumo wa matokeo na uwajibikaji (Malabo) na sasa hadi ajenda ya mifumo ya kilimo inayobadilisha (Kampala), na kuwa nguzo kuu ya mpango wa maendeleo wa Umoja wa Afrika.

**8. UKITAMBUA ZAIDI** uwiano imara wa CAADP na matarajio na malengo ya Ajenda 2063, hasa Azma ya 1 kuhusu Afrika yenye ustawi inayotegemea ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu, na jukumu lake la uwezeshaji mtambuka wa mipango mingine mikuu ya bara ikiwa ni pamoja na Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA) na Mkakati wa Bidhaa za Afrika, Mkakati wa Uchumi wa Bluu, na Mkataba wa Vijana wa Afrika;

**9. UKIREJELEA** uamuzi EX/CL/Dec.998 (XXXII) Rev.1 kuhusu upangaji upya na uainishaji upya wa miradi mikuu kwa Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi, ukisisitiza hitaji la kuzingatia programu zenye matokeo makubwa, kichocheo, na zinazomilikiwa kisiasa ili kuharakisha maendeleo kuelekea Ajenda 2063.

10. **UNAZINGATIA** Azimio la CAADP la Kampala (Ext./Assembly/Decl./3(XIX)), Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa CAADP (2026–2035), na Miongozo ya Utekelezaji wa CAADP, ambayo hutoa mfumo jumuishi wa kutafsiri ahadi za bara kuwa vitendo katika ngazi za kitaifa na kikanda kupitia Mipango ya Kitaifa na Kikanda ya Uwekezaji wa Kilimo (NASIPs na RASIPs);

11. **UNATAMBUA** uwiano mkubwa wa CAADP na Nadharia ya Mageuzi ya STYIP, ikijumuisha mshikamano wa sera, ubunifu, ushirikiano wa kimkakati, ushiriki wa raia, na ufadhili wa ndani, pamoja na mchango wake katika Malengo ya STYIP ikijumuisha:

(i) Mafanikio: Kuendesha ukuaji wa uzalishaji wa chakula na uwekezaji;
Iliyounganishwa: Kuimarisha biashara ya ndani ya Afrika na utekelezaji wa AfCFTA;
(ii) Inaendeshwa na watu: Kuwawezesha vijana, wanawake, na makundi yaliyo hatarini;
(iii) Amani: Kushughulikia ukosefu wa usalama wa chakula na ukosefu wa ajira vijijini;
(iv) Kidemokrasia: Kuimarisha uwajibikaji na utawala kupitia mchakato wa Mapitio ya Miaka Miwili.

12. **UNAREJELEA** vigezo vya uteuzi wa mradi mkuu chini ya STYIP, ikiwa ni pamoja na matokeo makubwa, athari ya kichocheo, umiliki wa kisiasa, na mifumo ya uwajibikaji, na **UNAZINGATIA** kwamba CAADP inakidhi na kuzidi vigezo hivi;

13. **UNAIDHINISHA** CAADP kama mpango mkuu wa Ajenda 2063 ili:

(i) Uhamasishwe katika ngazi ya juu zaidi ya kisiasa, ukiwa na hadidu za rejea zilizo wazi na taratibu za kuripoti kwa Mkutano Mkuu wa AU;

(ii) Umejumuishwa katika Mpango wa Utekelezaji Mkuu wa Ajenda 2063 kama afua ya kipaumbele ili kuharakisha mageuzi ya kilimo;

(iii) Unaungwa mkono kwa kutumia rasilimali na mifumo ya uwekezaji, ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Utekelezaji wa CAADP;

(iv) Unafuatiliwa kupitia mpango thabiti wa uwajibikaji, ikiwa ni pamoja na kuripoti kila baada ya miaka miwili na kuunganishwa katika Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa AU kwa ajili ya Ajenda 2063.

## UAMUZI KUHUSU UTEUZI WA WAJUMBE KUMI (10) WA BARAZA LA AMANI NA USALAMA LA UMOJA WA AFRIKA

**Doc. EX.CL/1684(XLVIII)**

**Mkutano Mkuu**,

1. **UNAZINGATIA** uchaguzi wa Wajumbe Kumi (10) wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika uliofanywa na Baraza Kuu;

2. **UNATEUA Nchi Kumi** (10) Wanachama katika Baraza la Amani na Usalama kwa muhula wa miaka miwili (2):

| NA. | NCHI | KANDA |
|---|---|---|
| 1. | D.R. Congo | Kati |
| 2. | Gabon | Kati |
| 3. | Somalia | Mashariki |
| 4. | Uganda | Mashariki |
| 5. | Morocco | Kaskazini |
| 6. | Lesotho | Kusini |
| 7. | Afrika Kusini | Kusini |
| 8. | Benin | Magharibi |
| 9. | Côte d'Ivoire | Magharibi |
| 10. | Sierra Leone | Magharibi |

# UAMUZI KUHUSU UCHAGUZI WA UONGOZI WA MKUTANO MKUU WA UMOJA WA AFRIKA KWA MWAKA 2026

**Mkutano Mkuu**,

**1.** UNACHAGUA Uongozi wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika kwa mwaka 2026, kama ifuatavyo:

(i) Mwenyekiti: Jamhuri ya Burundi

(ii) Makamu wa 1 wa Mwenyekiti: Jamhuri ya Ghana

(iii) Makamu wa 2 wa Mwenyekiti: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(iv) Makamu wa 3 wa Mwenyekiti: Kanda ya Kaskazini

(v) Mwandishi: Jamhuri ya Angola

# UAMUZI KUHUSU TAREHE NA UKUMBI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA 40 CHA MKUTANO MKUU WA UMOJA WA AFRIKA

**Mkutano**,

1. **UNAAMUA** kwamba tarehe za Kikao cha 40 cha Kawaida cha Mkutano Mkuu, kitakachofanyika Addis Ababa, Ethiopia, zitakuwa kama ifuatavyo:

   i Kikao cha Hamsini na Tatu (53) cha Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC), kuanzia tarehe 07 hadi 22 Desemba 2026;
   ii Kikao cha Hamsini (50) cha Baraza Kuu, tarehe 27-28 Januari 2027;
   iii Kikao cha Arobaini (40) cha Mkutano Mkuu, tarehe 30-31 Januari 2027.

2. **UNAIOMBA** Kamisheni kufanya taratibu zote muhimu kwa ajili ya kufanyika kwa mafanikio Kikao cha Arobaini (40) cha Mkutano Mkuu na mikutano ya maandalizi ya Baraza Kuu na PRC kulingana na tarehe zilizotajwa hapo juu

## UAMUZI KUHUSU TAREHE NA UKUMBI WA MKUTANO WA NANE (8) WA URATIBU WA NUSU MWAKA

**Mkutano Mkuu**,

1. **UNAREJELEA** MAAMUZI Assembly/AU/Dec. 635 (XXVIII) na Assembly/AU/Dec.687 (XXX) yaliyopitishwa Januari 2017 na Januari 2018 mtawalia, kuhusu Mkutano wa Uratibu wa Nusu Mwaka;

2. **UNAAMUA** kwamba tarehe za Mkutano wa 8 wa Uratibu wa Nusu Mwaka na Vikao vya Baraza Kuu na PRC vinavyotangulia, zitakuwa kama ifuatavyo:

   i Kikao cha Kawaida cha Hamsini na Mbili (52) cha PRC kuanzia Mei 14 hadi Juni 04, 2026 mjini Addis Ababa, Ethiopia;
   ii Kikao cha Kawaida cha Arobaini na Tisa (49) cha Baraza Kuu kuanzia Juni 24 na 25, 2026, mjini El Alamein, Misri
   iii Mkutano wa Nane (8) wa Uratibu wa Nusu Mwaka wa Umoja wa Afrika na RECs tarehe 27Juni 2026, mjini El Alamein, Misri

3. **UNAOMBA** Kamisheni kuchukua hatua zote muhimu ili kuandaa Mkutano wa Nane (8) wa Uratibu wa Nusu Mwaka pamoja na mikutano ya maandalizi ya Baraza Kuu na PRC kulingana na tarehe zilizotajwa hapo juu.

4. **UNAZINGATIA** mapendekezo yaliyotolewa na Jamhuri za Gabon, Liberia, na Zimbabwe ya kuandaa Mkutano wa 9 wa Uratibu wa Nusu Mwaka kabla ya Mkutano wa Baraza Kuu mwezi Juni/Julai 2027 na **UNAZIHIMIZA** Nchi Tatu Wanachama kufanya mashauriano kwa lengo la kufikia makubaliano kuhusu mipango ya kuandaa.

## UAMUZI KUHUSU KIWANGO CHA TATHMINI NA MICHANGO

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJELEA** uamuzi wa Mkutano Mkuu Assembly/AU/Dec.938(XXXVIII) wa Februari 2025, uliobainisha kuwa mwaka 2026 ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa kiwango cha sasa cha tathmini ya michango ya Nchi Wanachama (2024–2026), na kuielekeza Kamisheni kuanza mchakato wa kuandaa kiwango kipya cha tathmini kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali Februari 2026, kwa kufuata taratibu stahiki.

2. **UNAPOKEA KWA SHUKRANI ZA DHATI** uamuzi wa Jamhuri ya Angola wa kuendelea kubaki katika hadhi ya Kundi la Kwanza, hatua inayothibitisha dhamira endelevu ya Nchi Mwanachama hiyo katika kuhakikisha uendelevu wa kifedha na utendaji bora wa Umoja wa Afrika; **UNATAMBUA** kuwa uamuzi huu utachangia kupunguza mzigo wa kifedha kwa ujumla kwa wanachama wengine wa Umoja.

3. **UNAZINGATIA** uamuzi wa Baraza Kuu kuhusu taarifa ya kikao cha pamoja cha Kamati ya Mawaziri kuhusu Kiwango cha Tathmini na Michango na Kamati ya Mawaziri Kumi na Watano wa Fedha (F15), ulioridhia ombi la Nchi Wanachama kupewa muda wa ziada ili kufanya majadiliano zaidi na wataalamu husika katika nchi zao, pamoja na ombi kwa Kamisheni na Wataalamu wa F15 la kuendelea na mashauriano kuhusu Kiwango cha Tathmini kilichopendekezwa kwa kipindi cha 2027–2029, kwa kuzingatia ombi la Jamhuri ya Angola, na kuwasilisha chaguo moja pekee kwenye Kikao cha Kawaida cha 49 cha Baraza Kuu kitakachofanyika Juni 2026, kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa, kwa kufuata taratibu stahiki.

4. **UNAAMUA** kukabidhi kwa Baraza Kuu mamlaka ya kupitisha kiwango kipya cha tathmini katika Kikao chake cha Kawaida cha 49 kitakachofanyika Juni 2026.

## UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA MKUTANO WA TANO (5) WA KAWAIDA WA KAMATI YA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI WA VITUO VYA KUDHIBITI NA KUZUIA MAGONJWA AFRIKA (Africa CDC)
## Doc. Assembly/AU/9 (XXXIX)

**Mkutano Mkuu,**

1. **UKIREJELEA** Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika, hasa Ibara ya 9(1)(a), ambayo inaupa Mkutano Mkuu mamlaka ya kubaini sera za pamoja za Umoja wa Afrika;

2. **PIA UKIREJELEA** Sheria Iliyorekebishwa ya Africa CDC, ambayo inaanzisha Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali kama chombo cha juu zaidi katika muundo wa Africa CDC kinachotoa usimamizi wa kisiasa na mwongozo wa kimkakati;

3. **UKIREJELEA ZAIDI** Assembly/AU/Dec.924(XXXVIII), ambao *"UNATAMBUA NA KUTHIBITISHA VIKALI jukumu muhimu linalotekelezwa na Africa CDC katika kulinda afya ya umma ya Afrika kwa kutoa mwelekeo na usaidizi wa kimkakati, kwa Nchi Wanachama kutokana na jukumu lake kama shirika la Afya ya Umma la Afrika, kwa mujibu wa Sheria zake, na kwa kufanya kazi kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, AUDA-NEPAD, AMA, AfCFTA na Vyombo vingine vya AU, katika nyanja zote za afya ya umma ikiwa ni pamoja na zile zinazohusiana na ufadhili wa afya wa ndani na kimataifa, utengenezaji wa ndani wa bidhaa za afya, Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja wa Afrika, ushiriki wa jamii, uwekaji kidijitali wa mifumo ya taarifa za afya, na ubunifu mwingine mbalimbali katika afya."*

4. **UNAPITISHA** Ripoti ya Mkutano wa Tano wa Kawaida wa CHSG wa Afrika CDC uliofanyika tarehe 9 Februari 2026, pamoja na mapendekezo yake.

5. **UNATHIBITISHA TENA** ahadi ya bara kwa Ajenda ya Usalama na Utawala wa Afya Afrika (AHSS) na **UNAIDHINISHA** mageuzi kutoka *Agizo Jipya la Afya ya Umma (NPHO)* hadi AHSS kama mfumo unaoongoza wa bara kwa uhuru wa afya wa muda mrefu, uhimilivu, na kujitegemea;

6. **UNAELEZEA WASIWASI** kuhusu utegemezi endelevu wa Afrika kwenye misaada ya maendeleo ya nje kwa ajili ya afya na **UNAUNGA MKONO** matokeo ya utafiti uliofanywa na kutolewa na Africa CDC unaoitwa " *athari za kifedha za AHSS*"[1] unaolenga kushughulikia ukosefu wa ufanisi katika sekta ya afya, kupanua nafasi ya fedha kwa ajili ya afya, kuimarisha ukusanyaji wa rasilimali za ndani, na kuharakisha utengenezaji wa ndani wa bidhaa za afya;

[1] https://africacdc.org/news-item/financing-africashealth-security-and-sovereignty/

7. **UNAIPONGEZA** Africa CDC kwa uongozi imara wa bara, maendeleo ya taasisi, utawala, na usimamizi wa fedha kuanzia mwaka 2023 hadi sasa chini ya uongozi wa Mkurugenzi Mkuu, Dkt. Jean Kaseya, na kusababisha:
   (i) utangazaji wa dira ya wazi ya bara kupitia Ajenda ya AHSS;
   (ii) ongezeko la ruzuku inayosimamiwa ndani kutoka dola milioni 52 mwaka 2022 hadi dola milioni 462 mwaka 2025, na ukusanyaji wa dola takriban bilioni 40 katika usaidizi wa moja kwa moja wa washirika kwa Nchi Wanachama;
   (iii) utekelezaji bora wa bajeti kutoka 34% hadi 95% katika kipindi hicho hicho; na
   (iv) kupungua kwa milipuko ya magonjwa mwaka 2025 ikilinganishwa na miaka mitatu iliyopita, hali inayoonesha uwekezaji endelevu katika ufuatiliaji, mpangilio wa kijenetiki, Taasisi za Kitaifa za Afya ya Umma, Vituo vya Uendeshaji wa Dharura za Afya ya Umma, afya ya kidijitali, utengenezaji wa ndani, na mipango inayohusiana;

8. **PIA UNAIPONGEZA** Africa CDC kwa kujitolea kwake katika uwazi na uwajibikaji kupitia utoaji wa ripoti wa kimfumo kwa Nchi Mwanachama kuhusu rasilimali zilizokusanywa na uwekezaji unaoungwa mkono kupitia utetezi wake na washirika;

9. **UNAIPONGEZA ZAIDI** Africa CDC kwa tamko la kihistoria, usimamizi mzuri, na kuondoa Mpox kama Dharura ya Afya ya Umma ya Usalama wa Bara (PHECS) mnamo Januari 2026;

10. **UNAMPONGEZA Rais John Dramani Mahama** kwa Mpango wa *Accra Reset Initiative*, unaoendana na ajenda ya uhuru ya Afrika, na kwa kutambuliwa kwake miongoni mwa viongozi wa kimataifa wa Devex Power 50;

11. **PIA UNAMPONGEZA Rais João Manuel Gonçalves Lourenço** na Jamhuri ya Angola kwa mchango wao wa hiari wa dola milioni 5 kwa mwaka kwa Africa CDC, ambao ulichochea ahadi kama hizo kutoka kwa Nchi zingine Wanachama kwa ajili ya umiliki na uhuru wa Africa CDC, na **KUIDHINISHA" Mpango wa Rais Lourenço wa mchango wa hiari kwa Africa CDC"** wa kuongeza michango ya Afrika kwa Africa CDC na Mfuko wa Magonjwa ya Mlipuko wa Afrika (AfEF) kama njia ya kutekeleza uhuru wa afya katika ngazi ya bara;

12. **UNAVIOMBA** vyombo husika vya sera vya AU, katika muktadha wa kupungua kwa msaada wa maendeleo wa nje kwa ajili ya afya kwa Nchi Wanachama wa Afrika na kurejelea uamuzi Assembly/AU/Dec.924(XXXVIII), kuzingatia suala la ufadhili endelevu kwa Africa CDC, ikiwa ni pamoja na muundo wake wa wafanyakazi, utakaofadhiliwa na Nchi Wanachama ili kuhakikisha utendaji kazi kamili na utekelezaji mzuri wa mamlaka yake, kulingana na kanuni na michakato iliyowekwa, pamoja na mipango kama hiyo inayotumika kwa vyombo vingine vya AU.;

13. **UNAIAGIZA** Africa CDC kushirikiana na Tume ili kuhakikisha uwakilishi wa Afrika ndani ya Mipango ya Afya Duniani, ikiwa ni pamoja na Gavi, CEPI, Mfuko wa Dunia, na Mfuko wa Janga, na ndani ya mabaraza ya utawala wa afya duniani, ikiwa ni pamoja na G20, G7, Baraza la Afya Duniani, FOCAC na majukwaa mengine muhimu ya pande nyingi; na UNAIAGIZA ZAIDI Africa CDC kuripoti maendeleo kwa vyombo vya sera vya AU;

14. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuhakikisha usaidizi unaotabirika na endelevu kwa Nchi Wanachama kulingana na Ajenda ya AHSS; **na KUZIHIMIZA ZAIDI** Nchi Wanachama kupanua ufadhili wa ndani na wa kiuvumbuzi kwa ajili ya afya kwa mujibu wa mapendekezo ya AHSS.

15. **UNAMPONGEZA Mhe. William Ruto**, Rais wa Jamhuri ya Kenya na Kinara wa AU wa Uzalishaji wa Ndani, kwa kuitisha Mkutano Maalum kuhusu utengenezaji wa ndnai wa bidhaa za afya mnamo Aprili 2026 jijini Nairobi, na **UNAIOMBA** Africa CDC kufanya kazi na AUC-HHS, AUDA-NEPAD, AMA, na AfCFTA ili kusaidia uandaaji mzuri wa Mkutano huu Maalum na kuripoti matokeo kwa Mkutano wa 40 wa kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU. Katika suala hili, **UNAPENDEKEZA** kwamba Mkutano Mkuu Maalum uandaliwe pmoja na Mkutano Mkuu Maalumu wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Afya ili kuhakikisha uthabiti wa mwelekeo wa sera, ujumbe na ushiriki, au Mkutano Mkuu Maalumu wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Viwanda vya Ndani uandaliwe mwaka 2027;

16. **UNAIDHINISHA** kuanzishwa kwa Kamati huru ya Sayansi ya Tiba ya Afrika ya Ngazi ya Juu chini ya usimamizi wa Africa CDC kwa ushirikiano na Shirika la Dawa Afrika (AMA) na Kamisheni ili kutambua ubora bora wa Kiafrika katika dawa na afya ya umma; **UNAIDHINISHA** kuundwa kwa **"Tuzo ya Dawa ya Afrika"**; na **UNAAMUA** kwamba Tuzo hiyo itatolewa kila mwaka, kando ya Mkutano Mkuu wa AU, na itatolewa na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika;

17. **PIA UNAIDHINISHA** kuanzishwa na kuteuliwa kwa Kamati ya Mawaziri ya Ngazi ya Juu ya Afrika kuhusu Mageuzi ya Muundo wa Afya Duniani, na **UNAIOMBA** Africa CDC kutoa ripoti kuhusu maendeleo yaliyopatikana;

18. **UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Afrika Kusini na Africa CDC kwa kuandaa CPHIA 2025 kwa mafanikio jijini Durban na **UNAISHUKURU** Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia kwa kukubali kuandaa CPHIA 2026 mwezi Novemba 2026;

19. **UNAZITAKA** Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika:
a. Kusaini Mkataba wa Kubadilishana Data wa Africa CDC; na
**b.** Kusaini uanachama wa Mpango wa Ununuzi wa Pamoja wa Afrika (APPM);

20. **UNAIDHINISHA** uteuzi wa:
**a. Mhe. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama Kinara wa Umoja wa Afrika wa Afya ya Mama na Mtoto;
**b. Mhe. Abiy Ahmed Ali,** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia, kama Kinara wa Umoja wa Afrika wa Akili Mnemba na Afya ya Kidijitali;

21. **UNAIAGIZA** Africa CDC kutoa ripoti kuhusu maendeleo katika Mkutano wa Nane wa Uratibu wa Nusu Mwaka (Juni 2026), Mikutano ya Kawaida ya 49 na 50 ya Baraza Kuu, na mkutano wa Kawaida wa 40 wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu utekelezaji wa Ajenda ya AHSS, Ajenda ya Lusaka, APPM, AfEF, mageuzi ya kidijitali, na uimarishaji wa uwezo wa PPPR.

**UAMUZI WA RIPOTI KUHUSU MAENDELEO YA MAGEUZI YA KITAASISI YA UMOJA WA AFRIKA NA WILLIAM S. RUTO, PhD, RAIS WA JAMHURI YA KENYA**
**Doc. Assembly/AU/5(XXXIX)**

**Mkutano Mkuu,**

**1. UKIREJEA** maamuzi yake ya awali kuhusu Mageuzi ya Kitaasisi ya Umoja wa Afrika, ikiwa ni pamoja na maamuzi ya Mkutano Mkuu AU/Dec.635 (XXVIII) (2017), AU/Dec.687 (XXX) (2018), AU/Dec.733 (XXXII) (2019) na AU/Dec.798 (XXXIV) (2021), pamoja na uamuzi AU/Dec.605 (XXVII) (2016) kuhusu Ufadhili wa Umoja wa Afrika;

**2. UKIREJEA ZAIDI** maamuzi ya Mkutano Mkuu Assembly/AU/Dec.815(XXXV) na Assembly/AU/Dec.842(XXXVI), yaliyopitishwa mwaka 2022 na 2023, mtawalia, ambayo yalisisitiza haja ya kuimarisha ufanisi wa vyombo, taasisi, na mashirika ya AU;

**3. UKIZINGATIA KWA MASIKITIKO** kuongezeka kwa vitisho na changamoto kubwa na mazingira ya usalama duniani na ya bara yanayobadilika kwa kasi ambayo yamezuia muundo wa sasa wa amani na usalama wa AU;

**4. UKIAZIMIA** kuimarisha mpango wa amani na usalama wa Muungano kupitia ufanisi wa kitaasisi, ufanisi, ufadhili unaotabirika, uhusiano imara zaidi na RECs na RMs;

**5. UKIAZIMIA ZAIDI** kuimarisha uongozi wa AU katika upatanishi, diplomasia ya kuzuia migogoro, shughuli za ulinzi wa amani, onyo la mapema na uingiliaji wa haraka;

**6. UKIREJEA** Ajenda 2063, ambayo inasisitiza kujitegemea kwa Afrika, uhuru wa kifedha, na ufanisi wa kitaasisi;

**7. UKITHIBITISHA TENA** umuhimu wa ufadhili endelevu, utawala bora, na mshikamano wa kitaasisi katika kuhakikisha kwamba Umoja wa Afrika unatekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

**8. UKITAMBUA** haja ya kuimarisha mageuzi ya kitaasisi yanayoendelea, kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa bajeti, kurahisisha ajenda ya Mkutano Mkuu, na kuhalalisha vyombo, taasisi, na mashirika ya AU kwa ajili ya kuboresha utendaji na uwajibikaji;

**UNAAMUA KAMA IFUATAVYO :**

9. **UNAAMUA** kuendesha mchakato wa Mageuzi ya AU kwa ufanisi na kwa wakati unaofaa kwa njia ya suala moja baada ya jingine kuanzia Februari 2026, kwa ushirikiano na PRC na kupitia vyombo husika vya sera chini ya uongozi wa Kinara wa Mageuzi

**Kuhusu Amani na Usalama**

**10. UNAKARIBISHA** kuanzishwa kwa Jopo la Ngazi ya Juu sambamba na Uamuzi Uamuzi wa Mkutano Mkuu Assembly/AU/Dec.920(XXXVIII) uliopitishwa na Mkutano wa Kawaida wa 38 wa wakuu wa Nchi na Serikali wa mwezi Februari 2025**;**

11. **UNAZINGATIA** matokeo na ripoti ya Jopo la Ngazi ya Juu ya Mapitio ya Mifumo ya Utawala, Amani na Usalama ya AU, kama hatua muhimu katika kufufua mipango ya amani na usalama ya pamoja ya Afrika;

12. **UNAMUOMBA** Mwenyekiti wa Kamisheni kuandaa mapendekezo kuhusu kuimarisha utendaji wa kikazi wa muundo wa amani na usalama wa Afrika katika maeneo muhimu ya upatanishi, mazungumzo, diplomasia ya kuzuia migogoro, tahadhari ya mapema na mwitikio, vita dhidi ya ugaidi na operesheni za kusaidia kuleta amani na kuwasilisha mapendekezo halisi, kufuatia mchakato unaostahiki, kwa Mkutano Mkuu mnamo Januari 2027.

13. **UNAMUAGIZA** Mwenyekiti wa AU kusambaza wito kwa Nchi Wanachama, ifikapo Julai 2026 wa kuteua jopo huru la wataalamu watano (5) (jeshi, wasomi, taasisi za kutunga sera, au nyanja za kidiplomasia) kutoka kila ukanda kati ya kanda tano, kwa kusaidiwa na Kikosi Kazi cha Pamoja cha AUC, kuunda rasimu ya mpango wa utekelezaji wa AGA-APSA uliooanishwa ambao unaondoa utengamano na kuimarisha mshikamano wa kitaasisi;

14. **UNAAGIZA ZAIDI** kwamba jopo huru la wataalamu litashauriana na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs), Vyombo vya ulinzi wa haki (RMs), Baraza la Amani na Usalama (PSC), Nchi Wanachama, na wadau wengine husika kadri inavyofaa, na kuwasilisha ripoti yake kwa Mwenyekiti kwa ajili ya kuwasilishwa zaidi, kufuatia mchakato unaostahili, kwa Wakuu wa Nchi na Serikali wakati wa Mkutano wao wa Kawaida wa 40 wa mwezi Februari 2027.

**15.** **UNAIHIMIZA** PSC ya AU kuhakikisha panakuwepo na majadiliano ya mara kwa mara na Kamati ya Wajumbe Kumi (C10) katika ngazi ya Mabalozi, na Nchi tatu Wanachama wa Umoja wa Afrika zinazohudumu katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (A3+) ili kujenga makubaliano juu ya masuala ya amani na usalama na kufikia katika Misimamo ya Pamoja ya Afrika .

16. **UNAZINGATIA** maendeleo yaliyopatikana katika kusasisha Mpango Mkuu wa AU wa Hatua za Vitendo za Kusitisha Mapigano na matokeo ya Kikao kazi kuhusu Tathmini ya Kimkakati ya Nusu Muhula ya Mwongozo Mkuu wa AU (AUMR) wa Hatua za Kivitendo za Kusitisha Mapigano Afrika.

17. **UNATAMBUA** kwamba mpango mkuu wa Kusitisha Mapigano unafikia kikomo mwaka 2030, na **UNASISITIZA** haja ya kupitia na kusasisha Mwongozo Mkuu wa AU kulingana na mafunzo yaliyopatikana kuwa mwongozo rahisi, mahususi kwa muktadha na unaoweza kubadilika; Mwongozo Mkuu wa AU unapaswa kupitiwa mara kwa mara.

18. **UNAZINGATIA ZAIDI** juhudi kubwa za kushughulikia mageuzi ya serikali kinyume cha katiba barani Afrika kupitia vyombo husika vya AU na **UNAMUHIMIZA** Mwenyekiti wa AUC kuendelea kutumia Ofisi zake Nzuri na Mifumo iliyopo katika kufikia nchi zilizowekewa vikwazo na kuziunga mkono katika kuandaa na kutekeleza **miongozo kwa ajili ya mageuzi kuelekea kwenye mfumo wa kikatiba.**

**Kubadili tena Nafasi ya Afrika Katikati ya Mageuzi ya Kijiografia na Kisiasa na Kufufua Umajumui wa Afrika**

19. **UNAMUAGIZA** Mwenyekiti wa AUC kusambaza kwa Nchi Wanachama wito wa uteuzi wa wataalamu watano (5) wakuu wa sera za kigeni, mmoja (1) kutoka kila ukanda, ili kuandaa rasimu ya Mfumo wa Sera za Kigeni wa Afrika unaozingatia maadili ya pamoja ya Afrika, mshikamano, ustawi wa pamoja na usalama wa pamoja, unaozingatiwa kwenye Sheria ya Anzilishi(*Constitutive Act*) ya AU, na unaolenga kuimarisha uwakala wa Afrika katika mahusiano ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na miktadha ya kimataifa ya pande nyingi.

20. **UNAWAAGIZA ZAIDI** wataalamu kuwasilisha ripoti kwa Mwenyekiti wa AUC kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu, kufuatia mchakato unaostahili, kwa ajili ya kujadiliwa katika Mkutano wake wa Kawaida wa 40 mwezi Januari 2027. Wataalamu kushauriana na vyombo vya AU, Nchi Wanachama na wadau wengine kadri inavyofaa.

**Kuziba Pengo la Tahadhari ya Mapema na Hatua za Mapema**

21. **UNAIOMBA** Kamisheni kurasimisha mifumo ya kufuata sheria na uwajibikaji kwa kutumia mazungumzo ya kisiasa ya Ngazi ya Juu na mapitio ya rika ikiwa ni pamoja na mashauriano ya kila mwaka ya Baraza la Amani na Usalama la AU/Vyombo vya Mikoa ili kuhakikisha hatua za mapema zinafuata tahadhari ya mapema.

22. **UNAIOMBA ZAIDI** Kamisheni ya AU, kupitia Idara ya Masuala ya Siasa, Amani na Usalama, kuandaa rasimu ya mwongozo wa Utekelezaji wa Mapema wa AU unaofafanua vichocheo, vizingiti, na kurasimisha mwitikio kwa ratiba na kuiwasilisha kwa PSC ifikapo Julai 2026 kwa ajili ya kujadiliwa.

**Kuhusu Kuimarisha Mashauriano, Maarifa, na Umiliki wa AU kwa Raia wa Afrika na Diaspora**

**23.** **UNAMUOMBA** Mwenyekiti **wa Kamisheni kufufua Mkakati wa Mawasiliano wa Bara la Afrika**, kuwashirikisha watangazaji wa Kiafrika, waandishi wa habari, wataalamu wa mahusiano ya umma, vijana, na wataalamu wa vyombo vya habari vya kidijitali ili **kuongeza uelewa wa raia na diaspora, ushiriki, na umiliki wa AU** , na **kuripoti kwa Baraza Kuu ifikapo Januari 2027.**

**Kuhusu Kutumia Teknolojia za Kisasa kwa ajili ya Mageuzi na Uhimilivu wa Afrika**

24. **UNAZINGATIA** maendeleo ya Kamisheni katika maendeleo ya kimkakati ya sera na mifumo ya udhibiti inayohusiana na Akili mnemba , uwezo wa mtandao, na matumizi ya amani ya anga za juu**.**

25. UNAIOMBA Kamisheni itengeneze mifumo ya tahadhari mapema kulingana na AI na teknolojia za anga za juu ili kuongeza uelewa wa hali, tathmini ya hatari, kinga, na kufanya maamuzi sahihi kwa ajili ya hatua za mapema**.**

**Kuimarisha Diplomasia ya Kuzuia Migogoro na Upatanishi**

26. **UNAIOMBA** Kamisheni kupitia idara yake husika kuanzisha Kikosi kazi kinachohusisha idara tofauti ili kusaidia Jopo la Wenye Busara kwa uwezo wa kutumia na kudumisha mazungumzo ya kisiasa katika mazingira ya mgogoro.

**Kuhusu Ufadhili wa Umoja wa Afrika**

27. **UNAREJEA** uamuzi wa AU/Dec.578(XXV) Juni 2015, ambapo Nchi Wanachama ziliahidi kufadhili 100% ya bajeti ya uendeshaji ya AU, 75% ya bajeti ya programu, na 25% ya bajeti ya shughuli za amani.

28. **PIA UNAREJEA** uamuzi wa AU/Dec. 605 (XXVII) wa Julai 2016, ulioanzisha ushuru wa uagizaji wa 0.2% kwa bidhaa zinazostahiki kutoka nje kama utaratibu endelevu wa ufadhili kwa Umoja wa Afrika.

**29.** **UNATAMBUA** kwamba Nchi Wanachama kwa sasa zinafadhili asilimia ishirini na nne pekee (24%) ya bajeti ya mpango wa Umoja wa Afrika , kwamba malengo yaliyo hapo juu yanabaki kutekelezwa kwa kiasi kidogo tu, na kwamba bajeti ya Operesheni za Kulinda Amani inaendelea kutegemea sana washirika wa nje **.**

**30.** **UNATHIBITISHA** TENA ahadi yake ya kuhakikisha kwamba Umoja wa Afrika unafadhiliwa kwa njia inayoweza kutabirika, endelevu, ya usawa, na inayowajibika, huku umiliki wake kamili ukifanywa na Nchi Wanachama wake **;**

31. **UNAZINGATIA** pendekezo la Jopo la Ngazi ya Juu la kupanua mfuko wa Amani kutoka dola za Kimarekani milioni 400 hadi dola bilioni 1 kwa kubadilisha vyanzo vya ufadhili na kuanzisha utaratibu wa kujaza tena; kuendeleza ushirikiano na Umoja wa Taasisi za Fedha za Afrika; na kutumia mamlaka ya Wakuu wa Nchi kuhamasisha taasisi za fedha, viongozi wa sekta binafsi na wahisani kuchangia Mfuko wa Amani.

32. **UNAMUOMBA** Mwakilishi Mkuu wa Kufadhili Umoja wa Afrika, kwa usaidizi wa Kamisheni, kufanya mashauriano zaidi na Nchi Wanachama ili kuimarisha makubaliano juu ya masuala muhimu ya ufadhili wa kimkakati.

33. **UKIREJEA** uamuzi wa Mkutano Mkuu **Assembly/AU/Dec. 920(XXXVIII)** wa Februari 2025:

    **(a)** **UNAMUOMBA** Mwakilishi Mkuu wa AU wa Kufadhili Umoja wa Afrika kuharakisha mashauriano kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika Ufadhili Umoja wa Afrika kwa ujumla;

    **(b)** **UNALIAGIZA** Baraza Kuu kuitisha Mkutano Maalum, ukiwakutanisha Mawaziri wa Mambo ya Nje na Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama ili kuimarisha Ufadhili wa Umoja wa Afrika na Mfuko wa Amani, kulingana na Uamuzi wa Mkutano Mkuu **Assembly/AU/Dec.687 (XXX) wa Januari 2018,** kabla ya Novemba 2026.

34. **UNAMUOMBA ZAIDI** Mwakilishi wa Ngazi ya Juu wa AU kuhusu Ufadhili Umoja wa Afrika kuwasilisha ripoti kwenye Mkutano Maalum wa Baraza Kuu uliotajwa hapo juu.

35. **UNAAMUA** kutumia rasilimali za kifedha za ndani na usaidizi wa Taasisi za Fedha za Afrika ili kukamilisha michango ya Nchi Wanachama katika kufadhili programu za kipaumbele za Ajenda 2063; na **UNAAGIZA** Baraza Kuu kualika Maafisa Wakuu wa Taasisi za Fedha za Afrika waalikwe kushiriki Mkutano Maalum ili kuzingatia mbinu za ufadhili wa programu za kipaumbele za Ajenda 2063.

**36.** **UNAWAOMBA,** Mwenyekiti wa Kamisheni **na** Mwakilishi Mkuu wa Ufadhili wa AU, kwa kushauriana kwa karibu na Uongozi wa Mkutano Mkuu, PSC na Wajumbe watatu wa Afrika wa Baraza la Ualama la Unn(A3+) **kushiriki** upya na kutetea utekelezaji wa Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa nambari 2719 (2023) kuhusu ufadhili unaotabirika na endelevu kwa ajili ya Operesheni za Ulinzi wa Amani (PSOs) zinazoongozwa na AU **.**

**Kuhusu Kubadilisha Ajenda ya Mkutano Mkuu**

37. **UNAREJEA** uamuzi wa AU/Dec. 582 na Uamuzi wa AU/ 635 (2017), kuhakikisha kwamba kila ajenda ya Mkutano Mkuu inazingatia vipengele vitatu (3) vya kimkakati na vyenye athari kubwa barani **(**Masuala ya Siasa, Amani na Usalama; Ujumuishaji wa Kiuchumi, ikiwa ni pamoja na AfCFTA; na uwakilishi na Sauti ya Afrika duniani ), sambamba na malengo ya mageuzi ya kitaasisi Uamuzi wa AU/920.

38. **KUWEKA** Ajenda kwenye kikomo cha siku moja na nusu ili kuhakikisha ushiriki wa Nchi zote Wanachama katika ngazi ya juu iwezekanavyo, na kuruhusu kufanya maamuzi juu ya vipengele vya kimkakati vya umuhimu wa bara.

39. **UNAAMUA** kupitisha muundo mpya wa Ajenda kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika, kulingana na uamuzi 635 (2017). Umeambatishwa Muundo wa Ajenda iliyorekebishwa kama *Kiambatisho 1* cha uamuzi huu.

**Kuhusu Uainishaji wa Maamuzi ya Mkutano Mkuu**

**40.** **UNAZINGATIA** maendeleo yaliyopatikana katika Utafiti kuhusu Uainishaji wa Maamuzi ya Vyombo vya Sera vya AU;

41. **UNAAGIZA** PRC, kupitia Kamati zake Ndogo za Sheria, Sifa na Viwango, na Mageuzi ya Miundo, ikifanya kazi kwa ushirikiano na vyombo na taasisi zingine husika za AU, kukamilisha kazi hiyo na kuwasilisha mapendekezo kwenye Mkutano wa 39 wa Kawaida wa Baraza Kuu mwezi Juni 2026.

**Kuhusu Uendeshaji wa Mahakama ya Umoja wa Afrika**

42. **UNAREJEA** Protokali ya Mahakama ya Haki ya Umoja wa Afrika, ambayo ilipitishwa na Mkutano mkuu wa 2 wa Kawaida mnamo Julai 2003 huko Maputo, Msumbiji, na ambayo ilianza kutumika tarehe 11 Februari 2009;

43. **UNAREJEA ZAIDI** uamuzi wa **Mkutano Mkuu Assembly/AU/Dec.920(XXXVIII)**, uliopitishwa na Mkutano Mkuu wa 38 wa Kawaida mnamo Februari 2025, ambaco **uliiomba** Kamisheni, Jamhuri ya Watu wa China, na wadau husika kutoa athari za kisheria, kimuundo, na kifedha za uendeshaji wa Mahakama ya Haki, na kuwasilisha ripoti yake kwa Baraza Kuu mnamo Juni 2026;

44. **UNAOMBA** utekelezaji wa haraka wa uamuzi huo na uwasilishaji wa ripoti hiyo kwenye Mkutano wa 39 wa Kawaida wa Baraza Kuu mnamo Juni 2026.

**Kuhusu Bunge la Afrika**

45. **UNAUOMBA** Uongozi wa PAP na Wabunge wote wa PAP, kwa msaada wa AUC, kuongeza uhamasishaji na mashauriano na Nchi Wanachama ili ziidhinishe Protokali ya Malabo.

**Kuhusu Mageuzi ya Muundo wa Vyombo, Mashirika, na Ofisi za AU**

**46.** **UNAZINGATIA** maendeleo yaliyopatikana kwa kuzingatia vyombo thelathini na saba (37) na Kamati Ndogo ya Mageuzi ya Miundo ya PRC chini ya Awamu ya I;

47. **UNAAGIZA** kwamba ripoti ya mapitio ya miundo chini ya Awamu ya Pili iwasilishwe kwa PRC bila kuchelewa, ili kuiwezesha PRC kuwasilisha mapendekezo yake kwa Baraza Kuu katika Kikao chake cha Kawaida mnamo Januari 2027.

**48.** **UNAAGIZA ZAIDI** kwamba athari za kifedha zinazotokana na marekebisho ya vyombo, mashirika na ofisi za AU zijadiliwe na Mkutano Maalum wa Baraza Kuu uliotajwa hapo juu, ulioitishwa ili kuimarisha ufadhili wa Umoja wa Afrika na Mfuko wa Amani.

### Kuhusu Mgawanyo wa Kazi

49. **UNAZINGATIA** maendeleo yaliyopatikana katika kukamilisha mfumo wa Mgawanyo wa Kazi na **UNAIHIMIZA** Kamisheni kukamilisha mashauriano miongoni mwa AU, RECs, RMs, na Nchi Wanachama ili kukamilisha Mfumo huo kwa ajili ya kupitishwa na Mkutano wake Mkuu wa 40 wa Kawaida mwezi Januari 2027.

### Kuhusu Bajeti

50. **UNAAMUA** kuidhinisha bajeti ya dola 950,000 kutoka kwa fedha zilizopo za sekta binafsi ili kuwezesha Kamisheni kutekeleza shughuli zinazohusiana na mageuzi, ikiwa ni pamoja na Mkutano Maalum wa Baraza Kuu unaowakutanisha Mawaziri wa Mambo ya Nje na Mawaziri wa Fedha, mwaka 2026.

**UAMUZI KUHUSU TAARIFA YA RAIS CYRIL RAMAPHOSA KUHUSU MATOKEO YA MKUTANO WA UONGOZI WA G20, WA TAREHE 22–23 NOVEMBA 2025, JOHANNESBURG UTEKELEZAJI WA BARA WA MATOKEO YA G20 Doc. Assembly/AU/6(XXXIX)**

**Mkutano Mkuu**,

1. **UNASISITIZA** uamuzi wake wa awali **Assembly/AU/Dec.873 (XXXVII)** kuhusu mbinu za ushiriki wa Umoja wa Afrika katika G20 na vipaumbele vya awali vya G20 vinavyopaswa kutekelezwa.

2. **UNAIPOKEA KWA SHUKRANI** taarifa iliyowasilishwa na Mhe. Rais Cyril Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini, kwa nafasi yake kama Rais wa G20 mwaka 2025, kuhusu matokeo muhimu ya Urais wa Afrika Kusini wa G20, na msisitizo wake juu ya falsafa ya ubuntu, mshikamano, usawa na uendelevu, huku ukuaji na maendeleo ya Afrika yakitajwa kuwa nguzo kuu ya ajenda ya mwaka G20.

3. **UNAIMPONGEZA** Afrika Kusini kwa kufanikisha Mkutano wa Wakuu wa G20 na **UNAPOKEA** matokeo ya G20 yaliyopatikana Johannesburg ambayo yalichangia kuendeleza maslahi ya Afrika, ikiwa ni pamoja na:

   3.1. Vipaumbele vinne vya juu vya G20, ambavyo ni: kuchukua hatua za kuimarisha uhimilivu na ushughulikiaji wa majanga; kuhakikisha uwezo wa kumudu madeni kwa nchi zenye kipato cha chini; kuhamasisha upatikanaji na ongezeko la fedha linalotabirika na kwa ajili ya kuwa na usawa katika kipindi cha mpito cha masuala ya nishati; na kutumia madini muhimu kwa ajili ya ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu.

   3.2. Vikosikazi vitatu kuhusu: Ukuaji wa Uchumi Jumuishi, Ujenzi wa Viwanda, Ajira, na Kupunguza Ukosefu wa Usawa; Usalama wa Chakula; na Akiliunde, Usimamizi wa Data na Ubunifu kwa Maendeleo Endelevu, pamoja na Matokeo ya Makubwa kama Mkataba na Afrika (Compact with Africa) na Mapitio ya G20@20.

   3.3. Uanzishwaji wa Ripoti ya Jopo la Wataalamu wa G20 Afrika kuhusu Ukuaji, Deni na Maendeleo: Fursa za Ushirikiano Mpya wa Afrika, na wito wa Jopo miongoni mwa mambo mengine, kwa ushirikiano mpya wa kimataifa unaozingatia Afrika ili kuchochea ukuaji endelevu na ustawi wa pamoja katika karne ya 21;

3.4. Uanzishwaji wa Kamati Maalumu ya Wataalamu Huru wa G20 kuhusu Ukosefu wa Usawa Duniani. **PIA UNAPOKEA** mapendekezo ya Kamati kuhusu kuanzishwa kwa Jopo la Kudumu la Kushughulikia Ukosefu wa Usawa.

**4.** **UNATAMBUA** hatua kubwa isiyo kifani ya Afrika Kusini ya kudhamini Mikutano mitatu ya G20 kwenye Bara, ambayo ni: Mkutano wa Kikosikazi cha Pili cha Usalama wa Chakula uliofanyika Kairo, Misri, tarehe 1–3 Septemba 2025; Mkutano wa Ushirikishwaji wa Afrika G20 (*G20 Africa Outreach*) kuhusu Viwanda na Kilimo uliofanyika Abuja, Nigeria, tarehe 3 Novemba 2025; na Tukio la Pembeni la Ngazi za Juu kuhusu Uwezo wa Kumudu Madeni na Gharama ya Mtaji, uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, tarehe 10 Novemba 2025.

**5.** **VILEVILE UNATAMBUA** jitihada za Urais wa G20 wa Afrika Kusini kuimarisha Mkataba wa G20 na Afrika, ikiwamo kupitia uzinduzi wa awamu ya pili (2025–2033) iliyosaidiwa na uanzishwaji wa mfuko wa wafadhili wengi wa Benki ya Dunia, na **UNATAMBUA** wanachama wapya wa Mkataba, Jamhuri ya Zambia na Jamhuri ya Angola.

**UNAAMUA KAMA IFUATAVYO:**

## I. URATIBU WA BARA NA UFUATILIAJI WA G20

**6.** **UNAAMUA** kuanzisha Mfumo wa Uratibu wa Bara wa Muda wa Kufuatilia Matokeo ya G20**,** unaoandaliwa na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, ili kuhakikisha uwiano wa hatua za kibara, kikanda na kitaifa zinazotokana na matokeo ya G20 yanayohusu Afrika.

## II. KUSHUGHULIKIA UKOSEFU WA USAWA NA USIMAMIZI NYENZO ZA MAENDELEO

**7.** **UNAIDHINISHA** ripoti na mapendekezo ya Kamati ya Maalumu ya G20 kuhusu Ukosefu wa Usawa Duniani.

**8.** **UNAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kwa kushirikiana na Nchi Wanachama na washirika, kuandaa Mfumo wa Bara wa Kupunguza Ukosefu wa Usawa unaounganisha juhudi zilizopo, kuimarisha data na ushahidi, na kuunga mkono ujifunzaji wa sera katika nchi mbalimbali.

## III. USHIRIKIANO MPYA WA KIMATAIFA NA AFRIKA

**9.** **UNAIDHINISHA** ripoti na mapendekezo ya Jopo la Wataalamu wa G20 Afrika.

**10.** **UNAPOKEA** wito wa Jopo la Wataalamu wa G20 Afrika kuhusu Ushirikiano Mpya wa Afrika unaoizingatia Afrika, ili kuchochea ukuaji endelevu na ustawi wa pamoja katika karne ya 21. **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kuachana na mifumo ya maendeleo inayotegemea misaada na kuelekea maendeleo yanayoongozwa na uwekezaji wenye tija, yanayoungwa mkono na sera thabiti za ndani, taasisi zenye ufanisi za kiafrika, na utangamano wa kikanda, na **PIA, UNATOA WITO kwa G20 na jumuia ya kimataifa** kuchukua hatua za haraka kupitia uwekezaji, mageuzi, na ushirikiano wa kweli ili kufanya Afrika kuwa nguzo ya dunia yenye uhimilivu, na ustawi.

## IV. KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO ZA KIUCHUMI NA KIFEDHA

**11.** **UNATAMBUA** kuimarika kwa Mfumo wa Fedha wa G20 mwaka 2025 katika kushughulikia changamoto za kiuchumi na kifedha barani Afrika, zikiwamo uendelevu wa deni, gharama kubwa ya mtaji, maendeleo ya miundombinu, uhimilivu wa uchumi mkubwa, ujumuishaji wa kifedha, uhamasishaji wa rasilimali za ndani, fedha endelevu, pamoja na maandalizi ya kukabiliana na majanga ya kiafya kupitia ushirikiano wa karibu na taasisi na wadau wa Afrika.

**12.** **UNAKARIBISHA** kupitishwa kwa *Mfumo wa Ushirikiano wa Afrika wa Mfumo wa Fedha wa G20* kwa kipindi cha **2026–2030,** kama utaratibu wa kudumu wa kuimarisha ushirikiano uliopangwa, kulinganisha msaada wa G20 na vipaumbele vya maendeleo ya Afrika, na kuhakikisha urithi wa kudumu wa Afrika hata baada ya Urais wa Afrika Kusini wa G20 kukamilika.

**13.** **UNAHIMIZA** utekelezaji madhubuti wa *Mfumo wa Ushirikiano wa Afrika* (AEF) kupitia umiliki thabiti wa Waafrika, uongozi na uratibu imara, unaojikita katika **Umoja wa Afrika**, **Ajenda ya mwaka 2063**, na **Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA)**, **UNAAMUA** kushirikiana kwa njia ya kujenga na washirika wa G20, taasisi za kimataifa za kifedha, pamoja na sekta binafsi, kwa lengo la kupunguza gharama ya mtaji barani Afrika, kuimarisha uimara, kuimarisha uwezo wa ukusanyaji wa kodi, na kuendeleza ukuaji jumuishi na endelevu katika bara zima.

**14.** **UNABAINISHA** kuongezeka kwa umuhimu wa mifuko ya pensheni ya Afrika, mifuko ya utajiri wa taifa, pamoja na akiba nyingine za muda mrefu kama nguzo muhimu za ufadhili wa maendeleo; **UNAKUBALI** kuanzisha **Kamati ya Wataalamu Huru wa Kiafrika** ili kuchunguza na kuwasilisha chaguzi, katika Mkutano ujao wa Wakuu wa Nchi na Serikali, kuhusu kuanzishwa kwa **Mfuko wa Utajiri wa Taifa.**

## V. MADINI MUHIMU NA UONGEZAJI THAMANI VIWANDANI

15. **UNASISITIZA** kuwa rasilimali za madini muhimu za Afrika ni mali ya kimkakati kwa ajili ya kuendeleza uanuwai wa kiuchumi, ujenzi wa viwanda, na mageuzi ya kimuundo kwa mujibu wa Ajenda ya mwaka 2063.

16. **UNAPOKEA Mfumo wa G20 wa Madini Muhimu,** ambao ni mwongozo wa hiari, usiowafunga kisheria ili kuhakikisha kuwa rasilimali za madini muhimu zinakuwa kichocheo muhimu cha ustawi na maendeleo endelevu, na **UNAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kwa kushirikiana na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda na Sekretarieti ya AfCFTA, kuandaa Mfumo wa Kibara wa Uongezaji Thamani ya Madini Muhimu unaolenga minyororo ya thamani ya kikanda, uongezaji thamani wa ndani nchi, kukuza ujuzi, viwango vya mazingira, kijamii na usimamizi, na mgawanyo wa manufaa kwa usawa.

17. **UNAAMUA** kuwa Mawaziri wa Madini wa Afrika wataripoti mara kwa mara kwa Baraza la Kuu na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika kuendeleza ajenda ya madini muhimu ya Afrika na mchango wake katika uchumi na mageuzi ya kimuundo.

## VI. USALAMA WA CHAKULA

18. **UNATO WITO** kwa sekta za umma na binafsi kutekeleza motisha maalum zinazohamasisha uendeshaji wa biashara unaoheshimu taratibu na uwajibikaji wa wazalishaji, wafanyabiashara, na wahusika wengine katika minyororo ya usambazaji, na pia kuongeza uwekezaji katika miundombinu, hifadhi za chakula za dharura za kikanda na kitaifa, utafiti na maendeleo, pamoja na elimu na mafunzo, hasa kwa wakulima wadogo na wanafamilia, na hususan vijana na wanawake katika kilimo.

19. **UNAKARIBISHA** Mbinu za Ubuntu za G20 kuhusu Usalama wa Chakula na Lishe, na Mageuzi Makubwa ya Bei ya Chakula**,** zilizojadiliwa kwenye Mkutano wa Mawaziri wa Usalama wa Chakula wa G20, ambazo zinalenga kushughulikia athari mbaya za mageuzi makubwa ya bei ya chakula, hususan kwa kaya zenye kipato cha chini, na zinatambulisha azma yetu ya pamoja ya kuunda mustakabali ambapo kila mtu anaweza kupata chakula cha kutosha, salama, nafuu na chenye viritubisho.

20. **UNAHIMIZA Nchi Wanachama,** zikisaidiwa na AUDA-NEPAD na mashirika mengine ya Umoja wa Afrika, kuongeza kasi ya utekelezaji wa hatua za hifadhi ya jamii na utayari wa kitaasisi, kama minyororo ya usambazaji wa chakula shuleni na uhamishaji maalum wa msaada, ili kuhakikisha utu na lishe bora kwa jamii zilizo hatarini.

## VII. AKILI MNEMBA NA MIUNDOMBINU YA UMMA YA KIDIJITALI

21. **UNAKARIBISHA** uzinduzi wa Mpango wa AI kwa Afrika na Kituo cha Usaidizi wa Sera za Teknolojia (TPAF), chini ya Urais wa Afrika Kusini wa G20, vyote vikilenga kutumia jukwaa la G20 kuendeleza AI barani Afrika, kwa mujibu wa Mkakati wa Kikanda wa Umoja wa Afrika kuhusu AI, na kuchochea mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii, ukuaji wa ujuzi na ubunifu.

22. **AIDHA, UNAKARIBISHA**, tangazo la Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) wakati wa Mkutano wa G20 Johannesburg, kuhusu mpango wa maendeleo wa AI wa Dola bilioni 1 za Marekani ili kupanua miundombinu ya AI na huduma zinazotumia AI barani Afrika, na **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama, Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda kushirikiana na UAE kuhakikisha kuwa mpango huu unasaidia nchi za Afrika kutimiza vipaumbele vya maendeleo ya kitaifa katika nyanja kama elimu, huduma za afya, na kuhimili mageuzi ya tabianchi.

23. **UNAAMUA** kuanzisha Mkutano wa Kila Mwaka wa AI kwa Afrika, kufuatia Mkutano wa Kwanza wa AI kwa Afrika uliofanyika Cape Town chini ya Urais wa Afrika Kusini wa G20 tarehe 30 Septemba na 1 Oktoba 2025, ili kuwakutanisha pamoja viongozi kutoka G20 na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, benki za maendeleo, taasisi za kitaaluma, mashirika ya kimataifa, asasi za kiraia, na sekta binafsi, ili kujadili na kuboresha mustakabali wa kidijitali wa Afrika.

24. **UNAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kwa kushauriana na Nchi Wanachama na washirika, kuandaa Mpango wa Utekelezaji ya Afrika kuhusu Akiliunde na Miundombinu ya Umma ya Kidijitali, inayoshughulikia masuala ya ujuzi, usimamizi wa data, miundombinu ya kompyuta, na matumizi ya kipaumbele kwa maslahi ya umma, pamoja na udhibiti madhubuti.

## VIII. UTEKELEZAJI, USHIRIKIANO NA UTOAJI TAARIFA

25. **UNAAMUA** kuendelea kushughulikia kwa karibu utekelezaji wa vipaumbele vya Umoja wa Afrika ndani ya G20.

# UAMUZI KUHUSU RASIMU YA MKATABA WA MAELEWANO WA UMOJA WA AFRIKA NA JUMUIYA ZA KIUCHUMI ZA KANDA NA MPANGO WA KANDA KUHUSU MATUMIZI YA KIKOSI MAALUM CHA UMOJA WA AFRIKA – Doc Assembly/AU/4(XXXIX)

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNATHIBITISHA TENA** jukumu la Kikosi cha Kudumu cha Afrika kama chombo muhimu cha kukuza amani, usalama, na utulivu barani Afrika, sambamba na Sheria ya Umoja wa Afrika, Protokali Inayohusiana na Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika;

2. **UNAZINGATIA** uamuzi EX.CL/Dec.1220(XLIII) wa Julai 2023 kuhusu ripoti ya Mkutano wa Kawaida wa 15 wa Kamati Maalum ya Kiufundi ya Ulinzi, Utulivu na Usalama (STCDSS) wa Mei 2023, ambao ulipendekeza Mkutano Mkuu Rasimu ya Mkataba wa Makubaliano kati ya Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na Mifumo ya Kikanda juu ya Matumizi ya Kikosi cha Kudumu cha Afrika;

3. **UNAREJEA** uamuzi Assembly/AU/Dec.869(XXXVII) wa Februari 2024, ambalo uliamua kuahirisha kuzingatia Rasimu ya Mkataba wa Maelewano kati ya Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na Mifumo ya Kikanda juu ya Matumizi ya Kikosi cha Kudumu cha Afrika hadi Mkutano Mkuu wa Kawaida ujao mnamo Februari 2025;

4. **UNAREJEA ZAIDI** uamuzi Assembly/AU/Dec.918(XXXVIII) wa Februari 2025, kuhusu haja ya kukamilisha Rasimu ya Mkataba wa Maelewano kati ya Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na Mifumo ya Kikanda kuhusu Matumizi ya Kikosi cha Kudumu cha Afrika itakayowasilishwa kwaenye Mkutano Mkuu wa Kawaida wa 39 wa Kawaida wa mwezi Februari 2026;

5. **UNAKARIBISHA** uamuzi wa EX.CL/Dec.1324(XLVIII) wa Februari 2026 kuhusu ripoti ya Mkutano wa 17 wa Kawaida wa STCDSS wa Desemba 2025, ambao uliidhinisha Ripoti kuhusu Mapitio ya Kimkakati ya Kikosi cha Kudumu cha Afrika na kupendekeza kupitishwa na Mkutano Mkuu kwa Rasimu ya Mkataba wa Maelewano kati ya Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda na Mipango ya Kikanda za Matumizi ya Kikosi cha Kudumu cha Afrika;

6. **UNAPITISHA** Mkataba wa Maelewano kati ya AU na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda na Mipango ya Kikanda juu ya Matumizi ya Kikosi cha Kudumu cha Afrika;

7. **UNAIAGIZA** Kamisheni kuharakisha utiaji saini na utekelezaji wa Mkataba wa Makubaliano kati ya AU na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs) na Mipango ya Kikanda (RMs) kuhusu Matumizi ya Kikosi cha Kudumu cha Afrika na **UNAIAGIZA**

Kamisheni kutoa taarifa mara kwa mara kuhusu hali ya utekelezaji wake kwa STCD.

## UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA KINARA WA AJENDA 2063 Doc.Assembly/AU/16(XXXIX)

**Mkutano**,

1. **UNAREJELEA** maamuzi yake ya awali ya kupitisha Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP) wa Ajenda 2063 (2024–2033) na kutangaza kipindi cha 2024–2033 kama Muongo wa Kuongeza Kasi.

2. **UNAREJELEA** majukumu ya Kinara wa Ajenda 2063 ya kukuza uongozi wa kisiasa, umiliki wa ndani, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini, na utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya Ajenda 2063.

3. **UNAZINGATIA** Ripoti ya Tano (5) ya Bara ya Kinara wa Ajenda 2063 (2024–2025), ikiongozwa na matokeo ya awali ya Ripoti ya Kwanza ya Utendaji wa Miaka Miwili ya Bara kuhusu utekelezaji wa STYIP na **UNATAMBUA** maendeleo yaliyopatikana katika kuimarisha mifumo ya kitaasisi, uratibu, ufuatiliaji, utoaji taarifa, na kidijitali kwa ajili ya utekelezaji wa Ajenda 2063;

4. **UNASIKITISHWA** kwamba licha ya maendeleo yanayoweza kupimika, kasi na kiwango cha mageuzi bado hakitoshi kufikia malengo ya Ajenda 2063 ifikapo mwaka 2033, hasa katika mageuzi ya kimuundo, maendeleo ya rasilimali watu, ajira zenye tija, amani na usalama, utafutaji wa rasilimali za ndani, na uhimilivu wa tabianchi;

5. **UNAMPONGEZA** Mhe. Alassane Ouattara, Rais wa Jamhuri ya Côte d'Ivoire na Kinara wa Ajenda 2063, kwa uongozi wake na utetezi endelevu katika kuendeleza Ajenda 2063 kote barani na duniani kote;

6. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuimarisha umiliki wa kitaifa, umiliki wa ndani, na utekelezaji wa Ajenda 2063 kwa kuunganisha kikamilifu Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi katika mipango ya maendeleo ya kitaifa na ya ngazi ya chini ya kitaifa, mifumo ya matumizi ya muda wa kati, na mikakati ya sekta;

7. **UNAAMUA** kwamba Ripoti ya Utendaji ya Miaka Miwili kwenye Ajenda 2063 itawekwa kama chombo kikuu cha uwajibikaji wa bara, ufuatiliaji, na ujifunzaji wa pamoja kwa ajili ya kufuatilia maendeleo chini ya Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi;

8. **UNAZIAGIZA** Nchi Wanachama, RECs, na Vyombo vya Umoja wa Afrika kuimarisha uwezo wa utekelezaji, ikiwa ni pamoja na mifumo ya uratibu, mifumo ya

utoaji, mifumo ikolojia ya data, na mifumo ya ufuatiliaji, tathmini, na utoaji wa taarifa kulingana na matokeo;

9. **UNATOA WITO** wa kuharakishwa kwa utekelezaji wa hati endelevu na mbalimbali za ufadhili kwa Ajenda 2063, ikiwa ni pamoja na utekelezaji mzuri wa Mkakati wa Utafutaji wa Rasilimali za Ndani kwa ajili ya Ajenda 2063; na utekelezaji wa haraka wa Mfuko wa Maendeleo wa Ajenda 2063 na **UNAZITAKA** Nchi Wanachama kuongeza juhudi za kupunguza utegemezi wa ufadhili wa nje, kupambana na mtiririko wa fedha haramu, kupanua misingi ya mapato ya ndani, na kuhamasisha mtaji binafsi, rasilimali za diaspora, na hati bunifu za ufadhili zinazoendana na vipaumbele vya maendeleo vya Afrika;

10. **UNASISITIZA** hitaji la kuharakisha utekelezaji wa Matarajio na Miradi ya Kimkakati na Miongozo ya Ajenda 2063, hasa AfCFTA, mageuzi ya kidijitali, nishati, usafiri, na uhuru wa watu kutembea, kupitia uongozi imara wa kisiasa, maandalizi ya miradi inayoweza kufadhiliwa, na ushiriki ulioimarishwa wa sekta binafsi.

11. **UNATOA WITO** kwa vyombo vya Umoja wa Afrika RECs, washirika wa maendeleo, na wadau wasio wa kiserikali kuoanisha msaada chini ya mkakati wa "Mfumo Mmoja, Ajenda Mbili", kuhakikisha uongozi wa Afrika, mshikamano wa kisera, kupunguzwa kwa mgawanyiko, na ushirikiano unaozingatia matokeo.

# UAMUZI KUHUSU JUKWAA LA AFRIKA KUHUSU UTAMADUNI WA AMANI NA KUTOKUWEPO VUGURU BARANI AFRIKA “BIENNALE LUANDA”
# Doc.EX.CL/1672(XLVIII)

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZINGATIA** uamuzi EX.CL/Dec.17(XLVIII) wa Mkutano wa 48 waKawaida wa Baraza Kuu wa Februari 2026.

2. **UNAAMUA** kuhusu kufanyika kwa Awamu ya 4 la Jukwaa la Afrika la Utamaduni wa Amani na Kutokuwa na Vurugu, “Luanda Biennale”, lenye kaulimbiu "Kuimarisha Usimamizi wa Maji Barani Afrika kama Chombo cha Kuzuia, Kusuluhisha na Kutatua Migogoro, katika awamu mbili (02) yaani kuanzia Machi hadi Juni, katika eneo litakaloamuliwa kati ya Addis Ababa, Luanda au Paris, na tarehe 22–23 Oktoba 2026, mjini Luanda, Jamhuri ya Angola.

3. **UNAIHIMIZA** Serikali ya Jamhuri ya Angola, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni na UNESCO kuandaa Awamu ya 4 la Jukwaa la Afrika kuhusu Utamaduni wa Amani na Kutokuwa na Vurugu barani Afrika, "Luanda Biennale" na kusambaza shughuli na programu zinazohusiana na mada hiyo katika mwaka mzima wa 2026.

4. **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda, ndani ya mpango wa utekelezaji wa Programu ya Kaulimbiu ya Mwaka 2026, kujumuisha shughuli zinazohusiana na kaulimbiu ya Awamu ya 4 ya Jukwaa la Afrika kuhusu Utamaduni wa Amani na Kutokuwa na Vurugu barani Afrika, "Luanda Biennale".

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA MPANGO WA KUJITATHMINI AFRIKA (APRM)

**Mkutano Mkuu**,

1. **UNAZINGATIA** Ripoti ya Mkutano wa 35 wa Jukwaa la Mpango wa Kujitathmini Afrika la Wakuu wa Nchi na Serikali za Nchi Wanachama wa Mpango wa Kujitathmini Afrika (APRM) uliofanyika tarehe 13 Februari 2025;
2. **UNASISITIZA** kwamba APRM bado ni chombo cha utawala bora cha Kiafrika kilichokuzwa ndani ya Afrika, kilichoanzishwa mwaka 2003 na kukubaliwa kwa hiari na Nchi Wanachama arobaini na tano (45) zinazowakilisha zaidi ya theluthi mbili ya Nchi Wanachama wa AU;
3. **UNAMPONGEZA** Mhe. Jenerali Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda, kwa kuchaguliwa kwake kama Mwenyekiti mpya wa Jukwaa la Kujitathmini Afrika (APR) la Wakuu wa Nchi na Serikali, na **UNAMPONGEZA** Mhe. Abdelmadjid TEBBOUNE, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria na Mwenyekiti anayemaliza muda wake wa Jukwaa la Wakuu wa Nchi na Serikali la Kujitathmini Afrika (APR), kwa uongozi wake na kujitolea kwake kwa Mpango huo, ikiwa ni pamoja na mchango wa hiari uliotolewa kwa mpango huo kwa ajili ya kukamilisha kwa mafanikio Ripoti ya Mapitio ya Nchi ya Kizazi cha Pili ya Jamhuri ya Sierra Leone, Ripoti za Mapitio Lengwa za Zimbabwe na São Tomé na Príncipe, msaada wa Tahadhari ya Mapema na Tathmini za Udhaifu wa Kimuundo wa Nchi na Uhimilivu. **UNAZINGATIA ZAIDI** kuhusu mafanikio chini ya uongozi wake, ikiwa ni pamoja na kuitishwa kwa Kongamano la 5 la Vijana la APRM na Jukwaa la 3 la Ngazi ya Juu la Afrika kuhusu Ushirikiano wa Kusini-Kusini na Pembetatu kwa Maendeleo Endelevu;

4. **UNAPOKEA KWA SHUKRANI** Ripoti ya kwanza ya Mwaka ya Sekretarieti ya Bara ya APRM chini ya uongozi wa Afisa Mkuu Mtendaji ("Mkurugenzi Mtendaji") wa Sekretarieti ya Bara ya APRM, Balozi Marie-Antoinette Rose-Quatre
5. **UNAMPONGEZA** Mwenyekiti wa Kamisheni, Mhe. Mahmoud Ali Youssouf na Afisa Mkuu Mtendaji wa Sekretarieti ya Bara ya APRM, Balozi Marie-Antoinette Rose-Quatre, kwa uongozi wao wa ushirikiano na mafanikio makubwa yaliyopatikana hadi sasa katika kuhakikisha kwamba APRM inatekeleza mamlaka yake kwa ufanisi.
6. **UNAREJELEA** uamuzi Ext/Assembly/AU/Dec. 1-4(XI), ambapo Mkutano Mkuu ulisisitiza tena hitaji la kuimarisha uwezo wa APRM kutekeleza mamlaka yake yaliyopanuliwa na kuongeza uhuru wake wa kiutendaji.
7. **UNASISITIZA** hitaji la APRM kupewa rasilimali watu wa kutosha na mgao wa bajeti ili kutekeleza mamlaka yake kwa ufanisi.
8. **UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Shirikisho ya Somalia kwa kujiunga na Mpango huo kama mwanachama wa 45 wa APRM; **UNATOA SHUKRANI** kwa Mhe. Hassan Sheikh Mohamud, Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Samaria, kwa uamuzi wake wa

ujasiri wa kujiunga na APRM, Mpango mkuu wa utawala bora wa Afrika uliokuzwa ndani ya bara.

9. **UNAZIHIMIZA** Nchi zote Wanachama wa AU ambazo bado hazijajiunga na APRM kujiunga na Mpango huo.
10. **UNAPOKEA KWA SHUKRANI** Ripoti ya Mapitio Lengwa ya Jamhuri ya Ghana kuhusu Utawala wa Mashirika kama Kichocheo cha Utekelezaji wa AfCFTA katika Jamhuri ya Ghana, Ripoti ya Mapitio Lengwa ya Jamhuri ya Zimbabwe kuhusu Utawala na Usimamizi wa Uchumi, na Ripoti ya Mapitio Lengwa ya Jamhuri ya São Tomé na Príncipe kuhusu Utalii kama Kichocheo cha Maendeleo ya Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni huko São Tomé na Príncipe;.
11. **UNAWASHUKURU** Mhe. John Dramani Mahama, Rais wa Jamhuri ya Ghana, Mhe. Emmerson Mnangagwa, Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe, na Mhe. Américo d'Oliveira dos Ramos, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya São Tomé na Príncipe, kwa kujitolea kwao kwa ajili ya utawala bora pamoja na vipengele vyake vyote vitano, ikiwa ni pamoja na maendeleo endelevu na mapana ya kijamii na kiuchumi.
12. **UNAIHIMIZA** Jamhuri ya Ghana, Jamhuri ya Zimbabwe na Jamhuri ya São Tomé na Príncipe kuzingatia maoni yaliyotolewa na Nchi Shiriki kwenye Ripoti zao Lengwa za Mapitio, pamoja na mapendekezo yaliyomo katika ripoti za uundaji na utekelezaji wa Programu za Kitaifa za Utekelezaji kama hatua muhimu kuelekea kufikia maendeleo endelevu na mapana ya kijamii na kiuchumi
13. **UNALIPONGEZA** Jopo la APR la Watu Mashuhuri lililoongoza Mapitio Lengwa
14. **UNALIPONGEZA** Jopo la APR la Watu Mashuhuri lililoongoza Mapitio ya Nchi ya Sierra Leone, na Mapitio Lengwa ya Togo, Ghana, Zimbabwe na São Tomé and Príncipe, kwa uhimilivu na kujitolea kwao kwa ajili ya mchakato wa mapitio ya APRM na kuhakikisha uadilifu wake, uhuru, taaluma na uaminifu;
15. **UNAZIHIMIZA** Nchi wanachama wa APRM ambazo bado hazijafanya mapitio kuchukua hatua zinazohitajika ili kuhakikisha kwamba mapitio ya nchi yanafanywa na kwamba ripoti zinawasilishwa kwenye Jukwaa la APR kwa kufanyiwa mapitio na wenzao;
16. **UNAZITAKA ZAIDI** Nchi wanachama wa APRM ambazo zimefanyiwa mapitio kutekeleza Programu zao za Kitaifa za Utendaji na mapitio ya mapendekezo ili kutoa taarifa kuhusu mageuzi ya kitaasisi katika ngazi ya kitaifa na kuepuka changamoto zilizobainishwa katika ripoti zao za mapitio.
17. **UNAPOKEA KWA SHUKRANI** Ripoti ya Maendeleo ya Jamhuri ya Msumbiji kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo katika Ripoti yake ya Pili ya Mapitio ya Nchi; **UNAMPONGEZA** Mhe. Daniel Francisco Chapo, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, kwa uongozi wake bora na juhudi thabiti za kuboresha utawala katika nchi yake na barani;
18. **UNAPOKEA KWA SHUKRANI** Ripoti ya Maendeleo ya Jamhuri ya Djibouti kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo katika Ripoti yake ya kwanza ya Mapitio ya Nchi; **UNAMPONGEZA** Mhe. Ismail Omar Guelleh, Rais wa Jamhuri ya Djibouti, kwa uongozi wake bora na juhudi thabiti za kuboresha utawala katika nchi yake na barani;

19. **UNAREJELEA ZAIDI** uamuzi wake wa awali Assembly/AU/Dec. 631(XXVIII), ambapo Mkutano Mkuu ulikaribisha ahadi za kuifufua APRM, ikiwa ni pamoja na, miongoni mwa mambo mengine, kushirikisha muundo wa mfano wa APRM, uzoefu, na maarifa na maeneo mengine ya dunia kwa madhumuni ya kulinganisha na kuimarisha utambuzi wa kimataifa wa Mpango huu.
20. **UNATAMBUA KWA SHUKRANI** juhudi za APRM za kujenga uwezo wa kitaifa wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika katika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Ajenda 2063 na Ajenda 2030, ikiwa ni pamoja na kupitia mchakato wa Kuripoti kwa Hiari wa Kitaifa (VNR), Jumuiya ya Kitaifa ya Mipango ya Maendeleo, na shughuli za kujifunza kwa wengine zilizofanywa wakati wa Jukwaa la Kisiasa la Ngazi ya Juu la Umoja wa Mataifa.
21. **UNAIPONGEZA** Sekretarieti ya Bara ya APRM kwa ushirikiano wake na Umoja wa Mataifa na taasisi zake, ikiongozwa na Mpango wa AU-UN, katika kuunga mkono utekelezaji wa Ajenda ya 2030 na Ajenda ya 2063; na **UNATAMBUA** kwamba ushirikiano na UNECA, CEPA, AfDB, UNESCO, UNDP, na wadau wengine ni muhimu kwa utekelezaji wa programu muhimu za bara zinazotekelezwa na APRM.
22. **UNASISITIZA** umuhimu wa Ushirikiano wa Kusini-Kusini na Pembetatu katika kukuza utawala bora na mabadiliko ya kiuchumi barani; **UNAPITISHA** Hitimisho la Jukwaa la 3 la Ngazi ya Juu la Afrika kuhusu Ushirikiano wa Kusini-Kusini na Pembetatu kwa Maendeleo Endelevu lililoandaliwa na Serikali ya Sierra Leone mjini Freetown, mnamo Mei 2025.
23. **UNAREJELEA** uamuzi wake wa awali Assembly/AU/Dec.686(XXX) ambapo Mkutano Mkuu ulikaribisha hatua zilizochukuliwa ili kuiweka APRM kama chombo cha tahadhari ya mapema kwa ajili ya kuzuia migogoro barani, kwa maelewano na ushirikiano na Mpango wa Amani na Usalama wa Afrika, na Mpango wa Utawala wa Afrika.

24. **UNAPOKEA KWA SHUKRANI** hitimisho lililotolewa la Mkutano wa 4 wa Pamoja kati ya Baraza la Amani na Usalama la AU na Mpango wa Kujitathmini Afrika uliofanyika tarehe 7–8 Aprili 2025 mjini Johannesburg, Afrika Kusini, **UNAPOKEA** Hitimisho la Mkutano wa 4 wa Pamoja na kuzielekeza taasisi hizo mbili kuhakikisha utekelezaji wa mapendekezo yake.
25. **UNAIHIMIZA** Sekretarieti ya Bara ya APRM, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Nchi Wanachama, kuendelea kuandaa Mkutano wa Pamoja kati ya Jopo la Watu Mashuhuri la APR na Jopo la Watu Wenye Busara la AU, pamoja na Mkutano wa Pamoja kati ya APRM na Baraza la Amani na Usalama la AU;
26. **UNAPITISHA** Hitimisho la Mkutano wa 5 wa Vijana wa APRM uliofanyika tarehe 10–11 Desemba 2025, katika makao makuu ya Bunge la Afrika Kusini mjini Johannesburg, Jamhuri ya Afrika Kusini, chini ya kaulimbiu "Vijana katika Utawala: Kutoka Ahadi hadi Ustawi"
27. **UNAREJELEA** uamuzi Assembly/AU/Dec.720(XXXII) ambapo Mkutano Mkuu uliamua kwamba Ripoti ya Utawala wa Afrika itaandaliwa na APRM, kwa

ushirikiano na Mpango wa Utawala wa Afrika (AGA), na itawasilishwa kila baada ya miaka miwili (2) kwa ajili ya kujadiliwa na Mkutano Mkuu katika Vikao vyake vya Kawaida.

28. **UNAIPONGEZA** Sekretarieti ya Bara ya APRM na wanachama wa Jukwaa la AGA kwa uzinduzi uliofanikiwa wa Ripoti ya Utawala wa Afrika 2025, ambayo inazingatia Utawala wa Maliasili, uliofanyika Julai 2025 mjini Accra, Ghana, pembezoni mwa Mkutano wa Uratibu wa Nusu Mwaka.
29. **UNAREJELEA** umuhimu wa kutafuta rasilimali za kutosha za kifedha kwa ajili ya usambazaji wa Ripoti ya Utawala wa Afrika 2025 (AGR-2025) na utekelezaji wa mapendekezo yake; **UNAWATAKA** wanachama wote wa Jukwaa la AGA kujumuisha Ripoti hiyo katika mipango yao ya kazi ya kila mwaka; na **UNAZITAKA** Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika kuandaa ripoti za utawala wa kitaifa kama chombo cha kujitathmini ili kukuza utawala bora na usimamizi bora na wenye ufanisi wa maliasili, sambamba na mapendekezo ya AGR-2025
30. **UNAREJELEA** Uamuzi wa Mkutano Mkuu wa 38 wa Kawaida wa AU, ambao uliielekeza APRM, kwa kushirikiana na AGA, kuandaa kaulimbiu na mwelekeo wa Ripoti ya Sita ya Utawala wa Afrika na kuwasilisha Ripoti hiyo kwenye Mkutano Mkuu wa 40 wa Kawaida, uliopangwa kufanyika Januari 2027.
31. **UNAWAHIMIZA** washirika wote kuendelea kuunga mkono mpango wa Ripoti ya Utawala wa Afrika, ikiwa ni pamoja na uundaji wa AGR-2027.
32. **UNAPITISHA** kaulimbiu iliyopendekezwa kwa ajili ya Ripoti ya Utawala wa Afrika 2027, kama ilivyopendekezwa na mkutano wa 35 wa Jukwaa la APR na Kongamano la Vijana la APRM, yaani: "Vijana katika Utawala: Kutoka Ahadi hadi Ustawi".
33. **UNAREJELEA** Uamuzi wa Mkutano Mkuu wa 38 wa Kawaida uliofanyika Februari 2025, ambao uliielekeza Sekretarieti kuanza mchakato wa kuajiri na kuchagua wajumbe wapya wa Jopo la APR la Watu Mashuhuri ifikapo Februari 2026, kufuatia kumalizika kwa muda wa wajumbe wa sasa.
34. **UNAIDHINISHA** pendekezo la wagombea wafuatao kama wajumbe wapya wa Jopo la APR la Watu Mashuhuri:
    - i. **Profesa Gilbert Maoundonodj** kutoka Chad, anayewakilisha kanda ya Kati;
    - ii. **Profesa Désiré Manirakiza** kutoka Burundi, anayewakilisha kanda ya Kati;
    - iii. **Dkt. Moeketsi Majoro** kutoka Lesotho, anayewakilisha kanda ya Kusini;
    - iv. **Balozi Sibusiso Ndebele** kutoka Afrika Kusini, anayewakilisha kanda ya Kusini;
    - v. **Dkt. Thelma Awori** kutoka Liberia, anayewakilisha kanda ya Magharibi;
    - vi. **Dkt. Oluwakemi Adeola Obauelu** kutoka Nigeria, anayewakilisha kanda ya Magharibi
    - vii. **Balozi Agnes Kalibala Kadama** kutoka Uganda, anayewakilisha kanda ya Mashariki;
    - viii. **Profesa Olive Mugenda** kutoka Kenya, anayewakilisha kanda ya Mashariki;

ix. **Profesa Ben Abdallah Youcef** kutoka Algeria, anayewakilisha kanda ya Kaskazini; na

x. **Balozi Soha Samir Nashid Gendi** kutoka Misri, anayewakilisha kanda ya Kaskazini.

35. **UNAIDHINISHA** muundo wa Uongozi wa Jopo la Watu Mashuri la APR kwa mwaka 2026, huku **Prof. Olive Mugenda** (anayewakilisha kanda ya Mashariki) akiwa Mwenyekiti na **Prof. Désiré Manirakiza** (anayewakilisha kanda ya Kati) akiwa Makamu Mwenyekiti na Mwenyekiti Mtarajiwa kwa mwaka 2027.

36. **UNATOA SHUKRANI ZA DHATI** kwa Wajumbe wa Jopo la APR waliostaafu, **Balozi Aly El-Hefny, Balozi Ali Ahmed Araita, Dkt. Abdoulie Janneh, Balozi Cherif Rahmani, Mheshimiwa Lydia Wanyoto-Mutende na Bw. Mathew Gowaseb**, kwa utumishi wao wa mfano wakati wa uongozi wao katika Jopo la Watu Mashuhuri la APR.

37. **UNATOA SHUKRANI** kwa Jukwaa la APR na vyombo vyote vya APRM na AU kwa kufanya kazi bila kuchoka kuhakikisha kwamba APRM inatekeleza mamlaka yake.

38. **UNAPOKEA KWA SHUKRANI** ahadi ya Jamhuri ya Uganda ya kuchangia jumla ya **dola 1,000,000** (Dola milioni moja) ili kusaidia shughuli za APRM

39. **UNAMPONGEZA** Mwenyekiti Anayemaliza muda wake wa Jukwaa la APR, Mhe. Abdelmadjid Tebboune, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, kwa uongozi bora kwa APRM na mafanikio ya kipekee ya Mpango huu chini ya uongozi wake.

**UAMUZI KUHUSU RIPOTI ILIYOWASILISHWA NA MHE. ABDEL FATTAH EL-SISI, RAIS WA JAMHURI YA KIARABU YA MISRI NA MWENYEKITI WA KAMATI ELEKEZAJI YA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI WA AUDA-NEPAD (HSGOC)**

**Mkutano mkuu :**

1. **UNAZINGATIA NA KUTHAMINI** ripoti ya Mhe. Abdel Fattah El-Sisi , Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na Mwenyekiti wa Kamati elekezi ya Wakuu wa Nchi na Serikali (HSGOC) ya Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika – Mpango mpya wa Maendeleo ya Afrika (AUDA- NEPAD).

2. **UNAIDHINISHA** mahitimisho na mapendekezo ya Mkutano wa 43 wa Kamati elekezi ya Wakuu wa Nchi na Serikali ya AUDA-NEPAD, uliofanyika tarehe 10 Februari 2026, sambamba na sheria na taratibu za AU.

3. **UNAREJEA** mahitimisho na mapendekezo ya Mikutano ya kamati elekezi ya Wakuu wa nchi na Serikali 40 , 41 , na 42 , iliyofanyika mtawalia mnamo Februari 2023, 2024, na 2025; na **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa maendeleo ya kuvutia yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne iliyopita.

4. **UNASHUKURU** uwasilishaji wa Mkurugenzi Mtendaji wa AUDA-NEPAD kuhusu safari ya mabadiliko ya Shirika hilo katika kipindi cha miaka minne iliyopita, kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Athari na Tafakari ya Miaka 4 ya AUDA-NEPAD, ikiangazia mafanikio ya kiprogramu na athari kubwa tangu 2022.

5. **UNATHIBITISHA TENA** jukumu kuu la AUDA-NEPAD na umuhimu wake wa kudumu kama Wakala mkuu wa maendeleo wa bara la Afrika.

6. **UNATHIBITISHA** kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya AUDA-NEPAD, Kamati elekezi ya Wakuu wa Nchi na Serikali (HSGOC), Kamati ya Uongozi, na Sekretarieti ndizo miundo pekee ya utawala ya AUDA-NEPAD.

7. **UNAREJEA** uamuzi wa Mkutano mkuu Assembly/AU/Dec.813-838(XXXV) ukiitaka AUDA-NEPAD kuharakisha uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo; **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa maendeleo katika kukamilisha Utafiti wa Upembuzi yakinifu kupitia mashauriano ya kina na Kamati ya Uongozi, Kamati ya AU, Vyombo husika vya AU, Nchi Wanachama, na F15; **UNAKARIBISHA** ushirikiano na Benki za Maendeleo za Kimataifa na Taasisi za Fedha za Maendeleo, ikiwa ni pamoja na AAMFI; na **UNAIOMBA** Kamisheni kukamilisha haraka mapitio ya kiufundi na kuidhinisha rasmi Utafiti wa Upembuzi yakinifu ili kuwasilishwa kwenye Mkutano wa Uratibu wa Katikati ya Mwaka wa AU mnamo Juni 2026, na kuwezesha utekelezaji wa Mfuko kwa wakati.

8. **UNAREJEA** maamuzi ya Mkutano mkuu Assembly/AU/December 6-32 (II),

Assembly/AU/December 268-288 (XIV), na Ext/AU/December 1-4 (XI) kuhusu michango ya hiari ya Nchi Wanachama; **UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama ambazo tayari zinachangia; na **UNAREJEA** hitaji la haraka la Nchi Wanachama kutoa michango ya hiari inayohitajika kwa utekelezaji bora wa AUDA-NEPAD wa mamlaka yake.

**9.** **UNAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.691 (XXXI) wa Julai 2018 kuhusu uanzishwaji wa AUDA-NEPAD na Uamuzi EX.CL/Dec.1057(XXXV) aya ya 35, ambao uliidhinisha muundo wa Shirika unaopaswa kupitiwa baada ya miaka mitatu hadi minne ya utekelezaji; **UNATAMBUA** mandhari inayobadilika ya bara na umuhimu wa kudumisha taasisi inayofaa kutekeleza Ajenda 2063; na kwa hivyo **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD kuanzisha mapitio rasmi ya muundo wake wa shirika ili kuongeza ufanisi wa uendeshaji na uwezo wa kiufundi, na kusababisha muundo ulioboreshwa kuwasilishwa kwa miundo husika ya AU kwa ajili ya kuzingatiwa kabla ya kuwasilishwa kwenye Mkutano wa 44 Kamati elekezi ya Wakuu wa nchi na Serikali ya mwaka 2027.

**10.** **UNAREJEA** maamuzi ya Mkutano Mkuu Assembly/AU/December 852 (XXXVI), Assembly/AU/December 9 (XXXVII ), na Assembly/AU/December 922 (XXXVIII) kuhusu upanuzi wa uwepo wa kitaifa na kikanda wa AUDA-NEPAD; **UNAPOKEA nia** ya Nchi 14 Wanachama kutaka kuandaa ofisi za AUDA-NEPAD kwa gharama zao; na **UNAITAKA** AUDA-NEPAD kupanua uwepo wake kupitia Mpango wake kabambe unaoendeshwa na mahitaji kulingana na maombi ya nchi wanachama na bila mzigo wa ziada wa kifedha.

**11.** **UNASHUKURU kwa** Ripoti Mh. Abdel Fattah El-Sisi , Rais wa Jamhuri ya Misri na ya Mwenyekiti wa Kamati elekezi ya Wakuu wa nchi na serikali wa AUDA-NEPAD, iliyowasilishwa na iliyopitishwa katika Mkutano wa 7 wa Katikati ya Mwaka wa Uratibu (Malabo, Guinea ya Ikweta; 13 Julai 2025) kuhusu Jukumu la AUDA-NEPAD katika Kuimarisha Ujumuishaji wa Kikanda, kwa Ushirikiano na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na **UNAIDHINISHA** mapendekezo yaliyomo humo.

**12.** **UNATAMBUA** jukumu muhimu la sekta binafsi katika kukuza ukuaji wa uchumi na uvumbuzi kote Afrika na kuharakisha utekelezaji wa Ajenda ya 2063; **UNAAMUA** kufanya Jukwaa la Biashara kila baada ya miaka miwili, nchini Misri, kuanzia mwaka 2026, ili kushirikisha sekta binafsi ya Afrika na kuongeza ushirikiano katika kuunga mkono Ajenda ya 2063; na **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD kuwezesha upangaji wa Jukwaa kwa ushirikiano na wadau husika, ikiwa ni pamoja na benki za maendeleo za pande nyingi za Afrika na taasisi za fedha.

**13.** **UNAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/DEC.922 (XXXVIII) kuhusu Kampeni ya Uhamasishaji wa Rasilimali za Timu ya Afrika , **UNAKARIBISHA** kuidhinishwa

kwa Hati yake ya Programu na Mkutano wa 7 wa Uratibu wa Katikati ya Mwaka (Malabo, Guinea ya Ikweta; Julai 2025) na **UNAWAHIMIZA** washirika wa maendeleo, Benki za Maendeleo za Kimataifa, na sekta binafsi kuunga mkono kikamilifu kampeni hiyo.

14. **UNAREJEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1280(XLVI) kuhusu uundaji wa jukwaa la kidijitali; **UNAZIELEKEZA** AUC na AUDA-NEPAD kutekeleza jukwaa moja la kidijitali la AU la Ajenda 2063 na kuripoti maendeleo katika Mkutano wa Uratibu wa Katikati ya Mwaka wa AU mnamo Juni 2026.

15. **UNAMPONGEZA** Rais Cyril Ramaphosa na Jamhuri ya Afrika Kusini kwa kuitisha Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa PICI mnamo tarehe 30 Januari 2026, na **UNATHIBITISHA tena** kujitolea kwake kwa maendeleo ya miundombinu kama kichocheo kikuu cha AfCFTA na Ajenda ya 2063, huku akitambua changamoto zinazoendelea za uwezo wa kifedha wa miradi na mapungufu ya ufadhili wa uendeshaji wa Sekretarieti ya PICI. **UNATOA WITO KWA** Nchi Wanachama kuunga mkono juhudi zote za kuhamasisha uwekezaji ulioongezeka wa kimataifa kwa ajili ya miundombinu ya Afrika, **UNAOMBA** Timu ya Kazi ya Kiufundi ya PICI kupanga upya michakato yake mara moja—kubadilisha kutoka usimamizi hadi uwezeshaji wa kimkakati—na kuanzisha mfumo imara wa kuongeza usaidizi wa kiufundi kwa Nchi Wanachama kwa ajili ya kuharakisha utoaji wa miradi ya kipaumbele; na **UNAOMBA ZAIDI** Sekretarieti ya PICI na Mwenyekiti wa Mawaziri wa PICI kuitisha mkutano wa majadiliano ya ufadhili wa kimkakati na washirika walengwa, ikiwa ni pamoja na taasisi za maendeleo ya ufadhili wa kikanda, benki, na washirika wa maendeleo.

16. **UNAMPONGEZA** Abdelmadjid Tebboune, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, kwa kuandaa Maonyesho ya Biashara ya Ndani ya Afrika (IATF 2025) mnamo Septemba 2025, na **UNATAMBUA** jukumu kuu la Algeria katika ujumuishaji wa bara, lililoonyeshwa kupitia utekelezaji wa miradi mikubwa inayounganisha nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika - ikiwa ni pamoja na Barabara Kuu ya Trans-Saharan (TSH), Mgongo wa Fiber ya Optiki ya Trans-Saharan (DTSO), na miradi ya mipango ya reli ya trans-Saharan - kwa mujibu kamili wa matarajio ya Ajenda ya 2063.

17. **UNAIAGIZA** AUDA-NEPAD, kwa kushirikiana na AUC, RECs, na wadau husika, kuharakisha ushirikiano na Nchi Wanachama ili kukamilisha **PAIDA ya bara inayoweza kutekelezwa** ( Programu ya Maendeleo ya Viwanda ya Kuharakisha Afrika); **UNAAGIZA** uwasilishaji wake kwa STC inayofuata ili kuzingatiwa, kwa lengo la uwasilishaji wake kwa Kikao kijacho cha Kawaida cha Bunge la Muungano kwa ajili ya kupitishwa rasmi; **UNAAGIZA ZAIDI** AUDA-NEPAD, UNIDO, na ARSO kuunda Mpango Mkuu wa Uwekezaji katika Miundombinu Bora, uliokamilika na mfumo wa bara wa ufadhili na ujenzi wa uwezo; **UNAAGIZA**

AUDA-NEPAD na AUC kuhakikisha kwamba PAIDA inaimarisha uwezo wa Nchi Wanachama wa kubuni na kufuatilia sera za viwanda zinazoendana kikamilifu na Eneo la Biashara Huria la Bara la Afrika (AfCFTA); na **UNASISITIZA** hitaji la zana zilizoboreshwa za upangaji wa viwanda, uwezo wa kuwezesha uwekezaji, na uratibu wa wizara mbalimbali ili kuboresha Soko Moja la Afrika.

**18.** **UNAMPONGEZA** João Manuel Gonçalves Lourenço, Rais wa Jamhuri ya Angola, kwa kufanikiwa kuandaa Mkutano wa Ufadhili wa Luanda (LFS) mnamo Oktoba 2025; **UNARIDHISHWA na** matokeo yake; **UNAIDHINISHA** Azimio la Luanda kuhusu Ufadhili wa Maendeleo ya Miundombinu ya Afrika na kwingineko ya miradi inayoweza kufadhiliwa iliyowasilishwa katika Mkutano huo, na **UNAZITAKIA** AUDA-NEPAD, AUC, RECs na washirika kuharakisha ufuatiliaji wa njia zilizokubaliwa za utekelezaji na uhamasishaji wa uwekezaji unaotokana na LFS.

**19.** **UNAKARIBISHA** ahadi ya Muungano wa Taasisi za Fedha za Afrika (AAMFI) ya kusaidia miradi 11 ya PIDA PAP2 inayowakilisha dola bilioni 18 za Marekani; na **UNATAKA** kuongeza mifumo ya ufadhili inayoongozwa na Afrika, ikiwa ni pamoja na vyombo vya kupunguza hatari, vifaa vya maandalizi ya miradi, na miundo mchanganyiko ya fedha.

**20.** **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa uzinduzi wa Programu ya Maji, Usafi wa Mazingira, na Usafi (WASH) na **UNAZIPONGEZA** nchi za Mpango wa Awamu ya 1 wa Programu ya Awamu Nyingi (MPA) —Angola, Burundi, Comoro, DRC, Ethiopia, Madagaska, Malawi, Msumbiji, Somalia, Sudan Kusini, Tanzania, na Zambia — kwa uongozi wao wa ngazi ya juu, **UNAZITAKA** NCHI Wanachama kuendeleza na kutekeleza Mikataba ya Kitaifa ya WASH kama vyombo vinavyomilikiwa kitaifa kwa uwajibikaji na vipaumbele, na ili kuunga mkono hili, **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD, kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, AfDB, UNICEF, na WHO, kutoa msaada wa kiufundi katika kuendeleza Mikataba hii, **UNAWAHIMIZA** washirika wa kimataifa kuongeza usaidizi wa kiufundi na kifedha ili kushughulikia upungufu wa fedha uliopo na **UNATAKA** kuoanisha WASH MPA na Mikataba ya Kitaifa ili kuhakikisha kwamba hatua zinazochukuliwa zinabaki kuwa nafuu, endelevu, na zinazostahimili changamoto zinazohusiana na hali ya hewa kote barani.

**21.** **UNAKARIBISHA Mkakati wa** Ukusanyaji wa Rasilimali kwa Programu ya Viwanda vya Uchimbaji Barani (CEIP); **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD kuiwasilisha kwa STC kuhusu Biashara, Viwanda na Madini kwa ajili ya mapitio; na **UNAAlika** STC, kufuatia mapitio yake, kuzingatia kuichagua CEIP kama mradi mkuu chini ya STYIP.

**22.** **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD na AUC kwa kukamilisha na kuzindua Mpango wa Utekelezaji wa STISA-2034; **UNAZITAKIA** Nchi Wanachama, RECs, vyombo

na washirika wa AU kuhamasisha rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wake mzuri; **UNAZITAKIA** Nchi Wanachama kuingiza STISA-2034 katika mikakati ya kitaifa na kuoanisha mipango ya STI ipasavyo; na **UNASISITIZA TENA** jukumu la uratibu la AUDA-NEPAD na AUC (ESTI), **UNAWAELEKEZA** kufuatilia utekelezaji na kuripoti maendeleo katika Mkutano ujao wa AU.

**23.** **UNAKARIBISHA** mpango wa Maono na Mpango wa African EdTech 2030, unaoendana na Mkakati wa Elimu ya Kidijitali wa AU, CESA 2026–2035 na STISA-2034; **UNATOA WITO KWA** NCHI WANACHAMA kupitisha na kubinafsisha Mpango huo, ikiwa ni pamoja na kupitia uwekezaji katika miundombinu ya umma ya kidijitali kwa ajili ya elimu na uwezo wa kidijitali wa walimu; na **UNAAGIZA** AUDA-NEPAD, kwa kushirikiana na AUC na RECs, kusaidia utekelezaji kupitia usaidizi wa kiufundi na uhamasishaji wa rasilimali na kuripoti maendeleo katika Mkutano ujao wa AU.

**24.** **UNATAMBUA** Jopo la Ngazi ya Juu la AU kuhusu Teknolojia Zinazoibuka (APET) kama utaratibu muhimu wa ushauri wa Umoja wa Afrika kuhusu teknolojia zinazoibuka; **UNAPONGEZA** utambuzi wake wa teknolojia za kipaumbele, ikiwa ni pamoja na akili bandia, jenomu na nanoteknolojia; **UNAAGIZA** AUDA-NEPAD na AUC, kama Sekretarieti ya Pamoja ya APET, kusaidia Nchi Wanachama na REC kupitia mifumo ya udhibiti na mwongozo wa kiufundi wa kupitishwa; na **UNAAGIZA** APET kutambua seti inayofuata ya teknolojia zinazoibuka muhimu kwa maendeleo ya Afrika.

**25.** **UNAZISIHI Nchi Wanachama** kutoa ufadhili ili kuendeleza ukusanyaji na uchambuzi wa data kwa ajili ya maendeleo ya sera zinazotegemea ushahidi na Ufuatiliaji na Tathmini kupitia maeneo maalum ya kitaifa kwa ajili ya utoaji wa ripoti za kitaifa, kikanda, na bara kwa wakati unaofaa.

**26.** **UNAREJEA** Uamuzi wa Mkutano mkuu Assembly/AU/Dec.866(XXXVII) kuhusu kuanzishwa kwa Wakala wa Dawa za Kiafrika (AMA ); **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa miaka kumi na saba ya uongozi mzuri katika uratibu wa udhibiti wa bidhaa za matibabu na mchango katika uanzishwaji wa AMA, **UNAAMUA kwamba** Programu ya Uratibu wa Udhibiti wa Dawa za Kiafrika (AMRH) ya AUDA-NEPAD na Ufuatiliaji wa Usalama Mahiri wa Umoja wa Afrika (AU-3S) zihamishiwe kwa AMA.

**27.** **UNAREJEA** utekelezaji wa majaribio wa SIFA uliofanikiwa na **UNATAMBUA** hitaji la kupanua usaidizi kwa Nchi Wanachama zaidi; **UNATAMBUA** umuhimu wa kimkakati wa SIFA 2.0 unaoendana na Ajenda ya 2063, CESA, na CTVET; **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa kutengeneza SIFA 2.0; **UNAAMUA** kuharakisha utekelezaji wa SIFA 2.0 kama mpango mkuu wa bara ; na **UNAHIMIZA** AUDA-NEPAD kuhamasisha Nchi Wanachama zaidi katika SIFA 2.0.

28. **UNAZINGATIA** matokeo ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Dunia kuhusu Maendeleo ya Jamii na Mkutano Mkuu wa Kijamii wa G20; **UNAREJEA** maamuzi muhimu ya AU kuhusu maendeleo ya kijamii, ulinzi wa kijamii, na utawala jumuishi; **UNATAMBUA** jukumu la kimkakati la mpango wa Kuimarisha Taasisi za Kitaifa Zinazofanya Kazi na Jamii Zilizo Katika Mazingira Hatarishi (SNVC) katika kusaidia Nchi Wanachama na **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD, kwa kushirikiana na AUC na RECs, ili: ( i ) kuendeleza Mfumo Kamili wa Ulinzi wa Jamii wa Afrika (CASPF) kama mfumo wa marejeleo wa bara; (ii) kuunga mkono utekelezaji na upanuzi wa SNVC katika Nchi Wanachama kwa kuendana na WSSD, G20, Ajenda 2063, na mifumo husika ya AU; (iii) kuhamasisha ushirikiano na rasilimali kutoka kwa washirika wa maendeleo; na (iv) kuripoti mara kwa mara kwa vyombo vya sera vya AU kuhusu maendeleo.

29. **UNAPONGEZA** maendeleo yaliyopatikana katika kutekeleza Mpango wa Kipengele cha Demografia ya Afrika na Afya ya Ngono na Uzazi (A2DSRH); **UNAITAKA** AUDA-NEPAD kupanua mpango huo hadi Nchi Wanachama na REC za ziada; na **UNAZITAKA ZAIDI** Nchi Wanachama, kwa kushirikiana na AUDA-NEPAD na AUC, kuharakisha utekelezaji wa Mpango wa Utekelezaji wa Maputo (2016–2030), Mpango wa AU wa 2017 wa Kutumia Kipengele cha Demografia ya Idadi ya Watu kupitia Uwekezaji kwa Vijana, na kutimiza ahadi za Afrika kwa Mpango wa Utekelezaji wa Mkutano wa Kimataifa wa Idadi ya Watu na Maendeleo (ICPD).

30. **UNASISITIZA** uwezeshaji wa vijana kama msingi wa Ajenda ya 2063; na **UNAKARIBISHA** pendekezo la Mhe. Evariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi, Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, na Kinara wa Umoja wa Afrika wa Vijana, Amani na Usalama (YPS), la kuandaa, pamoja na AUDA-NEPAD, chini ya Ajenda ya YPS na Mfumo wa Energize Africa, Mazungumzo ya Bara na Mkutano wa Vijana kuhusu Kutumia Mgawanyiko wa Idadi ya Watu wa Afrika kupitia Uwekezaji kwa Vijana, utakaofanyika baadaye mwaka huu huko Bujumbura, Jamhuri ya Burundi.

31. **UNAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.922(XXXVIII), ambao uliipongeza AUDA-NEPAD kwa kutengeneza mwongozo wa Akili Bandia ya Bara na Mwongozo; **UNAPOKEA** rasimu ya Miongozo ya Bara ya Akili Bandia Inayowajibika na Yenye Malengo ya Maendeleo iliyoandaliwa na AUDA-NEPAD, **UNAPONGEZA** sera ya Akili Bandia na mafunzo ya kujenga uwezo wa udhibiti yaliyofanywa na kupangwa ili kusaidia maendeleo ya rasilimali watu, na **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD, kwa kushirikiana na washirika husika, kuendelea na mafunzo kama hayo, kukamilisha Miongozo, na kuripoti maendeleo.

32. **UNAKARIBISHA** maendeleo yaliyopatikana kuelekea utekelezaji wa Kituo cha Ubora cha AUDA-NEPAD kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Uhimilivu na

Marekebisho huko Cairo, kinachoandaliwa na Serikali ya Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, na kinachokusudiwa kutumika kama jukwaa la kubadilishana maarifa, masomo ya kuona mbele, na jamii za utendaji; na **UNATARAJIA** uzinduzi wake rasmi na utekelezaji kamili mnamo 2026.

**33.** **UNAREJEA** Azimio la CAADP Kampala lililopitishwa na Mkutano Mkuu Maalumu mnamo Januari 2025 na Ripoti ya Mawaziri ya Kikao cha Sita cha Kawaida cha STC-ARDWE (Addis Ababa, 21-24 Oktoba 2025), na **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD, kwa ushirikiano na washirika, kuzisaidia Nchi Wanachama na REC katika kufanya tathmini ya haraka ya Mipango ya Kitaifa ya Uwekezaji wa Kilimo (NAIPs) iliyopo na Mipango ya Uwekezaji wa Kilimo cha Kikanda (RAIPs) kama msingi wa kutengeneza mipya inayoendana na CAADP Kampala.

**34.** **UNATAMBUA** jukumu la AUDA-NEPAD katika kuimarisha uwezo wa udhibiti na kitaasisi kupitia programu yake ya usalama wa viumbe , na **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD kusaidia zaidi taasisi za kitaifa na kikanda kutumia teknolojia ya kibiolojia na teknolojia zinazoibuka, ikiwa ni pamoja na uhariri wa jenomu, sambamba na mifumo bora ya utawala wa usalama wa viumbe.

**35.** **UNATAMBUA** fursa ya uhariri wa jenomu na **UNAZISIHI** Nchi Wanachama kuweka kipaumbele uwekezaji unaowajibika katika ubunifu wa bioteknolojia ili kuendeleza matokeo ya maendeleo endelevu.

**36.** **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD, kwa ushirikiano na AUC na Nchi Wanachama, kuratibu maendeleo ya misimamo ya pamoja ya Kiafrika kwa ajili ya Mkataba wa Tofauti za Kibiolojia COP-17 na Mikutano inayohusiana ya Nchi Husika kwa Protokali zake, itakayofanyika Oktoba 2026.

**37.** **UNAZINGATIA KWA WASIWASI** kuhusu mgawanyiko wa sera na uwekezaji katika usalama wa chakula, biashara, miundombinu, na hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, jambo ambalo linazuia uzalishaji na uhimilivu, na **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD, kwa ushirikiano na AUC, RECs, na washirika, kusaidia Nchi Wanachama katika kuendeleza uwekezaji endelevu wa kilimo kupitia mbinu ya ukanda wa bara.

**38.** **UNAREJEA** maamuzi ya Mkutano mkuu yanayoiamuru AUDA-NEPAD kuongoza maendeleo ya Kiwango cha Dhahabu cha Afrika kuhusu Mikopo ya Kaboni na kukuza mbinu bora katika masoko ya kaboni; **UNAKARIBISHA** Kanuni za Kiafrika kuhusu Uadilifu na Usawa katika Masoko ya Kaboni katika kuongoza ushiriki wa Afrika katika masoko ya kaboni.

**39.** **UNAIOMBA ZAIDI** AUDA-NEPAD, kwa kushirikiana na washirika, kuanzisha utaratibu wa uratibu na kutoa usaidizi wa kujenga uwezo kwa Nchi Wanachama kuhusu masoko ya kaboni.

40. **UNAIPONGEZA** Ethiopia kwa kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa COP32 mnamo Novemba 2027 katika ardhi ya Afrika; **UNATAMBUA** umuhimu wa kimkakati wa COP32 kwa vipaumbele vya hali ya hewa vya Afrika; **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD kutoa usaidizi wa kiufundi na kifedha, kupitia programu zake za Hali ya Hewa na programu zingine, pamoja na kuhamasisha ufadhili wa ziada kutoka vyanzo vingine kwa ajili ya kuandaa COP 32, ikiwa ni pamoja na nchi zingine za Afrika. taasisi, washirika wa maendeleo, na Nchi Wanachama katika mzunguko mzima wa COP32.

41. **UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Afrika Kusini kwa matokeo muhimu yaliyopatikana wakati wa Urais wake wa kihistoria wa G20; **UNATAMBUA** michango muhimu ya AUDA-NEPAD katika mchakato wa G20 mwaka 2025, **UNAITAKA** AUDA-NEPAD kuendelea kuhusika kwake kikamilifu, na **UNAOMBA** ushiriki wake rasmi katika mikutano yote ya G20 itakayofanyika mwaka 2026, ikiwa ni pamoja na Mkutano wa Viongozi.

42. **UNAMPONGEZA** Mhe. Abdel Fattah El-Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, kwa uongozi wake bora kama Mwenyekiti wa AUDA-NEPAD HSGOC katika kipindi chake cha miaka mitatu kuanzia Februari 2023 hadi Februari 2026, **UNAPONGEZA** mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya mwongozo wake na **UNATOA** shukrani za dhati kwa maono yake ya kimkakati, ambayo yameathiri sana mwelekeo na ufanisi wa Shirika hilo na kwa kujitolea kwake kusikoyumba kwa maendeleo endelevu ya bara letu.

43. Sambamba na Kanuni za Taratibu za miundo ya Utawala ya AUDA-NEPAD iliyopitishwa na uamuzi EX.cl/Dec.1063(XXXV), na baada ya mashauriano yanayofaa na Viongozi wa HSGOC, **UNAIDHINISHA** kuchaguliwa kwa Mhe João Manuel Gonçalves Lourenço, Rais wa Jamhuri ya Angola, kama Mwenyekiti mpya wa AUDA-NEPAD HSGOC, pamoja na Makamu Wenyeviti wanne (4) kwa muhula mmoja wa miaka miwili (2). Nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa nne na Mwandishi itashikiliwa na Mwenyekiti anayeondoka wa AUDA-NEPAD HSGOC, na Makamu Wenyeviti wengine watatu (3) watateuliwa baada ya mashauriano ya kikanda.

44. **UNAMPONGEZA** Mhe**.** João Manuel Gonçalves Lourenço, Rais wa Jamhuri ya Angola, kwa kuchaguliwa kwake kama Mwenyekiti mpya wa AUDA-NEPAD HSGOC na **UNATARAJIA** uongozi na mwongozo wake wa muundo wa utawala wa juu na wenye nguvu zaidi wa Shirika hilo.

45. **KWA KUTAMBUA** uongozi wenye maono na uwezo mkubwa wa Mkurugenzi Mtendaji wa AUDA-NEPAD Bi. Nardos Bekele-Thomas katika kipindi cha miaka minne iliyopita, pamoja na ubora wa hali ya juu wa matokeo ya kiufundi ya AUDA-NEPAD na matokeo ya ajabu ya maendeleo yaliyopatikana wakati wa muhula

wake wa kwanza, **UNAIDHINISHA** kuongezwa kwa muhula wake kama Afisa Mkuu Mtendaji wa AUDA-NEPAD kwa miaka mingine minne (4), **UNAMPONGEZA** na **UNAMTAKIA** mafanikio yake endelevu katika kuongoza safari ya mabadiliko ya shirika hilo.

**46.** **UNAREJEA** Ibara 7 cha Sheria ya AUDA-NEPAD kuhusu uanachama wa AUDA-NEPAD HSGOC na mashauriano ya kikanda yanayofuata **unaidhinisha** muundo mpya wa HSGOC kwa kipindi cha Februari 2026 hadi Februari 2028 kama ifuatavyo:

| **Kanda ya Kati** | **Kanda ya Mashariki** | **Kanda ya Kaskazini** | **Kanda ya Kusini** | **Kanda ya Maghari bi** |
|---|---|---|---|---|
| 1. Cameroon. | 6. Comoro . | 11. **Algeria*** | 16. Angola. | 21. Cote d'Ivoire. |
| 2. DRC. | 7. Ethiopia . | 12. **Misri*** | 17. Afrika **Kusini *** | 22. **Nigeria*.** |
| 3. Afrika ya Kati . | 8. Kenya. | 13. | 18. Zimbabwe. | 23. **Senegal*.** |
| 4. Guinea ya Ikweta . | 9. Somalia . | 14. | 19. | 24. Togo. |
| 5. Gabon. | 10. Uganda. | 15. | 20. | 25 **.** |

*** isiyo ya mzunguko Kwa Nchi waanzilishi**

| **WAKUU WA NCHI NA SERIKALI WA NANE (8) WENYEVITI WA JUMUIYA ZA KIUCHUMI ZA KANDA – 2026** | | |
|---|---|---|
| 26. | **ECOWAS** | Sierra Leone. |
| 27. | **ECCAS** | Ikweta Gine |
| 28. | **IGAD** | Jibuti |
| 29. | **UMA** | Libya |
| 30. | **COMESA** | Kenya. |
| 31. | **SADC** | Afrika Kusini. |
| 32 | **Jumuiya ya Afrika Mashariki** | Kenya |
| 33. | **CENSAD** | Chad |

**47.** **UNAREJEA** kwamba, kulingana na Kanuni za Taratibu za AUDA-NEPAD na

kulingana na mashauriano ya kikanda, Hali ya muundo mpya wa Ofisi ya Kamati elekezi ya Wakuu wa nchi na Serikali kwa kipindi cha Februari 2026-Februari 2028 ni kama ifuatavyo:

- Makamu mwenyekiti wa Kwanza: Guinea ya Ikweta (Kanda ya Kati).
- Makamu mwenyekiti wa Pili: Wazi
- Makamu mwenyekiti wa Tatu : Wazi
- Makamu mwenyekiti wa nne/Mratibu: Misri ( Mwenyekiti wa Kamati elekezi ya Wakuu wa Nchi na Serikali anayemaliza muda wake / Kanda ya Kaskazini).

**48.** **UNAHIMIZA** Kanda zenye nafasi zilizo wazi kukamilisha haraka mashauriano yao ya kikanda na kuwasilisha uteuzi wa viti vilivyobaki visivyo vya kuanzisha; na **UNAZIALIKA** Kanda za Mashariki na Magharibi kuteua wagombea wa nafasi za Makamu Mwenyekiti wa Pili na wa Tatu, mtawalia, kwa mujibu wa Kanuni ya 15 (mara tu wakuu wa kanda watakapokamilisha mashauriano muhimu na kuwasilisha wateule, OLC itazunguka kwa ajili ya kupitishwa kupitia utaratibu wa ukimya).

# UAMUZI WA CAHOSCC KUHUSU RIPOTI YA MRATIBU WA KAMATI YA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI WA AFRIKA KUHUSU MABADILIKO YA TABIANCHI (CAHOSCC)

**Mkutano Mkuu**,

**1. UNAKARIBISHA** ripoti ya Mratibu wa Mratibu wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (CAHOSCC), Mhe. Dkt. William Samoei Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya, **UNATOA SHUKRANI** kwa Jamhuri ya Kenya kwa kuratibu kazi ya CAHOSCC na **UNAIDHINISHA** maamuzi yaliyomo ndani yake.

**2. UNAZINGATIA** na kukaribisha matokeo ya Mkutano wa Pili wa Tabianchi wa Afrika (ACS2) uliofanyika kuanzia tarehe 8 - 10 Septemba 2025 mjini Addis Ababa, Ethiopia;

3. **UNAMPONGEZA** Mhe. Abiy Ahmed Ali, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia, kwa kuandaa Mkutano wa Pili wa Tabianchi wa Afrika (ACS2) wenye athari kubwa na mafanikio;

**4. UNAMPONGEZA ZAIDI** Mhe. Abiy Ahmed (Ph.D), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Shirikisho la Ethiopia, kwa mpango wake wa maono wa kuanzisha Mkataba wa Uvumbuzi wa Tabianchi wa Afrika (ACIC) na Kituo cha Tabianchi cha Afrika (ACF), kwa lengo la kukusanya dola bilioni 50 kutekeleza suluhu 1,000 za tabianchi zilizobuniwa kiafrika ifikapo mwaka 2030 na UNAPANUA uungaji mkono kamili kwa juhudi hii.

5. **PIA UNAMPONGEZA** Mhe. Mahmoud Ali Youssouf, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kwa uongozi wake wa mfano katika kuitisha Mkutano wa Pili wa Tabianchi wa Afrika (ACS2);

**6. UNAIOMBA** Kamisheni ya AU kuandaa mwongozo na mpango wa utekelezaji wa *Azimio la Viongozi wa Afrika la Addis Ababa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na Wito wa Kuchukua Hatua*, na kukusanya rasilimali ili kuharakisha utekelezaji wake;

**7. UNAZINGATIA** ripoti kuhusu utekelezaji wa Azimio la Nairobi la Viongozi wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na Wito wa kuchukua Hatua.; na **UNATOA WITO** wa mbinu iliyoratibiwa ya utekelezaji wa matokeo ya Mikutano ya Tabianchi Afrika.

**8. UNATHIBITISHA** tena kujitolea kwa ushirikiano wa pande nyingi chini ya UNFCCC na Mkataba wa Paris, na kuchukua hatua za pamoja za kimataifa kushughulikia mabadiliko ya tabianchi, huku ukitoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuimarisha ushirikiano, mshikamano, na uaminifu katika kutoa matokeo ya tabianchi yenye malengo makubwa, usawa, na yanayozingatia sheria yanayokidhi mahitaji na vipaumbele vya nchi zinazoendelea, hasa Afrika.

9. **UNAPONGEZA** jukumu lililofanywa na Mkutano wa Mawaziri wa Afrika kuhusu Mazingira (AMCEN) na Kundi la Wazungumzaji wa Afrika (AGN) kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi katika maandalizi na ushiriki katika COP30. **UNASHUKURU** kwa jitihada na uongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuongoza AGN katika COP30 na **UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Ghana kuhusu kushika uenyekiti wa AGN kwa kipindi cha 2026 na 2027.

10. **UNAIPONGEZA PIA** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake bora katika kuendeleza vipaumbele vya kimkakati vya Afrika, kukuza umoja na kuimarisha kina cha kiufundi cha Kundi wakati wa kipindi cha uongozi wao; na kuadhimisha miaka 30 ya ushiriki na mchango wa AGN katika mazungumzo ya tabianchi;

11. **UNAKARIBISHA** matokeo ya mikutano muhimu ya kimkakati iliyoitishwa Zanzibar na Dar es Salaam, ambayo iliimarisha uratibu kati ya Wawakilishi wa Kitaifa na Waratibu Wakuu;

12. **UNAREJELEA** uamuzi Assembly/AU/Dec.257(XIII) wa Julai 2009 na uamuzi wa Baraza Kuu EX.CL/Dec.500(XV), ambao ulianzisha Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (CAHOSCC) na kuamua muundo wake wa awali; UNAKUMBUKA ZAIDI ombi rasmi lililowasilishwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2024 kwa Sekretarieti ya CAHOSCC likielezea nia yake ya kuwa mwanachama wa kudumu wa Kamati hiyo ili kuchangia mwongozo wa kisiasa wa ngazi ya juu wa bara kuhusu mabadiliko ya tabianchi;

13. **UNAIDHINISHA** ombi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **UNALIPITISHA** kama mwanachama wa kudumu wa CAHOSCC, anayeanza mara moja, ili kuhakikisha mwendelezo wa utaalamu wa kimkakati na kiufundi ulioonyeshwa wakati wa Uenyekiti wake wa AGN;

14. **UNAIOMBA** Kamisheni kusasisha rekodi za muundo wa Kamati na kuwezesha ushiriki kamili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika shughuli zote zijazo za CAHOSCC.

15. **UNAIOMBA** Kamisheni kukusanya rasilimali endelevu kwa ajili ya kusaidia mazungumzo ya mabadiliko ya tabianchi ili kuhakikisha ushiriki endelevu wa wataalamu wa Afrika katika michakato ya UNFCCC.

16. **UNAKARIBISHA ZAIDI** kuanzishwa kwa Kituo cha Majadiliano ya Tabianchi cha Vijana wa Afrika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama ilivyopitishwa na Uamuzi wa AMCEN AMCEN/20/8, kama hatua muhimu ya kimkakati katika kujenga uwezo wa muda mrefu wa wazungumzaji wa Afrika na kuhakikisha usawa baina ya vizazi;

**17. UNAIPONGEZA** Jamhuri ya shirikisho la Brazili kwa kufanikiwa kuandaa Mkutano wa Thelathini wa Mkutano wa Nchi Zilizoridhia (COP30) huko Belém, ambao uliashiria kumbukumbu ya miaka kumi ya Mkataba wa Paris na kuthibitisha tena ahadi ya kimataifa kwa ushirikiano wa pande nyingi juu ya mabadiliko ya tabianchi.

**18. UNAKARIBISHA** kupitishwa kwa Kifurushi cha Kisiasa cha Belém, ikiwa ni pamoja na Uamuzi wa Mutirão, ambao uliashiria mabadiliko kutoka mazungumzo hadi utekelezaji, ulithibitisha tena ahadi ya lengo la nyuzijoto 1.5, na kutoa wito wa kuharakishwa kwa hatua za pamoja na ushirikiano wa kimataifa kupitia utekelezaji ulioimarishwa wa NDCs na mipango ya kitaifa ya kukabiliana na hali, pamoja na maendeleo yaliyofikiwa katika kuendeleza Lengo la Kimataifa la Kukabiliana na Hali (GGA), tathmini ya maendeleo ya hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi *(Global Stocktake)* na kuanzishwa kwa Mfumo wa Mabadiliko ya Haki.

**19. UNAKARIBISHA** uthibitisho tena wa COP30 kwamba hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ikiwa ni pamoja na zile za upande mmoja, hazipaswi kuwa ubaguzi wa kiholela au usio na msingi au kizuizi kilichofichwa kwenye biashara, unatambua kuanzishwa kwa mazungumzo yaliyoamriwa kuhusu fursa, changamoto na vikwazo vya kuimarisha ushirikiano wa kimataifa unaohusiana na jukumu la biashara na unahimiza nchi zote za Afrika kushiriki kikamilifu katika mazungumzo haya ili kuhakikisha kwamba athari za hatua za upande mmoja kwenye maendeleo endelevu na utokomezaji wa umaskini zinaakisiwa kikamilifu, na kwamba kipaumbele cha Afrika kinaunda matokeo ya mchakato huu.

**20. UNAZINGATIA ZAIDI** kwa wasiwasi maendeleo machache yaliyopatikana katika ufadhili wa tabianchi katika COP30, ikiwa ni pamoja na mapengo yanayoendelea katika utoaji, ukubwa, utabiri wa upatikanaji, na upatikanaji wa fedha kwa nchi zinazoendelea, hasa kwa ajili ya kukabiliana na hali, hasara na uharibifu, na vipaumbele vya mabadiliko ya haki. Katika suala hili, **UNASISITIZA** kwamba mizigo mikubwa na inayoongezeka ya madeni inazidi kuzuia nafasi ya fedha na kudhoofisha uwezo wa nchi za Afrika kuwekeza katika hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na **UNASISITIZA** haja ya dharura ya utelkelezaji mzuri wa *Collective Quantified Goal on Climate Finance,* mageuzi kwenye muundo wa fedha ya tabianchi ya kimataifa na ushirikiano wa kimataifa ulioimarishwa.

**21. UNATOA WITO** KWA nchi zilizoendelea, benki za maendeleo za kimataifa, na taasisi za fedha za kimataifa kuongeza ufadhili, ruzuku, na dhamana zenye masharti nafuu na zisizo za kuleta madeni, na kuendesha mabadilishano ya deni kwa tabianchi na deni kwa asili, vifungu vya deni vinavyostahimili mabadiliko ya tabianchi, na ufadhili wa muda mrefu na wa gharama nafuu ili kusaidia mabadiliko ya nishati, viwanda na mahitaji ya kukabiliana na mabadiliko ya Afrika.

**22. UNAAMUA** kwamba kuongeza ufadhili wa kukabiliana na mabadiliko kwa Afrika ni kipaumbele cha dharura na cha haraka, na unatoa wito wa uhamasishaji unaotabirika

na utoaji wa ufadhili wa mabadiliko ulioongezeka kwa kiasi kikubwa, unaotegemea ruzuku na wenye masharti nafuu sana, ikiwa ni pamoja na njia iliyo wazi ya angalau ufadhili wa kukabiliana na mabadiliko mara tatu katika muda mfupi ujao; pamoja na ubora ulioboreshwa na upatikanaji wa fedha kupitia ufikiaji rahisi, ufikiaji ulioboreshwa kwa taasisi za Afrika, na gharama iliyopunguzwa ya mtaji; unahimiza benki za maendeleo za kimataifa na taasisi za fedha za kimataifa kurekebisha haraka mamlaka zao, vyombo, na mbinu za mizania ili kuweka kipaumbele ukuaji unaotokana na kukabiliana na mabadiliko na uhimilivu;

23. **UNAKARIBISHA** uamuzi wa COP 30 unaoidhinisha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia kama mwenyeji wa Kikao cha 32 cha Mkutano wa Nchi Zilizoridhia Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP32) utakaofanyika kuanzia Novemba 8-19, 2027 huko Addis Ababa, Ethiopia na unasisitiza umuhimu wa kutumia COP32 ili kuendeleza vipaumbele na maslahi ya Afrika.

24. **UNAKARIBISHA ZAIDI** uteuzi wa Mhe. Gedion Timothewos, Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia kama Rais Mteule wa COP32 na **UNAIOMBA** Kamisheni kuhamasisha Nchi Wanachama wote wa AU na washirika kuunga mkono Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia katika maandalizi na kuwa mwenyeji wa COP32.

25. **UNAZINGATIA** ripoti ya Tume za Tabianchi za Afrika na unaiomba Kamisheni kuanzisha mfumo wa uratibu ulioboreshwa kwa Tume za Tabianchi na Mipango mingine ya Tabianchi ya bara na kuunga mkono utekelezaji na utoaji wa ripoti zake;

26. **UNATOA WITO** washirika wa maendeleo, taasisi za fedha za kimataifa, na mashirika husika ya pande nyingi kuimarisha usaidizi ulioratibiwa kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, uhimilivu, ujenzi wa amani, na maendeleo endelevu katika Sahel na maeneo mengine yaliyo hatarini barani humo.

27. **UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Afrika Kusini kwa kufanikiwa kuwa mwenyeji na uongozi wa Urais wa G20 mwaka wa 2025, na inatoa wito wa ushiriki wa Kiafrika ulioimarishwa na kuratibiwa na ujumbe wa pamoja katika njia za ushiriki wa G20 na vikundi vya kazi ili kuendeleza vipaumbele vya Afrika kuhusu fedha za tabianchi, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uhimilivu, mabadiliko ya haki, na mageuzi ya usanifu wa fedha wa kimataifa, ikiwa ni pamoja na kupitia ushirikiano wa karibu kati ya CAHOSCC, Kamishmmi ya Umoja wa Afrika, na taasisi husika za Kiafrika za Afrika.

28. **UNAOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kukusanya rasilimali kwa ajili ya kufuatilia kwa haraka utekelezaji wa Mifumo ya Tahadhari ya Mapema ya Hatari Nyingi na Programu ya Hatua za Mapema, Programu ya Hatua za kukabiliana na Mabadiliko

ya tabianchi ya Afrika (AfCAP), Programu ya Uhimilivu wa Mijini na mipango mingine ya kikanda na ya Kusini-Kusini ili kuongeza ujenzi wa uhimilivu barani Afrika;

**29. UKIWA** na wasiwasi kwamba uhamaji unaosababishwa na majanga na aina nyingine za harakati za kulazimishwa zinaendelea kukua kutokana na mabadiliko ya tabianchi na mazingira barani Afrika, na katika muktadha wa kimataifa wa maadili yanayopungua ya pande nyingi na kupungua kwa utambuzi wa mabadiliko ya tabianchi kama jukumu la kimataifa, UNATOA WITO KWA Nchi Wanachama kufanya kazi kwa ushirikiano na Kamisheni na washirika ili kukuza uhimilivu na ustawi wa pamoja wa Afrika.

**30. UNAZINGATIA** ombi la Mheshimiwa Denis Sassou N'Guesso, Rais wa Jamhuri ya Kongo na Rais wa Tume ya Tabianchi ya Bonde la Kongo (CBCC) la kuendesha Redio na Televisheni ya Bonde la Kongo chini ya Tume ya Tabianchi ya Bonde la Kongo.

**31. UNAKARIBISHA** pendekezo la ya Jamhuri ya Kongo ya kuandaa Mkutano wa Tatu wa Tabianchi wa Afrika (ACS3), huko Brazzaville, na **UNAZINGATIA** mchakato unaofanywa na Kamisheni ya Umoja wa Afrika wa kuwapa Nchi Wanachama wote fursa ya kugombea kuandaa ACSC3. **UNAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kukamilisha uteuzi wa mwenyeji anayefuata mara tu makataa ya kuonesha nia yatakapofungwa na kutoa taarifa mpya katika kikao kijacho cha CAHOSCC.

**32. UNAZINGATIA** maendeleo katika utekelezaji wa Mpango wa Utekelezaji wa Afrika kuhusu Masoko ya Kaboni na maendeleo ya Kiwango cha Dhahabu cha Afrika kwa Masoko ya Kaboni na uwezo wao wa kufungua ufadhili kwa Afrika.

**33. UNATAMBUA** kwamba umaskini unaoendelea wa nishati na dhiki kubwa ya deni vinaimarisha vikwazo kwa pande zote mbili kwenye azma ya Afrika ya tabianchi, huku nafasi ndogo ya kifedha ikidhoofisha uwekezaji katika nishati mbadala, kukabiliana na hali, na miundombinu thabiti.

**34. UNATHIBITISHA** njia za mabadiliko ya nishati ya haki na yenye usawa barani Afrika, zilizojikita katika utumiaji wa haraka wa nishati mbadala, ufanisi wa nishati, mabwawa ya umeme ya kikanda, na miundombinu wezeshi, huku ikifanya kazi kushughulikia tofauti za kijiografia katika suala la ufadhili na kuruhusu njia tofauti za kitaifa zinazoakisi hali za nchi, rasilimali na vipaumbele vya maendeleo.

**35. UNAKARIBISHA** maendeleo yaliyopatikana mwaka 2025 kupitia utekelezaji wa awali wa Mpango wa Viwanda vya Kijani Afrika (AGII), ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Sekretarieti ya AGII jijini Nairobi, Kenya; na **UNAIOMBA** Sekretarieti ya AfCFTA na Serikali ya Jamhuri ya Kenya kuendelea kufanya kazi kwa karibu kuelekea kukamilisha mipango ya kitaasisi ya Sekretarieti ya AGII.

**36. UNAMPONGEZA** Mhe. Dkt. William Samoei Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya, na Sekretarieti ya AfCFTA kwa kuhamasisha Taasisi za Fedha za Maendeleo ya Afrika chini ya Mpango wa Viwanda vya Kijani Afrika, na kusababisha kusainiwa kwa Mfumo wa Ushirikiano wa AGII; **UNAKARIBISHA** ukusanyaji wa takriban dola bilioni 100 katika ahadi kuelekea viwanda vya kijani; na **UNATOA** WITO kwa wabia wa maendeleo, taasisi za fedha za kimataifa na kikanda, na sekta binafsi kusaidia utekelezaji wa mabadiliko ya viwanda vya kijani Afrika.

**37. UNAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika na taasisi zingine za Afrika kukusanya rasilimali na kutoa msaada kwa Kundi la Wazungumzaji la Afrika kuhusu UNCCD kwa ajili ya kuandaa protokali ya kisheria kuhusu usimamizi wa ukame na msimamo wa pamoja, na kuandaa mikutano ya maandalizi ya Afrika mwaka 2026 na kuendelea. **PIA UNAOMBA** wabia wa maendeleo kuiunga mkono Kamisheni katika kuitisha Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Afrika kuhusu Ukame uliopangwa kufanyika katikati ya mwaka 2026 katika juhudi za kujenga uhimilivu dhidi ya tofauti za tabianchi.

**38. UNATAMBUA** jukumu la kimkakati la Mfuko wa Tabianchi wa Kijani (GCF), Mfuko wa Kukabiliana na Mabadiliko (AF), na Mfuko wa Kuitikia Hasara na Uharibifu (FRLD), Mfuko wa Nchi Zilizoendelea Kidogo (LDCF) katika kuunga mkono vipaumbele vya tabianchi na maendeleo vya Afrika.

**39. UNAWAPONGEZA** Waheshimiwa, Wakuu wa Nchi na Serikali na wajumbe wa CAHOSCC kwa mwongozo endelevu kuhusu ushiriki wa Afrika katika mabadiliko ya tabianchi.

# MAAMUZI KUHUSU RIPOTI MKUTANO WA KWANZA (1) WA KAMATI YA MKUTANO WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI INAYOHUSIKA NA UTEKELEZAJI WA AfCFTA

***Mkutano Mkuu:***

1. **UNAMPONGEZA** Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Mkutano kuhusu Utekelezaji wa AfCFTA na Ujumuishaji wa Kiuchumi, pamoja na Katibu Mkuu wa Sekretarieti ya AfCFTA kwa kuendesha kuanzisha utekelezaji wake kwa mujibu wa uamuzi Assembly/AU/Dec.911(XXXVIII); na **UNAPOKEA** Taarifa ya Kamati na Hadidu za Rejea (ToR) zilizopitishwa na Kamati;

2. **UNAELEZEA** wasiwasi mkubwa kuhusu kudhoofika na kuvurugwa kwa mfumo wa kuhusisha pande nyingi na misingi yake; **UNAENDELEA KUELEZEA** uungwaji mkono kwa mfumo wa biashara wa pande nyingi unaozingatia sheria, ukiwa na Shirika la Biashara Duniani (WTO) kama mhimili wake, na VILEVILE **UNAONYESHA** wasiwasi kuhusu uwekaji wa hatua za kibiashara za upande mmoja zenye vizuizi vinavyoathiri vibaya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika na malengo ya Mkataba Ulioanzisha AfCFTA;

3. **INAPONGEZA** Jamhuri ya Kiarabu ya Misri katika nafasi yake kama Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri Wanaohusika na Biashara, pamoja na Baraza hilo, kwa kufanikisha kukamilisha majadiliano ya Protokali za Awamu ya Pili, na **KUAGIZA** kuharakishwa kwa mpito wa Mkataba wa Kuanzisha AfCFTA kutoka hatua ya majadiliano kwenda hatua ya utekelezaji;

4. **UNATOA** shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Mahamadou Issoufou, Rais wa zamani wa Jamhuri ya Niger, katika jukumu lake kama Kinara wa AfCFTA, kwa uongozi wake uliofanikisha majadiliano ya Awamu ya Kwanza na ya Pili ya AfCFTA;

5. **UNAKUMBUKA** uamuzi Assembly/AU/Dec.927(XXXVIII) unaozitaka Nchi Wanachama kuridhia nyaraka za kisheria za AU na **UNAZIHIMIZA KWA DHATI** Nchi Wanachama kuridhia Protokali za AfCFTA kuhusu Uwekezaji, Sera ya Ushindani, Haki Miliki, Biashara ya Kidijitali, na Wanawake na Vijana katika Biashara ifikapo mwisho wa mwaka 2026, na pale inapohitajika, kuarifu uridhiaji huo ili kuhakikisha unaanza kutekelezwa kwa haraka;

6. **UNAOMBA** Kamati ya Mkutano kuhamasisha Nchi Wanachama, kwa mujibu wa taratibu zao za kikatiba, kukamilisha mchakato wa kuridhia Protokali za AfCFTA kuhusu Uwekezaji, Sera ya Ushindani, Haki Miliki, Biashara ya Kidijitali, na Wanawake na Vijana katika Biashara ifikapo mwisho wa mwaka 2026, na kuwasilisha ripoti za maendeleo kila mwaka kuanzia Kikao cha 40 cha Kawaida cha Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mwaka 2027.

7. **UNAELEZEA** wasiwasi yake kuhusu kuongezeka kwa sera za kulinda soko zinazosababisha kugawanyika kwa minyororo ya thamani ya kimataifa na kuimarisha hali ya kudhoofika kwa viwanda barani Afrika, na **UNAELEKEZA** Baraza la Mawaziri kuanzisha majadiliano kuhusu Protokali ya Sera na Maendeleo ya Viwanda kama sehemu muhimu ya mfumo wa kisheria wa AfCFTA;

8. **UNAELEKEZA** Katibu Mkuu wa Sekretarieti ya AfCFTA na Baraza la Mawaziri kutekeleza kikamilifu Ibara ya 11 (k), (l), (m) na (n) pamoja na Ibara ya 13 za Mkataba wa AfCFTA kuhusu uendeshaji wa kitaasisi wa Sekretarieti, kwa mujibu wa matakwa ya Mkataba;

9. **UNAAMUA** kujumuisha katika Kamati ya Mkutano kuhusu Utekelezaji wa AfCFTA na Ujumuishaji wa Kiuchumi, MaKinara wa AU katika masuala yanayohusiana na utekelezaji wa Mkataba wa Kuanzisha AfCFTA; na **PIA UNAAMUA** kuwa Ripoti ya Kamati iwe sehemu ya Ajenda ya Kimkakati ya Mkutano kuhusu Ujumuishaji wa Kiuchumi;

10. **UNAPONGEZA** Jamhuri ya Madagascar kwa kuridhia Mkataba wa Kuanzisha AfCFTA na kuweka Hati yake ya Uridhiaji; **PIA UNAPONGEZA** Jamhuri ya Shirikisho ya Somalia kwa kuridhia Mkataba huo na inahimiza kuwekwa kwa haraka kwa Hati yake ya Uridhiaji; na **UNAZIHIMIZA** Benin, Libya, Sudan Kusini na Sudan kuharakisha michakato yao ya kuridhia;

11. **AIDHA UNAKUPONGEZA** Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho ya Ethiopia na Jamhuri za Msumbiji na Namibia kwa kukamilisha taratibu zao za ndani za kuchapisha katika Gazeti Rasmi Ratiba za Muda za Mapunguzo ya Ushuru wa Forodha, na **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama zilizobaki ambazo bado hazijachapisha Ratiba zao za Muda za Mapunguzo ya Ushuru wa Forodha kukamilisha taratibu zao za ndani na kuhitimisha michakato yao ya kitaifa ili kuanza biashara kwa mujibu wa kanuni za Mkataba wa Kuanzisha AfCFTA, ifikapo mwisho wa mwaka 2026.

12. **UNAIAGIZA** Sekretarieti ya AfCFTA kuharakisha utekelezaji wa dirisha moja la kidijitali linaloweza kuunganishwa katika ngazi ya bara, ili kuongeza ufanisi wa taratibu za forodha, kuwezesha usafirishaji wa bidhaa kwa ufanisi, na kurahisisha upatikanaji wa kidijitali wa nyenzo za biashara kwa waendeshaji wa kiuchumi;

13. **UNAKUMBUKA** Maamuzi EX.CL/Dec.1221(XLIII) na EX.CL/Dec.1241(XLIV) yaliyoielekeza Sekretarieti ya AfCFTA kujihusisha na shughuli za kuzalisha mapato na uhamasishaji wa rasilimali kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji kamili wa Mkataba wa Kuanzisha AfCFTA; na **KUELEKEZA** Sekretarieti ya AfCFTA kushirikiana na taasisi husika za kifedha pamoja na sekta binafsi ili kuanzisha na kuendesha mifumo ya kuzalisha mapato kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa

AfCFTA na kupunguza utegemezi mkubwa kwa washirika wa maendeleo wa nje, kwa mujibu wa Ibara ya 11 ya Mkataba wa Kuanzisha AfCFTA; na **UNAAMUA** kuwa mapato yatakayozalishwa yaelekezwe kupitia Mfuko wa Marekebisho wa AfCFTA ulioanzishwa na kuanza kutumika chini ya Uamuzi wa Mkutano Assembly/AU/Dec.911(XXXVIII), ili kutumika kuunga mkono shughuli za uendeshaji na programu za Sekretarieti ya AfCFTA, kwa mujibu wa mfumo wa uongozi wa Mfuko huo na Kanuni za Fedha za AU zinazotumika;

14. **UNAONYESHA** wasiwasi kuhusu kasi ndogo ya utekelezaji wa upunguzaji wa ushuru chini ya taratibu za sasa na **UNALIAGIZA** Baraza la Mawaziri Wenye dhamana ya Biashara kufanya mapitio kamili ya taratibu za kuondoa ushuru kulingana na kifungu cha Mkataba;

15. **UNAELEKEZA ZAIDI** Baraza la Mawaziri Wanaohusika na Biashara kuwasilisha katika Kikao cha 40 cha Kawaida cha Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali, utaratibu ulioboreshwa na kuimarishwa wa huria ya ushuru ambao utahakikisha uondoshaji kamili wa ushuru wa forodha kwa bidhaa zote zinazozwa ndani ya Afrika kwa mujibu wa kanuni za Mkataba wa Kuanzisha AfCFTA;

16. **UNAAMUA** kwamba utekelezaji wa utaratibu huo ulioboreshwa lazima uhakikishe uondoshaji kamili wa ushuru kwa bidhaa zote zinazouzwa chini ya Mkataba wa Kuanzisha AfCFTA, pamoja na kuanza kutumika kwa kiwango cha ushuru sifuri kwa biashara zote stahiki za ndani ya Afrika; na **UNAELEKEZA** Nchi Wanachama kuchukua hatua zote muhimu za kisheria, kiutawala na kitaasisi ili kuwezesha utekelezaji wa uamuzi huu kwa wakati na kuunga mkono uendeshaji madhubuti wa soko la bara lililohurishwa kikamilifu, kwa mujibu wa Mkataba wa Abuja;

17. **UNAKUMBUKA** uamuzi Assembly/AU/Dec.692(XXXI), ambao kwao Mkutano uliahidi kushirikiana na wabia wa nje kama kundi moja, na kusema kwa sauti moja, na kuzihimiza Nchi Wanachama kujiepusha kuingia mikataba ya kibiashara ya pande mbili isiyolingana na malengo ya Mkataba wa Kuanzisha AfCFTA; na **UNAKUMBUKA ZAIDI** uamuzi Assembly/AU/Dec.845(XXXVI) kuhusu uwakilishi ulioratibiwa na wa pamoja wa Umoja wa Afrika katika mfumo wa G20 kama mfano na rejea muhimu ya kufanikisha malengo yaliyowekwa katika Uamuzi Assembly/AU/Dec.692(XXXI);

18. **UNAAMUA**, katika kuendeleza malengo ya Mkataba Ulioanzisha AfCFTA, kuimarisha ushirikiano wa pamoja na ulioratibiwa na nchi za tatu na washirika wa kimkakati katika masuala yanayohusiana na biashara na uwekezaji, kwa kutumia Mkataba wa Kuanzisha AfCFTA kama mfumo wa kisheria wa bara kwa ujumuishaji wa biashara na uchumi wa Afrika, kwa lengo la kuimarisha sauti ya pamoja ya Afrika na mshikamano wake katika utawala wa uchumi wa kimataifa;

19. **UNAAMUA ZAIDI** kwamba Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri Wanaohusika na Biashara, akisaidiwa na Katibu Mkuu wa Sekretarieti ya AfCFTA, atawezesha ushirikiano huo ulioratibiwa ndani ya mfumo wa Mkataba wa Kuanzisha AfCFTA; na **UNAELEKEZA** Sekretarieti ya AfCFTA kutoa ripoti kwa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu matokeo ya ushirikiano na nchi za tatu na kambi za kibiashara;

20. **UNAMPONGEZA** Mhe. Mahamadou Issoufou, Rais wa zamani wa Jamhuri ya Niger na Kinara wa AfCFTA, kwa kuendelea kujitolea kwa kazi hyake na uongozi wake katika kuendeleza Mkataba wa Kuanzisha AfCFTA; **UNAHIMIZA** kuendelea na utetezi wa ngazi ya juu kutoka kwa Kinara wa AfCFTA katika kukuza ujumuishaji wa kiuchumi wa bara; na **UNAAMUA** kwamba Kinara wa AfCFTA atatoa ripoti kwa Mkutano kupitia Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Utekelezaji wa AfCFTA na Utangamano wa Kiuchumi.

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA KAMATI YA WAKUU KUMI (C-10) WA NCHI NA SERIKALI KUHUSU MAGEUZI YA BARAZA LA USALAMA LA UMOJA WA MATAIFA, NA MHE JULIUS MAADA BIO, RAIS WA JAMHURI YA SIERRA LEONE

**Mkutano Mkuu:**

1. **UNAPOKEA** Ripoti ya 26 ya Kamati ya Wakuu Kumi wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (C-10) kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

2. **UNAREJELEA** Uamuzi wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali Assembly/AU/Desemba 923(XXXVIII) na maamuzi ya awali kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

3. **UNASISITIZA** kwamba mageuzi kamili ya Umoja wa Mataifa, ikiwa ni pamoja na Baraza la Usalama, yanabaki kuwa muhimu ili kuoanisha Taasisi hiyo na hali halisi ya kijiografia ya kisasa na **kurekebisha dhuluma ya kihistoria dhidi ya Afrika**, ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa Afrika katika kundi la kudumu na uwakilishi wake mdogo katika kundi la uanachama usio wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

4. **UNATAMBUA KWA SHUKRANI** kuendelea kwa ushiriki wa C-10 katika kukuza, kulinda na kutetea Msimamo wa Pamoja wa Afrika (CAP), kama ilivyoainishwa katika **Makubaliano ya Ezulwini** na **Azimio la Sirte**, na msaada unaoongezeka na kasi kwa ajili ya CAP, hususani kama ilivyoainishwa katika Lengo la 39, aya (a) ya Mkataba wa Siku za Baadaye, ambao unaunga mkono umuhimu wa kurekebisha dhuluma ya kihistoria dhidi ya Afrika kama kipaumbele ikiwa ni pamoja na kuichukulia Afrika kama suala maalum.

5. **UNAKARIBISHA** uratibu ulioimarishwa wa ndani na uhamasishaji uliofanywa na **C-10 wakati wa kipindi cha kuripoti, ikiwa ni pamoja na Mikutano ya Wawakilishi wa Kudumu wa C-10** iliyoandaliwa na Jamhuri ya Sierra Leone mjini **Freetown (25–26 Aprili 2025)**, ambayo iliimarisha umoja na kutoa **rasimu ya Mfumo wa Kiafrika kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (Mfumo wa Mageuzi ya Afrika), Mpango Mkakati, na Muhtasari wa Masuala Muhimu** (Nyaraka za Matokeo ya Mkutano wa Freetown), na **UNAZINGATIA** uelewa kwamba Mpango Mikakati na Muhtasari wa Masuala Muhimu zitabaki kuwa hati za ndani za C-10 ili kuongoza kazi yake iliyoratibiwa.

6. **UNAKARIBISHA ZAIDI** mkutano wa **13 wa Mawaziri wa C-10** uliofanyika kwa mafaniko wa ulioandaliwa na Jamhuri ya Zambia mjini **Lusaka**, ukitanguliwa na Mkutano wa Maafisa Wakuu, ambao ulipitia maendeleo, ukaidhinisha rasimu ya Hati za Matokeo ya Mkutano wa Freetown, na kupitisha Hati ya **Matokeo ya Mkutano wa Lusaka**.

7. **UNAKARIBISHA PIA** matokeo ya **Mkutano wa 6 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa C-10 (kwa njia ya mtandao, tarehe 25 Julai 2025**) ambao **ulipitisha Makubaliano ya Mfumo wa Mageuzi ya Afrika**, ukithibitisha tena CAP na kusisitiza jinsi Afrika inavyochukuliwa kama suala maalum..

8. **UNAKARIBISHA** kuitishwa kwa **Mkutano wa 7 wa C-10 (21 Septemba 2025, Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, mjini New York)** kuadhimisha kumbukumbu ya miaka 20 ya Makubaliano ya Ezulwini na Azimio la Sirte na **UNAPONGEZA** uthibitisho wake wa umoja wa Afrika na kutambuliwa kwa ukubwa kwa uhalali wa mahitaji ya Afrika ya uwakilishi sawa katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

9. **UNATHIBITISHA TENA** dhamira yake kwa Msimamo wa Pamoja wa Afrika, kama chaguo pekee kwa uwakilishi kamili wa Afrika katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lililofanyiwa mageuzi, na **UNATHIBITISHA TENA** Majadiliano ya Serikali Mbalimbali (IGN), yaliyoanzishwa na Uamuzi 62/557, kama jukwaa halali la mageuzi.

10. **UNASISITIZA** kwamba uwakilishi kamili wa Afrika katika Baraza la Usalama lililofanyiwa mageuzi unahusisha

    (i) Si chini ya **viti viwili (02) vya kudumu** vyenye haki na stahiki zote, ikiwa ni pamoja na **haki ya kupiga kura ya turufu, ikiwa vitapatikana**;
    (ii) **Viti vitano (05) visivyo vya kudumu**; na
    (iii) **Haki ya Umoja wa Afrika kuchagua** wawakilishi wake katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ili kufanya kazi kwa niaba yake.

11. **UNAIOMBA**

    (i) C-10 iendelea kushiriki katika majadiliano ya ngazi za juu za kisiasa, ikiwa ni pamoja na Wajumbe watano wa Kudumu wa Baraza la Usalama, ili kuendeleza Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa;

    (ii) C-10 iendelee kuimarisha ushirikiano wake na Makundi mengine yenye Maslahi na Kikanda na wadau, ikitegemea maendeleo yaliyopatikana katika kuendeleza Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Katika suala hili, **UNAITAKA** Kamati ya Wakuu Kumi wa Nchi na Serikali kufanya Mikutano ya Ngazi ya Juu pembezoni mwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika;

    (iii) Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika kuongea lugha moja ili kuendeleza Msimamo wa Pamoja wa Afrika katika Taarifa zao za Kitaifa

wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa 81 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwezi Septemba 2026, ikisisitiza wito wa mageuzi kamili ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, na kutekeleza ahadi ya kurekebisha dhuluma ya kihistoria dhidi ya Afrika kama kipaumbele na kuifanya Afrika kama suala maalum;

(iv) Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika zitoe kipaumbele kwenye suala la mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa katika ushirikiano wao wa sera za kigeni na washirika wasio wa Afrika, hasa zikisisitiza hitaji la kurekebisha dhuluma ya kihistoria ambayo Afrika inaendelea kukabiliana nayo, na kuichukulia Afrika kama suala maalum na kipaumbele katika mchakato wa mageuzi.

12. **UNATOA WITO** kwa Afrika kushiriki tu katika majadiliano kwa njia ya maandishi mradi tu kuna makubaliano ya awali kati ya Nchi Wanachama kuhusu makundi matano na mpangp uliokubaliwa, ambao kwa ujumla unashughulikia suala la dhuluma ya kihistoria, ambao una makubaliano mapana, na mpango wa mageuzi unaoshughulikia waziwazi upanuzi katika makundi yote mawili ya UNSC.

13. **UNATOA WITO ZAIDI** kwa Nchi zote Wanachama wa AU kuendelea kuzungumza kwa sauti moja, ikiwa ni pamoja na kupitia matumizi thabiti ya lugha ya pamoja iliyokubaliwa, na kuepuka misimamo au uhusiano unaokinzana na CAP, ikiwa ni pamoja na kujiondoa kutoka kwenye uanachama wa pande mbili usiofaa.

14. **UNAAMUA**:

(i) **Kuidhinisha** Mfumo wa Mageuzi ya Afrika, na kuagiza kwamba C-10 iuwasilishe kwenye mazungumzo yaliyopangwa **ya Majadiliano ya Serikali za Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (IGN)**;

(ii) Kwamba Mageuzi ya Baraza la Usalama yatabaki kuwa **kipengele cha kimkakati** kwenye ajenda na mpango kazi wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali, na **KUTHIBITISHA** umuhimu wa Kamisheni kuendelea kutoa ufadhili na msaada unaohitajika ili kuwezesha kazi ya C-10;

(iii) **Kuongeza mgao** katika bajeti za Kamisheni na Ujumbe wa Kudumu wa Waangalizi wa AU ili kutoa fedha zinazopatikana ili kuwezesha shughuli za C-10, na **KUHIMIZA** michango ya hiari ya Nchi Wanachama ili kusaidia kazi ya C-10;

(iv) Kwamba C-10 itaendelea kutekeleza mamlaka yake hadi Afrika itakapofikia malengo yake kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

**UAMUZI KUHUSU KURASIMISHA JUKWAA LA KATIBA KUHUSU HAKI NA DHAMANA ZA WASICHANA NA WATOTO WA KIAFRIKA**
**Doc. EX.CL/1674(XLVIII)**

**Mkutano Mkuu*:***

1. **UNAZINGATIA** uamuzi EX.CL/Dec.18(XLVIII) wa Mkutano wa 48 wa Kawaida wa Baraza Kuu wa Februari 2026.

2. **UNAREJELEA** ufafanuzi uliotolewa na Mkataba wa Vijana wa Afrika ambapo “kijana”, anatajwa kuwa mtu mwenye umri kati ya miaka 15 na 35.

3. **UNAPONGEZA** mpango huu wa Jamhuri ya Angola, ambao unachangia katika kukuza haki za wasichana na watoto wa Kiafrika.

4. **UNAAMUA** kurasimisha Jukwaa la Katiba kuhusu Haki na Dhamana za Wanawake na Watoto Vijana wa Kiafrika kama jukwaa la kubadilishana miongoni mwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika na **UNAIAGIZA** Kamisheni kutangaza shughuli na programu zinazohusiana na Jukwaa hili, litakalofanyika kila baada ya miaka miwili (Jukwaa la Kila Baada ya Miaka Miwili).

# UAMUZI KUHUSU BARAZA LA AMANI NA USALAMA KUHUSU SHUGHULI ZAKE NA HALI YA AMANI NA USALAMA BARANI AFRIKA,

**Mkutano Mkuu;**

1. **UNAPITISHA** Repoti ya Baraza la Amani na Usalama kuhusu Shughuli zake na Hali ya Amani na Usalama barani Afrika; na **UNAIPONGEZA** PSC kwa kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kuhimiza utawala bora, amani, usalama na utulivu barani na **UNAZIOMBA** Nchi zote Wanachama wa **UA** na Kamisheni kutekeleza maamuzi ya PSC; **PIA UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Gabon na Jamhuri ya Gine kutekeleza kwa wakati mipango yao ya kipindi cha mpito ambako kulisababisha kufanyika kwa chaguzi na kuondolewa kwa adhabu ya kusimamishwa kulikowekwa na PSC na **UNAZIKARIBISHA** Nchi mbili Wanachama kurejea kushiriki katika shughuli za Umoja; **UNAUNGA MKONO** mahitimisho ya Mkutano wa Mwaka wa 17 wa Kimkakati wa PSC wa Mapitio ya Mbinu Zake za Kazi uliyofanyika kuanzia tarehe 6 hadi 7 Novemba 2025 huko Abuja, Nigeria; Mahitimisho ya Semina ya Kumi na Mbili ya Viongozi wa Ngazi ya Juu kuhusu Amani na Usalama barani Afrika: Kuwasaidia Wanachama Wapya wa Afrika wanaoingia katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) (A3) Kujiandaa Kushughulikia Masuala ya Amani na Usalama Barani (Mkutano wa Oran), iliyofanyika kuanzia tarehe 1 hadi 2 Desemba 2025 huko Algiers, Algeria, na Mwongozo wa Mbinu za Kuimarisha Uratibu Kati ya Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika na Wanachama wa Afrika wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, uliopitishwa na Tamko la PSC 1289, mwezi Julai 2025; **AIDHA, UNAZIPONGEZA** A3+ zinazomaliza muda, yaani, Algeria, Sierra Leone na Guyana kwa juhudi zao zisizokoma katika kuhifadhi na kukuza maslahi ya Afrika ndani ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na **UNAZIPONGEZA** A3+ za sasa, yaani, DRC, Liberia, na Somalia kwa kutimiza jukumu lao katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na **UNAZIHIMIZA** kuendeleza juhudi za kutetea na kuhimiza maslahi ya bara yanayoongozwa na uamuzi wa Vyombo vya UA na misimamo ya pamoja ya Afrika, **NA UNAIOMBA** PSC iendelee kushughulikia changamoto zinazolikabili Bara kuhusu utawala, amani na usalama kulingana na Mkataba Uliyoanzisha Umoja wa Afrika na Protokali ya PSC;

<u>**Kuhusu Kanda ya Afrika ya Kati:**</u>

2. **UNASISITIZA** dhamira yake dhati ya kuheshimu haki ya kujitawala, uhuru, umoja, na kuheshimu mipaka ya DRC, ukisisitiza kwamba kanuni za kutoingiliwa, ujirani mwema, na ushirikiano wa kanda lazima viheshimiwe kikamilifu, na unalaani ukiukaji wowote ndani ya DRC; na pia, **UNALAANI** unyonyaji haramu wa maliasili unaofanywa na vikundi vyenye silaha na vya kigaidi, ikiwa ni pamoja na AFC\M23, kuanzishwa kwa utawala wake usio ramsi na kuzihimiza Mataifa yote ya Afrika na yale ya Umoja wa Mataifa kutotambua utawala huu usio rasmi; na pia, **UNAZISIHI** nchi jirani za DRC kuchangia kwa namna nzuri katika kutafuta amani katika eneo la Maziwa Makuu kwa ujumla na hasa mashariki mwa DRC;

3. **UNAKARIBISHA** kusainiwa kwa Mikataba ya Amani kulikofanywa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Jamhuri ya Rwanda, ikiwa ni pamoja na Mkataba wa tarehe 27 Juni 2025 na tarehe 4 Desemba 2025, huko Washington, D.C., pamoja na Makubaliano ya Doha yaliyohuishwa tarehe 15 Novemba 2025 kati ya Serikali ya DRC na AFC/M23; **UNAWAPONGEZA**, Mhe. Félix Tshisekedi, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, na Mhe. Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda, kwa kujitolea kwao kuweka misingi ya amani na utulivu wa kudumu nchini DRC; **PIA UNAPONGEZA** jitihada za Mhe. Rais Faure Gnassingbé, Rais wa Baraza la Jamhuri ya Togo, Mpatanishi katika mazingira ya ukosefu wa usalama wa muda mrefu mashariki mwa DRC na **UNAUNGA MKONO** kazi ya Jopo la Wajumbe watano Wawezeshaji. **UNAMUOMBA** Mpatanishi wa Umoja wa Afrika (UA) na Wawezeshaji kuongeza kasi ya ushiriki wao katika diplomasia ya usuluhishi nchini DRC na Nchi za eneo la Maziwa Makuu, kwa ushirikiano wa karibu na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Uchumi ya Mataifa ya Afrika ya Kati (ECCAS), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Mkutano wa Kimataifa kuhusu Eneo la Maziwa Makuu (ICGLR) na Umoja wa Mataifa, ili kudumisha kasi ya mazungumzo ya amani yanayoendelea na kusaidia kupunguza makali mgogoro; Pia, **UNAMUUNGA MKONO** Mhe. João Lourenço wa Angola kwa msaada wake usio na kikomo katika mifumo na taratibu za kupunguza migogoro.

4. **UNALAANI VIKALI** shughuli za AFC/M23 na wafuasi wake, pamoja na zile za Allied Democratic Forces (ADF), Kikosi cha Kidemokrasia cha Ukombozi wa Rwanda (FDLR) na vikundi vingine vyenye silaha na inadai kusitishwa mara moja kwa msaada huo na pande/vikosi vyote vya nje; huku **UKISISITIZA** kwamba hakuna suluhisho la kijeshi kwa mgogoro huo, **UNAZIOMBA SANA** pande hizo kuzipa kipaumbele njia za kidiplomasia na kisiasa na kutoa wito wa kusitisha mapigano mara moja na bila masharti, na kuondolewa kwa vikosi vyote vya kigeni visivyoidhinishwa, vikundi vyenye silaha na vyombo vya kigaidi vinavyofanya kazi nchini DRC; **UNASISITIZA HAJA** ya pande husika kuheshimu ahadi zilizotolewa chini ya makubaliano ya amani, pamoja na kulinda raia; **UNALAANI** unyonyaji haramu wa maliasili inaofanywa na vikundi vyenye silaha na vya kigaidi, na wafadhili wao, AFC/M23 kuanzisha utawala usio rasmi na **UNAZIOMBA** nchi jirani kutotambua utawala kama huo usio rasmi na unaziomba kuchangia kwa namna nzuri katika kutafuta amani kwenye Ukanda wa Maziwa Makuu kwa ujumla na hasa mashariki mwa DRC; **UNAZIOMBA** pande zote kuhakikisha utekelezaji kamili wa maamuzi ya UA na Mikataba ya Amani iliyosainiwa Washington DC na Doha na kusisitiza umuhimu wa ulinganifu na uhusishaji wa mbinu mbalimbali pamoja na mazungumzo imara yanayoongozwa na Afrika; **UNASISITIZA** kwamba amani ya kudumu, usalama na utulivu mashariki mwa DRC vinategemea uratibu wa mazungumzo ya amani na utekelezaji wa kuaminika wa Mikataba iliyosainiwa na heshima kwa uongozi wa Afrika; **UNASISITIZA MAELEKEZO** kwa Kamisheni kuendelea kutoa msaada unaohitajika kupitia Sekretarieti Huru ya Pamoja ya AU/EAC/SADC iliyoanzishwa hivi karibuni kwa Mfumo wa Uthibitishaji wa Pamoja Uliopanuliwa Plus (EJVM+) kulingana na Mfumo wa Uangalizi na Uthibitishaji wa Kusitisha Mapigano uliosainiwa Doha tarehe 14 Oktoba 2025, na kupeleka mtaalamu wa usalama Goma ili kuunga mkono jukumu lake kama

mwangalizi kulingana na Mkataba wa Mfumo wa Ushirikiano wa Amani na Usalama mashariki mwa DRC na Kanda;

5. **UNAMPONGEZA SANA** Mhe. Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda kwa kuitisha Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Mpango wa Usimamizi wa Kanda (ROM) wa Nchi Zilizotia Saini Mpango wa Amani, Usalama na Ushirikiano (PCSF) kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Kanda, uliofanyika Entebbe mwezi Desemba 21, 2025 na **UNAMUOMBA** Rais wa Jamhuri ya Uganda kuendelea kutoa msaada wake mzuri na uzoefu wake katika kutafuta suluhu za kudumu kwa mgogoro huu;

6. **UNATAMBUA KWA MASIKITIKO** kuongezeka kwa mipango ya amani na migogoro ya Afrika kuingiliwa kutoka nje ambako kunadhoofisha juhudi za UA na katika suala hili, **UNATOA WITO WA DHATI** wa uoanishaji wa mipango ya amani chini ya uongozi wa UA na kwa njia hiyo hiyo, **UNAZIOMBA SANA** Nchi Wanachama wa UA kujiepusha na kuchukua hatua yoyote ambayo itaihusisha migogoro ya Afrika na mataifa nje, na hivyo kudhoofisha UA katika juhudi zake za amani na kuongeza muda wa migogoro barani humo; **UNASISITIZA UMUHIMU** wa UA katika mazungumzo ya amani na usalama barani Afrika; **UNATAKA** ufikiaji salama na usiozuiliwa wa misaada ya kibinadamu kwa watu walioathiriwa na uhasama, ulinzi wa raia, na urejeshaji wa huduma muhimu huko Goma, maeneo mengine yaliyoathiriwa, na jiji la Uvira, na kusisitiza tena wito wake wa kufunguliwa mara moja kwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Goma ili kurahisisha utoaji wa msaada wa kibinadamu; **UNATOA WITO** wa kuondolewa mara moja na kikamilifu kwa AFC/M23 kutoka Uvira na maeneo yote yaliyokaliwa mashariki mwa DRC, **HUKU UKITAMBUA** tangazo lililotolewa tarehe 16 Desemba 2025 kuhusu kuondolewa kwa vikosi vya AFC/M23 kutoka Uvira; **UNAZIOMBA SANA** pande zote kuheshimu Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu (IHL) na Sheria ya Kimataifa ya Haki za Binadamu (IHRL), hasa, ulinzi wa makambi ya raia ambao ni wakimbizi wa ndani na maeneo ya matibabu na ulinzi wa walinda amani; na **UNASISITIZA** kwamba mashambulizi dhidi ya raia na walinda amani ni uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu **UNAWAONYA VIKALI** wahusika kwamba watawajibika kwa matendo yao.

7. **UNAPONGEZA** mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mkataba wa Kisiasa wa Amani na Maridhiano katika Jamhuri ya Afrika ya Kati (PAPR-CAR) na maendeleo chanya ya usalama na kisiasa katika nchi; **UNAWAZIHIMIZA** viongozi wa CAR kuendelea kuimarisha mafanikio haya kwa msaada wa UA, Jumuiya ya Uchumi ya Mataifa ya Afrika ya Kati (ECCAS) na Mkutano wa Kimataifa wa Kanda ya Maziwa Makuu (ICGLR) na pia kutekeleza, kwa msaada wa washirika wa kanda na kimataifa, Mpango wa Maendeleo wa Kitaifa (2024-2028); **UNAMPONGEZA** Mhe. Faustin-Archange Touadéra, Rais wa CAR kwa kuchaguliwa tena kwa mafanikio, na serikali na watu wa CAR kwa maandalizi mazuri ya uchaguzi wa wabunge na rais uliofanyika tarehe 28 Desemba 2025;

8. **UNATOA WITO** kwa serikali ya CAR kuchukua hatua zinazohitajika ili kukuza zaidi utawala jumuishi, kuimarisha taasisi za kitaifa na kudumisha utawala wa sheria, kwa lengo la kuunda mazingira yanayofaa kwa amani na utulivu endelevu; **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA, kwa kushirikiana na ECCAS, ICGLR na Umoja wa Mataifa, kuendelea kuunga mkono mazungumzo ya kisiasa na mazungumzo ya DDR yanayoendelea; **UNASISITIZA WITO** wa kuondolewa kabisa kwa vikwazo vya silaha vilivyowekwa kwa CAR, ili kuchangia katika kuimarisha uwezo wa ulinzi na usalama ili kushughulikia kwa ufanisi zaidi hali ya sasa ya usalama; na **UNAZIOMBA** A3 kushughulikia upitishaji wa msimamo wa pamoja katika jambo hili ndani ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa;

9. **UNAELEZA MASIKITIKO MAKUBWA** kuhusu hali ya kibinadamu iliyopo katika nchi, inayozidishwa na wimbi la wakimbizi kutokana na mgogoro unaoendelea nchini Sudani na, katika suala hili, **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama zinazoweza kufanya hivyo, kwa moyo wa mshikamano wa Afrika nzima, pamoja na washirika wa kimataifa, kuongeza haraka jitihada za misaada ya kibinadamu na ulinzi ili kuziba pengo la upungufu wa misaada ya kibinadamu na kuunga mkono utekelezaji kamili wa Mahitimisho ya Mkutano wa Kimataifa wa tarehe 27 Aprili 2022 uliofanyika Yaoundé, Kameruni kuhusu kutafuta masuluhisho ya kudumu kwa wakimbizi wa ndani kutokana na mgogoro katika CAR;

10. **UNAMPONGEZA** Mhe. Rais Brice Clotaire Oligui Nguema kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Jamhuri ya Gabon, na **UNAPONGEZA** mipango yenye mafanikio ya uchaguzi wa rais tarehe 12 Aprili 2025, ambao uliashiria kurejea kwa utaratibu wa kidemokrasia wa katiba na kukomesha hali ya mabadiliko ya serikali kinyume cha katiba; **UNAIHIMIZA** Gabon, kwa msaada wa Kamisheni ya UA chini ya usimamizi wa Programu ya Maendeleo ya AU/UN (UNDP) Eneo la Afrika katika Kusaidia Mchakato wa Mabadiliko (AFSIT), kuendelea kuongeza juhudi zake katika mageuzi ya kitaasisi ili kuhakikisha ujumuishaji katika shughuli zote za amani na maendeleo nchini Gabon na kuzuia kurudi tena kwa hali hiyo; na **PIA, UNAPONGEZA** juhudi za uwezeshaji zilizofanywa na MHE. Faustin-Archange Touadéra, Rais wa Jamhuri ya Afrika ya Kati, katika kuunga mkono mchakato wa mabadiliko nchini Gabon.

**<u>Kuhusu Kanda ya Afrika Mashariki:</u>**

11. **UNAELEZEA MASIKITIKO MAKUBWA KUHUSU** kuendelea kwa mgogoro nchini Sudan, kati ya SAF, na RSF ya kijeshi na washirika wao, hasa kuendelea kwa uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu, ukiukwaji mwingine mkubwa wa haki za binadamu, ukiukaji wa Sheria ya Kimataifa ya Haki za Binadamu (IHRL) na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu (IHL); **UNASISITIZA TENA WITO** kwa Pande zote kuanzisha usitishaji mapigano wa mara moja, wa kudumu na usio na masharti na kurudi kwenye mazungumzo yakifuatiwa na mazungumzo jumuishi ya kitaifa na mabadiliko ya kisiasa, na **UNASISITIZA** kwamba hakuna suluhisho la kijeshi linalofaa na endelevu kwa mgogoro wa sasa wa smapigano; **UNAELEZA UMUHIMU MKUBWA SANA** wa mazungumzo ya kisiasa yanayoongozwa na Wasudani na kumilikiwa na Wasudani, kama njia pekee inayowezekana kuelekea suluhisho la makubaliano na endelevu kwa mgogoro wa sasa; **UNASISITIZA TENA** ahadi ya UA ya kuhakikisha ulinzi, uhifadhi na kuheshimu

uhuru, umoja, na uadilifu wa eneo la Jamhuri ya Sudani, na utatuzi wa amani wa mgogoro wa sasa unaoangamiza;

12. **UNALAANI KWA MANENO MAKALI** shughuli za uhalifu dhidi ya raia wa Sudani zinazofanywa na pande hizo, hasa Kikosi cha Usaidizi wa Haraka cha Kijeshi (RSF) huko El Fasher na sehemu nyingine za nchi na **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA, kwa kushirikiana na wadau husika, kuharakisha kukamilika kwa mpango wa kuwalinda raia;

13. **UNALAANI VIKALI** na **KUKATAA KABISA** kuigawanya Sudani na uundaji wa serikali inayojulikana "serikali isiyo rasmi" uliyofanywa na Muungano wa Waanzilishi wa Sudani (Tasis) unaoongozwa na RSF na **KATIKA SUALA HILI UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama wote wa UA na jumuiya ya kimataifa kukataa majaribio yote ya kuipinga Sudani na kutoitambua "serikaliisiyo rasmi" yoyote na **UNASISITIZA** umuhimu wa kuhifadhi taasisi za Serikali;

14. **UNALAANI** aina zote za uingiliaji kutoka nje, na kusitisha misaada yote ya kijeshi na kifedha kwa pande zinazopigana; **UNASISITIZA** shutuma kali za UA na kukataa uingiliaji kati kutoka nje katika masuala ya ndani ya Sudani na kuomba Kamati Ndogo ya Vikwazo ya PSC, ikifanya kazi kwa ushirikiano na Kamati ya Intelijensia na Huduma za Usalama za Afrika (CISSA) na Mfumo wa Ushirikiano wa Polisi wa UA (AFRIPOL), kutambua wahusika wote wanaochochea mgogoro nchini Sudani na kupendekeza hatua zinazopaswa kuchukuliwa na PSC kuwadhibiti;

15. **UNAELEZA KWA MASIKITIKO KUHUSU** kutokuwa na uratibu kati ya mipango mingi ya amani nchini Sudani, na **UNATOA WITO** wa kuimarisha uratibu; **WAKATI HUO UKIMUOMBA** Mwenyekiti wa Kamisheni kuhuisha majukwaa ya uratibu wa kimataifa ya watendaji wote wanaohusika katika juhudi za amani nchini Sudani kwa lengo la kuratibu juhudi za amani katika mchakato mmoja unaolenga kutatua mgogoro nchini Sudani, chini ya usimamizi wa UA na Mamlaka ya Serikali ya Maendeleo ya Kanda (IGAD), na kwa ushirikiano na Umoja wa Mataifa, nchi jirani na Umoja wa Mataifa ya Kiarabu, pamoja na watendaji wa pande mbili, **UNAZIPONGEZA SANA** nchi jirani na Sudani kwa kuwakaribisha na kuwasaidia wakimbizi wa Sudani; na **UNAPONGEZA** kuanzishwa kwa Quintet chini ya uongozi wa Umoja wa Afrika ili kuongeza uratibu wa juhudi za upatanishi kuelekea kuitisha mazungumzo jumuishi kati ya Sudani na **UNAWAOMBA** Wanachama wa Quintet na wahusika wengine kuratibu jitihada za upatanishi kwa pamoja, kuzuia mwingiliano na kuhakikisha mbinu thabiti, kwa lengo la kuhitimisha suluhisho la mazungumzo na la kudumu kwa mgogoro wa sasa nchini Sudani.

16. **UNAPONGEZA** jitihada za Somalia za kuharakisha utekelezaji wa vipaumbele muhimu vya kitaifa, na kuanzisha mazungumzo ya mara kwa mara na yaliyopangwa kati ya Serikali ya Shirikisho la Somalia (FGS), Nchi Wanachama wa Shirikisho (FMS), vyama vya upinzani, na wadau wengine muhimu, ili kweka makubaliano kuhusu vipaumbele vya kitaifa ili kuimarisha amani, usalama, na utulivu nchini Somalia, hasa kadri uchaguzi

unavyokaribia; **UNASISITIZA UMUHIMU** kwa wadau wote muhimu wa Somalia kuwa wazi kwa mazungumzo jumuishi ya kisiasa yanayolenga kufikia makubaliano ya kuaminika na mapana ambayo ni muhimu katika kuendeleza mchakato wa ujenzi wa serikali unaoongozwa na Somalia na unaomilikiwa na Somalia; na **UNATOA WITO** kwa Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Somalia na uongozi wa Jubaland, Puntland na Somaliland, kushiriki katika mazungumzo ya wazi na jumuishi, kushughulikia tofauti zao kwa njia ya kujenga ili kukuza uaminifu, ushirikiano, na mshikamano katika ngazi za shirikisho na kanda na kuheshimi mipaka ya Somalia;

17. **UNAPONGEZA** mafanikio ya hivi karibuni dhidi ya Al-Shabaab na **UNAVIHAMASISHA** Vikosi vya Usalama vya Somalia (SSF), kwa msaada wa Tume ya Msaada na Utulivu ya Umoja wa Afrika nchini Somalia (AUSSOM) na washirika muhimu wa usalama, kuendeleza operesheni hizi ili kuharibu na hatimaye kushinda tishio la Al-Shabaab na makundi mengine ya upinzani yenye silaha; **UNASISITIZA HAJA** ya uzalishaji wa haraka wa nguvu, kuzaliwa upya na ujumuishaji ikiwa ni pamoja na kuajiri Vikosi vya Ulinzi wa Jamii/Mitaa (LDF), na vikosi vinavyohama, kushikilia maeneo, na kufanya shughuli kama sehemu ya mkakati ulio wazi, wa kushikilia na kujenga, kama hatua muhimu katika kuarifu mkakati wa kuondoka; **UNAKIPONGEZA** Kikosi cha AUSSOM na Nchi Zinazochangia Polisi (TCCs/PCCs), na SSF ya Somalia kwa kujitolea kwa muda mrefu; pamoja na washirika wa kanda, wa nchi, na wa kimataifa kwa michango yao muhimu kwa amani na utulivu nchini Somalia; **UNAREJELEA** matamko ya PSC kuhusu uanzishaji wa AUSSOM, **UNAKARIBISHA** utayari wa Misri kupeleka vikosi vyake na kusisitiza haja ya kuharakisha upelekaji wa askari kutoka Misri na urejeshaji wa vikosi vya Burundi na Kitengo cha Polisi Kilichoundwa Ghana (FPU). **UNAREJELEA WITO WAKE**, wa kuongeza nguvu za kupata ufadhili endelevu, unaotabirika, na unaobadilika na wa miaka mingi kwa AUSSOM; **UNAZIPONGEZA** nchi ambazo zimepeleka wanajeshi wa ziada nchini Somalia kwa msingi wa mpangilio wa nchi na nchi, kama hatua ya muda mfupi, hasa Jamhuri ya Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho ya Ethiopia, kwa ahadi zao endelevu na kujitolea katika kushughulikia hali ya usalama iliyopo nchini Somalia; na **UNAPONGEZA** hatua muhimu ya kihistoria katika kufanya uchaguzi wa kwanza wa kitaifa wa manispaa nchini Somalia mwezi Desemba 2025;

18. **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kuendelea na mazungumzo yake na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu utekelezaji wa Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa 2719 (2023) kuhusu AUSSOM; na katika suala hili **UNALIOMBA** Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuheshimu jukumu lake kuu la kudumisha amani na usalama wa kimataifa; **UNAWAHAMASISHA** washirika kuendelea kuunga mkono juhudi za UA, ikiwa ni pamoja na kuchangia moja kwa moja katika ufadhili wa AUSSOM na **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kuongeza juhudi zake za kutafuta fedha kwa ajili ya ziara za Tume ikiwa ni pamoja na matumizi ya riba iliyopatikana kutoka kwa Mfuko wa Amani wa UA; **UNAIELEKEZA** Kamisheni ya UA kuwasilisha kwa PSC ripoti ya kina kuhusu chaguzi zilizopendekezwa kwa mustakabali wa AUSSOM, ikiwa ni pamoja na athari zake kwa uendelevu wa Misheni na shughuli zake; na Kamisheni kuitisha mkutano wa haraka wa TCC/PCC za AUSSOM katika ngazi ya Wakuu wa Majeshi ya Ulinzi,

kuchunguza chaguzi hizo tatu, na kuwasilisha mapendekezo yao kwa ajili ya kujadiliwa na Mkutano Mkuu na kuripoti katika kikao kijacho cha Mkutano Mkuu;

19. **UNAPINGA** uingiliaji wowote kutoka nje unaolenga kuigawa Somalia na **UNALAANI** kitendo chochote au utambuzi haramu unaodhoofisha uhuru, umoja na mamlaka ya kieneo ya Somalia, na **UNATOA WITO KWA** jumuiya ya kimataifa kuthibitisha uhuru na umoja wa Somalia; **UNAPINGA** vitendo vyote haramu vinavyodhoofisha kanuni za kimataifa, na UNASISITIZA mshikamano ili kudumisha umoja wa Afrika, uhalali wa kimataifa, na utulivu wa kikanda;

20. **UNATAMBUA KWA MASIKITIKO MAKUBWA** changamoto zinazoendelea za kisiasa, kiusalama, kibinadamu, kijamii na kiuchumi na mabadiliko ya kisiasa nchini Sudani Kusini; **UNATOA WITO** wa kusitisha mapigano mara moja miongoni mwa pande zinazozozana na kurudia ombi la suluhisho la kisiasa kwa changamoto kupitia mazungumzo jumuishi ya kisiasa, maridhiano na ujenzi wa makubaliano, kwa mujibu wa Mkataba Ulioboreshwa wa Utatuzi wa Mgogoro katika Jamhuri ya Sudani Kusini (R-ARCSS); **PIA, UNATOA WITO** wa kufanya uchaguzi jumuishi, wa wazi na wa kuaminika kama ilivyopangwa kwa mwezi Desemba 2026 na kwa pande zote husika kuharakisha maandalizi kwa ajili ya uchaguzi huo; kipekee **UNATOA WITO** kwa Serikali ya Mpito Iliyoboreshwa ya Umoja wa Kitaifa (RTGoNU) kuweka kipaumbele katika uendeshaji wa uchaguzi na kutoa rasilimali za kutosha kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Tume ya Taifa ya Mapitio ya Katiba na Baraza la Vyama vya Siasa, ili kuwawezesha kufanya maandalizi kwa wakati na yanayotosheleza;

21. **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA, Umoja wa Mataifa, na Jumuiya ya Kimataifa kuunga mkono jitihada za RTGoNU katika shughuli hii; pamoja na RTGoNU kutafuta masuluhisho ya matukio ya mara kwa mara ya vurugu za kijamii, na **KATIKA MUKTADHA HUU**,**UNAWAHIMIZA** wadau katika sehemu zote za nchi zilizoathiriwa na vurugu za kijamii, kubuni michakato jumuishi ya kushughulikia vyanzo vikuu kupitia programu za DDR, na kuboresha usimamizi wa silaha ndogo ndogo, kwa lengo la kukuza amani na usalama wa kudumu; **UNAZIPONGEZA** UA, IGAD, na wadau wengine kwa jitihada za kupunguza mvutano katika nchini hiyo na kusisitiza haja ya kutoa uhuru wa wazi wa kushiriki kwa ajili ya kuandaa katiba na michakato ya uchaguzi, pamoja na kukamilisha mafunzo na kupelekwa kikamilifu kwa Kikosi Maalum cha Pamoja (NUF);

22. **UNASISITIZA UMUHIMU** wa kuongeza juhudi kati ya RTGoNU, Kamisheni, IGAD na Umoja wa Mataifa kwa ajili ya kutumika kikamilifu kwa Tume ya Ukweli, Maridhiano na Uponyaji (CTRH), Mamlaka ya Fidia na Malipo (CRA), na Mahakama Mseto kuhusu Sudani Kusini; **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama wa UA, Kamati ya Maalumu ya Viongozi Watano wa Ngazi ya Juu kuhusu Sudan Kusini (C5), Jukwaa la Washirika wa Troika na IGAD (IPF), pamoja na Umoja wa Mataifa, EU na jumuiya nzima ya kimataifa kuendelea kutoa msaada muhimu kuelekea utekelezaji kamili wa R-ARCSS; **UNAELEZEA MASIKITIKO YAKE** kuhusu hali mbaya ya kibinadamu nchini Sudani Kusini na ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya hatua za kibinadamu katika bara; na **UNATOA WITO**

kwa Kamisheni ya UA, Umoja wa Mataifa na Washirika wa Kimataifa, wakiwemo washirika nje ya kundi hilo, kuchangia zaidi katika kupunguza mateso ya watu wasio na uhakika wa chakula, waliopoteza makazi na wakimbizi nchini; **WAKATI HUO UNAWAHIMIZA** viongozi wa Sudani Kusini kufuata mbinu bora katika kupanua uchumi, kupitisha masuluhisho ya kudumu kwa masuala ya kibinadamu, na kutumia uwezo mkubwa wa nchi hiyo ili kuboresha viwango vya maisha;

23. **UNAMPONGEZA** aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Burundi, Mhe. Domitien Ndayizeye, Mwenyekiti wa Jopo la Wenye Busara na Mkuu wa Ujumbe wa Tume ya Viongozi wa Juu wa UA nchini Madagascar, na Mjumbe Maalumu wa Madagaska, Mhe. Mohamed Idriss Farah, kwa juhudi zao bila ya kuchoka katika kutatua mgogoro wa Madagaska kufuatia mabadiliko ya serikali yasiyofuata katiba mwezi Oktoba, 2025; **UNAWAHIMIZA** viongozi wa Madagaska kuchukua hatua za kujenga uaminifu na kujiamini ili kuwezesha uendeshaji wa mazungumzo ya kitaifa katika mazingira mazuri, kuheshimu ratiba iliyowekwa ya mpito kwa lengo la kurudi kwenye utaratibu wa kikatiba na utawala wa kidemokrasia; na kuweka rmipango inayojumuisha, yenye makubaliano na isiyo na upendeleo, yenye makataa mafupi, na sahihi, zinazohusiana na kipindi cha mpito na kurudi kwenye utaratibu wa kikatiba; **UNAMUOMBA** Mwenyekiti wa Kamisheni kuchukua hatua zinazohitajika ili kuunga mkono mchakato jumuishi na halali wa kurudi kwa utaratibu wa kikatiba wa Madagaska, ikiwa ni pamoja na kutoa msaada wa kitaalamu na kifedha kwa mazungumzo ya kitaifa, uandishi wa Katiba mpya, na uendeshaji wa uchaguzi kupitia Kituo cha Afrika cha AU/UNDP cha Kusaidia Mabadiliko Jumuishi (AFSIT); na **UNATOA WITO** wa uratibu ulioimarishwa wa jitihada pamoja na SADC na kanda nyingine na mashirika ya kimataifa.

**<u>Kuhusu Kanda ya Kaskazini mwa Afrika:</u>**

24. **UNASISITIZA UJENZI** ili kuendeleza kasi ya kidiplomasia iliyowekwa mwaka 2025 na kuendelea kuimarishwa kwa juhudi za UA nchini Libya kupitia Kamati ya Viongozi wa Ngazi ya Juu, ikizingatia kupitishwa kwa Mkataba wa Amani na Maridhiano kote nchini na wadau wa Libya; **UNASISITIZA HAJA** ya kuanzishwa upya kwa Kikosikazi cha Utatu cha UA-Umoja wa Ulaya (EU)-UN kuhusu Hali ya Wahamiaji na Wakimbizi nchini Libya ili kuimarisha uratibu wa kimataifa, kuimarisha ulinzi wa wahamiaji, na kuhimiza suluhisho endelevu kwa mgogoro, pamoja na kuwasaidia viongozi wa Libya katika jitihada zao za kulinda haki za wahamiaji;

25. **UNAPINGA KABISA NA KULAANI** aina yoyote ya uingiliaji kati wa kigeni katika masuala ya ndani ya Libya; na **UNATOA WITO** kwa pande zote za nje kuacha kuingilia masuala ya ndani ya Libya; **UNATAKA** kuondolewa mara moja na bila masharti kwa vikosi vyote vya kigeni, wapiganaji wa kigeni, na mamluki kutoka eneo la Libya; **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kwa kushirikiana na jumuiya ya kimataifa kuendelea kutoa msaada wa kisiasa kwa Tume ya Pamoja ya Kijeshi ya 5+5 (JMC) ili kutekeleza kikamilifu makubaliano ya kusitisha mapigano ikiwa ni pamoja na kuungana tena kwa taasisi za kijeshi na kuanzishwa na kutekelezawa kwa mchakato wa kupokonya silaha, kuondoa

vikosi vya kijeshi na kuunganishwa tena (DDR); **UNALIOMBA** Baraza la Rais kuunga mkono kazi ya 5+5 JMC na kufanya kazi kuelekea mageuzi ya sekta ya usalama, na kuunganisha taasisi zote za kitaifa ili kuziwezesha kushughulikia mahitaji ya watu wa Libya ipasavyo;

26. **UNASISITIZA ULAZIMA** wa kudumisha utulivu na kuondoa vikosi vyenye silaha visivyo vya serikali katika mji mkuu na kuunga mkono jitihada za kurejesha utulivu wa raia na kutetea haki za kujumuika kwa amani na uhuru wa kujieleza kulingana na vyombo vya UA na sheria za kimataifa, pamoja na ulinzi mzuri wa raia na kuwaonya wale wote waliohusika na mashambulizi ya hivi karibuni dhidi ya raia kwamba watawajibika kwa matendo yao; **UNASISITIZA** dhamira ya UA ya kuunga mkono mchakato jumuishi wa kisiasa unaoongozwa na Libya na unaomilikiwa na Libya, ikiwa ni pamoja na maridhiano ya kitaifa, unaowezeshwa na Umoja wa Afrika kwa ushirikiano na Umoja wa Mataifa; **UNATOA WITO ZAIDI** wa kuimarishaji zaidi wa taasisi zote halali za Libya, ili kuunda mazingira mazuri ya kufanikiwa kwa kuandaa uchaguzi jumuishi, unaoaminika na wa wazi wa Rais na Wabunge nchini; **UNAMPONGEZA SANA** Mhe. Denis Sassou Nguesso, Rais wa Jamhuri ya Kongo na Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi wa Ngazi ya Juu ya UA kuhusu Libya, kwa kazi kubwa ambayo iliandaa Mkataba wa Maridhiano ya Libya uliyosainiwa Addis-Ababa tarehe 14 Februari 2025; UNAREJELEA kutiwa saini kwa Mkataba wa Amani na Maridhiano ya Kitaifa wa Libya na pande husika Februari 2025 ; na **UNAPONGEZA** kutiwa saini kwa Hati ya Maridhiano ya Kitaifa kulikofanywa na na Rais wa Baraza la Rais, Mohamed al-Manfi kama hatua muhimu kuelekea kufikia amani ya kudumu.

27. **UNATOA WITO** kwa pande zote zilizotia saini Mkataba wa Amani na Maridhiano ya Kitaifa kufuata masharti ya Mkataba huo, kwa kuunga mkono utekelezaji wake kamili na Baraza Kuu la Amani na Maridhiano ya Kitaifa, linalotokana na Mkataba huo, kutekeleza jukumu lake katika kutafuta mchakato wa maridhiano ya kitaifa unaojumuisha pande zote, bila kutengwa, kwa kuzingatia kanuni za haki, usawa na fidia;

28. **UNATARAJIA** mafanikio ya juhudi za maridhiano ya kitaifa miongoni mwa Walibya, kwa msaada wa Umoja wa Afrika, kurejesha imani katika mchakato wa kisiasa unaolenga kufanya uchaguzi mkuu ambao utamaliza awamu ndefu za mpito za miaka kumi na tano (15) iliyopita;

**<u>Kanda ya Kusini mwa Afrika:</u>**

29. **UNAIPONGEZA** Serikali ya Msumbiji kwa jitihada zinazoendelea katika kushughulikia hali ya usalama huko Cabo Delgado pamoja na Rwanda, Afrika Kusini na Tanzania kwa msaada wao wa pande mbili; na **UNAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuendelea na ushirikiano wake na Serikali ya Msumbiji, ikiwa ni pamoja na kutoa msaada unaohitajika katika mapambano dhidi ya magaidi huko Cabo Delgado, pamoja na kusaidia katika utoaji wa msaada wa kibinadamu kwa wakimbizi wa ndani na katika

utafutaji wa rasilimali ili kuiwezesha Serikali ya Msumbiji kukabiliana haraka na athari na kuimarisha amani katika muktadha wa ujenzi na maendeleo baada ya migogoro;

**Kanda ya Afrika Magharib:**

30. **UNAMPONGEZA** Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika anayemaliza muda wake mwaka 2025, Mhe. Manuel João Lourenço, Rais wa Jamhuri ya Angola, kwa juhudi zake za kukuza utulivu katika Sahel, hasa uteuzi wa Mhe. Évariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi, kuwa Mjumbe Maalumu wa UA katika eneo la Sahel, **HUKU UKIKARIBISHA** uteuzi wa Dkt. Mamadou Tangara, aliyekuwa waziri nchi Gambia, kuwa Mwakilishi Maalumu wa Mwenyekiti wa Tume ya Sahel na Mkuu wa MISAHEL, na **UNAWAHIMIZA** viongozi wote wawili kuimarisha ushirikiano wa bara na wadau wote katika kanda, pamoja na kuongoza msaada mpya wa kidiplomasia na kimkakati wa UA; **UNAITAMBUA** Kamisheni ya UA kwa kuanzisha jukwaa la mazungumzo na mshikamano wa juhudi kati ya UA na nchi zilizo katika kipindi cha mpito;

31. **UNASISITIZA** kuimarisha ushirikiano wa kanda kwa ajili ya ushughulikiaji thabiti na wa pamoja wa usalama kwa kusisitiza umuhimu wa uratibu ulioimarishwa kati ya Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Uchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS), na Umoja wa Mataifa ili kuoanisha mikakati ya kupambana na ugaidi katika eneo lote la Sahel, ikiwa ni pamoja na kupanga mifumo ya tahadhari ya mapema, kuimarisha shughuli za pamoja, na kupanua mifumo ya upatanishi katika eneo lote ili kushughulikia mvutano wa kisiasa unaochochea ukosefu wa usalama; **UNAIHAMASISHA** ECOWAS, kuharakisha kupelekwa kwa kikosi chake cha usalama cha kanda chenye watu 5,000, kwa lengo la kuziba haraka upungufu mkubwa wa usalama katika Sahel, ili kupunguza vurugu zinazoongezeka, kuongezeka kwa makundi ya kigaidi, na kudhoofika kwa uwezo wa usalama wa taifa kote Mali, Burkina Faso, na Niger;

32. **UNAHIMIZA** uratibu ulioimarishwa kati ya UA, ECOWAS, nchi zilizoko Sahel, washirika wa kimataifa ili kuhakikisha ushirikiano, utafutaji wa rasilimali, na mfumo mmoja wa amri—na hivyo kuongeza ufanisi na uhalali wa juhudi za kupambana na ugaidi na utulivu wa kanda; **UNATHAMINI** maendeleo ya Mpango wa Usalama wa Kanda wa Accra, kama michakato muhimu wa ufufuaji, kwa kuzingatia mazingira ya tishio yanayobadilika kwa kasi katika Sahel na kuenea kwake katika pwani ya Afrika Magharibi;

33. **UNASISITIZA UMUHIMU** wa kuimarisha mifumo hiyo ili kuhakikisha ubora wake, ushirikiano na uwezo wa kuzuia katika kushughulikia ugaidi wa mipakani, mitandao ya biashara haramu ya binadamu, na udhaifu wa ngazi ya jamii; **UNASISITIZA KUZINGATIA** kuimarishwa kwa ushirikiano wa kidiplomasia wa ngazi ya juu na nchi za Sahel zinazopitia mabadiliko ya kisiasa, kwa lengo la kujenga upya imani ya pande zote, kuwezesha mazungumzo jumuishi, na kuunga mkono michakato ya mpito inayoaminika na ya muda inayoimarisha utulivu, utaratibu wa kikatiba, na ushirikiano wa kanda;

34. **UNAWAHIMIZA** wadau nchini Burkina Faso, Niger, na Mali kushiriki katika mazungumzo yenye kujenga, kukuza utawala jumuishi na kuhakikisha mabadiliko ya

haraka ya kisiasa ili kushughulikia changamoto ambazo Nchi za Sahel zinakabiliwa nazo; na **UNASISITIZA WITO WAKE** kwa nchi za eneo hilo kufanya kazi ili kukuza utulivu, utaratibu wa kikatiba na maendeleo endelevu ili kutimiza matarajio ya watu wa eneo hilo; **UNAZIOMBA KWA DHATI** nchi zilizo katika mabadiliko ya kisiasa kupitisha mipango ya mabadiliko inayoonekana na kwa wakati, ikifuata mbinu jumuishi, za uwazi na za makubaliano; **UNAWAOMBA** viongozi wa mpito kuweka maslahi ya juu ya nchi zao na watu wao juu ya yote, na kuhakikisha utekelezaji makini wa mipango yao ya kipindi cha mpito, ndani ya muda uliokubaliwa, na kuendesha kamati za pamoja za ufuatiliaji wa mabadiliko katika nchi zao;

35. **UNAELEZEA MASIKITIKO YAKE** kuhusu mtiririko haramu wa fedha na uhalifu mwingine wa kifedha, ikiwa ni pamoja na wizi wa sarafu za dijitali unaofanywa na wahusika wa mtandao wenye nia mbaya; na UNAIOMBA Kamisheni ya UA, kwa kushirikiana na CISSA, AFRIPOL na Kituo cha Kupambana na Ugaidi cha Umoja wa Afrika (AUCTC), kuchunguza kwa kina janga la mtiririko haramu wa fedha, ikiangazia mitandao na kutoa taarifa kwa PSC haraka iwezekanavyo; **UNATOA WITO** kuanzishwa kwa kikosikazi cha bara kuhusu ufadhili haramu, ambacho pamoja na mambo mengine, kitahakikisha ufuatiliaji wa mitandao ya hawala/pesa za simu inayotumiwa na vikundi na mitandao ya kigaidi yenye msimamo mkali na uzinduzi wa protokali ya tahadhari ya mapema ya mipaka kwa ajili ya uhamisho unaotiliwa shaka unaohusishwa na kanda zinazoungana; **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama kuendelea kuimarisha taasisi za umma, kukuza ushiriki wa raia, ujumuishaji wa jamii, na kushughulikia malalamiko halali ya idadi ya watu miongoni mwa mengine kwa kutekeleza programu za uwezeshaji wa kijamii na kiuchumi ambazo zinalenga wanawake na vijana kama wadau muhimu katika kukuza amani, usalama na utulivu;

36. **UNAMPONGEZA** Mhe. Mamadou Doumbouya kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Jamhuri ya Gine, na watu wa Gine kwa kuandaa kwa mafanikio uchaguzi wa rais tarehe 28 Desemba 2025, ambao uliashiria kurudi kwa utaratibu wa kidemokrasia unaofuata katiba na kukomesha mabadiliko ya serikali kinyume cha katiba; **UNAIHIMIZA ZAIDI** Guinea, kwa msaada wa Kamisheni ya UA chini ya usimamizi wa AU/UNDP *Africa Facility to Support Inclusive Transitions* (AFSIT), kuendelea kuimarisha juhudi zake katika mageuzi ya kitaasisi ili kuhakikisha ujumuishaji katika shughuli zote za amani na maendeleo nchini Gine na kuzuia kurudi tena; **UNASISITIZA WITO** wa ushirikiano wowote wa usalama wa nje unazingatia kikamilifu viwango vya Afrika na kimataifa kuhusu haki za binadamu, uwazi, na uwajibikaji; **UNAIPONGEZA** ECOWAS kwa juhudi zake za kuanzisha Kikosi cha Kupambana na Ugaidi cha Kikanda kama kikosi cha kupambana na ugaidi cha kikanda, ikiwa ni pamoja na juhudi zinazofanywa katika kufafanua mikakati ya ufadhili kwa kikosi hicho na Mawaziri wa Fedha na Ulinzi wa Nchi Wanachama wa ECOWAS;

37. **UNAKIPONGEZA** Kituo cha Taifa cha Kupambana na Ugaidi cha Nijeria (NCTC), na Tume ya ECOWAS, kwa kuitisha "Mkutano wa Kanda wa Kupambana na Vikundi Vinavyoibuka vya Magaidi na Kuimarisha Usalama Endelevu katika Kanda ya ECOWAS

na Sahel", kama sehemu ya matukio ya kuadhimisha Jubilei ya Dhahabu ya ECOWAS iliyoandaliwa Abuja, mwezi Septemba, 2025, na **UNATOA WITO** kwa nchi zilizo katika kanda hiyo kutekeleza matokeo ya mkutano huo.

38. **UNALAANI VIKALI** mapinduzi ya kijeshi nchini Guinea-Bissau; **UNATAKA** kuachiwa mara moja na bila ya masharti kwa maofisa wote wa uchaguzi waliokamatwa na wanasiasa wengine wote na wale walioshiriki katika uchaguzi; **UNAWAOMBA SANA** viongozi wa kijeshi nchini Guinea-Bissau kuheshimu sheria za nchi, na matakwa ya watu, na kujiepusha na kuingiliwa zaidi katika michakato ya kisiasa nchini; na **UNAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kwa ushirikiano wa karibu na ECOWAS, Jumuiya ya Nchi Zinazozungumza Kireno (CPLP) na washirika wengine wote wa wa kimataifa kutoa msaada unaohitajika kwa Guinea-Bissau ili kuhakikisha kurejea kwa haraka kwa utaratibu wa kikatiba, ikiwa ni pamoja na kuandaa mazungumzo ya kitaifa na mageuzi ya taasisi za serikali kuelekea kuanzisha umoja wa kitaifa kwa ajili ya utatuzi wa amani wa mgogoro katika nchi;

39. **UNALAANI VIKALI** jaribio la mapinduzi nchini Benin mwezi Desemba 2025; na **UNAWAOMBA** viongozi wa Benin kuwawajibisha wahusika wa jaribio la mapinduzi nchini Benin kwa matendo yao kulingana na sheria za kitaifa; **UNASISITIZA UMUHIMU** wa kudumisha demokrasia, utawala bora, uhalali wa kikatiba na utawala wa sheria katika Nchi Wanachama kama nguzo za msingi za amani ya kudumu, usalama, utulivu na maendeleo; na **UNASISITIZA** kudumisha umakini mkubwa na kuendelea kufanya kazi na ECOWAS katika kufuatilia kwa karibu mabadiliko ya hali ilivyo katika eneoi;

**Kuhusu Utawala na Kuzuia Migogoro**

40. **UNAZIPONGEZA** Nchi zote Wanachama zilizofanya uchaguzi wa kidemokrasia kwa mafanikio mwaka 2025, hasa zile zilizoonyesha uhamishaji mzuri wa madaraka na kuhakikisha urejeshaji wa amani wenye utaratibu wa kikatiba kulingana na mifumo yao ya kitaifa; **UNAZIPONGEZA** Nchi zote Wanachama kwa juhudi zao zinazoendelea za kuendeleza utawala wa kidemokrasia, kuimarisha umiliki wa kitaifa wa michakato ya uchaguzi kupitia mageuzi endelevu ya kitaasisi, na kushikilia kanuni za uwazi, ujumuishaji, na uadilifu zilizoainishwa katika Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala; **UNAZIHAMASISHA** Nchi Wanachama zaidi kuanzisha hatua zinazokuza ushiriki mzuri wa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu katika michakato ya kisiasa na uchaguzi;

41. **UNALAANI** kuibuka tena kwa mapinduzi ya kijeshi katika mwaka huo na **UNATHIBITISHA** tena dhamira ya UA ya kukuza na kutetea katiba na kuimarisha utawala wa kidemokrasia katika Nchi zote Wanachama; na **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama wa UA kuendelea kuimarisha taasisi za utawala, kuharakisha programu za maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kushughulikia kikamilifu sababu za msingi za kimuundo na vichocheo vya Mabadiliko ya Serikali Kinyume cha Katiba, ikiwa ni pamoja na upungufu wa utawala, ukiukwaji wa haki za binadamu na kuongeza maradufu

uwekezaji katika miundombinu kwa ajili ya amani, na pia kushughulikia kwa njia chanya zaidi malalamiko halali ya watu katika kukuza uhusiano kati ya amani, usalama, utulivu na maendeleo;

42. **UNASISITIZA TENA** maadili yote ya pamoja ya UA na hati mbalimbali za kisheria, hususan Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala (ACDEG) (2007), ambao umehudumia kiwango muhimu cha bara kuhusu utawala wa kidemokrasia na uchaguzi tangu kupitishwa kwake; na **KWA KUTAMBUA** ukweli kwamba mwaka 2027 utakuwa ni miaka 20 ya ACDEG, Mkutano Mkuu unaweza kuzingatia kutangaza kaulimbiu ya UA ya 2028 kama "Mwaka wa Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala barani Afrika;" **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuwahusisha kikamilifu raia, hasa wanawake na vijana, kupitia mikakati na hatua zinazolenga kuhakikisha ushiriki wa watu wenye maana kulingana na ACDEG na Mkataba wa Vijana wa Afrika.

43. **UNAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuongeza jitihada zake za kutafuta rasilimali za ziada ili kutoa msaada wa kitaalamu kwa wakati unaozingatia muktadha na katika demokrasia na uchaguzi unaotolewa kwa Nchi Wanachama; **UNAHAMASISHA** kupelekwa mapema kwa timu za kitaalamu na Wakuu wa Tume za Misheni wakati wa awamu ya kabla ya uchaguzi wa mzunguko wa uchaguzi, kama njia ya kuimarisha diplomasia ya kuzuia, kuhakikisha utambuzi wa mapema wa changamoto zinazoweza kutokea, na kuunga mkono utatuzi wake kabla hazijaongezeka; **UNASISITIZA HAJA** ya kuimarisha zaidi Mfumo wa Tahadhari ya Mapema ya Bara ili kufuatilia michakato ya uchaguzi katika Nchi Wanachama kwa lengo la kuongeza zaidi uwezo wa PSC kuzuia migogoro na hali za migogoro zinazohusiana na uchaguzi; na **UNAVIHIMIZA** vyombo vya habari na mashirika ya kiraia kuendelea kutimiza jukumu la kujenga katika kuhakikisha uaminifu na uadilifu wa uchaguzi katika Nchi Wanachama na kujiepusha na kuchochea changamoto zinazohusiana na uchaguzi na kuchochea vurugu;

44. **UNAIELEKEZA** Kamisheni ya UA kudumisha kuendeleza ujumuishaji wa haki za binadamu ndani ya mifumo ya amani na usalama wa bara, kwa kuharakisha kupitishwa na kutekelezwa kwa Kanuni na Miongozo ya Umoja wa Afrika kuhusu Biashara na Haki za Binadamu (AUPG-BHR) na kuunga mkono utekelezwaji wa Taasisi ya Haki za Binadamu ya Afrika (PAHRI); **UNAIOMBA** Kamisheni kuongeza uwezo wa kujenga Mtazamo wa Haki za Binadamu (HRBA) kwa Tahadhari ya Mapema katika Nchi Wanachama, ikiwa ni pamoja na kupitia utekelezaji wa Vitengo vya Hatua za Kinga (PACs), matumizi ya viashiria sanifu vya HRBA, na msaada unaolenga Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu na Mifumo ya Kitaifa ya Tahadhari ya Mapema, **PIA UNAIOMBA** Kamisheni kuimarisha uhimilivu wa kitaasisi, diplomasia ya kuzuia, na juhudi za kuzuia migogoro nyeti kwa haki kulingana na Ajenda ya 2063 na mpango wa "Kuacha Mapigano"; na **UNATOA WITO** wa kuongeza rasilimali fedha na rasilimali watu ili kusaidia mipango ya haki za binadamu katika ngazi za bara, kanda na taifa ili kuhakikisha utekelezaji wa dira ya Muongo wa Haki za Binadamu wa AU.

45. **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA na Bodi ya Ushauri ya UA kuhusu Rushwa (AUABC) kuongeza juhudi za utekelezaji kuhusu Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu Urejeshaji wa Mali (CAPAR) na kuziunga mkono Nchi Wanachama kupitia Mfumo wa Utekelezaji wa CAPAR, Mfumo wa Mfano wa Kurejesha Mali za Afrika kati ya UA na nchi zisizo za Afrika; **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kuendelea na ushirikiano na Kikosikazi cha Kupambana na Rushwa cha G20 (ACWG) pamoja na kuzingatia maslahi na misimamo ya Nchi Wanachama; na **UNATOA WITO** kwa washirika wa kimataifa kukubaliana kuhusu ratiba ya uwazi na ufanisi ya kutafuta na kurejesha mali zilizoibiwa Afrika kwa heshima ipasavyo kwa uhuru wa Nchi na maslahi yao ya kitaifa;

46. **UNATOA WITO** kwa Kamisheni ya UA kubainisha na kutumia rasilimali za UA katika kutetea utashi wa kisiasa, pamoja na kufuatilia na kuongoza utekelezaji wa michakato ya Mageuzi ya Sekta ya Usalama (SSR) katika Nchi Wanachama, kwa usaidizi wa Mifumo muhimu ya Amani na Usalama wa Afrika (APSA), ikiwa ni pamoja na Jopo la Watu Mashuhuri; **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama wa AU kubuni mbinu mahususi zinazozingatia mazingira ili kuhakikisha michango endelevu ya SSR, ikiwa ni pamoja na amani endelevu, ujenzi mpya na maendeleo baada ya migogoro, pamoja na mipango ya ujenzi wa amani; **UNAZIOMBA** REC/RM kuandaa na kutekeleza sera na programu za SSR zinazoendana na Mfumo wa Sera wa SSR kwa msaada wa Kamisheni ya UA;

47. **UNAIELEKEZA ZAIDI** Kamisheni, ikishirikiana na RECs/RMs, kuzisaidia Nchi Wanachama katika kutumia matokeo ya utafiti wa "Ushirikiano kati ya Mikataba ya Kudhibiti Silaha za Kanda za Afrika na Mfumo wa Kimataifa wa Usimamizi wa Silaha za Kawaida (GFA)" ili kupitisha msimamo wa pamoja katika maandalizi ya Mkutano wa Mataifa utakaofanyika New York mwaka 2027; **PIA UNAIAGIZA** Kamisheni kufanya kazi na RECs/RMs kwa mamlaka ya utawala, amani na usalama, ili kusaidia maeneo ambayo bado hayajafanya hivyo ili kuendeleza Mipango yao ya Utekelezaji ya Kanda ya Kusitisha Mapigano; na **UNAHIMIZA** uandaaji wa msimamo ya pamoja ya Afrika kuhusu sheria ili kuongoza ushiriki wa bara katika mazungumzo ya kimataifa yanayoendelea;

48. **UNAIPONGEZA** Kamisheni ya UA kwa kuzindua Programu ya Kirafiki ya Upokonyaji Silaha na Kutosambaza Silaha na kuiomba Kamisheni iimarishe utoaji na kupanua ushiriki wa Programu ya Ushirika, ikiwa ni pamoja na kutengeneza mtaala wa kina na kutafuta rasilimali fedha ili kuhakikisha uendelevu wake;

49. **UNAPONGEZA** operesheni ya PSC- iliyoanzisha Kundila Ushauri la UA kuhusu Akili Mnemba katika Amani, Usalama na Utawala ili kutekeleza uamuzi wa PSC na **UNAWAOMBA** Wajumbe wa Kundi hilo kuharakisha utafiti na uandaaji wa Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu Akili Mnemba na athari zake kwa amani, usalama, demokrasia na maendeleo barani Afrika kwa kushauriana na Nchi zote Wanachama wa UA na **UNAIELEKEZA** Kamisheni ya UA kusaidia uwezo wa Nchi Wanachama katika kujumuisha usalama wa mtandao na AI katika mikakati ya kujenga amani na utawala.

50. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama ambazo bado hazijafanya hivyo kuidhinisha Mkataba wa Afrika kuhusu Ulinzi, Usalama, na Maendeleo ya Baharini, na **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA, kwa kushirikiana na RECs/RMs na Mashirika ya Serikali, kuanzisha Jukwaa la Walinzi wa Pwani wa Afrika ili kuendeleza juhudi zilizoratibiwa kwa ajili ya ulinzi na usalama wa baharini kote Afrika.

**Kuhusu Upatanishi na Mazungumzo:**

51. **UNASISITIZA TENA** jukumu kuu la Jopo la Watu Mashuhuri kama utaratibu mkuu wa Umoja wa Afrika wa diplomasia ya kuzuia, kwa mujibu wa Ibara ya 11 ya Protokali Inayohusiana na Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama, na **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutumia huduma zake za diplomasia ya kuzuia hasa, utendaji mzuri na kukubali ushauri wake kuhusu mabadiliko ya kisiasa, tathmini ya mabadiliko ya serikali yanayoweza kutokea kinyume cha katiba, yakileta wasiwasi wamuchaguzi, unaozingatia umiliki wa kitaifa; **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kuendelea kuunga mkono utumaji wa Jopo la Watu mashuhuri kwa wakati unaofaa na mahususi, ikiwa ni pamoja na ushiriki ulioanzishwa vya kutosha kabla ya hatua muhimu za kisiasa au za uchaguzi, pamoja na ushiriki endelevu wa ufuatiliaji;

52. **UNAUNGA MKONO** kuendelea kuimarishwa kwa ushirikiano kati ya Jopo la Watu Mashuhuri na mifumo kama hiyo katika ngazi za kanda na kanda ndogo, ikiwa ni pamoja na kupitia Mtandao wa PanWise, na kuhimiza kujihusisha kwa pamoja katika diplomasia ya kuzuia ambapo hatua zilizoratibiwa zinatathminiwa ili kuongeza thamani na zinafanywa kwa kushauriana na Nchi Wanachama na REC/RM husika ambazo zina mamlaka ya utawala, amani na usalama;

53. **UNAMPONGEZA** Mwakilishi Mkuu wa UA kwa Pembe ya Afrika, Mhe. Olusegun Obasanjo, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria na Wajumbe wa Jopo la Ngazi ya Juu la UA, yaani, Mhe. Uhuru Kenyatta, aliyekuwa Rais Jamhuri ya Kenya, na Mhe. Dkt. Phumzile Mlambo-Ngcuka, aliyekuwa Naibu Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini na pia Mjumbe wa Jopo la Watu Mashuhuri, kwa jitihada zao; **UNAHAMASISHA** Jopo kuendelea kushirikiana na Pande husika na washirika wa kimkakati ili kuunga mkono utekelezaji wa Mkataba wa Kukomesha Uadui Kabisa (CoHA), hasa katika maeneo kama vile DDR na kurejea kwa wakimbizi wa ndani (IDP) na **UNATAMBUA** jukumu muhimu linalotekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho ya Ethiopia katika utekelezaji wa CoHA;

**Kuhusu Operesheni za Misaada:**

54. **UNAPITISHA** Mkataba wa Makubaliano kati ya Umoja wa Afrika na Jumuiya za Uchumi za Kanda na Taratibu za Kanda za Matumizi ya Kikosi cha Akiba cha Afrika; **UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama, na RECs/RMs, pamoja na msaada wa Kamisheni ya UA, kwa kujitolea kwao kuendelea na michango ya pamoja katika utekelezaji wa Operesheni za Kusaidia Amani (PSOs) zinazosimamiwa na UA na Kikosi cha Akibai cha

Afrika (ASF); na **UNAIAGIZA** Kamisheni kuharakisha utiaji saini na utekelezaji wa Mkataba wa Makubaliano kati ya Umoja wa Afrika na Jumuiya za Uchumi za Kanda na Mifumo ya Kanda ya Matumizi ya Kikosi cha Akiba cha Afrika na kutoa ripoti mara kwa mara kuhusu hali ya utekelezaji wake;

55. **UNAIDHINISHA** kukamilika kwa Mapitio ya Mkakati ya ASF na **KUIELEKEZA** Kamisheni kuharakisha utekelezaji wa mapendekezo yake, kwa msisitizo katika utayari, kubadilishana taarifa, na mifumo endelevu ya ufadhili; **UNAZIHAMASISHA** Nchi Wanachama kuunga mkono uanzishwaji wa Taratibu za UA na C3IS za Kupeleka Vikosi na Vifaa, ikiwa ni pamoja na kupitia utoaji wa mali, utaalamu, na michango kwa mifumo ya pamoja ya kuwezesha ya AU-UN; **UNASISITIZA TENA UMUHIMU** wa kufuata sheria na uwajibikaji kama msingi wa uaminifu na uhalali wa PSO za UA, na kuhimiza kuendelea kujenga uwezo wa T/PCC na RECs/RM katika suala hili; **UNATOA WITO** kwa washirika kuongeza msaada wa kitaalamu na kifedha kwa shughuli zinazoagizwa na UA chini ya kanuni za umiliki na kugawana majukumu katika Afrika;

56. **UNATAMBUA** maendeleo yaliyopatikana katika kufungwa kwa Misheni ya Mpito ya UA nchini Somalia (ATMIS) na kuanzisha AUSSOM, na **UNAIPONGEZA** Kamisheni na T/PCC kwa kuhakikisha mwendelezo wa uendeshaji na uhifadhi wa mafanikio ya usalama yaliyopatikana kwa shida nchini Somalia; **UNAIAGIZA** Kamisheni kuendelea kuimarisha uratibu kati ya mihimili ya kisiasa, kiuendeshaji, na lojistiki ili kuhakikisha mipango thabiti, usambazaji vikosi, na uendelevu wa shughuli za amani za UA barani kote; na **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kuendelea kushirikisha Umoja wa Mataifa kwa ajili ya kutekeleza na kutumia azimio UNSC 2719 na kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya AUSSOM, ikiwa ni pamoja na matumizi ya Mfuko wa Amani wa UA;

57. **UNATAMBUA KWA MASIKITIKO MAKUBWA** ya kuondolewa kwa Jamhuri ya Niger kutoka nchi zinazochangia wanajeshi (TCCs) na athari zake katika shughuli za MJNTF na kuwatia moyo Wanachama wa MNJTF waliobaki kudumisha mshikamano na umoja wa kusudi katika mapambano dhidi ya kundi la kigaidi la Boko Haram ili kuepuka ombwe lolote la usalama na kuhifadhi kasi ya sasa na mafanikio yaliyopatikana hadi sasa; **UNAIOMBA** LCBC kuendelea kushirikiana na Jamhuri ya Niger ili kuhakikisha inarudi kikamilifu katika MNJTF; **PIA UNAWAOMBA** washirika wa kimataifa kuiunga mkono MNJTF kwa vifaa vya kisasa na lojistiki pamoja na kuongeza uwezo dhidi ya magaidi wa Boko Haram;

58. **UNAPONGEZA** mafanikio yaliyoletwa na Nchi Wanachama wa LCBC katika kurekebisha Mkakati wa Kanda wa Utulivu, Mkakati wa Urejeshaji na Uhimilivu kwa Maeneo Yaliyoathiriwa na Boko Haram kuanzia 2026 hadi 2030, na pia uhimilivu wa watu katika maeneo yaliyoathiriwa na mashambulizi ya kigaidi ya Boko Haram; **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama wa LCBC kuongeza jitihada zao maradufu katika kutekeleza Mkakati wa Kanda Uliorekebishwa; **UNATHAMINI** Umoja wa Mataifa na EU kwa msaada wao katika eneo hilo; na **HUKU UKITOA WITO** kwa washirika wengine wa pande mbili na

pande nyingi kuongeza msaada wao kuelekea utekelezaji kamili wa Mkakati wa Kanda Uliorekebishwa na ili kuhifadhi mafanikio ya usalama yaliyopatikana hadi sasa na kuboresha hali ya maisha ya wakazi wa kanda hiyo;

59. **UNATOA PONGEZI** kwa Serikali ya Nigeria kwa kuandaa Jukwaa la Pili la Uzoefu Uliyopatikana (LLF) kuhusu Operesheni ya Kusaidia Amani ya UA na Kikosi cha Akiba cha Afrika na kwa kujitolea kuwa mwenyeji wa Jukwaa la Tatu la LLF, huko Abuja, Nigeria mwaka 2027; na **PIA IUNAIELEKEZA** Kamisheni ya UA kutekeleza Mkataba wa Makubaliano wa pande mbili (MoU) uliosainiwa na Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria kuhusu utoaji wa usafiri wa kimkakati wa baharini ili kurahisisha usafirishaji wa vifaa kutoka Kituo cha Usafirishaji cha Bara (CLB) hadi kwenye vituo vya uendeshaji barani na kuhimiza Nchi Wanachama zilizo katika nafasi ya kufanya hivyo, kuzingatia kusaini na MoU kama hizo na Kamisheni ya UA.

**<u>Kuhusu Ujenzi Mpya na Maendeleo Baada ya Migogoro:</u>**

60. **UNAMPONGEZA** Mhe. Abdel F. El Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na Kinara wa Ujenzi Mpya na Maendeleo Baada ya Migogoro (PCRD) kwa jitihada zake zinazoendelea katika kukuza amani na maendeleo endelevu katika Bara; **PIA UNAIPONGEZA** Kamisheni ya UA kwa kuandaa kwa mafanikio Mradi wa matokeo ya haraka katika namna ya ukarabati wa shule ya umma katika Mji wa Kpor, Kaunti ya Margibi, kwa ushirikiano na Serikali ya Liberia, katika kurejesha na kuimarisha uhimilivu wa jamii; kwa madhumuni hayo, **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA, kwa ushirikiano wa karibu na taasisi na washirika wa maendeleo wa bara na kimataifa, kuongeza miradi hiyo katika Nchi Wanachama zinazopitia michakato ya baada ya migogoro na mabadiliko, kupitia Kituo cha AU PCRD; **UNAPONGEZA ZAIDI** uandaaji na kupitishwa kwa Msimamo wa Pamoja wa Afrika (CAP) kuhusu Mapitio ya Muundo wa Ujenzi wa Amani, na uandaaji wa Miongozo ya Msaada wa Kisaikolojia wa Afya ya Akili (MHPSS) kwa watu walioathiriwa katika mazingira ya kabla ya migogoro, wakati wa migogoro na baada ya migogoro na **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutumia kikamilifu zana na utaalamu uliopo katika PCRD, kupitia kituo cha AU PCRD, pamoja na kutekeleza Sera ya AU PCRD iliyorekebishwa ili kuzuia kujirudiarudia na kuimarisha maendeleo.

**<u>Kuhusu Kupambana na Ugaidi na Itikadi Mikali:</u>**

61. **UNAPONGEZA** jitihada za Kinara wa UA wa Kupambana na Ugaidi, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, Mheshimiwa Abdelmadjid Tebboune, katika kuendeleza ajenda ya UA ya kupambana na ugaidi na uasi, na katika suala hili, **UNATOA WITO** wa kuharakishwa kwa utekelezaji wa mapendekezo yake; **UNATAMBUA** mafanikio yaliyofikiwa na Kamisheni ya UA katika kupambana na ugaidi na uasi katika bara; **UNAKARIBISHA** uanzishwaji wa Kamati Ndogo ya PSC ya Kupambana na Ugaidi na **UNAIELEKEZA** AUC kuiunga mkono Kamati Ndogo ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa agizo lake la kukabiliana na ugaidi na uasi katika bara;

62. **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kuwasilisha Rasimu ya Mpango wa Utekelezaji uliokamilika kwa Baraza la Mawaziri la UA kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa, kufuatia taratibu zilizowekwa za UA, na hivyo kupata mamlaka muhimu ya kisiasa na kuhakikisha upatanifu wa bara zima katika kutekeleza mfumo wa 2026-2030; **PIA UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kuharakisha uandaaji wa Mpango Mpya wa Utekelezaji wa Kimkakati wa Bara wa UA wa Miaka Mitano kuhusu Kupambana na Ugaidi na, kufuatia mchakato jumuishi wa uthibitishaji na vyombo husika vya UA, kuuwasilisha kwa Baraza la Mawaziri la UA kwa ajili ya kujadiliwa kwa kufuata utaratibu unaostahili, ili kuhakikisha mwendelezo, mshikamano, na umiliki wa Afrika wa juhudi za kupambana na ugaidi za bara; **AIDHA, UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kukamilisha uandaaji wa Kibali cha Kukamatwa cha Afrika na Orodha ya UA ya Makundi ya Magaidi na Watu Binafsi, na kuoanisha sheria za kitaifa ipasavyo, ili kuziba mapengo ya mamlaka ya kisheria, kuzuia usafiri wa magaidi kuvuka mipaka, na kuimarisha ushirikiano wa kimahakama na utekelezaji wa sheria na kurasimisha vichocheo vya wazi vya hatua za mapema ndani ya Mfumo wa Tahadhari ya Mapema ya Bara, unaoungwa mkono na tathmini za vitisho vya Kituo cha Kupambana na Ugaidi cha UA (AUCTC), na kuziunganisha na hatua za kidiplomasia, usalama, na utulivu zilizoidhinishwa awali chini ya mwongozo wa PSC;

63. **UNAPONGEZA** juhudi za AFRIPOL katika kuchangia kupambana na uhalifu wa kimataifa na kwa Mfumo wa tahadhari za mapema wa Bara na UNAITAKA Kamisheni ya AU kuharakisha utekelezaji wa mageuzi yaliyoidhinishwa ya AFRIPOL;

64. **UNASISITIZA HAJA** ya kuweka kipaumbele vifurushi jumuishi vya uhimilivu wa Sahel na pwani vinavyochanganya shughuli za usalama, usimamizi wa mipaka, msaada wa utawala, na shughuli za utafutaji riziki ili kuzuia kuenea kwa mitandao ya itikadi kali kusini mwa Afrika Magharibi; na kwa Kamisheni ya UA kuandaa mfumo wa bara la Afrika wa kukabiliana na magaidi kutumia teknolojia zinazoibuka, ikiwa ni pamoja na ndege zisizo na rubani, majukwaa yaliyosimbwa kwa njia fiche, na fedha za dijitali, kujenga juu ya Kanuni Elekezi za Algeria na kuhakikisha ulinganifu na viwango vya kimataifa;

65. **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA, kupitia AUCTC, kufanya kazi kwa ushirikiano na ECOWAS katika kukuza mifumo ya tahadhari ya mapema inayotegemea jamii na kuwekeza katika programu za maendeleo ya ndani ili kupunguza ajira zitolewazo na watu wenye msimamo mkali; **PIA UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kuwashirikisha washirika wa kimataifa ili kuunga mkono juhudi za kupambana na ugaidi kupitia mafunzo, vifaa, na mipango ya kimkakati, huku ikihakikisha kwamba hatua zinaheshimu haki za binadamu na kuepuka kuwatenganisha wakazi wa eneo hilo; **UNATAMBUA** kuundwa kwa Kikosikazi cha Pamoja cha Baharini (CMTF) kwa Ghuba ya Guinea kama kikosi kilichosimama, tayari kupeleka askari, chenye uwezo wa kutoa majibu ya haraka na yaliyoratibiwa ya usalama wa baharini kote katika eneo hilo na kupongeza juhudi za Nchi Wanachama wa eneo la Ghuba ya Guinea na Kikosikazi cha Pamoja cha Baharini kwa kuongezeka kwa upatikanaji wao wa majukwaa ya baharini na katika suala hili, **UNAIAGIZA** Kamisheni ya UA kushirikiana na CMTF ya Ghuba ya Guinea na kutoa msaada, ikiwa ni pamoja na kutoka Kituo cha Usafirishaji cha Bara (CLB) ili kuiwezesha

CMTF kuwa sehemu muhimu ya jeshi la majini la Kikosi cha Akiba cha Afrika (ASF), kinachofanya kazi katika eneo la Ghuba ya Guinea;

66. Katika muktadha huu, **UNAIPONGEZA** Kamisheni kwa kusaini Mkataba wa Makubaliano (MoU) na Kituo cha Taifa cha Kupambana na Ugaidi Nigeria (NCTC) kuhusu jitihada za pamoja za kupambana na ugaidi, pamoja na mapitio ya utafiti uliopoi uliofanywa na AUCTC kama Kituo cha bara chenye ubora katika kupambana na ugaidi na **UNASISITIZA** haja ya utekelezaji wa vifungu vya MoU ili kutoa ripoti ya zoezi la uwekaji wa mipango;

67. **UNAIELEKEZA** AUCTC kuweka kipaumbele kuandikaji wa Sheria na Muundo wa AUCTC uliyorekebishwa kwa ajili ya kupitishwa na chombo cha sera ili kuimarisha mamlaka ya Kituo, wafanyakazi, na rasilimali, ili kukiwezesha kufanya kazi kwa ufanisi kama kitovu cha bara chenye ubora cha UA kwa ajili ya uchanganuzi, uratibu, na ujenzi wa uwezo wa kupambana na ugaidi;

**<u>Kuhusu Wanawake, Amani na Usalama:</u>**

68. **UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama zilizowasilisha ripoti kupitia jukwaa la Mfumo wa dijitali wa Matokeo ya Bara, huku ukizihimiza Nchi nyingine Wanachama zenye Mipango ya Kitaifa ya Utekelezaji kuhusu Wanawake, Amani na Usalama (WPS) kutimiza vivyo hivyo ahadi zao za kuripoti ili kuimarisha uwajibikaji, kujifunza, na utekelezaji wa pamoja wa ajenda ya WPS barani kote; **UNAIPONGEZA** Kamisheni kwa mafanikio yake makubwa katika kuendeleza ajenda ya WPS, hasa kupitia Azimio la kihistoria la Windhoek+25 na Utafiti ujao wa Bara, ambao utatathmini utekelezaji wa WPS barani Afrika; **UNAMPONGEZA** Mhe. Balozi Liberata Mulamula kwa kuteuliwa kwake kuwa Mjumbe Maalumu wa Umoja wa Afrika kuhusu Wanawake, Amani na Usalama na kwa juhudi zilizotumika tangu kuteuliwa kwake katika kutetea na kukuza ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama barani Afrika; na **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama na washirika kutoa msaada wao katika utekelezaji wa agizo lake; **UNAKUBALIANA** na Azimio la Tunis na Wito wake wa Kuchukua Hatua uliopitishwa katika Mkutano wa 6 wa Viongozi wa Ngazi ya Juu Afrika kuhusu Wanawake, Amani, na Usalama mwaka 2025; **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kuanzisha Ofisi ya Mjumbe Maalumu wa Wanawake, Amani, na Usalama, kwa kuhakikisha miundo yake, rasilimali, na mamlaka yanaimarishwa ili kusaidia utekelezaji mzuri wa ajenda ya WPS barani kote;

69. **UNAKARIBISHA** kuanzishwa kwa mifumo muhimu ya kitaasisi, ikiwa ni pamoja na Jukwaa la Mwaka la Umoja wa Afrika kuhusu Uongozi wa Wanawake katika Sekta ya Usalama na Jumuiya ya Utendaji kuhusu Jinsia katika Mifumo ya Tahadhari ya Mapema; **UNAIPONGEZA** FemWise-Africa kwa mchango wake muhimu katika kuhakikisha ushiriki kamili, ulio sawa, na wenye mafanikio wa wanawake katika michakato ya amani barani kote; **UNAIHIMIZA** Kamisheni kuanzisha utaratibu maalumu wa uratibu miongoni mwa UA, RECs/RMs, na Nchi Wanachama ili kushirikishana utendaji bora na kuimarisha uwezo wa wataalamu wa WPS;

70. **UNASISITIZA WITO** wa kuongeza msaada kwa viongozi wa kitaifa katika kutekeleza ahadi za WPS na kujumuisha kwa utaratibu mitazamo ya jinsia katika juhudi zote za utawala, amani, na usalama; **PIA UNAHIMIZA** kuendelea kusaidia Nchi Wanachama katika kutekeleza miradi inayolenga kuendeleza NAP zao kuhusu Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSCR) 1325 na kuziomba Nchi Wanachama na washirika kuhakikisha ufadhili unaotabirika na endelevu ili kutekeleza kikamilifu mipango hii muhimu ya WPS na kudumisha kasi kuelekea usawa wa jinsia katika amani na usalama katika Afrika; **NA UNAZIHIMIZA ZAIDI** Nchi Wanachama kuweka mazingira mazuri kwa ushiriki wenye manufaa wa wanawake katika mazungumzo ya amani, ikiwa ni pamoja na tahadhari za mapema, kuzuia migogoro, upatanishi na mazungumzo, na kuanzisha bajeti inayozingatia jinsia na kutenga rasilimali za taifa kwa ajili ya kutekeleza Mipango ya Utekelezaji ya Wanawake, Amani na Usalama ya Taifa na Kanda;

**Kuhusu Vijana, Amani na Usalama:**

71. **UNALIPONGEZA** Kundi la 3 la Mabalozi wa Amani Vijana wa Afrika (AYAPs) kwa kukamilisha kwa mafanikio mamlaka yao ya miaka 2 isiyorudiwa, na unakaribisha uteuzi wa Kundi la 4 la AYAPs; **UNATAMBUA NA KUPONGEZA** uongozi wa Kinara wa UA wa Amani na Usalama wa Vijana, Mhe. Evariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi, na **UNAMPONGEZA** kwa kuitisha Mazungumzo ya 4 ya Mwaka ya Bara kuhusu YPS;

72. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutenga rasilimali endelevu ya Vijana kwa ajili ya Programu ya Amani Afrika ili kuimarisha na kuongeza mipango ya amani inayoongozwa na vijana barani kote, na kuunganisha Vijana, Amani na Usalama katika sera zao za kitaifa za ulinzi, maendeleo na kuzuia migogoro, pamoja na kuimarisha uwezo wa kitaasisi unaohusika na kuratibu na kufuatilia Mipango ya Utekelezaji ya Taifa ya (NAPs) kwa Vijana, Amani na Usalama; **UNAZIPONGEZA** Nchi saba Wanachama, ambazo ni: Burundi, Malawi, Gambia, Liberia, Kameruni, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Nigeria, ambazo hadi sasa zimepitisha Mipango ya Utekelezaji ya Taifa kuhusu YPS; na **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama ambazo bado hazijafanya hivyo, kuongeza juhudi maradufu za kuendeleza NAPs zinazolenga vijana na kupata zaidi ufadhili unaotabirika na wa kutosha kwa utekelezaji wake; **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuwekeza kwa vijana kupitia kuwajengea uwezo, ushauri, elimu, mafunzo ya ufundi, ajira na mipango ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi inayowawezesha vijana kutekeleza majukumu yao kikamilifu katika kuendeleza amani, usalama, na utulivu, na **UNASISITIZA UMUHIMU** wa kuwekeza katika Amani ya Vijana na Uhamiaji, pamoja na kupitia Mfuko wa Uhamaji wa Vijana ili kuwawezesha vijana wa Kiafrika kutimiza ndoto zao katika Afrika;

**Kuhusu Ulinzi wa Watoto katika mazingira ya Migogoro ya Kivita:**

73. **UNAPONGEZA** jitihada zilizofanywa na Wenyeviti wenza wa Jukwaa la Afrika kuhusu Watoto Walioathiriwa na Migogoro ya Kivita (AP-CAAC) katika ajenda ya ulinzi wa watoto na **UNAUNGA MKONO** mafanikio yaliyofikiwa na Tume katika kuimarisha ulinzi

wa watoto katika mazingira ya migogoro ya silaha; na **UNAMPONGEZA** Mwenyekiti wa Kamisheni ya UA kwa kumteua Mhe. Balozi Jainaba Jagne kuwa Mjumbe Maalumu wa Kwanza wa Aina yake wa UA kwa Watoto Walioathirika na Migogoro ya Kivita kuhakikisha uongozi endelevu wa bara na ufuatiliaji ulioratibiwa wa jukumu la Watoto Walioathiriwa na Migogoro ya Kivita (CAAC); **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama, RECs/RMs na wadau wa kitaifa kuweka kipaumbele katika utekelezaji wa mikataba ya ulinzi wa watoto ya UA na kutenga rasilimali za kutosha ili kuimarisha mifumo ya ulinzi ya kitaifa;

74. **UNALAANI VIKALI** kuendelea kuwaajiri na kuwatumia watoto katika migogoro ya kivita kunakofanywa na magaidi na vikundi vyenye silaha katika sehemu za Bara la Afrika, kinyume cha Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu na Sheria ya Kimataifa ya Haki za Binadamu na unasisitiza kimsingi kwamba hakuna mtoto anayepaswa kuajiriwa na kutumiwa katika hali yoyote ya migogoro katika Bara; **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama, RECs/RMs, na Kamisheni ya UA kujumuisha ulinzi wa watoto katika mazungumzo ya upatanishi na amani na kusaidia utekelezaji mzuri wa vipengele vya ulinzi wa watoto ndani ya programu za PCRD, programu za Kuwatawanya, Upokonyaji Silaha na Urejeshwaji kwa jamii (DDR), pamoja na katika mifumo ya ujumuishaji upya;

75. **UNASISITIZA UMUHIMU** wa utekelezaji kamili na ulioratibiwa wa mifumo ya kanuni za UA na vyombo vya sera vinavyohusiana na ulinzi wa watoto, ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto, Sera ya Kuingiza Ulinzi wa Mtoto katika APSA, na Sera ya Ulinzi wa Mtoto katika Operesheni za Msaada wa Amani wa UA, ukisisitiza hasa kuhakikisha msaada endelevu wa kuunganishwa tena kwa watoto wanaohusishwa na vikosi vya kijeshi na vikundi vyenye silaha (CAAFAG) na ulinganishaji wa programu za ulinzi wa mtoto na viwango vya ulinzi wa mtoto vya Bara na kimataifa.

**<u>Kuhusu Programu ya Mipaka ya UA:</u>**

76. **UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama ambazo zimepiga hatua katika jitihada za utambuzi wa mipaka, uwekaji mipaka, na ushirikiano, na kuwahamasisha wale ambao bado hawajashiriki kikamilifu kuweka kipaumbele katika mipango hiyo kulingana na Mkataba wa Niamey; na **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama, kwa msaada wa kitaalamu wa Kamisheni, kuharakisha uandaaji wa mifumo ya uratibu wa kanda na majukwaa yanayoongozwa na jamii, kama vile Baraza la Viongozi wa Ateker, ili kuimarisha amani, utulivu, na ushirikiani barani kote.

**<u>Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Amani na Usalama:</u>**

77. **UNASISITIZA TENA** dhamira yake ya kisiasa katika kuendeleza na kupitisha Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Amani na Usalama, kama mfumo wa bara unaounganisha ili kuongoza ushiriki wa Afrika katika hatari za amani na usalama zinazohusiana na hali ya hewa katika ngazi za kitaifa, kikanda, bara, na kimataifa.

**<u>Kuhusu Mfuko wa Amani na Ufadhili wa Shughuli za Amani na Usalama za UA:</u>**

78. **UNATAMBUA** maendeleo chanya yaliyopatikana katika utekelezaji wa shughuli za amani na usalama kupitia matumizi ya riba iliyopatikana kutokana na uwekezaji wa Mfuko wa Amani, na Kituo chake cha Akiba ya Mgogoro (CRF); na **UNAIPONGEZA** Kamisheni ya UA kwa utekelezaji wa programu katika Nchi Wanachama zinazolenga kuzuia migogoro na kuimarisha amani katika jamii; **PIA UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama kwa ahadi zao za kufadhili na kumiliki ajenda ya amani na usalama; **UNAIELEKEZA** Kamisheni ya UA kuendelea na juhudi zake za kushirikisha Umoja wa Mataifa na wahusika wengine wote muhimu ili kuhakikisha utekelezaji kamili wa Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa 2719(2023) kuhusu kufadhili Operesheni za Msaada wa Amani zinazoongozwa na UA;

**<u>Kuhusu Programu za Kipaumbele za Amani na Usalama barani Afrika:</u>**

79. **UNATOA WITO** wa kuimarisha mfumo wa tahadhari za mapema barani kote, ikiwa ni pamoja na kuboresha zana za uchanganuzi, kuboresha Chumba cha Taarifa, na kuimarisha uwezo wa kutumia taarifa wa RECs/RMs, pamoja na kuongeza ushirikiano kati ya UA na RECs/RMs; **UNAZIHAMASISHA** Nchi Wanachama kuimarisha mifumo yao ya tahadhari za mapema na kuchukua hatua ili kuhakikisha tahadhari za mapema zinashughulikiwa kwa hatua za mapema; **UNATOA WITO** wa Utanzishaji wa Chombo cha Kufuatilia Usalama wa Bara, ikiwa ni pamoja na kutoa rasilimali kwa ajili ya mipango ya ufuatiliaji wa hatari kwa wakati halisi na bidhaa za kusaidia utoaji wa maamuzi; **UNAIELEKEZA** Kamisheni ya UA, pamoja na AUCTC, AFRIPOL, Kamati ya Intelijensia na Huduma za Usalama ya Afrika (CISSA) na Mfumo Tathmini ya Utawala Bora Afrika (APRM) kuanzisha na kuiruhusu PSC kurasimisha zana ya kuweka mipango ya kufuatilia hatari inayobadilika na inayohuishwa kila mara, kuimarisha uwezo wake wa kushiriki katika tahadhari za mapema kwa hatua za mapema, kwa kutoa picha iliyojumuishwa ya vitisho, udhaifu, na vichocheo vinavyoweza kutokea, kwa lengo la kuongeza uwezo wa UA wa kuzuia migogoro kwa ufanisi na kuongoza diplomasia ya kuzuia; **PIA, UNAIELEKEZA** Kamisheni kuharakisha uanzishwaji wa Mfumo wa Tahadhari ya Mapema wa Bara (CEWS)–AUCTC Kituo cha Pamoja cha Uchanganuzi na kuhakikisha uendelevu wake wa muda mrefu kupitia ufadhili unaotabirika na wafanyakazi wataalamu; na UNA**ZIHIMIZA** RECs/RMs kuoanisha zana zao za onyo la mapema na CEWS na kuimarisha uchambuzi wa pamoja, protokali za hatua za mapema na msaada ulioratibiwa kwa Nchi Wanachama, hasa zile zinazokabiliwa na udhaifu wa utawala au kutokuwa na utulivu wa mara kwa mara;

80. **UNAUPONGEZA** Mtandao wa UA wa Taasisi ya Utafiti wa Migogoro (NetTT4Peace) kwa utoaji wake wa bidhaa muhimu zilizoandikwa, ikiwa ni pamoja na pendekezo la sera kuhusu Dira Mpya ya Kupunguza Silaha, na kwa upangaji wake uliofanikiwa wa mafunzo muhimu ya kujenga uwezo na mijadala ya sera kuhusu kupunguza silaha, ujumuishaji wa wanawake, operesheni za amani, na ushirikishwaji wa vijana; **UNAUHAMASISHA** Mtandao kuendelea kutoa muungano huu muhimu kati ya utafiti na sera, kuhakikisha maarifa haya yanayotokana na ushahidi yanajumuishwa kikamilifu katika ajenda ya amani na usalama ya Umoja; na **UNAKUBALIANA** na

mahitimisho ya Toleo la Tano la Jukwaa la Aswan la Amani Endelevu na Maendeleo, lililofanyika tarehe 19-20 Oktoba huko Aswan, mfululizo na Mkutano wa 16 wa Viongozi wa Juu wa UA kuhusu Kuhimiza Amani, Usalama na Utulivu barani Afrika.

81. **UNAIPONGEZA** AUC na RECs/RM kwa kuitisha kwa mafanikio Kikao cha Nne cha Sera cha Ubadilishanaji wa Maarifa wa Kikanda wa UA (I-RECKE); **UNAIDHINISHA** Mkakati wa Pamoja wa Uhtafutaji wa Rasilimali wa AU-RECs/RMs kama mfumo muhimu wa kupata ufadhili unaotabirika na endelevu, na **UNAELEKEZA** utekelezaji wake mara moja huku ukithibitisha tena umuhimu wa masuluhisho yanayoongozwa na Waafrika na hatua za ushirikiano katika kushughulikia changamoto za amani na usalama za bara.

82. **UNAPONGEZA** ushirikiano wa PSC na RECs/RMs na kusisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano wake na RECs/RMs ambazo zina mamlaka ya utawala, amani na usalama katika utekelezaji wa mamlaka za kanda na za bara zinazohusiana na utawala, amani, na usalama ikiwa ni pamoja na ICGLR, ambayo ina mamlaka kwa eneo la Maziwa Makuu; **UNATAMBUA** mchango mkubwa na wa kina wa ICGLR katika kukuza amani, usalama na utulivu katika eneo la Maziwa Makuu linalojumuisha nchi kumi na mbili (12) za Afrika, hasa mashariki mwa DRC; kulingana na Ibara ya 16 ya Protokali ya PSC, **UNAZINGATIA** Ripoti ya Tathmini iliyofanywa na Kamisheni ya UA, kuhusu ushirikiano na ICGLR;

83. **UNAIDHINISHA** pendekezo kwa UA kutambua rasmi ICGLR kama mbia wa ushirikiano wa kanda kutokana na jukumu lake na michango ya kusifiwa katika utulivu wa eneo la Maziwa Makuu pamoja na hali yake ya sasa kama Mwangalizi katika Mkutano Mkuu wa UN tangu Desemba 2009; **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA na ICGLR kufanyia kazi kwa pamoja vyombo muhimu vya ushirikiano wa kitaasisi na taratibu zilizokubaliwa;

84. **UNAPONGEZA** mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kuimarisha ushirikiano wa kimkakati na wa manufaa kwa pande zote kwa ajili ya amani na usalama; **UNAUNGA MKONO** kukamilika kwa Programu mpya ya Utawala, Amani na Usalama ya EU (2026-2029) na **UNAIDHINISHA** mabadiliko ya Mfumo wa Ushughulikiaji wa Mapema (ERM) III kuelekea ufadhili endelevu kupitia Kituo cha Akiba ya Mgogoro cha Mfuko wa Amani wa UA; **UNAOMBA** utekelezaji wa haraka na kamili wa Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa 2719 (2023) ili kupata ufadhili unaotabirika kwa Operesheni za Msaada wa Amani zinazoongozwa na UA; **UNATAMBUA** matokeo muhimu ya TICAD 9 na **UNATOA WITO** wa kuimarishwa kwa uwekezaji katika masuluhisho yanayoongozwa na Afrika, ikijumuisha kuzuia migogoro, usimamizi, ujenzi upya baada ya migogoro, na utawala, kupitia ushirikiano mzuri unaotumia uvumbuzi, teknolojia, na ubadilishanaji wa maarifa ili kujenga bara imara na linalojitegemea; na

85. **UNAZINGATIA** jitihadai zinazofanywa na Kamisheni ya UA kupitia Idara ya Masuala ya Siasa, Amani na Usalama (D-PAPS) ili kuandaa mfumo wake wa usimamizi wa maarifa kwa ajili ya PSC; Katika suala hili, inalipongeza Jopo la Wataalamu Mashuhuri la Ngazi ya Juu kwa mapitio ya Taasisi ya Amani na Usalama wa Afrika (APSA) na Taasisi

ya Utawala wa Afrika (AGA), na inazingatia ripoti yao na mapendekezo yake; na **UNAHIMIZA** kuendelea na uandaaji wa Mkakati wa Usimamizi wa Maarifa wa Idara nzima unaolenga kurasimisha ujifunzaji na kuhakikisha kwamba uzoefu unachangia uundaji, upangaji na utekelezaji wa sera kwa njia inayounga mkono Maamuzi ya PSC.

[9]Jopo la Wataalamu Mashuhuri la Ngazi ya Juu liliundwa na Mhe. Dkt. Phumzile Mlambo-Ngcuka, aliyekuwa Makamu wa Rais wa Afrika Kusini (Mwenyekiti), Mhe. Profesa Ibrahim Gambari, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria, Mhe. Mahamat Saleh Annadif, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Chad, Mhe. Sam Kutesa, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Uganda, na Mhe. Amr Moussa, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri.

**UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA MWAKA YA MWENYEKITI PAMOJA NA RIPOTI ZA VINARA ZILIZOAMBATISHWA**
**Doc. Assembly/AU/8(XXXIX)**

**Mkutano Mkuu,**

**1.** **UNAPOKEA KWA SHUKRANI** ripoti ya mwaka ya Mwenyekiti, ikijumuisha Ripoti za Vinara, uinapitisha yaliyomo na **UNAIDHINISHA** mapendekezo ambayo utekelezaji wake unategemea mchakato unaofaa wa kutathmini athari zake za kifedha, kisheria na kimuundo**.**

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA KINARA KUHUSU TAASISI ZA FEDHA ZA UMOJA WA AFRIKA NA MHE. JOHN DRAMANI MAHAMA, RAIS WA JAMHURI YA GHANA

**Mkutano Mkuu,**

**Kuhusu Benki Kuu ya Afrika**

1. **UNAPOKEA** kupitishwa kwa Katiba ya AMI;[2];

2. **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kuhakikisha utekelezaji wa AMI ifikapo Septemba 2026;;

3. **UNAITAKA** Kamisheni kufanya kazi kulingana na ratiba zilizokubaliwa na AACB kwa ajili ya utekelezaji wa AMI ifikapo Septemba 2026;

4. **UNAITAKA ZAIDI** Benki Kuu kuipa AMI wafanyakazi ili kupunguza gharama za kuanza na kuingiza gharama za utekelezaji wa AMI katika mipango yao ya bajeti ya 2026;

5. **UNATOA WITO ZAIDI** kwa Nchi Wanachama kutenga rasilimali muhimu kupitia Benki Kuu zao, ili kuhakikisha kwamba AMI ina ufadhili wa kutosha kuanza shughuli ifikapo Septemba 2026; na

6. **PIA UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kuendeleza uzingatiaji wa kiwango cha wa utekelezaji mzuri wa vigezo vya muunganiko wa uchumi mkuu.

**Kuhusu Mfuko wa Fedha wa Afrika, Benki ya Uwekezaji ya Afrika na Soko la Hisa la Afrika**

7. UNATOA WITO kwa Nchi Wanachama kusaini na kuridhia Protokali zinazoanzisha AMF na AIB; na

8. UNAITAKA Kamisheni kuboresha utafiti kuhusu masuala ya kitaalamu yanayohusiana na utekelezaji wa AUFI na kuitaka Afreximbank na wanachama wengine wa AAMFI kutoa msaada muhimu wa kifedha na kitaalamu.

Hatua Muhimu za Kuharakisha Uanzishwaji wa AUFI

**A.** Usimamizi wa Deni la Umma

[2] Pingamizi liliwekwa na Jamhuri ya Afrika Kusini na Jamhuri ya Kiarabu ya Misri

9. **UNAUOMBA** Mkutano Mkuu kupitisha KIPIMO CHA DENI na Azimio Maalum la Mkutano Mkluu kuhusu KIPIMO CHA DENI na Ufadhili Endelevu;

10. **UNAIOMBA** Kamisheni na Nchi Wanachama kutumia hati hizo mbili kama mpango wa kimkakati wa mazungumzo kuhusu deni katika mijadala ya kimataifa, na kwa ajili ya kuendeleza usimamizi endelevu wa deni;

11. **UNAIOMBA** Kamisheni ifafanue ratiba na majukumu ya utekelezaji ili kuhakikisha kwamba KIPIMO cha Madeni kinaweza kutekelezwa na si cha matarajio tu; na

12. **UNAITAKA** AUC kutekeleza ADMM ndani ya Idara ya ETTIM kama jukwaa la mtandaoni lisilo na mzigo wa kisheria, kimuundo na kifedha kwa Nchi Wanachama na kuialika AAMFI kutoa msaada wa kifedha na kitaalam unaohitajika.

**B. Mpango wa Hatua Muhimu za Kufikia Ukuaji Jumuishi na Maendeleo Endelevu barani Afrika**

13. **UNAOMBA** Kamisheni, AfDB na AUDA-NEPAD kutoa msaada unaohitajika kwa Nchi Wanachama, ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo kwa Nchi Wanachama katika kutekeleza mapendekezo ya Mpango; na

14. **UNAIOMBA** AfDB kuchukua jukumu la kuongoza katika utekelezaji wa Mpango huo kupitia utoaji wa rasilimali fedha zinazohitajika.

**C. Kuimarisha Ukusanyaji wa Rasilimali za Ndani**

15. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuimarisha ushirikiano na Kamisheni, ATAF, TJNA, UNECA, ACBF na wadau wengine ili kutekeleza mikakati ya kodi ya AU na IFF; na

16. **UNAZIHMIZA** AUC, ATAF, TJNA, ACBF na UNECA kuendelea kuunga mkono Kundi la Afrika na wataalamu wa Afrika wanaoshiriki katika mazungumzo, ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Mpango wa Umoja wa Mataifa kuhusu Ushirikiano wa Ushuru wa Kimataifa.

**D. Kuanzishwa kwa Shirika la Ukadiriaji wa Mikopo wa Afrika**

17. **UNAIPONGEZA** Mauritius kwa kuteuliwa kwake kama mamlaka kuu ya AfCRA na **UNATOA WITO** kwa nchi mwenyeji kutoa msaada unaohitajika kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa AfCRA mwaka wa 2026; na

18. **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama zinazopenda kujiandikisha kama mamlaka za pili za AfCRA kuwasilisha Maombi yao kwa APRM ili yapitiwe na Mshauri wa Kifedha

# UAMUZI KUHUSU KUTOKOMEZA NDOA ZA UTOTONI AFRIKA NA MHE. HAKAINDE HICHILEMA, RAIS WA JAMHURI YA ZAMBIA NA KINARA WA UMOJA WA AFRIKA WA KUTOKOMEZA NDOA ZA UTOTONI

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAPOKEA** kwa shukrani ripoti ya Mhe. Hakainde Hichilema, Rais wa Jamhuri ya Zambia na Mtetezi wa Kutokomeza Ndoa za Utotoni barani Afrika;

2. **UNAMPONGEZA** Rais Hichilema kwa kujitolea kwake na mafanikio yake muhimu katika kuongoza juhudi za kutokomeza ndoa za utotoni barani Afrika, na **UNAZINGATIA ZAIDI** ombi lake la kuanzisha Kundi la Mabalozi wa Kukomesha Vitendo Vibaya ambalo litaongozwa na Zambia, ili kufanya utetezi endelevu na uangalizi wa suala la vitendo vibaya barani Afrika.;

3. **UNAZIPONGEZA** Nchi zote Wanachama wa AU ambazo zimeandaa mipango ya kitaifa ya utekelezaji wa gharama za kutokomeza ndoa za utotoni katika mamlaka zao na **UNAZITAKA** zile ambazo hazijafanya hivyo, kuharakisha kufanya hivyo;

4. **UNATAMBUA** kwamba umaskini ni kichocheo kikuu cha ndoa za utotoni, huku wasichana kutoka kaya maskini zaidi wakikabiliwa na hatari kubwa zaidi, na kwa hivyo **UNAZITAKA** Nchi Wanachama wa AU kuongeza uwekezaji wao katika programu za hifadhi ya jamii kama hatua muhimu ya kushughulikia sababu kuu za ndoa za utotoni barani Afrika;

5. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuondoa vikwazo vinavyowazuia wasichana kuendelea na masomo hadi ngazi ya juu, bila kujali hali yao, zikizingatia mchango unaowezekana wa wasichana katika ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu;

6. **UNAZIHIMIZA ZAIDI** Nchi Wanachama ambazo hazijafanya hivyo, kutaja umri wa chini kabisa wa ndoa kulingana na Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto na Protokali ya Maputo kuhusu Haki za Wanawake na kuchukua hatua mwafaka za kisheria za kitaifa ili kuhakikisha kwamba kila ndoa itarekodiwa kwa maandishi na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria za kitaifa, ili kutambuliwa kisheria;

7. **UNALAANI VIKALI** utekaji nyara na ndoa za lazima za wasichana, hasa katika hali za migogoro na umedhamiria kuwashtaki wahusika wa ukiukwaji huu mbaya na **UNAITAKA** Kamisheni kufanya utafiti wa bara kuhusu uhusiano kati ya migogoro, migogoro ya kibinadamu na desturi zenye madhara barani Afrika;

8. **UNATOA WITO** kwa Nchi zote Wanachama wa AU kutoa taarifa na data kwa wakati unaofaa kwa Kinara wa AU wa Kutokomeza Ndoa za Utotoni barani Afrika kwa ajili ya matumizi katika kuandika ripoti zake kwa Mkutano Mkuu.;

**9.** UNAIAGIZA Kamisheni kuandaa mpango wa ufuatiliaji kuhusu kutokomeza ndoa za utotoni barani Afrika ili kumsaidia Kinara wa Umoja wa Afrika wa Kutomokeza Ndoa za Utotoni barani Afrika katika kubadilishana michakato mikubwa ya kutokomeza janga la ndoa za utotoni ili kuarifu Mkutano Mkuu katika Kikao chake kijacho kuhusu matokeo yake ya utetezi na maendeleo yanayofikiwa na Nchi Wanachama ili kutokomeza ndoa za utotoni katika mamlaka zao; na;

**10.** UNAMUOMBA Kinara wa AU wa Kutokomeza Ndoa za Utotoni barani Afrika kuwasilisha Ripoti nyingine katika Mkutano Mkuu wake wa 40.

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA MWAKA YA KINARA WA UMOJA WA AFRIKA KUHUSU KUZUIA, KUJIANDAA NA KUKABILIANA NA MAGONJWA YA MLIPUKO NA MHE. RAIS MATAMELA CYRIL RAMAPHOSA

**Mkutano Mkuu**,

1. **UNAPOKEA KWA SHUKRANI** Ripoti ya Mwaka ya Kinara wa AU wa Kuzuia, Kujiandaa na Kukabiliana na Magonjwa ya Mlipuko (PPPR) Mhe. Matamela Cyril Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini;

2. **UNAMPONGEZA** Kinara kwa mchango wake muhimu na **UNAKUBALI** mapendekezo yake kama ifuatavyo:

Kutokana na maendeleo haya, kipaumbele cha AU sasa ni kuimarisha taasisi na kuongeza mafanikio haya ili magonjwa ya mlipuko yazuiliwe mara kwa mara au yadhibitiwe mahali yalipoanzia, badala ya kuruhusiwa kuongezeka hadi kuwa migogoro ya kikanda au ya kimataifa. Kinara anatoa mapendekezo yafuatayo, yanayoongozwa na Ajenda ya Usalama wa Afya na Uhuru wa Afrika, ili kusaidia uimarishaji endelevu wa uwezo wa PPPR kote barani.

<u>**Jukwaa la uratibu wa maandalizi na mwitikio**</u>:

• Africa CDC na WHO Afro zinapaswa kuimarisha utayari na mwitikio wa kukabiliana na magonjwa ya mlipuko katika jukwaa la bara kwa kutumia mfumo wa IMST, unaozingatia kanuni ya "4".

• Nchi Wanachama zinapaswa kukamilisha makubaliano ya Ushirikishanaji wa Data na Africa CDC na kuweka kipaumbele cha ufuatiliaji kwa wakati halisi, ushirikiano wa kidijitali, na taarifa utabiri wa janga, ikijumuisha data ya maabara, jenomu, tabianchi, na jamii.

<u>**Uhuru wa ufadhili**</u>

• Umoja wa Afrika unapaswa kuthibitisha tena PPPR kama uwekezaji wa kimkakati, si gharama ya dharura ya mara kwa mara, na kuunganisha kimfumo vigezo vya maandalizi na ufadhili unaotabirika kupitia AfEF, hati za Mfuko wa Majanga, na rasilimali za ndani.

• Mfuko wa Majanga Afrika (AfEF) unapaswa kuendeshwa kikamilifu kama utaratibu mkuu wa ufadhili wa kukabiliana kwa haraka, kuwezesha kutolewa kwa fedha mara moja baada ya kutangazwa kwa mlipuko au kuongezeka.

<u>**Sera ya Afya ya Kimataifa na Diplomasia**</u>

• Kuimarisha Msimamo wa Pamoja wa Afrika ili kuhakikisha Kundi la Afrika linaweza kujadili na kupitisha Kiambatisho cha Upatikanaji na Ushirikishanaji wa Faida za Vimelea chenye msingi imara katika kanuni za usawa, haki, na uwazi.

• Kuunga mkono utekelezaji wa Ushirika wa Diplomasia ya Afya Duniani ili kujenga kundi la wanadiplomasia wenye ujuzi wa AU ambao wanaweza kuwakilisha bara kwa ufanisi katika mazungumzo ya afya duniani, ikiwa ni pamoja na mageuzi ya muundo wa afya duniani kote kwa kutoa maoni kwa Wakuu wa Nchi na Serikali.

**<u>Uzalishaji wa Viwandani na Uzalishaji wa Ndani wa Kikanda</u>**

• Wakuu wa Nchi na Serikali kuthibitisha tena uzalishaji wa kikanda kama nguzo kuu ya Kuzuia, Kujiandaa na Kukabiliana na Magonjwa ya Mlipuko na Ajenda ya Usalama na Utawala wa Afya Afrika, wakiunganisha waziwazi uzalishaji wa ndani na upatikanaji sawa wa chanjo, uchunguzi, matibabu, na zana za kudhibiti vekta.

• Mkutano Mkuu wa AU kuomba ripoti ya kila mwaka, kupitia Africa CDC, kuhusu maendeleo kuelekea lengo la utengenezaji ndani ya bara, ikiwa ni pamoja na idadi ya vifaa vya uendeshaji, idadi ya bidhaa zinazofikia viwango vya awali vya WHO au soko, na sehemu ya mahitaji ya kikanda yanayotimizwa na wazalishaji wa Afrika ambao ubora wao umehakikishwa.

Sambamba na Usalama na Utawala wa Afya Afrika, mapendekezo haya yanapaswa kuungwa mkono kwa kushirikiana na kuratibu na washirika wa kitaifa, kikanda, na kimataifa kupitia ushirikiano wenye heshima na unaozingatia vitendo.

# MATAMKO

# TAMKO KUHUSU HALI YA PALESTINA NA MASHARIKI YA KATI
## Doc. Assembly/AU/21(XXXIX)

**SISI** , Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tulikusanyika katika Mkutano Mkuu wa Kawaida wa thelathini na tisa (39) wa Umoja wa Afrika huko Addis Ababa mnamo tarehe 14 hadi 15 Februari 2026;

**TUKIZINGATIA** ripoti kuhusu hali katika Maeneo ya Palestina na Mashariki ya Kati, iliyowasilishwa na Kamisheni kwenye Mkutano Mkuu;

**TUKITHIBITISHA TENA** maazimio na maamuzi yote ya Shirika la Umoja wa Afrika na Umoja wa Afrika kuhusu hali ya Palestina ili kufikia amani na usalama wa kudumu Mashariki ya Kati;

**PIA TUKITHIBITISHA** Mshikamano wetu usioyumba na watu wa Palestina katika mapambano yao halali ya uhuru, kujitawala, na kuanzishwa kwa Nchi huru katika ardhi yao iliyokaliwa, ikiwa ni pamoja na Ukanda wa Gaza, Ukingo wa Magharibi, na Yerusalemu Mashariki, kwa mujibu wa maazimio na kanuni husika za Umoja wa Mataifa za sheria za kimataifa, zinazowakilishwa na Shirika la Ukombozi wa Palestina linaloongozwa na Mheshimiwa Rais Mahmoud Abbas;

**TUKITHIBITISHA ZAIDI** hadhi na umuhimu wa mapamabano halali ya Palestina, na msimamo wetu thabiti wa kuunga mkono Palestina, kwa kuzingatia kanuni na maadili ya pamoja ya uhuru na ukombozi kutoka kwa ukoloni, ukandamizaji, ubaguzi wa rangi, na dhuluma;

**TUKISISITIZA** tena shauku na dhamira yetu ya kuunga mkono suluhisho la amani na haki kwa mzozo wa Waarabu na Israeli kwa mujibu wa sheria za kimataifa na maazimio yote husika ya Umoja wa Mataifa na kwa mujibu wa Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa 194;

**TUKIREJELEA** Mkataba wa Amani wa Gaza, ambao uliwasilishwa wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Amani ulioandaliwa na Misri mjini Sharm el-Sheikh tarehe 13 Oktoba 2025.

**TUKIREJELEA PIA** azimio 2803 lililopitishwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa mnamo tarehe 17 Novemba 2025, linaloidhinisha "Mpango Kamili wa Kukomesha Mgogoro wa Gaza" wa tarehe 29 Septemba 2025.

**TUKIKARIBISHA** kutambuliwa kwa Nchi ya Palestina na Nchi kadhaa Wanachama wa Umoja wa Mataifa wakati wa Mkutano Mkuu mnamo Septemba 2025, ambayo ni maendeleo makubwa katika kuendeleza mchakato wa Amani katika eneo hilo kupitia kuanzisha Taifa la Palestina.

**TUKIZIHIMIZA** Nchi zote Wanachama wa AU kuendelea kutoa msaada kwa harakati za Palestina kwa njia inayohakikisha utekelezaji wa maadili na tunu bora ambazo ni msingi wa kuanzishwa kwa Shirika la Umoja wa Afrika/Muungano wa Afrika; miongoni mwazo ni pamoja na kuunga mkono harakati za ukombozi na haki ya watu kujitawala, na kujiepusha na kitendo chochote kinachoweza kudhoofisha mshikamano na harakati za Palestina na haki za watu wa Palestina;

**TUKIKATAA** ukiukaji wa Israeli, kama Taifa vamizi, wa haki za msingi na uhuru wa watu wa Palestina, na kuwanyima kabisa haki ya msingi ya kuishi, na kuendesha mfumo wa ubaguzi wa rangi unaobagua kwa misingi ya rangi na dini, na unaodumisha uvamizi wa Israeli.

**Tunaazimia yafuatayo:**

1. **TUNAUNGA MKONO** Mkataba wa Amani wa Gaza na **KUPONGEZA** kwa majukumu ya uongozi yaliyofanywa na Rais Donald J. Trump wa Marekani na Rais Abdul-Fattah Al-Sissi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, pamoja na Qatar na Türkiye, wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Amani ulioandaliwa na Misri, Sharm el-Sheikh, Oktoba 2025.

2. **TUNAUNGA MKONO ZAIDI** kupitishwa kwa Azimio namba 2803 lililopitishwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa mnamo tarehe 17 Novemba 2025, likiidhinisha "Mpango Kamili wa Kukomesha Mgogoro wa Gaza" wa tarehe 29 Septemba 2025.

3. **TUNAPINGA** kwa dhati pendekezo lolote au jaribio la kufifisha harakati za Palestina kwa kuwahamisha wapalestina kutoka nchi yao, ikiwa ni pamoja na Ukanda wa Gaza, jambo ambalo ni ukiukaji wa wazi wa Sheria ya Kimataifa na msimamo thabiti wa Umoja wa Afrika unaotaka haki ya watu wa Palestina ya kujiamulia mambo yao wenyewe.

4. **TUNATHIBITISHA** msimamo wetu kwamba amani ya haki, kamili na ya kudumu katika Mashariki ya Kati inalazimu kuondolewa kabisa kwa Israeli kutoka maeneo yote ya Palestina na Kiarabu yaliyokaliwa tangu Juni mwaka 1967, ikiwa ni pamoja na Milima ya Golani ya Syria na maeneo yaliyokaliwa kusini mwa Lebanon, na mfano halisi wa Nchi Uhuru ya Palestina yenye Yerusalemu Mashariki kama mji mkuu wake, na kurudi kwa wakimbizi wa Palestina majumbani mwao.

5. **TUNATHIBITISHA** uungaji mkono wa kisiasa, kiuchumi, na kifedha kwa Nchi ya Palestina, na umuhimu wa kuwezesha umoja wa kijiografia na kisiasa katika maeneo ya Palestina kati ya Ukingo wa Magharibi na Ukanda wa Gaza.

6. **TUNAKARIBISHA** kutambuliwa hivi karibuni kwa nchi ya Palestina na Jumuiya ya kimataifa na nchi nyingi wakati wa Mkutano Mkuu wa 80 Umoja wa Mataifa

uliofanyika Septemba 2025, kama hatua muhimu kuelekea suluhisho la haki na pana, na **TUNAZIHIMIZA** nchi zote ambazo bado hazijafanya hivyo, kutetea haki ya kimataifa kwa kutambua utaifa wa Palestina.

7. **TUNATOA WITO** kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kupendekeza kukubaliwa kwa Nchi ya Palestina kama mwanachama kamili wa Umoja wa Mataifa kwa mujibu wa dhamira iliyoonyeshwa na wanachama wengi wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

8. **TUNAKARIBISHA PIA** Mkutano wa Kimataifa wa Wafadhili unaopendekezwa utakaoandaliwa na Misri uliojitolea kwa ajili ya ujenzi upya wa Gaza, kama hatua mpya ya kuponya majeraha ya vita, na kupunguza mateso ya watu wa Palestina

9. **TUNATOA WITO** kwa jumuiya ya kimataifa kuhakikisha ulinzi wa Wapalestina kwa mujibu wa maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa nambari 605 (1987), 673 (1990), na 904 (1994), kulingana na Mikataba ya Geneva, pamoja na maazimio yaliyopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, ikijumuisha Mkutano wake maalum wa Julai 2018.

10. **TUNATOA WITO ZAIDI** kwa Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika kufanya kazi na jumuiya ya kimataifa kwa ajili ya misaada ya haraka kwa Ukanda wa Gaza ulioathiriwa na kuhakikisha misaada ya kibinadamu inatolewa kwa kuiwekea shinikizo Israeli, mamlaka inayoikalia, ili kuondoa kizuizi kisicho cha haki cha Israeli kwenye Ukanda huo na kuharakisha mchakato wa ujenzi mpya.

11. **TUNASISITIZA** haja ya haraka ya kujenga upya Gaza na kufungua mara moja njia salama za kibinadamu ili kupunguza mateso ya Watu wa Palestina na kulinda taasisi za tiba na wafanyakazi.

12. **TUNALAANI VIKALI** sera ya utawala ya Israeli ya kuwaweka kizuizini watu wengi bila kuwafungulia mashtaka na kuomba mamlaka ya Israeli kuwaachilia huru mara moja wafungwa wote wa Kipalestina, hasa watoto, wanawake, wazee, na wagonjwa, waliowekwa kizuizini katika mazingira magumu kinyume na haki zote zinazohakikishwa na sheria na mikataba ya kimataifa inayotumika.

13. **TUNALAANI ZAIDI** majaribio yote ya kuwaondoa kwa nguvu watu wa Palestina au kuifilisisha Palestina, ikisisitiza kwamba vitendo hivyo vinapingana na kanuni za Umoja wa Afrika na sheria za kimataifa za kibinadamu.

14. **TUNASISITIZA TENA** dhamira yetu kwa uthabiti wa harakati ya Watu wa Palestina kwa ajili ya nchi yao na kuendelea kwetu kuunga mkono suluhisho la amani na haki kwa mzozo wa Waarabu na Israeli kwa mujibu wa sheria za kimataifa na maazimio yote husika ya Umoja wa Mataifa, ambayo yanataka

kuanzishwa kwa Nchi Huru na Huru ya Palestina kwenye mipaka ya tarehe 4 Juni 1967, huku Yerusalemu Mashariki ikiwa mji mkuu wake.

**15.** **TUNASISITIZIA** umuhimu wa kutatua suala la Palestina ili kufikia amani kamili katika Mashariki ya Kati, kwa kuzingatia suluhisho la mataifa mawili, vifungu vya sheria za kimataifa, maazimio yote ya jumuiya ya kimataifa, Mpango wa Amani wa Kiarabu, maamuzi ya Umoja wa Afrika, na kuongozwa na maono ya Mheshimiwa, Rais Mahmoud Abbas, na wito wake wa mara kwa mara wa kufikia amani.

**16.** **TUNAZIOMBA** Nchi Wanachama wa AU na jumuiya ya kimataifa kuzingatia vifungu vya sheria za kimataifa na maazimio husika ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika, na kufanya kazi ya kukomesha uvamizi wa Israel, jambo ambalo linadhoofisha misingi ya sheria za kimataifa.

**17.** **TUNASISITIZIA** umuhimu wa kushughulikia sababu kuu za mgogoro huu wa muda mrefu, hasa uvamizi usio na haki na unaoendelea wa Israeli, Palestina kunyang'anywa ardhi yake, makazi ya Israel, na ukiukwaji wa sheria za kimataifa bila kudhibitiwa na mchakato wa amani uliokwama kwa kukiuka sheria za kimataifa na maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

**18.** **TUNAIHIMIZA** Jumuiya ya Kimataifa kufuatilia na kuripoti kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu katika magereza ya Israeli

**19.** **TUNASISITIZA** kwamba suluhisho la kisiasa pekee linalotegemea maono ya mataifa mawili ndiyo njia inayowezekana zaidi ya kuhakikisha amani, utulivu, na usalama kwa watu na Mataifa katika eneo hilo, na kwamba kuanzisha Taifa la Palestina ni msimamo thabiti na usioyumba wa Umoja wa Afrika.

## TAMKO KUHUSU KULINDA UHURU, HAKI YA KULINDA MIPAKA, UMOJA, NA UTULIVU WA JAMHURI YA SHIRIKISHO LA SOMALIA

**SISI**, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tulikutana katika mkutano wa thelathini na tisa wa Kawaida (39) wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mjini Addis Ababa tarehe 14 hadi 15 Februari 2026;

**TUKITHIBITISHA TENA** heshima ya AU kwa ajili ya kulinda uhuru, haki ya kulinda mipaka, umoja na utulivu wa Jamhuri ya Shirikisho ya Somalia;

**TUKIREJELEA** kanuni zilizoainishwa katika Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika, hasa Ibara ya 3(b) kuhusu ulinzi wa uhuru, ulinzi wa mipaka na uhuru wa Nchi Wanachama, na Ibara ya 4(b) kuhusu kuheshimu mipaka iliyopo wakati wa kupata uhuru;

**TUKITHIBITISHA KWA DHATI** dhamira yake isiyoyumba kwa uhuru, umoja, na ulinzi wa mipaka ya Jamhuri ya Shirikisho la Somalia, kwa mujibu wa Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika, haswa Ibara ya 4 ya Protokali Inayohusiana na Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa;

**TUKITHIBITISHA** dhamira ya muda mrefu ya Umoja wa Afrika na mtangulizi wake, Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU), kuhusiana na kanuni ya kutobadilisha mipaka iliyorithiwa, kama ilivyoahidiwa kwa dhati na Nchi zote Wanachama katika Azimio la AHG/Res. 16(I) lililopitishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali katika Mkutano wake wa Kwanza wa Kawaida mjini Cairo, Misri, kuanzia tarehe 17 hadi 21 Julai 1964;

**Tunaazimia masuala yafuatayo**:

1. **TUNAELEZA KWA MASIKITIKO MAKUBWA** kuhusu utambuzi wa upande mmoja wa "Jamhuri inayoitwa Somaliland" na Israeli kama nchi huru ambayo inatishia uhuru, haki ya kulinda mipaka, umoja na utulivu wa Jamhuri ya Shirikisho la Somalia;

2. **TUNALAANI VIKALI na KUPINGA** vitendo vyote vya wahusika wa nje, hasa utambuzi wa upande mmoja wa "kinachoitwa Jamhuri ya Somaliland" na Israeli kwa maneno makali na **KUTOA WITO** wa kufutwa kwake mara moja;

3. **TUNAIDHINISHA KIKAMILIFU** Taarifa ya Baraza la Amani na Usalama (PSC) la Umoja wa Afrika (AU) [PSC/MIN/COMM.1324 (20260] lililopitishwa tarehe 6 Januari 2026 katika ngazi ya Mawaziri, ikilaani na kukataa kutambuliwa kwa upande mmoja kwa ‘kinachoitwa Jamhuri ya Somaliland’ na Israeli; na kauli ya Mhe. Mahmoud Ali Youssouf, Mwenyekiti wa Kamisheni, iliyotolewa tarehe 26 Desemba 2025, ikikataa mpango wowote au hatua inayolenga kutambua eneo la kaskazini mwa Somalia (Somaliland) kama taifa huru, suala ambalo liinapingana

na kanuni za msingi za Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa na kuweka mfano hatari wenye athari kubwa kwa amani na utulivu kote barani;

4. **TUNASISITIZA** kwamba hakuna mhusika aliye na mamlaka au nafasi ya kubadilisha muundo wa eneo la Nchi Mwanachama wa AU, na kwamba tamko lolote kama hilo ni batili, na halina nguvu za kisheria chini ya sheria ya kimataifa;

5. **TUNATAMKA** kwamba jaribio lolote la kubadilisha mipaka kwa nguvu au kwa njia isiyo halali, au kudhoofisha umoja na ulinzi wa eneo ya Nchi Mwanachama wa AU, linakiuka Sheria Anzilishi na linahatarisha kuweka mfano hatari wenye athari kubwa kwa amani, usalama, na utulivu kote barani.

6. **TUNASIKITIKA** kwamba vitendo kama hivyo vinaweza kutishia amani na utulivu katika eneo la Pembe ya Afrika, kuzuia mipango ya pamoja ya usalama, na kuweka mfano usiokubalika ambao hauendani na kanuni zilizopo;

7. **TUNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama zote na washirika wa kimataifa kuthibitisha tena uhuru na umoja wa Somalia, kukataa vitendo vyote haramu vinavyodhoofisha kanuni hizi, na kuwa na mshikamano ili kudumisha umoja wa Afrika

**TAMKO KUHUSU RIPOTI KAMILI YA TANO YA MAPITIO YA MIAKA MIWILI (BR) YA MPANGO WA MAENDELEO YA KILIMO AFRIKA (CAADP)**

**Mkutano Mkuu**,

**SISI**, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tulikutana katika Mkutano wetu wa Thelathini na Tisa wa Kawaida mwezi Februari 2026,

**Tukirejelea** Azimio la Malabo kuhusu Ukuaji wa Kilimo na Mageuzi ya Haraka kwa Ustawi wa Pamoja na Maisha Bora (Assembly/AU/Decl.1(XXIII)), lililopitishwa mwezi Juni 2014, ambalo liliamuru Mapitio ya Miaka Miwili kama utaratibu mkuu wa uwajibikaji kwa utekelezaji wa CAADP.

***Tukirejelea Zaidi*** Azimio la CAADP la Kampala lililopitishwa Januari 2025, ambalo lilithibitisha tena dhamira ya Nchi Wanachama kuhusiana na mageuzi ya mifumo ya kilimo chini ya Ajenda 2063.

*T**ukizingatia*** Ripoti ya Tano ya Mapitio ya Miaka Miwili ya CAADP, iliyowasilishwa kwenye Kikao cha Sita cha Kawaida cha Kamati Maalum ya Kitaalamu ya Kilimo, Maendeleo Vijijini, Maji na Mazingira (STC ARDWE), kilichofanyika Addis Ababa, Ethiopia, kuanzia tarehe 21–24 Oktoba 2025 na kuidhinishwa baadaye na Baraza Kuu.

**TUNAAAMUA kama ifuatavyo**:

1. **TUNAPITISHA** Ripoti ya Tano ya Mapitio ya Miaka Miwili ya CAADP kama tathmini rasmi ya bara ya maendeleo chini ya Azimio la Malabo.

2. **TUNAPITISHA** CAADP kama mradi mkuu wa Ajenda 2063.

3. **TUNATOA WITO KWA** Nchi Wanachama kutumia matokeo ya Ripoti ya Tano ya Mapitio ya Miaka Miwili ili kuchochea mazungumzo ya sera za kitaifa na kikanda, kuimarisha uwajibikaji, na kuharakisha utekelezaji wa ahadi za mageuzi ya kilimo.

4. **TUNAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC), AUDA NEPAD, na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs) kutoa msaada wa kitaalamu ulioratibiwa kwa Nchi Wanachama katika kushughulikia mapengo yaliyotambuliwa katika Ripoti, hasa katika ubora wa data, utafutaji wa rasilimali, na uwezo wa kitaasisi.

5. **TUNAZIHIMIZA** RECs kuendelea kuimarisha mifumo ya mapitio ya pamoja na michakato ya uwajibikaji wa pande zote, kuhakikisha kwamba matokeo ya Mapitio ya Miaka Miwili yanasaidia mipango ya uwekezaji jumuishi wa kikanda na mifumo ya kilimo.

6. **TUNAIELEKEZA** AUC, AUDA NEPAD, na Nchi Wanachama kuunganisha michakato ya Mapitio ya Miaka Miwili katika mifumo ya kitaifa ya takwimu, ufuatiliaji, na tathmini, na kuioanisha na Mipango ya Kitaifa ya Uwekezaji kwenye Kilimo (NAIPs) na Mapitio ya Pamoja ya Sekta (JSRs).

7. **TUNAWAOMBA** washirika wa maendeleo kutoa msaada wa kitaalamu na kifedha kwa Nchi Wanachama, RECs, na AUC kwa ajili ya usambazaji na matumizi bora ya Ripoti ya Tano ya Mapitio ya Miaka Miwili.

8. **TUNAIELEKEZA ZAIDI** Kamisheni kuwasilisha kwa Mkutano Mkuu, katika Mkutano wake wa Arobaini wa Kawaida, ripoti ya maendeleo iliyojumuishwa kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yanayotokana na Mapitio ya Tano ya Miaka Miwili.

9. **TUNATOA SHUKRANI** kwa Mhe. Dkt. Abiy Ahmed, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia na Kinara wa CAADP kwa uongozi wake na **TUNAOMBA** kuwasilishwa kwa ripoti ya mapitio ya kila baada ya miaka miwili kuhusu Azimio la Kampala kwenye Mkutano wa 41 wa Wakuu wa Nchi na Serikali.

# TAMKO KUHUSU USHIRIKI WA AFRIKA NA USHIRIKI WA JAMHURI YA AFRIKA KUSINI KATIKA G20
**Doc. EX.CL/1683(XLVIII)**

**Sisi**, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tukikutana katika Mkutano wake wa Kawaida wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, uliochofanyika Addis Ababa, Ethiopia, tarehe 21 Februari 2026,

**TUKIREJELEA** Sheria anzilishi ya Umoja wa Afrika na ahadi ya Umoja kuhusu ushirikiano wa kimataifa, ujumuishi, usawa kati ya Nchi, na utawala wa dunia unaotegemea makubaliano;

**TUKIREJELEA PIA** Maamuzi na Matamko ya awali ya Mkutano wa Baraza Kuu yakithibitisha ushirikiano wa pamoja wa Afrika katika majukwaa ya utawala wa uchumi wa dunia, ikiwamo Kundi la Ishirini (G20);

**TUKITAMBUA** jukumu na wajibu unaokua wa Afrika katika kuunda matokeo ya uchumi, kifedha, na maendeleo duniani, kwa mujibu wa Ajenda 2063.

**Kutambua Urais wa G20 wa Afrika Kusini**

**TUNAPONGEZA KWA SHUKRANI KUBWA Urais** wa **G20 wa Jamhuri ya Afrika Kusini**, kwa uongozi wake katika kusukuma mbele vipaumbele vinavyolenga maendeleo, ujumuishi, na mustakabali katika mfumo wa G20;

**TUKITAMBUA** mafanikio makubwa ya Urais wa G20 wa Afrika Kusini, yakiwamo miongoni mwa mengine:

1. Kukuza **maendeleo, ukosefu wa usawa, na ukuaji jumuishi** kuwa nguzo kuu za majadiliano ya G20;
2. Kuimarishwa kwa mkazo kwenye mahitaji ya **upatikanaji wa fedha za maendeleo ya Afrika,** uimara wa deni, na mageuzi ya usanifu wa kifedha wa kimataifa;
3. Kukuza ushirikiano wa Ushirikiano wa Kusini–Kusini na sauti ya uchumi unaokua ndani ya utawala wa uchumi wa dunia;
4. Kuimarisha **uendelevu wa taasisi na umiliki** wa pamoja wa matokeo ya G20 katika urais unaofuata;
5. Ushirikiano chanya na mabenki ya maendeleo ya kimataifa, taasisi za kifedha za kimataifa, na mashirika ya kikanda, ikiwamo Umoja wa Afrika**.**

**Suala la Kutokushiriki**

**TUNAELEZEA MASIKITIKO** yetu kuhusu maendeleo ya hivi karibuni ya taratibu yaliyosababisha kutoshiriki kwa Jamhuri ya Afrika Kusini katika baadhi ya michakato ya maandalizi na majadiliano ya G20;
**UNASISITIZA** ushiriki wa Afrika Kusini katika G20 sio tu wa kipekee kitaifa bali pia ni muhimu kimkakati kwa pamoja kwa Afrika na Kusini Duniani;
**UNATAMBUA** kuwa ujumuishi, usawa wa ushiriki, na mfwendelezo wa urais ni kanuni za msingi zinazounga mkono uhalali na ufanisi wa G20;

**Kuthibitisha Upya Misimamo ya AU** (Ikiakisi PRC, Maamuzi ya Baraza Kuu na Serikali, Mkutano Mkuu)

1. **UNATAMBUA** tathmini na mwongozo uliotolewa na Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC);
2. **UNASISITIZA** nafasi ya Baraza Kuu kuwa G20 inabaki kuwa jukwaa la kipekee kwa ushirikiano jumuishi wa Kaskazini–Kusini na Kusini–Kusini;
3. **UNASISITIZA** dhamira ya Wakuu wa Nchi na Serikali katika mfumo wa kimataifa unaotegemea kanuni, ujumuishi, na uwakilishi, ambapo wanachama wote wa G20 washiriki kikamilifu na kwa ufanisi;

**WITO WA WANACHAMA WA G20 NA URAIS UJAO**

4. **UNATOA WITO** kwa wanachama wote wa G20 wote kuzingatia kanuni za ujumuishi, usawa, na makubaliano zinazounga mkono G20;
5. **UNAHIMIZA** ushirikiano chanya na wa kuangalia mbele ili kuhakikisha ushiriki kamili na wa ufanisi wa Afrika Kusini katika michakato yote ya G20;

**Kutambua Uungaji mkono Kutoka kwa Wanachama wa Mwanzo wa G20**

6. **UNATOA SHUKRANI ZAKE** kwa wanachama wa mwanzo wa G20 ambao wameeleza kwa uwazi na kwa uthabiti msaada wao thabiti kwa ujumuishaji wa Afrika Kusini katika majadiliano ya G20;
7. **UNATAMBUA** msimamo wao wa kikanuni unaounga mkono ujumuishi, mfululizo wa urais, na heshima kwa kanuni zilizowekwa za G20;

**Wito kwa Rais wa Marekani**

8. **UNATOA WITO KWA MAREKANI**, katika nafasi yake ya Urais ujao wa G20, kufanya yafuatayo:
   - Kuchukulia kwa uzito maoni yaliyotolewa na wanachama wa mwanzo wa G20;
   - Kuzingatia kanuni za ujumuishi na usawa wa ushiriki;
   - Kuwezesha mipangilio chanya inayoongeza umoja, uhalali, na ufanisi wa G20**.**

**Majukumu ya Kamisheni**

9. **UNAINAOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika

- Kuendelea na ushirikiano wa kikanuni, ulioratibiwa, na usioingiza mzozo na washirika wa G20;
- Kuripoti, pale inapofaa, kwa Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC), Baraza Kuu, na Mkutano Mkuu kuhusu maendeleo yaliyopo;
- Kuhakikisha mshikamano kati ya ushiriki wa Afrika katika G20 na michakato ya kimataifa yenye ujumuishi zaidi.

**Hitimisho**

10. **UNASISITIZA** kuwa ushiriki wa ufanisi wa Afrika katika utawala wa uchumi wa dunia ni muhimu sana katika kushughulikia changamoto za pamoja za kimataifa na kusukuma mbele maendeleo endelevu;
11. **UNASISITIZA** kuwa ujumuishaji wa Afrika Kusini unaimarisha na sio kudhoofisha uhalali, uwakilishi, na umuhimu wa G20 kwa siku za usoni.

# TAMKO LA MKUTANO WA 7 WA URATIBU WA NUSU MWAKA KATI YA UMOJA WA AFRIKA, JUMUIYA ZA KIUCHUMI ZA KANDA NA VYOMBO VYA KIKANDA

**SISI** Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tulikutana tarehe 15 Februari, 2026 katika Mkutano wetu wa 39 wa Kawaida mjini Addis Ababa, Ethiopia;

**TUNAPITISHA** Tamko lililoambatanishwa la Mkutano wa Saba wa Uratibu wa Nusu Mwaka kati ya Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs) na Vyombo vya Kikanda (RMs) uliofanyika tarehe 13 Julai 2025 Malabo, jiji la Sipopo, Guinea ya Ikweta.

# TAMKO
# MKUTANO WA SABA WA NUSU-MWAKA WA URATIBU KATI YA UMOJA WA AFRIKA, JUMUIYA ZA KIUCHUMI ZA KIKANDA NA VYOMBO VYA KIKANDA

**SISI,** Wakuu wa Nchi na Serikali, tukiwakilisha Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika na Wenyeviti wa Jumuiya Nane (8) za Kiuchumi za Kikanda (RECs) pamoja na Vyombo vya Kikanda (RMs), tukikutana hapa Malabo, mji wa Sipopo, Equatorial Guinea tarehe 13 Julai 2025, katika Mkutano wa Saba wa Nusu-Mwaka wa Uratibu unaoongozwa na Mwenyekiti Mhe. **João Manuel Gonçalves Lourenço,** Rais wa Jamhuri ya Angola na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU);

**TUKIREJELEA** matokeo ya Mikutano sita ya awali ya Nusu-Mwaka ya Uratibu, ambapo wa mwisho kati ya mikutano hiyo ulifanyika tarehe 21 Julai 2024 huko Accra, Ghana ambao tamko lake limo katika nyaraka Na. MYCM/AU/ Dec.(VI).

**TUKISISITIZA** haja ya kukuza utangamano wa kina wa bara na ustawi wa pamoja, kwa kuongozwa na matokeo ya Ripoti ya Utangamano wa Kikanda wa Afrika ya mwka 2025, ambayo ilitokana na Ripoti ya Kielezo cha Utangamano wa Kikanda wa Afrika (ASRII).

**TUKITAMBUA** kwamba utendaji thabiti wa utangamano wa Afrika unatokana na usafirishaji huru wa watu, bidhaa na huduma, na uratibu wa uchumi mpana.

**TUKISIKITISHWA** na utendaji wa wastani wa utangamano wa bara kama ilivyodhihirishwa na matokeo ya Ripoti ya Utangamano wa Kikanda Afrika ya mwaka 2025.

**TUKISIKITISHWA PIA** na maendeleo hafifu katika ujumuishaji wa uzalishaji na miundombinu.

**TUNAAZIMIA:**

1. **KUMPONGEZA** Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, **Mhe**. **João Manuel Gonçalves Lourenço,** Rais wa Jamhuri ya Angola, kwa juhudi zake za kukuza amani, usalama na haki za binadamu katika bara la Afrika.

## HALI YA UTANGAMANO

2. **KUZINGATIA** Ripoti ya Kamisheni ya AU kuhusu Utangamano wa Bara la Afrika na **PIA KUZINGATIA na KUPOKEA** Ripoti za Wenyeviti wa Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na Vyomo vya Ulinzi wa Haki kuhusu hali ya Utangamano wa Kikanda kama ifuatavyo:

i. **Mhe. Mohammad Younis Menfi**, Rais wa Baraza la Uongozi la Nchi ya Libya na Mwenyekiti wa Umoja Kiarabu wa Maghreb (AMU);
ii. **Mhe. Mahamat Hii Deby**, Rais wa Jamhuri ya Chad na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Nchi za Sahel-Sahara (CEN-SAD);
iii. **Mhe. William Samoei Ruto**, Rais wa Jamhuri ya Kenya na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC);
iv. **Mhe. Évariste Ndayishimiye**, Rais wa Jamhuri ya Burundi na Mwenyekiti wa Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA)
v. **Mhe. Teodoro Obiang Nguema Mbasogo**, Rais wa Jamhuri ya Guinea ya Ikweta na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika ya Kati (ECCAS);
vi. **Mhe. Brig. Mstaafu Dkt. Julius Maada Bio**, Rais wa Jamhuri ya Sierra Leone na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS);
vii. **Mhe. Ismail Omar Guelleh**, Rais wa Jamhuri ya Djibouti na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Maendeleo ya Kiserikali (IGAD); na
viii. **Mhe**. **Emmerson Dambudzo Mnangagwa**, Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).
ix. **Mhe. Abdel Fattah El-Sisi**, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na Mwenyekiti wa *North African Regional Capability* na **KUIDHINISHA** mapendekezo yaliyomo ndani yake.
x. **Mhe. Hassan Sheikh Mohamud**, Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Somalia, Mwenyekiti wa Mkutano wa Kikosi kaiz cha Dharura cha Afrika mashariki, na **KUIDHINISHA** mapendelkezo yaliyomo ndani yake.

3. **KUTHIBITISHA** dhamira yetu ya utekelezaji kamili wa AfCFTA na Eneo Huria la Biashara ya Utatu (TFTA), tukizitumia ili kuinua utangamano wa kibiashara zaidi ya viwango vya sasa;

4. **KUIOMBA** AUC, RECs na RMs, kutekeleza mapendekezo ya Ripoti za Utangamano wa Kikanda Afrika za mwaka 2025.

**RIPOTI ZA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI NA VINARA WENYE NYADHIFA MAALUM.**

5. **KUZINGATIA** ripoti za Waheshimiwa na Vinara wa Nyadhifa Maalum**:**

i. **Mhe. Abdel Fattah El- Sisi**, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na Mwenyekiti wa Kamati ya Maelekezo ya Wakuu wa Nchi na Serikali (HSGOC) ya Kamati ya Mwelekeo ya Wakala wa Maendeleo wa Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD) na **KUPITISHA** mapendekezo yaliyomo.
ii. **Mhe. Issoufou Mahamadou,** Kiongozi na Kinara wa AfCFTA na Rais wa zamani wa Jamhuri ya Niger, na **KUPITISHA** mapendekezo yaliyomo.

## RIPOTI ZA KAMISHENI YA AU, VYOMBO VYAKE NA WABIA KUHUSU HALI YA UTANGAMANO AFRIKA

6. **KUPOKEA** ripoti ya Mwenyekiti wa AUC kuhusu utangamano wa kikanda na bara na kubainisha maendeleo yaliyopatikana katika mihimili minne ya utangamano, ambayo ni, siasa, uchumi, miundombinu na maendeleo ya watu.

7. **KUBAINI** kwa masikitiko kuibuka upya kwa sera za kulinda masoko ya ndani na kupungua kwa misaada ya maendeleo, kuongezeka kwa mizigo ya madeni, na nafasi finyu ya kifedha ambayo inapunguza uwezo wa Afrika kufadhili uwekezaji katika kuleta mageuzi.

8. **KUBAINI PIA** ukuaji mdogo wa mageuzi ya kidijitali unaotokana na miundombinu duni, ufikiaji usio sawa wa kidijitali, mifumo dhaifu ya udhibiti, na ujuzi mdogo wa kidijitali; na

9. **KUTOA** wito wa kuchukua hatua zifuatavyo:

    **(i)** **Kuharakisha Uridhiaji na Utekelezaji:** Kuhimiza Nchi Wanachama kuridhia na kutekeleza mara moja vyombo muhimu vya kisheria vya AU, hasa vile vinavyohusu usafirishaji huru, utawala, elimu na haki.

    **(ii)** **Kuwekeza katika Rasilimali Watu:** Kuweka kipaumbele katika uwekezaji wa kikanda katika elimu, afya, utafiti, na mifumo ya ujumuishi ya kijamii ili kuoana na Ajenda 2063 na kukuza ukuaji jumuishi.

    **(iii)** **Kuimarisha Uratibu:** Kuhimiza AUC kuimarisha uratibu na umiliki wa mifumo ya bara kati ya RECs na Nchi Wanachama ili kuhakikisha utekelezaji na ufuatiliaji unaofaa.

    **(iv)** **Kukuza Mageuzi ya Kidijitali:** Kushughulikia mapungufu ya miundombinu, kuoanisha sheria za kidijitali, na kuwekeza katika ujuzi wa kidijitali ili kufungua uwezo kamili wa uchumi wa kidijitali barani Afrika.

    **(v)** **Kukusanya Rasilimali Endelevu:** Kubuni mikakati bunifu ya kukusanya rasilimali ili kupunguza utegemezi wa misaada kutoka nje na kupata ufadhili endelevu kwa ajili ya mipango ya ujumuishaji kupitia mgao katika bajeti za kawaida za AUC, RECs na RMs kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 22 ya Protokali ya 2020 kuhusu uhusiano kati ya AU na RECs.

    **(vi)** Kuharakisha utekelezaji wa Mkakati wa Programu ya Kina ya Kilimo Afrika (CAADP) na Mpango Kazi 2026-2035 kwa ajili ya kujenga mifumo ya kilimo na chakula barani Afrika ambayo inahimili mageuzi ya tabianchi pamoja na misukosuko mingine, na ambayo inaendana na maendeleo ya teknolojia.

10. **KUIOMBA** Kamisheni ya AU na washirika kuchapisha ripoti ya maendeleo ya kila mwaka kwa kutumia vipimo vya ASRII, pamoja na vikao vya mapitio ya ukaguzi wa nusu-mwaka ili kuelekeza hatua za kurekebisha.

**KUBAINISHA MAENDELEO YA JIOGRAFIA YA KISIASA NA ATHARI ZAKE KWA AFRIKA- MTAZAMO WA SADC**

11. **KUPOKEA** ripoti na matokeo ya Uchunguzi wa SADC na **KUPITISHA** mapendekezo yaliyomo.

12. **KUBAINI** kwa masikitiko ushuru unaotozwa na Marekani kwa bidhaa zinazozalishwa na kusafirishwa kutoka Afrika.

13. **KUTOA WITO** kwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kutumia fursa zinazotolewa na AfCFTA na kufanya biashara baina yao zaidi.

**MPANGO WA AU WA KUBADILISHANA MAARIFA BAINA YA KANDA (I-RECKE) KUHUSU TAHADHARI YA MAPEMA NA KUZUIA MIGOGORO**

14. **KUZINGATIA** kuitishwa kwa Kikao cha Nne cha Sera cha Mpango wa Umoja wa Afrika wa Kubadilishana Maarifa baina ya Kanda (I-RECKE) kuhusu Tahadhari ya Mapema na Kuzuia Migogoro, kilichofanyika pembezoni mwa Mkutano wa Saba wa Nusu-Mwaka wa Uratibu chini ya kaulimbiu *"Kuzuia Migogoro ya Kimfumo*: *Mambo ya Kujifunza kwa Bara na Kanda", na* **KUPOKEA** ripoti ya Mkutano.

15. **KUTAMBUA** umuhimu wa kuzuia migogoro ya kimfumo na haja ya kutendesha mwendelezo wa hatua za tahadhari-hadi- mapema kwa AU na RECs/RMs; katika suala hili, **KULIPONGEZA** jukwaa la I-RECKE kwa kuendeleza mbinu za pamoja, kushirikisha mbinu bora, na kukuza uwiano wa kimkakati katika kusaidia juhudi za Nchi Wanachama kushughulikia vyanzo vya migogoro, hasa ndani ya muktadha wa Ajenda 2063 na Ramani Ongozi ya Njia ya AU kuhusu Kunyamazisha Bunduki;

16. **KUPONGEZA** kuanzishwa kwa Mkakati wa Pamoja wa Uhamasishaji wa Rasilimali za AU-RECs/RMs kwa ajili ya Utawala, Amani na Usalama kama ufuatiliaji wa moja kwa moja wa matokeo ya Kikao cha Tatu cha Sera cha I-RECKE; na **KUTAMBUA** thamani yake ya kimkakati katika kuendeleza mbinu iliyoratibiwa na endelevu ya kushughulikia vipaumbele vya utawala, amani na usalama katika bara zima. Mkakati hu unaonesha dhamira ya pamoja ya Umoja wa Afrika na RECs/RMs ya kuimarisha uwezo wa kujitegemea, kukuza ufadhili wa ziada, na kuimarisha uendelevu wa muda mrefu wa afua, katika kukabiliana na changamoto zinazozidi kuwa tata na zilizounganishwa ambazo zinahitaji hatua za pamoja na ushirikiano katika ngazi zote;

17. **KUIOMBA** Kamisheni, kwa kushirikiana na RECs/RMs na wadau husika, kuharakisha utekelezaji wa matokeo ya Kikao cha Nne cha Sera, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Mkakati wa Pamoja wa Kukusanya Rasilimali, na kuwasilisha ripoti ya hatua iliyofikiwa katika Mkutano wa Nane wa Nusu-Mwaka wa Uratibu.

**RIPOTI KUHUSU HALI YA MGAWANYO WA KAZI KATI YA UMOJA WA AFRIKA, JUMUIYA ZA KIUCHUMI ZA KANDA/VYOMBO VYA KIKANDA NA NCHI WANACHAMA**

**18.** **KUPOKEA** ripoti ya Mhe. Profesa **Pierre** Mbonjo Moukoko, Mkuu wa Kitengo cha Utekelezaji wa Mageuzi cha Kamisheni ya AU, na mapendekezo yaliyomo;

**19.** **KUPOKEA** hatua zilizofikiwa katika utendeshaji wa mpango wa Mgawanyo wa Kazi, hasa kukamilisha na kusambaza awamu ya kwanza inayohusu Masuala ya Kisiasa, Amani na Usalama, na Biashara. Pia tunahimiza utekelezaji wa haraka wa sekta hizi tatu zilizopitishwa na pia kuthibitisha dhamira yetu ya pamoja ya kuwa na utawala ulioanishwa, unaofaa na wenye msingi-saidizi katika kuunga mkono Ajenda 2063;

**20.** **KUPITISHA** kuitishwa kwa Mkutano Mkuu Maalum wa Maboresho ya AU mwezi Novemba 2025 ambao, pamoja na mambo mengine, utakamilisha na kupitisha sekta tano zilizosalia za Mpango wa Mgawanyo wa Kazi kwa kufuata taratibu muafaka za Vyombo vya Umoja wa Afrika, ikiwa ni pamoja na PRC na Baraza Kuu;

**21.** **KUHIMIZA Vyombo vyote vya AU, RECs/RMs, na Nchi Wanachama kuthibitisha utashi wao wa kisiasa na kuharakisha kuwasilisha maoni ambayo hayajawasilishwa kufikia mwezi Agosti 2025.**

**RIPOTI KUHUSU KAULIMBIU YA MWAKA**

**22.** **TUNAPOKEA,** kwa shukrani, ripoti iliyowasilishwa na Mhe. Selma Malika Haddadi, Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni, na **KUPITISHA** mapendekezo yaliyomo;

**23.** **TUNAZINGATIA** hatua iliyofikiwa katika uratibu wa mfumo mzima na kujumuishwa kwa kaulimbiu katika mfumo wote wa AU, katika maendeleo ya kitaasisi ya vyombo vilivyopewa majukumu hayo, katika juhudi zinazolenga kuandaa ajena hiyo, kujenga uelewa na hamasa katika majukwa ya kimataifa na wadau, pamoja na kujenga mashirikiano hasa na Jamii ya Karibian.

**24.** **TUNATOA WITO** wa kukusanya raslimali za ziada, ikiwa ni pamoja na kupitia michango ya hiyari, kwa ajili ya utekelezaji kamilifu wa kazi zilizopangwa na mkutano mkuu na matokeo yanayotakiwa kuhusiana na Kaulimbiu ya Mwaka 2025, ambayo inatakiwa kupanuliwa na kujumuisha Muongo (2026-2036) wa Haki kwa Waafrika na Watu wenye Asili ya Afrika kwa njia ya Fidia.

**AUDA-NEPAD**

**25.** **KUPOKEA KWA SHUKRANI** ripoti ya Mhe. Abdel Fattah El- Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na Mwenyekiti wa Kamati ya Maelekezo ya Wakuu wa Nchi na Serikali (HSGOC) wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA NEPAD) kuhusu Wajibu wa AUDA-NEPAD katika Kuimarisha Utangamano wa Bara na Kanda kwa kushirikiana na RECs, na **KUPITISHA** mapendekezo yaliyomo.

**26.** **KUTHIBITISHA** jukumu kubwa la uratibu la AUDA-NEPAD kuhusiana na shughuli zote za maendeleo za kikanda na bara la Afrika, kwa mujibu wa mamlaka yake kama wakala mkuu wa maendeleo wa Umoja wa Afrika.

**27.** **KUHIMIZA** Nchi Wanachama, RECs, na washirika kuimarisha uwezo wa kitaasisi katika kupangilia vipaumbele, uchambuzi tabirifu, ufuatiliaji na tathmini, kuimarisha maarifa, na mawasiliano na uhamasishaji ili kuharakisha utekelezaji wa Mpango wa Miaka Kumi ya Pili ya Utekelezaji (STYIP).

**28.** **KUTOA WITO** kwa AUC na AUDA-NEPAD kuharakisha mchakato wa uandaaji, utekelezaji na utoaji taarifa za Mpango wa Miaka Kumi ya Pili ya Utekelezaji (STYIP) wa Ajenda 2063 katika ngazi za kanda na taifa, hasa kwa kuimarisha uwezo wa Nchi Wanachama na RECs, na kupeleka nyenzo muhimu - kama vile Kijitabu cha Viashiria vya Agenda 2063, Mwongozo Ufuatiliaji na Tathmini (M&E), Dashibodi ya Ajenda 2063, na Mkakati wa Mawasiliano na Uhamasishaji - ili kuharakisha utekelezaji na kufuatilia maendeleo.

**29.** **KUHIMIZA** Nchi Wanachama, RECs, na washirika kutumia Jukwaa la Dijitali la Agenda 2063 kama hazina kuu ya bara la kuripoti uratibu, usambazaji wa maarifa, na ufuatiliaji wa maendeleo ya Mpango wa Miaka Kumi ya Pili ya Utekelezaji.

**30.** **KUPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa kuanzisha na kuendeleza, kwa pamoja na AUC na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs), Kampeni ya Timu ya Afrika ya Ukusanyaji wa Rasilimali, iliyozinduliwa katika Mkutano wa 5 wa Nusu-Mwaka wa Uratibu uliofanyika Nairobi, Kenya, Julai 2023, kwa ushirikiano na AfCFTA, Africa CDC, APRM na PAP, ambayo inatumika kama utaratibu wa pamoja kwa ajili ya uoanishaji, utekelezaji na uhamasishaji wa rasilimali kama njia ya Mipango ya Uwekezaji yenye Matokeo ya Hali ya Juu inayolenga kuharakisha utekelezaji wa STYIP; na **KUPOKEA** uidhinishaji wa Mkutano wa 7 wa Nusu-Mwaka wa Uratibu wa Nyaraka Programu ya Timu ya Afrika, ikiashiria kuanza kwa awamu ya utendaji wa Kampeni, pamoja na utekelezaji utakaofanywa kwa ushirikiano na RECs na kwa msaada wa washirika wa maendeleo, Benki za Maendeleo za Kimataifa, na sekta binafsi.

**SHUKRANI**

31. **KURIDHISHWA na** juhudi zinazofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Guinea ya Ikweta katika kufanikisha Mkutano wa Saba wa Nusu-Mwaka wa Uratibu kati ya Umoja wa Afrika, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na Vyombo vya Kikanda.

**Limefanyika tarehe 13 Julai 2025 mjini Malabo, Guinea ya Ikweta**

# TAMKO LA MKUTANO WA PILI WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI KUHUSU TABIANCHI AFRIKA (ACS2)

**SISI** Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tulikutana tarehe 15 Februari 2026 katika Mkutano wetu wa 39 wa Kawaida mjini Addis Ababa, Ethiopia;

**TUNAPITISHA** Tamko lililoambatanishwa la Mkutano wa Pili wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu tabianchi Afrika (ACS2) uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, kuanzia tarehe 8 hadi 10 Septemba 2025.

## [1] TAMKO LA MKUTANO MKUU WA PILI WA AFRIKA KUHUSU TABIANCHI (ACS2)

## TAMKO LA ADDIS ABABA LA VIONGOZI WA AFRIKA JUU YA MABADILIKO YA TABIANCHI NA WITO WA KUCHUKULIWA HATUA HATUA

### A. DIBAJI

**Sisi**, Wakuu wa Nchi na Serikali za Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, tukiongozwa na kanuni za Ajenda 2063 na malengo ya maendeleo endelevu, tulikusanyika kwa ajili ya mkutano mkuu wa pili wa Afrika kuhusu Tabianchi (ACS2) mjini Addis Ababa, Ethiopia, kutoka tarehe 8 hadi 10 Septemba 2025, pia walikuwepo viongozi wengine wa Kimataifa, kiserikali, mashirika, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, mashirika ya Umoja wa Mataifa, sekta binafsi, mashirika ya kiraia, Wazawa, wenyeji, Vyama vya ushirika vya wakulima, watoto, vijana, wanawake na wasomi, hapa tuna:

1. **TUNAREJEA** maamuzi ya Mkutano mkuu Assembly(AU/December 723(XXXII), Assembly/AU/December 764 (XXXIII) na Assembly/AU/December 926(XXXVIII) yaliyoiomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuandaa Mkutano wa Kilele wa Afrika kuhusu hali tabianchi na kuidhinisha ofa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho ya Ethiopia ya kuandaa Mkutano mkuu wa pili chini ya kaulimbiu, Kuharakisha Masuluhisho ya Tabianchi Duniani na Ufadhili kwa Maendeleo ya Kijani na Uhimilivu wa Afrika ;

2. **TUNAIPONGEZA** Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia, chini ya uongozi wenye maono wa Mh. Waziri Mkuu Dkt. Abiy Ahmed na mwenyeji wa Mkutano wa Pili wa Tabianchi wa Afrika (ACS2), na kwa kujitolea kwake kwa utunzaji wa mazingira kama inavyoonyeshwa na Mpango wa Urithi wa Kijani, mwitikio wa ndani ambao umehamasisha mamilioni kote Ethiopia kupanda mabilioni ya miti, kurejesha mandhari zilizoharibika, na kuhamasisha harakati za bara kuelekea urejeshaji wa ikolojia;

3. **TUNAZINGATIA** kwamba Mkutano mkuu wa Pili wa Afrika kuhusu Tabianchi ni mwendelezo wa Mkutano wa Uzinduzi uliofanyika jijini Nairobi, Kenya, kutoka tarehe 4-6 Septemba 2023 , ambao ulipitisha Azimio la Viongozi wa Kiafrika la Nairobi kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na wito wa kuchukua hatua.

4. **TUNATAMBUA** ahadi zilizotolewa katika Azimio la kwanza la Viongozi wa Afrika jijini Nairobi lililosisitizia haja ya Kudai haki ya mazingira, usawa ufadhili, na hatua za haraka za kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa;

5. **TUNATHIBITISHA** tena kwamba mabadiliko ya tabianchi ni kizidishi cha hatari kinachozidisha shinikizo kwenye maliasili, na kuathiri amani na

utulivu;

6. **TUNASISITIZA** umuhimu wa kukamilisha na kuanza kuufanyia kazi msimamo wa pamoja wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Amani na Usalama (CAP-CPS) kama hatua muhimu na chombo cha utetezi kuelekea mwitikio wa pamoja na wa kimkakati wa bara kwa changamoto hizi zinazohusiana;

7. **TUNASISITIZA** kwamba Afrika si tu mwathirika wa mabadiliko ya tabianchi bali ni nguvu inayotokana na rasilimali na inayofanya kazi katika kutengeneza masuluhisho bunifu, endelevu, na jumuishi yanayoakisi nguvu na matarajio ya kipekee ya bara; na hivyo kuibadilisha Afrika ili kujitahidi kuwa kitovu cha kimataifa cha utengenezaji wa kaboni kidogo na biashara ya kijani ndani ya Afrika, kwa kutumia mifumo kama vile Eneo la Biashara Huria la Bara la Afrika (AfCFTA) ili kuwezesha na maendeleo jumuishi ya kiuchumi kote barani Afrika, na kuweka juhudi za kuendeleza njia ya 'kijani kwanza' kwa maendeleo ya kiuchumi ;

8. **TUNATAMBUA** kwamba nchi za Kiafrika, licha ya mchango wao mdogo katika uzalishaji wa gesi chafu duniani, ndizo zilizoathiriwa zaidi na athari za mabadiliko ya tabianchi na hazina uwezo wa kukidhi gharama za kukabiliana na hali hiyo, uhimilivu, maendeleo endelevu na kupunguza athari zake, na tunathibitisha umuhimu wa kuharakisha hatua za uhamiaji kutoka kwa Washirika, huku nchi zilizoendelea zikiongoza kupunguza ongezeko la halijoto duniani hadi chini ya nyuzi joto 2 juu ya viwango vya kabla ya viwanda na kujitahidi kuweka kikomo cha ongezeko la halijoto la nyuzi 1.5 kwa msingi wa usawa, kwa kuzingatia mchango wa kila nchi husika;

9. **TUNATAMBUA** jukumu muhimu la misitu barani Afrika, hasa msitu wa mvua wa Bonde la Kongo, katika kudhibiti mabadiliko ya tabianchi duniani;

10. **TUNATAMBUA** kazi za Tume tatu za Mabadiliko ya Tabia nchi kwaajili ya Bonde la Kongo, Nchi za Saheli na Nchi za Visiwa - mpango uliozinduliwa wakati wa COP22 na kuandaliwa na Ufalme wa Moroko huko Marrakech, unatambua zaidi michango ya miradi mingine inayoshughulikia na tabianchi ya Afrika kama vile Mpango wa Kukabiliana na Marekebisho Afrika (AAI), Mpango wa Nishati Jadidifu Africa(AREI), Mpango wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kilimo cha Afrika (AAA), Ushirikiano wa Kuharakisha Nishati Jadidifu barani Afrika(APRA), na Mpango wa Maendeleo ya Viwanda Rafiki kwa Mazingira barani Afrika (AGII); na tunakaribisha Mpango wa Nishati Safi ya Kupikia uliozinduliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mpango wa kuunganisha watu milioni 300 na umeme ifikapo 2030 na zaidi tunatambua mipango ya ushirikiano katika ngazi ndogo za kikanda na za nchi inayolenga mipango ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza athari;

11. **TUNAIPONGEZA** Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika ya Mabadiliko ya Tabia nchi (CAHOSCC), chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. William Ruto wa Kenya, kwa kutoa mbinu ya umoja na uongozi wa kisiasa na ufadhili kwaajili ya Maendeleo ya Mazingira bora ya Afrika na ukuaji thabiti;

12. **TUNATHIBITISHA** tena utayari wetu wa kuhakikisha ufanisi wa mbinu ya pande nyingi katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi kupitia Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) na Mkataba wake wa Paris, na kurudia azimio letu la kuyatekeleza kwa mujibu wa kanuni na vifungu vya Mkataba huo, huku tukisisitiza kufikiwa kwa maendeleo endelevu, haki ya maendeleo, na kutokomeza umaskini barani;

13. **TUNAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.883(XXXVII), ambao unaiomba AUC kuanzisha mchakato wa kuzindua Mfuko wa Afrika wa Mabadiliko ya Tabianchi ;

14. **TUNASIKITISHWA SANA** kwa kuwa Afrika inapata mabadiliko ya tabianchi kwa kasi zaidi duniani kuliko sehemu zingine na kwamba, ikiwa hayatadhibitiwa, mabadiliko ya tabianchi yataendelea kuathiri vibaya ukuaji wa uchumi wa Afrika kama ilivyothibitishwa na Ripoti ya Tathmini ya Sita ya Jopo la Serikali Mbalimbali kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (AR6 ya IPCC); tunathibitisha kwamba hatua zinazochukuliwa "zinatoa kipaumbele cha usawa, haki ya tabianchi, haki ya kijamii na ujumuishaji," zinaongoza kwa matokeo endelevu zaidi; na tunatambua kwamba nchi za Kiafrika, licha ya kuchangia kidogo zaidi katika uzalishaji wa gesi chafu duniani, zinakabiliwa na changamoto kubwa katika ufadhili wa juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza athari zake;

15. **TUNATAMBUA** jukumu muhimu la hali ya hewa imara, inayoweza kutekelezwa, sayansi inayoendana na mazingira ya Afrika katika kutoa taarifa kulingana na sera zinazojikita katika ushahidi, kuongoza uwekezaji wenye tija, na kupima maendeleo kuelekea malengo yetu ya tabianchi na maendeleo. Tunasisitiza kuziba pengo la data na kuimarisha uwezo wa kisayansi kote Barani Afrika ni muhimu katika kubuni hatua zinazofaa na zenye usawa.

16. **TUNATAMBUA** kazi inayoendelea ya Awamu ya Tathmini ya Saba ya IPCC (AR7), ambayo inalenga kuboresha zaidi sayansi ya tabianchi, tathmini ya athari, na mwongozo wa masuluhisho ya hali ya hewa yenye usawa na ufanisi kwa maeneo yaliyo hatarini kama vile Afrika.

17. **TUNATAMBUA** ripoti ya mchango muhimu wa Jopo la Serikali Mbalimbali la Mabadiliko ya Tabianchi katika kutoa taarifa za hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuanzisha Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa

Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi na makubaliano yake ya Paris, na mchango wake katika hesabu ya kwanza ya hisa duniani;

18. **TUSISITIZA** haja ya haraka sana ya kujumuisha uhimilivu wa tabianchi katika mikakati ya amani na usalama wa Afrika, kuimarisha mapema mifumo ya onyo na mifumo ya uokozi wa haraka, na kuhakikisha mshikamano kati ya tabianchi, usalama, biashara, uwekezaji, na ajenda za maendeleo; na tunasisitiza kwamba majanga ya tabianchi huvuruga biashara ya mipakani, minyororo ya usambazaji, na miundombinu, huku mtiririko mdogo wa uwekezaji ukipunguza uwezo wa Afrika kufanya mapinduzi ya kiviwanda.

19. **TUNATHIBITISA** tena utayari wetu usioyumba wa utekelezaji kamili wa UNFCCC na Mkataba wake wa Paris na kwa kuimarisha malengo Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabia nchi, kupitia hatua kabambe na zenye usawa za kupunguza, kukabiliana na tabianchi, na unapaswa kuwezeshwa na nchi tajiri kutekeleza hatua zake za kukabiliana na tabianchi kwa kuchangia vitendea kazi vya utekelezaji wake na kuongozwa na kanuni za usawa na majukumu ya kawaida lakini tofauti na uwezo husika kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Paris. Katika maadhimisho ya miaka kumi ya kupitishwa kwa Mkataba wa Paris, tunasherehekea umuhimu wake wa kudumu na kusisitiza umuhimu wa kuhakikisha utekelezaji wake kamili, mzuri, na wa kasi.

20. **TUNAZINGATIA** kwamba nchi za Kiafrika, licha ya mchango wao mdogo katika uzalishaji wa gesi chafu duniani, hazina uwezo wa kukidhi gharama za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza athari zake;

21. **TUNAOMBA** mchango mkubwa zaidi wa jumuiya ya kimataifa na ushirikiano ili kuziba pengo la kifedha, vipaumbele vya michango jumla ya fedha za kukabiliana na tabianchi ielezekezwe moja kwa moja katika nchi maskini(LDC) na Nchi Zinazoendelea za Visiwa Vidogo (SIDS);

22. **TUNASISITIZA** umuhimu wa ushirikiano wa kikanda katika utafiti, uvumbuzi, na ubadilishanaji wa maarifa, mifumo imara ya ufuatiliaji, na ushirikianoimara zaidi kati ya mataifa ya Afrika, ambao utaharakisha maendeleo yanayostahimili mabadiliko ya tabianchi;

23. **TUNASISITIZIA** tena umuhimu wa umoja wa Afrika katika mchakato wa mazungumzo juu ya tabia nchi, hasa kuelekea Mkutano mkuu wa COP30 katika mji wa Belem, Brazili, kwa kuimarisha jukumu la Afrika katika kuunda maamuzi ya kimataifa, hasa kulingana na matokeo ya COP29 huko Baku, hasa uamuzi kuhusu lengo jipya la pamoja lililopimwa la ufadhili wa tabianchi.

## B. UFADHILI WA TABIANCHI UNAOWEZA KUPANULIWA

24. **TUNATHIBITISHA** tena Agenda ya Addis Ababa ya Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Ufadhili wa Maendeleo ni sehemu muhimu ya Ajenda 2030 na kwamba utekelezaji wake kamili ni muhimu kwa ajili ya kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na malengo yake, na kuzingatia Mkutano wa nne wa Kimataifa wa Ufadhili kwa Ajili ya Maendeleo, unaoshughulikia changamoto za sasa na zinazoibuka za ufadhili ili kushughulikia mapengo katika usanifu wa deni, mageuzi ya usanifu wa fedha wa kimataifa, na mchakato wa Mkataba wa kodi wa kimataifa.

25. **TUNASISITIZA** umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa wa pande nyingi uliojikita katika chata na misingi ya Umoja wa Mataifa , sisi tunasisitizia umuhimu wa Ushirikiano wa kimataifa kwa kushughulikia changamoto za kimataifa kama vile mabadiliko ya tabianchi ndani ya mfumo wa maendeleo endelevu, haki ya maendeleo, na kuondoa umaskini.

26. **TUNATAMBUA** kwamba misaada ya kifedha inayotolewa na nchi zilizoendelea kiviwanda ni takwa la kisheria na sio hisani, kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi na Mkataba wake wa Paris.

27. **TUNATAMBUA ZAIDI** kwamba Afrika inahitaji zaidi ya Dola za Marekani trilioni tatu kwaajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi mwaka 2030, lakini imepokea dola bilioni 30 pekee kati ya 2021 na 2022, tunaomba ushirikiano imara zaidi wa kimataifa ili kuziba pengo la ufadhili na kuunga mkono marekebisho, uhimilivu, na maendeleo endelevu, na tunatoa wito wa mageuzi ya haraka katika mifumo ya ufadhili wa tabianchi ili kuhakikisha usawa, utoshelevu, upatikanaji, na uwezo wa kumudu gharama, na tukiweka msisitizo zaidi katika upatikanaji wa ruzuku badala ya mikopo kwa epuka kuzidi kwa mzigo wa madeni, na fedha hizo kutolewa kwa wakati sahihi.

28. **TUNAKARIBISHA** mwongozo wa Baku na Belem wa Dola za Marekani Trilioni 1.3 kama hatua ya kuziba pengo la fedha tukisisitizia umuhimu wa ufadhili zaidi, unaotegemea ruzuku na wenye masharti nafuu kwa ajili ya mahitaji ya kukabiliana na hasara barani Afrika, tunasisitiza kwamba utoaji wa fedha lazima uepuke mifumo inayounda madeni ambayo itakuwa sehemu ya mageuzi ya usanifu wa fedha wa kimataifa na kutoa wito kwa nchi zilizoendelea kuwa mstari wa mbele katika kusimamia utekelezaji mzuri wa lengo hilo.

29. **TUNATHIBITISHA** tena umuhimu wa ufadhili wa Afrika kupitia taasisi zetu za fedha za bara, na tunatoa wito kwa Nchi Wanachama kuharakisha kukamilisha taratibu za kuridhia vyombo vya uanzishaji wa taasisi hizi, ili kuongeza uwezo wao wa kuhamasisha rasilimali na kusaidia ufadhili wa

afua za mabadiliko ya tabianchi barani Afrika, katika kuhudumia vipaumbele vya bara vya maendeleo na uendelevu.

30. **TUNATAMBUA** mahitaji yanayoongezeka ya Afrika ya karibu dola bilioni 53 za Marekani hadi dola bilioni 106 za Marekani kwa mwaka, na tuna wasiwasi mkubwa sana na utoaji wa fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa mifumo ya mikopo, takriban 53% ya mtiririko wote wa fedha za kukabiliana na mabadiliko kwenda Afrika, huku 69% ikiwa mikopo ya masharti nafuu, wakati inayobaki ilitarajiwa kati ya 2021 na 2022.

31. **TUNASISITIZA** haja ya nchi zilizoendelea kuheshimu ahadi zao za kifedha, kwa kuhakikisha utoaji wa fedha za kutosha, zinazotabirika, na zinazopatikana kwa urahisi chini ya Mkataba na Mkataba wake wa Paris, na kusisitiza hitaji la kutoa rasilimali katika mfumo wa ruzuku, ikiwa ni pamoja na marekebisho na kupunguza madeni, na ufadhili wa masharti nafuu kwa nchi za Afrika, haswa kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, hasara na uharibifu, na hatua za utekelezaji. Tunasisitiza zaidi haja ya kuongeza kiwango cha fedha za tabianchi kwa nchi za Afrika.

32. **TUNAELEZEA MASIKITIKO YETU** kuhusu Lengo Jipya la Pamoja la Ufadhili wa Mabadiliko ya Tabia Nchi (NCQG) la kuhamasisha angalau kiasi cha dola bilioni 300 za Marekani hadi ifikapo 2035, lengo hili halifikii mahitaji ya utekelezaji wa Mashirika ya Maendeleo ya Mataifa ya Afrika (NDCs), inayokadiriwa kiasi cha Dola za Marekani 2.8 trilioni ifikapo 2030, unatakiwa msukumo wa haraka wa utoaji, sambamba na upotezaji na Uharibifu wa Mfuko wa utekelezaji, lakini pia, tuna wasiwasi mkubwa kuhusu viwango vya chini vya matarajio na michango midogo inayoendelea kutolewa kwa Mfuko wa mabadiliko ya Kijani ya Tabia Nchi (GCF), na Mfuko wa Kukabiliana na Mabadiliko na vyombo vingine vya uendeshaji vya utaratibu wa kifedha wa UNFCCC.

33. **TUNASIKITIKA** kwamba mahitaji ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi katika nchi za Afrika yanaongezeka karibia dola bilioni 84 za Kimarekani kwa mwaka, huku mtiririko wa sasa ukipungua hadi dola bilioni 14 za Kimarekani pekee yake kwa mwaka 2021 na 2022, na hivyo kuongeza pengo la fedha za kukabiliana na mabadiliko hayo.

34. **TUNASISITIZA** kwamba uwasilishaji wa marekebisho ya masuala ya kifedha lazima uepuke kusababisha vishawishi vya madeni na kuzingatia mageuzi ya mifumo ya kifedha ya kimataifa, na kutoa wito kwa nchi zilizoendelea kuongoza katika kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa Lengo la Kimataifa la Kukabiliana na Mabadiliko (GGA).

35. **TUNAHIMIZA** kuharakisha mageuzi ya mifumo ya kifedha ya kimataifa ili kukidhi mahitaji ya mabadiliko ya tabia nchi kwa nchi za Afrika na kuboresha uwakilishi, na sauti ya utawala ya Mwafrika, kuwezesha ufikiaji wenye masharti nafuu ya kifedha, na kuwezesha uhimizaji wa mitaji

binafsi katika Afrika kwa ajili ya viwanda vya kijani, mabadiliko ya nishati, na ufadhili wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, uhimilivu, na maendeleo endelevu.

36. **TUNATOA WITO** wa kuharakishwa kwa mageuzi ya Mifumo ya Benki za Maendeleo za Kimataifa (MDBs) ili kuhakikisha inakidhi makusudi ya zama hizi za mabadiliko ya tabia nchi na wao kuongeza makubaliano ya kifedha na masharti nafuu, kupunguza gharama ya kukopa kwa nchi zinazoendelea, na hasa nchi za Afrika, na kurekebisha miundo yao ya utawala ili kuboresha uwakilishi wa Mwafrika. Tunawasihi MDB kuongeza uwekezaji wao katika miradi inayostahimili mabadiliko ya tabia nchi na miradi ya kijani.

37. **TUNAKARIBISHA** utekelezaji wa Ibara cha 6 cha Mkataba wa Paris, kikisisitiza haja ya kupanua masoko ya kaboni yenye uadilifu wa hali ya juu, kuhakikisha kiwango halali cha bei cha lazima ili kuhakikisha thamani kwa nchi mwenyeji, kudumisha uadilifu wa mazingira na kijamii, na kuanzisha mifumo thabiti ya kugawana faida inayotoa kipaumbele kwa jamii za wenyeji na kuhakikisha uwazi.

38. **TUNASISITIZA** umuhimu wa kuanzisha mifumo ya uwazi inayohakikisha faida kwa jamii za wenyeji na kuzuia unyonyaji na watendaji wa nje.

39. **TUNATAMBUA** Mpango wa Utekelezaji wa Afrika wa Masoko ya Kaboni (AAPCM), ambao unalenga kusaidia Nchi wanachama wa AU, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, na Tume ya Afrika ya Tabianchi kwa kuimarisha uwezo na kuanzisha udhibiti imara wa mifumo ya masoko ya kaboni kwa kuhakikisha uadilifu wa mazingira, uwazi, na kugawana faida kwa usawa kwa jamii za Kiafrika, na Tunazihimiza Nchi Wanachama kuimarisha uwezo wao wa kitaifa na kuanzisha mifumo imara ya udhibiti wa masoko ya kaboni ili kuhakikisha uadilifu wa mazingira, uwazi, na kugawana faida kwa usawa kwa jamii za Kiafrika.

40. **TUNAKARIBISHA** kuanzishwa kwa Mkataba wa Ubunifu kuhusu Tabianchi barani Afrika (ACIC) na Kituo cha Hali ya Hewa cha Afrika (ACF), chini ya mpango wa Mheshimiwa Abiy Ahmed, Prime Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Shirikisho la Kidemokrasia ya Ethiopia, kujitolea kukusanya dola bilioni 50 za Marekani kila mwaka katika ufadhili wa kichocheo ili kutetea masuluhisho ya hali ya hewa yanayoharakisha uvumbuzi na kupanua masuluhisho ya hali ya hewa ya ndani kote barani.

41. **TUNATOA WITO** wa kuepuka hatua za upande mmoja zilizotamkwa wakati wa COP 28 na kusisitiza hitaji la nishati safi ya kimataifa ya haki na usawa kulingana na muktadha wa kitaifa, na unaoshughulikia mahitaji ya kipekee ambayo huepuka kuadhibu nchi zinazoendelea, na kwamba sera za biashara lazima ziundwe kupitia ushirikiano wa pande nyingi ili kuakisi majukumu ya pamoja lakini tofauti, na kuwezesha ushiriki wa haki katika

uchumi wa kijani.

42. **TUNAHOFIA** kwamba hatua za upande mmoja, za adhabu, na za kibaguzi za kulinda, ambazo haziendani na sheria za kimataifa, kwa kisingizio cha wasiwasi wa mazingira kama vile Mfumo wa Marekebisho ya Mpaka wa Kaboni wa Umoja wa Ulaya na kanuni za ukataji miti, zinaweka hatua kali kwa mauzo ya nje ya mazao ya kilimo, na kudhoofisha malengo ya hali ya hewa na maendeleo, na mifumo kama hiyo ya nchi zilizoendelea, inaweza kusababisha kushuka kwa mauzo ya nje ya Afrika kwa EU kwa takribani 6% na kupelekea kupungua kwa 1.12% kwa ukuaji Pato la Taifa la Bara, likiwa na athari kubwa zinazotarajiwa kwa muda mrefu zinazodhoofisha malengo ya hali ya hewa na maendeleo, tunatoa wito wa mpito halali wa kimataifa na wa haki unaozingatia muktadha huo kuepuka kuadhibu nchi zinazoendelea, na sera za kibiashara lazima ziundwe kupitia mfumo wa pande nyingi ili kuakisi majukumu ya pamoja lakini tofauti.

## C. UPATIKANAJI WA NISHATI, NISHATI JADIDIFU, NA NISHATI SAFI

43. **TUNATOA WITO** wa haki na usawa wa nishati safi ya kimataifa ambayo inaheshimu kikamilifu misingi ya Azimio la Rio la 1992, ikijumuisha kanuni ya majukumu ya pamoja lakini tofauti na uwezo husika, na ambayo yamejikita katika miktadha ya kitaifa.

44. **TUNATHIBITISHA** tena kwamba Afrika ina uwezo wa kipekee wa kuwa na nishati mbadala unaolifanya bara hili kuwa si mtendaji mkuu pekee bali kiongozi wa kimataifa katika kutoa nishati safi. Kwa kuwa na dhamira ya pamoja ya kufikia 300 GW na kuwa na uwezo wa nishati jadidifu ifikapo mwaka 2030, Afrika inatafuta kujumuisha nishati safi kuelekea viwanda vya kijani, utengenezaji wa ajira, upatikanaji wa nishati kwa wote, na ulinzi wa mazingira.

45. **TUNATHIBITISHA** kwamba Afrika ina uwezo mkubwa wa nishati jadidifu ambayo inabadilika muda wote kutokana na teknolojia mpya, na kuliweka bara la Afrika katika nafasi ya kuwa kama kiongozi wa kimataifa katika kutoa nishati mbadala, na kufanya matamanio ya bara zima la Afrika kuwa na uwezo wa kutoa nishati jadidifu kwa kipimo cha 300 GW ifikapo mwaka 2030 na kwamba juhudi hizi zinaonesha suluhisho la kufanya Afrika kuwa na viwanda vya kijani, kutengeneza ajira, kuhakikisha upatikanaji wa nishati kwa wote huku tukipunguza athari za mazingira.

46. **TUNASISITIZA** umuhimu wa upatikanaji wa nishati safi kwa angalau Waafrika milioni 300 kati ya milioni 600 wasio kuwa na nishati safi ifikapo 2030 chini ya Mpango wa Ajenda 300 wa Suluhisho la nishati safi ya Kupikia kwa Waafrika milioni 900 kama kipaumbele cha Afrika katika mabadiliko ya kutaka kuwa na nishati mbadala. Si lazima kuiachia sekta ya nishati pekee,

bali pia kujumuisha sekta nyingine kama vile kilimo na maji, na hivyo kuhakikisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi yenye usawa.

47. **TUNAZINGATIA KWA MASIKITIKO** kwamba licha ya kuchangia takriban 40% ya raslimali ya nishati mbadala duniani, Afrika bado ina zaidi ya watu 600 milioni wasio na umeme na milioni 900 wasio na nishati safi ya kupikia, jambo linalosisitiza umuhimu wa kujumuisha nishati safi, na nishati mbadala, na kuweka msisitizo kwamba jambo hili lisiachwe kwa sekta ya nishati sekta peke yake, bali pia lijumuishe sekta nyingine muhimu kama vile kilimo na maji, na hivyo kuhakikisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi yenye usawa.

48. **TUNASISITIZA** wito wetu kwa nchi zilizoendelea kutoa msaada unaohitajika na kufanya mageuzi kwa kuongeza ushiriki wa nchi za Afrika katika kutumia nishati jadidifu kimataifa kwa angalau 20% ifikapo mwaka wa 2030, kutoka 2% ya sasa, na hivyo kuhakikisha nishati mbadala sawia, endelevu na nishati mbadala yenye tija Kimataifa kwa wote.

49. **TUNATAMBUA** jukumu la rasilimali ya nishati mbadala katika kuhakikisha nishati safi ambayo inalinda usalama wa nishati wa nchi zinazoendelea.

50. **TUNASISITIZA** kipaumbele cha umma na uwekezaji unayoongozwa na watu binafsi kama uti wa mgongo wa miundombinu ya nishati ili kusaidia nishati mbadala, sambamba na umuhimu mkubwa wa Usaidizi wa kifedha unaotolewa na MDB, na ya hitaji la nchi zinazoendelea kutimiza ahadi zao kama ilivyokubaliwa katika matokeo yote ya UNFCCC, na kwamba mamlaka za umma na taasisi za kikanda lazima ziongoze katika kupanua miundombinu ya gridi ya taifa, viunganishi vya kikanda, na gridi ndogo za kijamii ili kuhakikisha upatikanaji wa nishati kwa wote, maendeleo jumuishi, na ya muda mrefu na kuendeleza sera na motisha za kuchochea uwekezaji binafsi endelevu na mifumo ya nishati jadidifu uliyogatuliwa na gridi ndogo za kijamii ili kufanikisha maili ya mwisho ya upatikanaji wa nishati safi kwa wote.

51. **TUNATOA WITO ZAIDI** kwa serikali na wadau wote husika kuweka kipaumbele katika maendeleo endelevu na miundombinu stahimilifu ya mabadiliko ya tabia nchi ambayo huongeza tija endelevu na nishati zenye kaboni kidogo, ufanisi wa nishati, Akili Mnemba (AI), na teknolojia zingine za kidijitali.

## D. NJIA ZA NISHATI MBADALA

52. **TUNAKARIBISHA** uanzishwaji wa program ya nishati mbadala ya UAE katika COP27, na kusisitiza kwamba njia za nishati mbadala zinapaswa kuzingatiwa katika utekelezaji wa nguzo zote za hatua za mabadiliko ya tabia nchi chini ya Mkataba wa Paris, kama ilivyoainishwa katika Ibara cha

2, na lazima kiwe katika muktadha wa maendeleo endelevu na juhudi za kutokomeza umaskini, kuhakikisha hatua za mabadiliko ya tabia nchi zinasawazisha vipengele vya kijamii, kiuchumi, na kimazingira kwa njia iliyo sawa na jumuishi, zikionesha kanuni za usawa na Majukumu ya Pamoja lakini Yaliyotofautiana na Uwezo Husika (CBDR-RC), kwa kuzingatia hali tofauti za kitaifa ikiwa ni pamoja na mahitaji na mazingira maalum ya Afrika.

53. **TUNATAMBUA** kwamba nishati mbadala inashughulikia maendeleo katika muktadha wa jumla ambao unaenda zaidi ya sekta ya nishati katika harakati za kufikia uzalishaji mdogo wa gesi chafu na uhimilivu zaidi wa uchumi na maendeleo katika muktadha wa maendeleo endelevu na kuondoa umaskini.

54. **TUNATOA WITO** wa kuchagiza mabadiliko katika muktadha wa mbinu za nishati mbadala na kuelewa jinsi mabadiliko ya tabia nchi na uhimilivu mpana kwa kila aina ya mshtuko wa kuchangia kuelekea tu mabadiliko ya jamii, kutambua kwamba mabadiliko hayo yanategemea uwezo wetu wote kupunguza na kudhibiti athari zinazohusiana na mabadiliko ya tabia nchi.

55. **TUNATHIBITISHA** kwamba njia za utekelezaji ni muhimu kwa kufikia malengo yaliyowekwa na makubaliano ya pande nyingi, ikiwa ni pamoja na UNFCCC na Mkataba wake wa Paris, pamoja na uamuzi 1/CMA.4, unaobainisha uhusiano muhimu kati ya njia za utekelezaji na kufikia njia za nishati mbadala. Bila fedha za kutosha, maendeleo ya teknolojia, ujenzi wa uwezo kwa nchi zinazoendelea kupitia ushirikiano wa kimataifa wenye maana, mabadiliko mbadala hayatawezekana au kuwa sawa.

56. **TUNASISITIZA** kwamba ushirikiano wa kimataifa ni muhimu katika kufikia nishati mbadala, na hatua za vikwazo vya biashara ya upande mmoja, kinyume chake, ni kikwazo kikubwa kwa nishati mbadala, hasa kwa nchi zinazoendelea.

57. **TUNATAMBUA** umuhimu wa utekelezaji wa kazi ya mradi wa njia za nishati mbadala, unaolenga kuunga mkono ufanisi wa utekelezaji wa UNFCCC na makubaliano yake ya Paris, huku tukitambua kwamba njia za nishati mbadala zinarithi masuala mtambuka na zinapaswa kuendeleza vipaumbele vya Afrika kwa kuchagiza maendeleo endelevu, kuimarisha uhimilivu wa mabadiliko ya tabia nchi, na kuhakikisha tija za pamoja kutokana na hatua za kupunguza hali hiyo katika roho ya usawa na mshikamano.

## E. NISHATI SAFI YA RASILIMALI YA MADINI

58. **TUNAMBUA** hitaji la dharura la kuhakikisha upatikanaji wa nishati mbadala, unaowajibika, mtambuka, stahimilifu, wenye usawa, endelevu na mnyororo wa nishati safi ya madini ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya kiteknolojia, yanayopatikana kwa kiwango cha chini cha uzalishaji, usalama

wa nishati, na ustahimilifu wa minyororo ya usambazaji wa nishati, ili kuhakikisha ongezeko la thamani na kiuchumi mtambuka katika nchi zenye rasilimali nyingi, huku zikihifadhi kikamilifu haki za uhuru wa rasilimali zao za madini.

59. **TUNAKARIBISHA** uzinduzi w a M k a k a t i wa Nishati safi ya madini ya Afrika kama nyenzo ya kuunganisha faida ya utajiri mkubwa wa Afrika kwa ajili ya maendeleo ya Ustahimilifu wa Mabadiliko ya tabia nchi.

60. **TUNASITIZA** umuhimu wa kujenga minyororo ya thamani iliyotangamanishwa, kukuza uboreshaji wa ndani, na kuhakikisha kwamba rasilimali za madini za Afrika zinachochea ukuaji jumuishi, na nishati mbadala, na umuhimu wa Mradi wa Viwanda vya Kijani wa Afrika (AGII) uliozinduliwa katika COP28 na kupongeza juhudi za Miradi hiyo katika kuchagiza ushirikiano wa kimkakati na taasisi za Fedha za Maendeleo ya Afrika na wadau wengine, kuhimiza ahadi za kukuza uwekezaji katika viwanda safi na kuiweka Afrika kama kitovu cha kimataifa cha utengenezaji wa mabadiliko ya viwanda safi.

61. **TUNATHIBITISHA** nishati safi lazima iwe jumuishi, yenye usawa, na iliyojikita katika vipaumbele vya maendeleo ya Afrika vya muda mrefu, na kwamba uchimbaji wa rasimali za madini lazima kuongozwa na utawala wa uwazi, utunzaji wa mazingira, na vipaumbele vya maendeleo vya kitaifa.

## F. CHAKULA NA KILIMO

62. **TUNATAMBUA** kipaumbele cha msingi cha kudumisha usalama wa chakula na kutokomeza njaa, sambamba na mazingira maalum na hatarishi ya mifumo ya kilimo na uzalishaji wa chakula barani Afrika kwa kuondoa athari mbaya za mabadiliko ya tabia nchi, na tunasisitiza kuimarisha uhimilivu wa mifumo ya kilimo na uzalishaji wa chakula kunahitaji ufikiaji endelevu na unaotabirika wa njia za kutosha za utekelezaji, ikiwa ni pamoja na ufadhili, maendeleo, kuhamisha teknolojia na ujenzi wa uwezo kwa nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika.

63. **TUNAKARIBISHA** utekelezaji wa Program kamili ya Kampala ya Maendeleo ya Kilimo Afrika (CAADP) kama Azimio la Kampala kuhusu Kujenga Mifumo ya Kilimo Endelevu na Imara barani Afrika pamoja na Mkakati wake unaohusiana na Mpango wa Utekelezaji (2026-2035). Tunatoa wito kwa nchi zilizoendelea na mifuko ya kimataifa kutoa usaidizi wa moja kwa moja unaotegemea ruzuku kwa mifuko ya kitaifa inayoelekeza fedha kwa wakulima wadogo, hasa wanawake, kwa ajili ya upatikanaji wa mbegu, umwagiliaji, na bima zinazostahimili mabadiliko ya tabia nchi.

64. **TUNAKUZA** majukwaa makubwa ya Afrika kwa ajili ya kushiriki mbinu bora, ubunifu wa masuluhisho, na utafiti juu ya marekebisho, ikijumuisha kilimo

cha kidijitali, mifumo ya data za mabadiliko ya tabia nchi na muundo wa miundombinu stahimilifu.

65. **TUNAKARIBISHA** matokeo ya Mkutano wa Mifumo ya Chakula ya Umoja wa Mataifa ulioandaliwa kuanzia tarehe 27-29 Julai 2025 huko Addis Ababa na kujitolea kuunga mkono juhudi za kutafuta fedha, uvumbuzi, na mshikamano wa kimataifa ili kujenga mustakabali wa usalama wa chakula na unaostahimili mabadiliko ya tabia nchi.

66. **TUNAKARIBISHA** Mradi wa Chakula na Kilimo kwa Mabadiliko Endelevu (FAST), uliozinduliwa katika COP27 na Kazi ya Pamoja ya Sharm El-Sheikh kuhusu Utekelezaji wa Hatua za Mabadiliko ya Tabia nchi katika Kilimo na Usalama wa Chakula (SSJW).

67. **TUNATAMBUA** kwamba uwekezaji katika utafiti, uvumbuzi, na mifumo ya chakula imara utasaidia kuhakikisha kwamba mabadiliko ya tabia nchi yaliyo na uvumbuzi si maendeleo pekee bali pia iliyoundwa kulingana na mazingira ya Afrika na kupitishwa haraka kwa kiwango kikubwa, na kuwawezesha wakulima wadogo kwa zana, maarifa, na usaidizi wa mifumo inayohitajika ili kurekebisha kwa kuhamisha mabadiliko ya tabia nchi, kulinda riziki, na kujenga uhimilivu wao.

68. **TUNAKUZA** lishe mseto na uzalishaji wa chakula unaokidhi mahitaji ya lishe kwa idadi ya watu wetu huku tukihifadhi bioanuwai na kuimarisha minyororo ya thamani ya chakula na kilimo, kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno, na kuboresha miundombinu ya uhifadhi na usambazaji wa chakula, ambayo ni muhimu katika kufanikisha mamlaka ya chakula na kukomesha njaa kote barani Afrika.

69. **TUNATAMBUA** jukumu la mifumo ya maarifa ya jadi, ardhi endelevu na matumizi ya maji katika uhimilivu wa kilimo, na tunathibitisha tena kujitolea kwetu kuimarisha sera zinazolinda mabonde ya maji, kurejesha ardhi zilizoharibika, na kukuza mifumo bora ya umwagiliaji bora, jumuishi na kupanga matumizi ya ardhi, inayoongozwa na juhudi za jamii za uhifadhi ili kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu.

70. **TUNAISITIZA** umuhimu wa ushirikiano wa kikanda katika utafiti, uvumbuzi, na ubadilishanaji wa maarifa, na kuimarisha ushirikiano kati ya mataifa ya Afrika ili kuharakisha maendeleo na upanuzi wa mazao yanayostahimili mabadiliko ya tabianchi, kilimo cha kidijitali, na minyororo ya thamani endelevu.

## G. MASULUHISHO YANAYOZINGATIA MAZINGIRA YA ASILI

71. **TUNASISITIZA** kwamba bara hilo liko katika hatari zaidi ya kupata majanga ya tabianchi lakini pia lina utajiri wa bayoanuwai na **TUNATHIBITISHA** dhamira yetu ya kukuza masuluhisho ya asili ambayo yamejikita katika uhalisia wa Kiafrika.

72. **TUNAZIHIMIZA** nchi za Kiafrika zinazopendelea kujumuisha masuluhisho yanayotegemea Mazingira katika NDCs na NAPs zao kufanya uamuzi huo kadri inavyofaa.

73. **TUNAHIMIZA** uundaji wa jukwaa la maarifa la masuluhisho yanayotegemea Asili barani ili kufuatilia maendeleo, kushiriki mbinu bora, na kukuza utafiti na uvumbuzi wa mikakati ya kukabiliana na mabadiliko na kupunguza athari zinazotegemea mfumo ikolojia.

74. **TUNATHIBITISHA** tena jukumu muhimu la urejeshaji wa ardhi na thamani ya mipango inayohusiana, ikiwa ni pamoja na Ukuta Mkuu wa Kijani na Mpango wa Urejeshaji wa Mazingira ya Misitu ya Afrika (AFR100).

75. **TUNAZIPONGEZA** nchi wanachama za Umoja wa, kwa mipango na juhudi endelevu zinazolenga urejeshaji wa mifumo ikolojia na mandhari na uhimilivu wa riziki, kama vile Mpango wa Ethiopia wa Urithi wa Kijani unaoendana na Mpango mkuu wa Umoja wa Afrika wa Ukuta wa Kijani, na Mpango wa Urejeshaji wa Mazingira ya Misitu ya Afrika, pamoja na mpango wa misitu wa Afrika ya Kati, na tumejitolea kusaidia uhamasishaji wa rasilimali fedha ikijumuisha kupitia pamoja mapendekezo ya kupata ufadhili wa kukabiliana na hali hiyo kutoka Mfuko wa Tabianchi ya Kijani.

76. **TUNAIPONGEZA** African Gold Standard, iliyoongozwa na AUDA-NEPAD, kwa mpangilio wa mfano wa miradi ya kaboni inayotoa kipaumbele kwa haki za jamii, ugawanaji sawa wa faida, na ulinganifu na muktadha wa kipekee wa kijamii, kiuchumi na kimazingira wa Afrika.

77. **TUNAJITOLEA** kwa mbinu jumuishi zinazowezesha jamii, hasa wanawake, vijana, na wazawa, watu wenye ulemavu (walemavu), na wazee, kwa muundo, kutekeleza, na kufaidika na masuluhisho ya asili, kuhakikisha Usimamizi wa ndani unabaki kuwa kitovu cha mwitikio wa Afrika katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

78. **TUNATAMBUA** jukumu lisiloweza kubadilishwa la mifumo ikolojia ya Afrika katika kudhibiti tabianchi, kuhifadhi bayoanuwai, na kusaidia kimaisha kulingana na masuluhisho ya mazingira ya asili ni muhimu kwa mkakati wetu wa tabianchi hali, tunatoa wito wa kuongeza uwekezaji katika urejesho na ulinzi wa mifumo ikolojia, unaoongozwa na usawa, sayansi, bei nzuri ya kaboni na maarifa ya kitamaduni na ya asili, huku umakini maalum ukitolewa kwa mifumo ikolojia dhaifu kama vile maeneo ya pwani, misitu ya Mediterania, chemchemi na maeneo oevu ambayo yanakabiliwa na vitisho

vya haraka kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

79. **TUNATAMBUA ZAIDI** umuhimu wa utawala wa bahari kwa jukumu lake muhimu katika mifumo ikolojia ya baharini katika kupunguza mabadiliko ya tabianchi, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na maendeleo endelevu.

80. **TUNATAMBUA** umuhimu wa maeneo ya pwani na bahari ya Afrika bahari kama vyanzo ya chakula, nishati, bioanuwai, ajira, na uhimilivu wa hali ya hewa, na kuthibitisha tena kujitolea kwetu kulinda na kusimamia mifumo ikolojia ya baharini na pwani kwa uendelevu, kupambana na uchafuzi wa mazingira, matumizi mabaya kupita kiasi, na athari za kupanda kwa kiwango cha bahari, wa kukuza uchumi wa bluu kama nyenzo ya kimkakati kwa maendeleo endelevu ya Afrika maendeleo .

## H. MASULUHISHO YA KITEKNOLOJIA

81. **TUNASISITIZA** haja ya kukuza mifumo ikolojia ya kidijitali jumuishi, kuwasaidia wajasiriamali wa teknolojia wa Kiafrika, na kuhakikisha kwamba teknolojia za mabadiliko ya tabianchi zinapatikana kwa urahisi, zina bei nafuu, na iliyoundwa mahsusi kwa kuzingatia mahitaji ya ndani, na hiyo teknolojia lazima ihudumie watu, isibadilishe asili, lakini iimarishe.

82. **TUNAWAHIMIZA** washirika wa kimataifa kuunga mkono mbinu mbili za Afrika—kuwekeza katika rasimali asilia na maendeleo ya kiteknolojia huku wakisisitizia kuwa fedha za mabadiliko ya tabianchi lazima zitoe kipaumbele kwa masuluhisho jumuishi yanayotoa faida za pamoja kwa watu na sayari, na kwa vipaumbele vya maendeleo ya teknolojia za gharama nafuu kwa mifumo ya tahadhari za mapema, kilimo kinachostahimili mabadiliko, usimamizi wa maji, na ulinzi wa pwani, zikisaidiwa na ujenzi wa uwezo wa kuziendesha na kuzitunza ndani ya bara.

83. **TUNAREJEA** kwamba juhudi za mpito lazima ziende zaidi ya sekta ya nishati, zikijumuisha nishati mbadala, maendeleo ya teknolojia, na vipimo vya uhamishaji katika mifumo ya chakula, usimamizi wa maji, huduma za afya, na sekta zingine muhimu za maendeleo, na kuwaomba washirika kutoa usaidizi halisi wa kiufundi na kifedha ili kuendeleza sekta hizi muhimu.

## I. KUKABILIANA NA UHIMILIVU

84. **TUNASISITIZA** kwamba kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kujenga uhimilivu dhidi ya majanga ndiyo vipaumbele vikuu vya Afrika.

85. **TUNASISITIZA** marekebisho hayo kwa mabadiliko ya tabianchi na kujenga uhimilivu dhidi ya majanga, ufikiaji wa maji safi na usafi wa mazingira, chakula na uhimilivu wa lishe, Miji na miundombinu inayostahimili mabadiliko ya tabianchi, mifumo ya afya inayostahimili mabadiliko ya tabianchi, na

upatikanaji wa nishati ya kuaminika ni miongoni mwa vipaumbele vya Afrika.

86. **TUNATHIBITISHA** tena dhamira kwa " Mpango wa Afrika wa Uhimilivu wa Mijini" wa Umoja wa Afrika (AURP), ukisisitiza ufadhili bunifu wa hali ya hewa mijini, uwezeshaji wa serikali za mitaa, uendelezaji wa miundombinu ya kijani, na uboreshaji jumuishi wa makazi yasiyo rasmi ili kujenga miji ya Kiafrika inayostahimili na endelevu.

87. **TUNATAMBUA** hitaji la dharura la kushughulikia udhaifu wa bara hili kutokana na majanga ya tabianchi kwa mikakati thabiti ya utekelezaji inayoongozwa na Afrika ili kujenga uhimilivu katika kilimo, maji, usalama wa chakula na nishati, mifumo ya tahadhari za mapema na miundombinu, wakati ulinzi muhimu wa bioanuai na mifumo ikolojia kama vile Msitu wa Mvua wa Bonde la Kongo.

88. **TUNATAMBUA** jukumu muhimu la kulinda, uhifadhi, na kurejesha mifumo ya maji na mifumo ikolojia inayohusiana na maji katika kutoa faida na faida za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, huku ikihakikisha ulinzi wa kijamii na kimazingira.

89. **TUNASISITIZA** umuhimu wa masuluhisho yanayoweza kupanuliwa na yenye mizizi ya ndani inayochanganya maarifa ya asili na ya kitamaduni na uvumbuzi wa kisasa, kama vile kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi, mifumo ya tahadhari za mapema, nishati mbadala, na uhamaji wa kielektroniki, na tunahimiza washirika wa kimataifa washirika kusaidia ubunifu wa Afrika kupitia ufadhili na uhamishaji wa teknolojia, ikijumuisha mikopo yenye masharti nafuu, taratibu za ufadhili na kuanzisha ushirikiano endelevu wa kisayansi na kiteknolojia.

90. **TUNATHIBITISHA** marekebisho na uhimilivu lazima ieendeshwe na nchi na inayozingatia watu , inayotambua jukumu muhimu la vijana, wanawake, watoto, wazawa, watu wenye ulemavu, na makundi mengine yaliyo hatarini katika kuunda majibu ya tabianchi inayokuza utawala jumuishi, upatikanaji sawa wa rasilimali, na ujenzi wa uwezo ili kuhakikisha kwamba juhudi za kukabiliana na hali hiyo ni endelevu na za haki.

91. **KUKUZA** usimamizi wa tabianchi unaowashirikisha wanawake, vijana, watoto, jamii zilizo hatarini, na wavumbuzi wa ndani kwa kuzingatia sauti na vipaumbele vya Kiafrika, na kurasimisha hatari ya hali ya hewa katika mipango ya kitaifa na kukuza ushirikiano wa kikanda.

92. **TUNATAMBUA** kwamba utekelezaji na ufadhili wa kitaifa wa mipango ya marekebisho ni nyenzo muhimu za kujenga uhimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

93. **KWA KUZINGATIA** umuhimu wa ushirikiano katika kutengeneza tathmini za hatari za tabianchi za kikanda na mifumo ya tahadhari za mapema inayovuka mipaka ili kushughulikia hatari zinazoendelea kama vile ukame na mafuriko ya ghafla, na ukosefu wa usalama wa mafuriko, tunatoa wito wa kuziunganisha katika mifumo na viashiria vya ujenzi wa uhimilivu vinavyoongozwa na Afrika.

94. **TUNATOA WITO** wa kushughulikia changamoto za maji ifikapo 2030 kwa kuboresha matumizi endelevu na usimamizi ya rasilimali ya maji, inayohusiana na mifumo ya maji , mifumo ikolojia, udongo na rasilimali ya ardhi, kuboresha usimamizi wa mazingira, kanuni bora za mazingira, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, ufuatiliaji na uchambuzi wa ubora wa maji, na mifumo ya tahadhari na ufuatiliaji wa mapema, na kusaidia kuhakikisha kuchakata tena, kutibu, na kutumia tena maji machafu, udhibiti wa mtiririko wa maji na hatua zingine muhimu.

95. **TUNASISITIZA** kwamba marekebisho lazima yajumuishwe kikamilifu katika mikakati ya maendeleo ya kitaifa, huku hatari ya mabadiliko ya tabianchi ikiwekwa katika mipango, bajeti, na uwekezaji wa miundombinu, ili kuepuka mabadiliko yasiyofaa na kuhakikisha faida za uhimilivu ni endelevu, na tunatoa wito wa kuimarisha kwa usaidizi wa kimataifa ili kuendeleza uundaji, utekelezaji, na ufadhili wa mipango ya kitaifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, tukiitambua kama vyombo muhimu vya kujenga uhimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

### J. HASARA NA UHARIBIFU

96. **TUNATAMBUA** matokeo ya COP27, iliyofanyika Sharm El Sheikh, Misri, COP ya Kiafrika, ambayo, miongoni mwa wengine, alizindua mpango kazi wa Sharm El Sheikh wa utekelezaji wa Kilimo na Hatua za Tabianchi (SSJW); na tunarejea mafanikio ya kihistoria yaliyosababisha uamuzi muhimu wa kuanzisha mpango mpya wa ufadhili uliowekwa wa kukabiliana na Hasara na Uharibifu.

97. **TUNASISITIZA** umuhimu wa zana zinazosambazwa kikanda, zilizotafsiriwa, na zinazofaa kwa mtumiaji ili kuwezesha majibu yenye taarifa na mahususi kwa muktadha; na kusisitiza hitaji la kuimarisha msingi wa maarifa wa kimataifa kuhusu hasara zisizo za kiuchumi na kuzisaidia nchi zinazoendelea katika kutathmini vyema na kugharimia mahitaji yao ya hasara na uharibifu kama kipaumbele cha pamoja.

98. **TUNATAMBUA** maendeleo yaliyofikiwa katika UNFCCC COP29 kwa kuanza Mfuko wa Kukabiliana na Hasara na Uharibifu (FRLD), na Mbinu za Utekelezaji za Barbados (BIMs) zilizofuata, zikiwezesha kusambaza pesa ifikapo mwaka 2025 ~~,~~ na kuimarisha Mfumo wa Kimataifa wa Warsaw (WIM) wa hasara na uharibifu.

99. **TUNATAMBUA** haja ya dharura ya kutekeleza Mfuko wa Hasara na Uharibifu ili kuhakikisha upatikanaji rahisi na wa moja kwa moja, hasa kwa nchi za LDC na SID, ili kushughulikia hasara za kiuchumi na zisizokuwa za kiuchumi, pamoja na kipengele maalum cha uhamiaji uliosababishwa na mabadiliko ya tabianchi na utoaji wa usaidizi wa kutosha wa kiufundi kwa nchi zinazoendelea.

100. **TUNAHIMIZA** utekelezaji wa Mfuko wa Hasara na Uharibifu ili kuhakikisha upatikanaji rahisi na wa moja kwa moja kwa LDC na SID kushughulikia kiuchumi na isiyo ya kiuchumi hasara, pamoja na dirisha maalum la matukio ya polepole na uhamaji unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

101. **URATIBU ULIOIMARISHWA**, mshikamano, na ukamilishano kati ya Kamati ya Utendaji ya Warsaw International Mechanism, Mtandao wa Santiago, na Mfuko wa Fidia kwa Hasara na Uharibifu, ikijumuisha sekretarieti husika, kwa lengo la kuimarisha upatikanaji, ufikiaji, na usaidizi kwa nchi zilizo mstari wa mbele wa athari za mabadiliko ya tabianchi.

## K. UHAMIAJI , AMANI NA USALAMA UNAOHUSIANA NA TABIANCHI

102. **TUNATAMBUA** hatari kubwa za mabadiliko ya tabianchi, kama tishio linalozidisha, kwa mazingira ya amani na usalama barani humo ikiwa ni pamoja na ukosefu wa usalama wa chakula na maji, upotevu wa riziki, kushindwa kwa usimamizi wa maliasili, uhaba wa rasilimali za maji, uhamaji unaosababishwa na hali ya hewa, na pengine kuzidisha udhaifu uliopo, mivutano na migogoro, na katika suala hili, msongo wa mawazo. ya hitaji kwa ya AU kwa endelea kuhamasisha a umoja Mwafrika mbele katika ya kiwango cha kimataifa, kwa zaidi kwa ufanisi punguza ya hasi athari ya hali ya hewa mabadiliko katika zote mbili, kitaifa kikanda na bara viwango, na kwa a Bara mfumo kwa ajili ya kukabiliana kwa vitendo na vitisho vya usalama vinavyosababishwa na matukio yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi.

103. **TUNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama wote na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na Mifumo ya Kikanda (RECs/RMs) kuboresha zaidi uwezo wao wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuendeleza mifumo ya tahadhari za mapema za tabianchi inayoaminika, pamoja na majibu jumuishi kwa hatari za usalama zinazohusiana na tabianchi.

104. Zaidi ya hayo, **TUNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuimarisha ushirikiano na ushirikiano katika kusimamia rasilimali za baharini zinazovuka mipaka, ardhi za wafugaji, misitu, wanyamapori, mito na maziwa yanayovuka mipaka.

105. **TUNATHIBITISHA** tena ahadi yetu ya pamoja ya kushughulikia changamoto za dharura na zinazohusiana imesimama na hali ya hewa mabadiliko, kulazimishwa uhamaji, na ya udhaifu ya amani na usalama kote barani, na kutambua athari kubwa ya uhamaji na migogoro inayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi inayozidishwa na mabadiliko ya tabianchi.

106. **TUNATAMBUA** kwamba mabadiliko ya tabianchi huzidisha uhamaji wa binadamu na kwamba uhamaji ofa njia za idadi ya watu walioathiriwa na hali ya hewa kufikia riziki mpya, hurahisisha malipo ya nje hiyo usaidizi jumuiya marekebisho, na huwezesha ujuzi maendeleo na kubadilishana muhimu kwa tu mabadiliko na kijani kazi; na kutoa wito wa majibu kamili zaidi kwa athari za mabadiliko ya hali ya hewa, ikiwa ni pamoja na kupanda kwa usawa wa bahari na kuenea kwa jangwa, chini ya mifumo husika ya kimataifa, na umuhimu muhimu wa ushirikiano na uratibu wa mipaka, kuimarisha ukusanyaji, ushiriki na uchambuzi wa data.

107. **TUNASISITIZA** hitaji la kuhakikisha kwamba majibu ya mabadiliko ya tabianchi yanazingatia migogoro na nyeti kwa usalama na hiyo wao mkuu ujenzi wa amani juhudi, pamoja na hitaji la mbinu jumuishi zinazoshughulikia uhusiano kati ya mabadiliko ya tabianchi na uhamaji wa binadamu katika mazingira yaliyoathiriwa na migogoro, kwa lengo la kutoa taarifa kuhusu muundo na utekelezaji wa sera na hatua zinazoshughulikia uhamaji unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi barani Afrika.

108. **TUNASISITIZA** umuhimu ya kuweka kipaumbele katika athari ya mabadiliko ya tabianchi kwenye suala la usalama wa maji na chakula usalama katika Afrika, huku tukikabiliana na hali ya hewa, amani, na usalama , kutokana na umuhimu wake kwa Bara la Afrika.

109. **TUNATAMBUA** kwamba uhamiaji unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi si tu janga la kibinadamu bali changamoto ya kimuundo inayohitaji majibu ya sera yaliyoratibiwa, mipango jumuishi, na uhimilivu miundombinu, na tunatoa wito wa ujumuishaji wa mabadiliko ya tabianchi katika mifumo ya maendeleo ya kitaifa na kikanda.

110. **TUNATHIBITISHA** kwamba uhimilivu wa tabianchi hauwezi kutenganishwa na ujenzi wa amani na kuzuia migogoro na tunazisihi serikali, washirika wa maendeleo, na asasi za kiraia kuwekeza katika mikakati ya amani inayozingatia hali ya hewa, mifumo ya tahadhari za mapema, na mifumo ya mazungumzo jumuishi ambayo hushughulikia sababu kuu za kutokuwa na utulivu.

## L. MABADILIKO YA TABIANCHI NA AFYA

111. **TUNATHIBITISHA** tena kujitolea kwetu kwa pamoja katika kuendeleza

suluhisho za hali ya hewa zinazoongozwa na Afrika ambazo zinaweka kipaumbele afya ya binadamu, uendelevu wa mazingira, na maendeleo ya usawa, kama vile kuongozwa na ya Mwafrika Muungano Ajenda 2063 na ya kanuni ya utandawazi wa pande nyingi, tambua ya dharura hitaji kwa anwani ya iliyounganishwa migogoro ya hali ya hewa mabadiliko na umma afya ng'ambo ya bara, na simu kwa kujitolea kifedha taratibu kwa ajili ya mambo yanayohusiana na tabianchi na afya na ya uhimilivu wa Mifumo maalum ya Afrika, Tunaangazia vitisho vinavyoongezeka vya mawimbi ya joto na uhaba wa maji, ambavyo vinaathiri vibaya afya ya umma, na tunatoa wito wa mifumo ya tahadhari mapema inayohusiana na huduma za afya.

112. **TUNATHIBITISHA** tena kuendelea mifumo ya afya inayostahimili mabadiliko ya tabianchi na **TUNATAMBUA** Mpango wa Utekelezaji wa Afya wa Belém kama mfumo muhimu wa kimataifa unaoendana na matarajio ya Afrika ya huduma ya afya yenye usawa, endelevu, na inayozingatia mabadiliko ya tabianchi.

## M. WITO WA KUCHUKUA HATUA

Sisi tunatoa wito wa kuchukua hatua katika masuala yafuatayo :

113. Kuendeleza nishati mbadala kuelekea kuwa na nishati safi kwa kuwekeza katika nishati mbadala , kilimo endelevu, uhimilivu wa maeneo ya mijini, utunzaji wa ardhi, kupunguza hatari, usimamizi wa majanga, na masuluhisho ya kiteknolojia.

114. Kusaidia utekelezaji wa haraka wa mifumo husika ya Umoja wa Afrika, ikiwa ni pamoja na Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi na Maendeleo Endelevu na Mpango wa Utekelezaji, Mkakati wa Kikanda wa Afrika wa Kupunguza Hatari za Maafa, Mkakati Jumuishi wa Afrika kuhusu Hali ya Hewa, Maji, na Mkakati wa Utawala wa Bahari ya Afrika.

115. Nchi zilizoendelea kuongeza ufadhili wa tabianchi , hasa fedha za kukabiliana na mabadiliko, zinazotolewa hasa katika mfumo wa ruzuku na masharti sawa na ruzuku katika muktadha wa utekelezaji wa NCQG na lengo la dola trilioni 1.3 za Marekani kwa mwaka ifikapo mwaka 2035, pamoja na fedha chini ya Ibara cha 9.1, taratibu za ufikiaji lazima zirahisishwe na ziendane na mahitaji maalum ya Afrika, ikiwa ni pamoja na zile za nchi za Afrika zilizo katika mazingira magumu.

116. Nchi zilizoendelea kuwezesha hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika nchi zinazoendelea kwa kutoa mafungu ya kutosha, mapya, yanayotabirika, na ziada ya ufadhili kutoka mifuko ya kimataifa ya hali ya hewa, sekta za umma na binafsi, mifumo ya hasara na uharibifu, na vyombo bunifu vya ufadhili ili kusaidia majibu ya dharura na ya muda mrefu ya masuluhisho ya hali ya hewa, ikitoa kipaumbele kwenye suala la kuhamisha teknolojia na kujengea uwezo .

117. Nishati mabadala ya kimataifa ya haki na usawa inayoheshimu kikamilifu kanuni za Azimio la Rio la 1992, ikiwa ni pamoja na kanuni ya majukumu ya pamoja lakini tofauti na uwezo husika, na ambayo yamejikita katika miktadha ya kitaifa.

118. Nchi zilizoendelea kuongeza ufadhili sawa , wa wazi na unaonyumbulika wa fedha za kukabiliana na tabia nchi katika mfumo wa ruzuku na unaofanana na huo, ikijumuisha kupitia kutekeleza mara tatu Mkataba wa Glasgow unaozidi maradufu ifikapo mwaka 2030 kutoka viwango vya 2025, na katika muktadha wa kutekeleza Mpango wa NCQG na Baku hadi Belém hadi dola trilioni 1.3 za Marekani kwa mwaka ifikapo mwaka 2035.

119. Lengo Jipya la Pamoja la Ukadiriaji lazima liende zaidi ya kutungwa kama "lengo la uwekezaji" pekee. Linapaswa kupimwa na kuthibitishwa kwa mujibu wa Vifungu 9.1, 9.3, na Ibara cha 9.4 cha Mkataba wa Paris, kuhakikisha usaidizi wa kutosha, unaotabirika, na unaopatikana kwa urahisi.

120. Nchi zilizoendelea kuheshimu ahadi zao za ufadhili kulingana na Vipaumbele vya Afrika, na kufanya juhudi za kuhamasisha ufadhili wa rasilimali za ndani na kuchagiza ubia wa umma na sekta binafsi, hasa katika utekelezaji wa Michango Iliyoainishwa Kitaifa (NDCs) na Mipango ya Kitaifa ya Marekebisho (NAPs), na Mpango wa Falme za Kiarabu wa Mfumo wa Uhimilivu wa Tabianchi wa Kimataifa , kama ilivyobainishwa katika Mpango wa Kimataifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.

121. Maendeleo ya Haraka ya uratibu wa madeni na kufuta madeni, mshikamano wa wakopaji, na utatuzi wa madeni unaozingatia sheria, ambazo ni zana muhimu kwa maendeleo yanayostahimili mabadiliko ya tabianchi na nishati mabadala .

122. Taratibu rahisi za upatikanaji wa fedha za mabadiliko ya tabianchi zinazozingatia mahitaji maalum ya Nchi za kiAfrika, ikijumuisha nchi maskini na za Visiwa Vidogo.

123. Nchi zilizoendelea zinapaswa kutimiza ahadi zao za kuziba pengo la fedha na usaidizi wa marekebisho, uhimilivu, na maendeleo endelevu, na haja ya mageuzi ya haraka katika mifumo ya ufadhili wa tabianchi ili kuhakikisha usawa, utoshelevu, ufikiaji, na uwezo wa kumudu gharama; na ikiweka msisitizo katika ruzuku badala yake mikopo ili kuepuka kuzidisha deni la Afrika, na utoaji wa rasilimali kwa wakati na kwa usawa.

124. Washirika wa kimataifa kupanua ufadhili wa tabianchi unaotolewa kwa ajili ya mazingira, wakisisitiza kwamba uwekezaji katika mazingira ya asili ya Afrika hutoa faida nyingi za ushirikiano kwa watu, bioanuwai, na ustawi, huku wakikuza utafiti wa ushirikiano, elimu, uvumbuzi, ujenzi wa uwezo, na

ubadilishanaji wa maarifa katika mipaka na sekta mbalimbali.

125. Kuongezeka kwa uwekezaji katika urejesho na ulinzi wa mfumo ikolojia, kuongozwa na usawa, sayansi husika, na maarifa ya kitamaduni na ya kiasili.

126. Mifumo ya biashara ya kaboni safi kulingana na muktadha wa ndani ulioundwa kupitia ushirikiano wa pande nyingi ili kuakisi Majukumu ya Pamoja lakini Yaliyotofautiana na Uwezo Husika, na kujitolea kuchukua hatua zinazohitajika na kuunda ushirikiano ili kuzuia uwekaji wa hatua za upande mmoja, ikiwa ni pamoja na kodi za kaboni zinazodhoofisha ajenda za bara kwa ajili ya ujumuishaji wa kikanda, muunganisho, kama vile katika maendeleo ya usafiri wa anga na meli, na hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

127. AUC na Nchi Wanachama kuendeleza mikakati ya afya ya hali ya hewa ambayo itaimarisha mifumo ya afya ya umma, kukuza miundombinu inayostahimili mabadiliko ya tabianchi, na kuhakikisha upatikanaji wa hewa safi, maji, na nishati kwa wote.

128. Umoja wa Afrika katika mchakato wa mazungumzo ya tabianchi , hasa katika kuelekea COP30 huko Belém, Brazili, na kwingineko, ili kuimarisha jukumu la Afrika katika kuunda maamuzi ya kimataifa.

129. Usaidizi ulioimarishwa na endelevu ili kuongeza utekelezaji ya ya Mipango ya hali ya hewa inayoongozwa na Waafrika, ikiwa ni pamoja na Tume tatu za Hali ya Hewa zilizozinduliwa katika COP22 na zingine, kulingana na uamuzi Assembly/AU/Dec.855 (XXXVI) wa Februari 2023.

130. Usaidizi ulioimarishwa na endelevu ili kuongeza utekelezaji wa Mipango ya hali ya hewa inayoongozwa na Waafrika, kama vile Mpango wa Umoja wa Afrika wa Ukuta Mkuu wa Kijani, Mpango wa Urejeshaji wa Mazingira ya Misitu ya Afrika, Mpango wa Urithi wa Kijani wa Ethiopia, na mingine.

131. Usaidizi wa Kimataifa kuelekea utekelezaji ya Afrika kuelekea Mipango kabambe ya Kikanda na bara ya ufikiaji wa nishati mbadala kwa kuendesha mabadiliko ya kiuchumi yanayojumuisha, yanayostahimili mabadiliko ya hali ya hewa na yenye kaboni kidogo ikijumuisha Soko la Umeme Moja la Afrika ( AfSEM ), Mpango Mkuu wa Mifumo ya Nishati ya Bara (CMP), Mkakati wa Ufanisi wa Nishati Afrika ( AfEES ), Dhamira 300, Programu ya Nishati safi ya Kupikia ya Afrika, Ushirikiano wa Kasi wa Vyakula Vinavyoweza Kurejeshwa Barani Afrika (APRA), na Mpango wa Nishati Mbadala Afrika.

132. Washirika wa Kimataifa kuisaidia Afrika kuwekeza katika maendeleo ya kiteknolojia huku ikisisitiza kwamba ufadhili wa hali ya hewa lazima utoe kipaumbele kwa teknolojia inayounga mkono marekebisho na upunguzaji

wa athari.

133. Uanzishwaji wa vipandikizi na vitovu vya teknolojia hiyo ili kuongeza maarifa kuhusu matumizi ya akili bandia ili kuwasaidia watoto na vijana katika uvumbuzi wao wa masuluhisho ya mabadiliko ya tabianchi.

134. Usaidizi ulioimarishwa na endelevu ili kuendeleza utekelezaji wa Mipango ya hali ya hewa inayoongozwa na Waafrika.

135. Utekelezaji mzuri wa programu ya kazi ya Sharm El Sheikh kuhusu utekelezaji wa Kilimo na Hatua za Tabianchi (SSJW), kuhakikisha kwamba matokeo yake yamejikita katika vipaumbele vya nchi zinazoendelea na za Afrika na kwamba inashughulikia changamoto mahususi zinazowakabili wakulima wadogo.

136. Kamisheni ya Umoja wa Afrika itachunguza na kuunga mkono uanzishwaji wa muungano wa nchi muhimu zinazozalisha madini barani Afrika ili kukuza ushirikiano wa kimkakati na endelevu wa kikanda, kuunga mkono uongezaji thamani, na unufaikaji.

## N. MATARAJIO NA AHADI

**Sisi kwa hiyo tunatarajia na kujitolea kama ifuatavyo:**

137. Kusaidia uundaji wa Huduma za kifedha zinazoongozwa na Waafrika kifedha kama vile dhamana ya kijani ya AfDB kijani dhamana na vituo vya uvumbuzi vinavyostahimili mabadiliko ya tabianchi vya kikanda ambavyo vitasaidia Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Afrika.

138. Kutoa kipaumbele kwa marekebisho kama changamoto kuu ya hali ya hewa barani Afrika, hasa kwa kuzingatia usalama wa maji na chakula, mifumo ikolojia dhaifu, na uhimilivu wa jamii, na kuhamasisha usaidizi wa kifedha na kiufundi ipasavyo.

139. Haja ya haraka ya kuendeleza na kuendesha mifumo mipya na bunifu ya fedha za mabadiliko ya tabianchi iliyoundwa mahsusi kwa bara, ikijumuisha mifumo jumuishi ya fedha,hati fungani za kijani na bluu, ubadilishaji wa madeni kwaajili ya mazingira , na ushirikiano wa kimkakati kati ya umma na sekta binafsi, ili kutofautisha vyanzo vya fedha na kuhamasisha rasilimali muhimu kwa ajili ya vipaumbele vyetu vya maendeleo endelevu.

140. Tunatetea mageuzi katika mifumo ya kifedha ya kimataifa inayorahisisha upatikanaji wa fedha za tabianchi kwa usawa, na kusaidia vyombo bunifu vya kifedha vilivyoundwa kulingana na mahitaji ya Afrika.

141. Kuratibu mikakati ya kitaifa na kikanda ili kuepuka kugawanyika na kukuza

ushirikiano katika sekta, kuongeza sera mshikamano, na epuka mwingiliano katika mipango ya masoko ya nishati, kilimo, na kaboni.

142. Kuimarisha uwezo wa kisheria na kitaasisi ili kunufaika kikamilifu na mbinu za ushirikiano chini ya Ibara cha 6 cha Mkataba wa Paris, na kutekeleza Mpango wa Utekelezaji wa Afrika wa Masoko ya Kaboni, huku ukilinda haki za kitaifa na kijamii, na kuhakikisha uwazi, kuheshimu uhuru wa kitaifa, na kuoanisha miamala na vipaumbele vya kitaifa.

143. Kuharakisha mashauriano kuhusu maendeleo ya Msimamo wa Pamoja wa Afrika wa mabadiliko ya tabianchi, amani, na usalama, ambao lazima uongozwe na data na kuarifiwa na michango ya Nchi Wanachama na taasisi za Umoja wa Afrika, kwa lengo la kuzingatiwa na kupitishwa kwake kupitia Vyombo husika vya Sera vya AU.

144. Kuunganisha uhamaji, tabianchi, amani, na usalama katika mifumo ya kitaifa na mikakati ya kikanda ya hali ya hewa, ikitambua wahamiaji kama mawakala muhimu wa mabadiliko katika kujenga Afrika inayostahimili tabianchi, yenye ustawi, na amani.

145. Kuboresha maendeleo ya kijani na uthabiti kwa kuwekeza katika nishati mbadala, kilimo endelevu, uhimilivu wa mijini, urejeshaji wa ardhi, kupunguza hatari za maafa, na teknolojia na suluhisho zinazotegemea asili.

146. Kusaidia wakulima, hasa wakulima wadogo, vijana, na wanawake, kupata taarifa za hali ya hewa, uwekezaji, mifumo ya tahadhari za mapema, na teknolojia bunifu zinazowawezesha kuendana na mabadiliko tabianchi na kutambua ya chemchem za maji kama mifumo ya kiAfrika ya kilimo endelevu ambacho lazima kilindwe na kuungwa mkono kwa ufadhili maalum wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

147. Utekelezaji Kamili wa Azimio la Kampala CAADP na kujumuisha ufadhili wa marekebisho ya kilimo katika bajeti za kitaifa, kuhakikisha uendelevu, katika uwekezaji katika chakula, usalama na uhimilivu wa tabianchi—zaidi ya utegemezi wa misaada ya fedha kutoka nje ya Bara.

148. Kuendesha Mkataba wa Ubunifu wa Tabianchi wa Afrika (ACIC) na Kituo cha Hali ya Hewa cha Afrika (ACF) ili kutetea masuluhisho ya hali ya hewa ya Afrika.

149. Utekelezaji wa nishati mbadala katika ngazi za kitaifa na kimataifa, unaungwa mkono na ushirikiano wa kimataifa na uwasilishaji wa muhimu wa njia za utekelezaji, katika muktadha wa maendeleo endelevu na kutokomeza umaskini.

150. Kuratibu mikakati ya kitaifa ya tabianchi, nishati, na maendeleo ili kuhakikisha mshikamano, kuepuka mgawanyiko wa sera, na kuwezesha

ufanisi wa utekelezaji wa nishati mbadala na kuratibu ufuatiliaji kwa kuhakikisha uthabiti wa sera".

151. Nchi zilizoendelea kuongeza juhudi za kitaifa na za pamoja kuelekea utoaji na uhamasishaji wa rasilimali za umma kwa njia inayotegemea ruzuku au kwa njia ya masharti nafuu kwa nchi za Kiafrika zinazoendelea kupunguza, na hasara na uharibifu;

152. Kutekeleza Mkakati wa Madini ya Kijani Afrika kwa lengo la kupunguza athari za kiikolojia za shughuli za uchimbaji madini kupitia utumiaji wa teknolojia safi, ukarabati wa ardhi zilizoharibika, na utekelezaji mkali wa kanuni za mazingira zinazotetea haki za jamii za wenyeji, kuhakikisha utendaji kazi wa haki, na kukuza usawa wa kijinsia katika sekta ya madini.

153. Kuunda mshikamano wa Kimajumui kwa hatua za tabianchi na maendeleo na endelevu.

154. Kuhakikisha sauti ya Afrika inasikika katika mazungumzo ya kimataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi na kuhimiza utambuzi wa haki wa michango ya Afrika.

155. Kuthibitisha tena hitaji la Kamisheni ya AU kuharakisha maendeleo ya Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu uhusiano kati ya mabadiliko ya tabianchi, amani, na usalama.

## O. AZIMIO

156. Kwa kutambua haja ya mipango ya kimkakati ya kina, utekelezaji wenye athari zaidi, na uratibu imara wa kikanda, tunapendekeza kwamba Mkutano mkuu wa tabianchi kuitishwa kila baada ya miaka mitatu badala ya miaka miwili na uandaliwe kwa kupeana mzunguko wa zamu ndani ya kanda tano za Umoja wa Afrika na hatua za ufuatiliaji zilizochukuliwa na Kundi la Wazungumzaji wa Afrika (AGN) na AMCEN chini ya uongozi wa CAHOSCC, kwa usaidizi wa Kamisheni ya AU na Sekretarieti ya ACS ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa ahadi zilizotolewa.

157. Tunaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia kwa kuandaa kwa ufanisi Mkutano mkuu wa Pili wa Kiafrika wa Tabianchi, na ukarimu uliooneshwa kwa wajumbe wote katika Mkutano huo.

**LIMEPITISHWA na Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika na Wawakilishi wa Ngazi za Juu wa Umoja wa Afrika mnamo tarehe 10 Septemba 2025, Addis Ababa, Ethiopia.**

i. " Maazimio ya Ufafanuzi " yaliyopitishwa na Ethiopia na Afrika Kusini Afrika katika aya 5, c, 18, 102, 103, 105, 107, 108, 110, 155, na katika kichwa cha habari cha Sehemu K, yakielezea kutokuelewa uhusiano kati ya mabadiliko ya tabianchi na amani na usalama, na kubainisha kwamba hakuna msimamo wa pamoja wa Kiafrika unaotambua hali kama hiyo, na suala la amani na usalama sio wajibu wa Mkutano Mkuu wa Tabianchi; Azimio la Ufafanuzi lililopitishwa na Ethiopia katika aya za 87, 104, 138, na 144, mtawalia, linafafanua kwamba maandishi yanayohusiana na uhimilivu wa Tabianchi ni kukubaliwa pekee na marejeleo ya marekebisho katika sekta; ushirikiano huo wa usimamizi wa mito unaeleweka kama matumizi ya haki na usawa; kwamba usalama wa maji na chakula hayajakukubaliwa; na inasisitiza kwamba pande zote hazijakubaliana kuhusu uhusiano kati ya mabadiliko ya tabianchi na amani na usalama".

## TAMKO LA MKUTANO WA UWEKEZAJI WA MAJI WA AFRIK

**SISI** Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tulikutana tarehe 15 Februari 2026 katika Mkutano wetu wa 39 wa Kawaida mjini Addis Ababa, Ethiopia;

**TUNAPITISHA** Tamko lililoambatanishwa la Mkutano wa Uwekezaji wa Maji wa Afrika uliofanyika Cape Town, Afrika Kusini, kuanzia tarehe 13 hadi 15 Agosti 2025

# TAMKO LA MKUTANO WA UWEKEZAJI KWENYE MAJI AFRIKA “TAMKO LA CAPE TOWN KUHUSU UWEKEZAJI WA AFRIKA KWENYE MAJI KATIKA MUKTADHA WA G20”

## DIBAJI

**SISI**, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika, wakiwepo viongozi wengine wa Dunia, tuliokusanyika mjini Cape Town kuanzia tarehe 13 hadi 15 Agosti, 2025 kwa ajili ya Mkutano wa Ufunguzi wa Uwekezaji wa Maji Afrika, ulioitishwa chini ya Umoja wa Afrika, Jopo la Ngazi ya Juu la Uwekezaji wa Maji kwa Afrika na Urais wa G20 wa Jamhuri ya Afrika Kusini.

Wengine waliohudhuria ni Mawaziri na Manaibu Mawaziri, taasisi za fedha, wawekezaji, washirika wa maendeleo, asasi za kiraia, wataalamu wa kiufundi, mashirika ya kujitolea, Mashirika ya Kiserikali, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Sekta Binafsi, Vijana, Wanawake na Wasomi.

**TUKIREJEA** ahadi ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mwezi Julai 2008, kupitia Azimio la Sharm El Sheik kuhusu Maji na Usafi wa Mazingira (Assembly/AU/Decl.1(xii), ambalo linalenga kuharakisha kufikia malengo ya maji na usafi wa mazingira barani Afrika.

**TUKIREJEA PIA** Dira ya Maji Afrika 2025, ambayo inatazamia “Afrika ambapo kuna matumizi na usimamizi sawa na endelevu wa rasilimali maji kwa ajili ya kupunguza umaskini, maendeleo ya kijamii na kiuchumi, ushirikiano wa kikanda na mazingira”.

**TUKITAMBUA** kwamba uwekezaji duni kwenye maji umeathiri mafaniko yaliyopatikana katika maeneo yote ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na jukumu muhimu la maji katika kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kufikia malengo ya Ajenda 2063.

**TUKITAMBUA** kwamba Programu ya Uwekezaji wa Maji ya Bara la Afrika (AIP) ni wazo la Jopo la Ngazi ya Juu la Umoja wa Mataifa na Benki ya Dunia kuhusu Maji (HLPW). Programu hii ilianzishwa na Katibu Mkuu wa Umoja Mataifa Ban Ki-Moon na Rais wa Benki ya Dunia Jim Yong Kim, ukijumuisha Marais na Mawaziri Wakuu kumi na mmoja walio madarakani.

**TUKITAMBUA** haja ya kujenga uhimilivu wa tabianchi kupitia uwekezaji wa maji barani Afrika ili kukabiliana na athari kubwa na za mara kwa mara zinazotarajiwa za mabadiliko ya tabianchi kama ilivyoelezwa kwenye Mkakati na Mpango Kazi wa Maendeleo wa Umoja wa Afrika wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (2022-2032).

**TUKIREJELEA** Programu ya Uwekezaji wa Maji ya Bara la Afrika (AIP) kama sehemu ya Programu ya Kuendeleza Miundombinu kwenye Mpango Kazi wa Pili wa Kipaumbele wa

Afrika (PIDA- PAP 2) iliyoidhinishwa na Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika wakati wa Kikao cha 34 cha Kawaida cha Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika uliofanyika mwezi Februari 2021 (EX.CL/1108(XXXVIII)).

**TUKIREJELEA** uzinduzi wa Jopo la Ngazi ya Juu kuhusu Uwekezaji wa Maji kwa Afrika wakati wa Jukwaa la 9 la Maji Duniani jijini Dakar tarehe 25 Machi 2022 ikijumuisha wenyeviti wenza waanzilishi; Jamhuri ya Senegali, Jamhuri ya Namibia; Ufalme wa Uholanzi, na Rais wa awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**TUKITAMBUA** kwamba wakati wa Mkutano wa Maji wa Umoja wa Mataifa mwaka 2023 huko New York, Umoja wa Afrika na Jopo la Ngazi ya Juu la Kimataifa walitoa Ripoti ya Jopo la Ngazi ya Juu, yenye kuelekeza njia kwa nchi kwa kuhamasisha angalau Dola bilioni 30 za Marekani kila mwaka ifikapo mwaka 2030 kwa ajili ya kuziba pengo la uwekezaji kwenye maji barani Afrika, kama sehemu ya Ajenda ya Umoja wa Mataifa ya Kuondoa Tatizo la Maji.

**TUKIREJELEA** kwamba mwezi Disemba 2023 wakati wa COP 28 huko Dubai, UAE, Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Jopo la Ngazi ya Juu la Kimataifa la AIP walizindua Mpango Kazi wa Uwekezaji wa Maji Afrika, ukielezea jinsi nchi zinavyoweza kuhamasisha fedha za ziada kiasi cha Dola bilioni 30 za Marekani kwa mwaka zinazohitajika ili kuhakikisha usalama wa maji na usafi endelevu wa mazingira barani Afrika.

**TUKIRIDHISHWA** na Azimio la AU Na. EX.CL/Dec.2(XLIV)Rev.1/42: LINALOIDHINISHA pendekezo la kupitisha "Kuhakikisha Upatikanaji Endelevu wa Maji na Mifumo Salama ya Usafi wa Mazingira ili Kufikia Malengo ya Ajenda 2063" kama Kaulimbiu ya Umoja wa Afrika ya mwaka 2026.

**TUKIUTAMBUA** Ufalme wa Saudi Arabia (KSA) kwa kuanzisha Majadiliano ya kwanza ya Maji ya G20 chini ya Urais wa KSA wa G20 mwaka 2020 ambayo yalizingatia maji kama ufunguo wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, yakiungwa mkono na Nchi Wanachama wa G20.

**TUKITAMBUA** kwamba Mkutano huo wa Wakuu wa Nchi na Serikali unafanyika katika kipindi cha kihistoria, kinachoashiria Urais wa kwanza wa G20 kuwa mwenyeji barani Afrika na kukubaliwa kwa Umoja wa Afrika katika uanachama wa G20.

**TUKISISITIZA** kwamba maji na usafi wa mazingira si tu msingi wa amani na ukuaji wa uchumi na maendeleo, heshima ya binadamu na afya ya jamii lakini pia ni muhimu kwa uhimilivu wa tabianchi, usalama wa chakula, mageuzi ya kiuchumi, na kupiga hatua katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu.

**TUKISHUKURU** kwa fursa iliyopatikana kupitia Urais wa G20 wa Afrika Kusini ili kuinua uwekezaji wa maji Afrika, kuzingatia pengo katika uwekezaji wa maji na kutumia uanachama wa Umoja wa Afrika kwenye G20 na fursa ya kuangazia matokeo ya Mkutano huo kwa umuhimu katika tamko hili.

**TUNAPOKEA** matokeo ya awali ya kifedha yaliyobainishwa kwenye vyanzo vilivyopo kwenye Mkutano huo, vinavyokadiriwa kufikia dola bilioni 10 hadi 12 kila mwaka zinazoweza kuwekezwa kutoka kwa baadhi ya Benki za Maendeleo, Wawekezaji, pande mbili na serikali, Barani kote.

**TUKIZINGATIA** kwamba yaliyoelezwa hapo juu hayajumuishi ahadi na uwekezaji unaotarajiwa ambao utaunganishwa. Wawekezaji zaidi katika vikao vya uoanishaji wameahidi kuwasilisha ahadi zao za awali kwa njia ya mtandao, ambazo zitaongeza jumla ya ahadi zilizotolewa, zilizopatikana katika Mkutano huu.

**TUNAAHIDI KUFANYA YAFUATAYO:**

1. Kuweka mazingira wezeshi ya kuimarisha uwekezaji kwa ajili ya maji na usafi wa mazingira, yanayoendana na mipango ya maendeleo ya kitaifa, SDG 6, na vipaumbele vya uhimilivu wa tabianchi.
2. Kuongeza fedha za ndani za sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya uwekezaji kwenye maji, ikijumuisha kupitia bajeti za kitaifa, na mifumo bunifu ya ufadhili.
3. Kuiomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuedelea kutoa mwongozo katika utekelezaji wa Programu ya Uwekezaji wa Maji Afrika (AIP), kufuatilia maendeleo kwa kutumia Viashiria vya Uwekezaji wa Maji vya AIP, na kusaidia Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda ili kuendeleza programu za uwekezaji wa maji zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi kitaifa na kikanda.
4. Pamoja na hayo, kuiomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuzisaidia Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda katika kuendeleza miradi ya kukusanya rasilimali, ikiwa ni pamoja na ufadhili wa tabianchi.
5. Kutoa wito wa mageuzi ya taasisi za fedha za kimataifa, kwa kuzingatia kuzingatia haja ya kuhakisha uwekezaji katika sekta ya maji na usafi wa mazingira, kwa kutoa kipaumbele kwa Afrika ili kuziba pengo la uwekezaji kwenye maji.
6. Kutumia njia za kupunguza athari ambapo zitaongeza thamani halisi - hasa katika maeneo ya vijijini na pembezoni ambayo hayajahudumiwa vya kutosha, maeneo tete na yaliyoathiriwa na migogoro, na kwa ajili ya suluhisho za kiasili.
7. Kuongeza upatikanaji wa maji ili kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi na kuboresha afya za watu, lishe na ustawi kote barani; kwa kutambua kwamba uwekezaji kwenye maji unaweza kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na kujenga uhimilivu.
8. Kutoa wito kwa serikali na washirika wao wa maendeleo kufanya kazi kwa pamoja kuweka mazingira yanayohitajika ili kuvutia na kupata uwekezaji mkubwa, ikiwa ni pamoja na ufadhili wa sekta ya umma na binafsi, katika kuongeza usalama wa maji na upatikanaji wa maji salama na usafi wa mazingira.
9. Kuhamasisha mtaji wa masharti nafuu na wezeshi ili kuwezesha uwekezaji pale ambapo mtaji binafsi pekee hauwezi kupatikana.
10. Kutoa kipaumbele kwa manufaa ya umma na umiliki wa ndani, hususan katika maeneo ambapo huduma za maji zinabaki kuwa muhimu kwa ajili ya haki za

binadamu na maendeleo.

11. Kutoa wito kwa taasisi za fedha za kitaifa, kimataifa na kikanda barani Afrika kuweka kipaumbele katika kufadhili miradi ya uwekezaji wa maji na usafi wa mazingira, ikiwa ni pamoja na mifumo bunifu ya ufadhili.

**Mwongozo na uwajibikaji**

12. Kuipongeza Afrika Kusini kwa Urais wa G20 na kuzindua Baraza la Mtazamo wa Kimataifa kuhusu Uwekezaji kwenye Maji, kama Mpango wa Kihistoria unaohamasisha uwekezaji kwenye maji katika ngazi za juu zaidi za diplomasia ya kimataifa.
13. Kuomba kujumuishwa kwa Tamko hili kama sehemu ya matokeo ya Urais wa Afrika wa G20, kufuatilia na kuripoti maendeleo mara kwa mara katika utekelezaji wa Mpango wa Kihistoria.
14. Kutoa wito kwa viongozi wa G20 kusaidia kupitishwa kwa maji kama kipaumbele cha uwekezaji katika kubadilisha taswira ya ufadhili wa kimataifa.
15. Kutoa wito kwa wenyeji-wenza wa Mkutano wa Umoja wa Matiafa wa Maji mwaka 2026, UAE na Senegali, kukazia Azimio hili katika mchakato wa maandalizi.
16. Kuazimia kuitisha Mikutano ya Uwekezaji wa Maji Afrika kila baada ya miaka 4 kwa mzunguko wa kikanda, chini ya uratibu wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika.
17. Kuiomba Jamhuri ya Afrika Kusini, kwa mamlaka yake ya Urais wa G20, kuwasilisha Tamko hili kwenye Kikao cha 39 cha Kawaida cha Mkutano wa Umoja wa Afrika wa Wakuu wa Nchi na Serikali mwezi Februari 2026 kwa ajili ya kuidhinishwa.

**Limepitishwa tarehe 15 Agosti 2025, mjini Cape Town, Afrika Kusini.**

---

## TAMKO LA MKUTANO WA KWANZA WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI KUHUSU BIOANUWAI AFRIKA

**SISI** Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tulikutana tarehe 15 Februari 2026 katika Mkutano wetu wa 39 wa Kawaida mjini Addis Ababa, Ethiopia;

**TUNAPITISHA** Tamko lililoambatanishwa la Mkutano wa Kwanza wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Bioanuwai Afrika uliofanyika Gaborone, Jamhuri ya Botswana, tarehe 5 Novemba 2025.

## TAMKO LA MKUTANO WA KWANZA WA BIOANUWAI AFRIKA

## TAMKO LA VIONGOZI WA AFRIKA LA GABORONE KUHUSU BIOANUWAI

1. **Sisi**, **Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika**, pamoja na wawakilishi wa mashirika ya kikanda na kimataifa, tumekutana Gaborone, Jamhuri ya Botswana, tarehe 5 Novemba 2025, kwa ajili ya Mkutano wa Kwanza wa Bioanuwai wa Afrika;

2. **TUKIREJELEA** maamuzi ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali Assembly (AU/Dec.15(XVI) Add.3 na Assembly/AU/Dec.926(XXXVIII)), ambayo kwa nyakati tofauti yalifanya bioanuwai kuwa mojawapo ya vipaumbele vya Umoja wa Afrika, yaliamua kuitisha Mkutano wa Kwanza wa Bioanuwai wa Afrika na kuomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuandaa Mkutano huo;

3. **TUKIIPONGEZA** Jamhuri ya Botswana, chini ya uongozi wenye maono wa Rais Duma Gideon Boko, kwa kuandaa na kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kwanza wa Bioanuwai wa Afrika;

4. **TUKIREJELEA** Ajenda ya mwaka 2063 ya Umoja wa Afrika na dira yake ya Afrika ambayo utajiri wa mazingira na huduma za mifumoikolojia zenye ubora, zinazothaminiwa na kulindwa, pamoja na Tamko la Gaborone kuhusu Uendelevu Barani Afrika lililopitishwa mwaka 2012 na azma yake ya “kuhakikisha mchango wa mtaji unaotokana na mazingira katika ukuaji endelevu wa uchumi”;

5. Pia, **TUKIREJELEA** uamuzi wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali Assembly/AU/Dec.15(XVI) Add.3 kuhusu Ajenda ya Mpango wa Bara la Afrika ya Kurejesha Mifumoikolojia kwa ajili ya Kuongeza Uhimilivu;

6. **TUKITAMBUA** kwamba Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi wa Ajenda ya mwaka 2063 ya Umoja wa Afrika unajumuisha bioanuwai kupitia mazingira endelevu na uchumi pamoja na jamii zinazohimili mabadiliko ya tabianchi, kama sehemu muhimu ya kufikia lengo kuu la “Afrika yenye ustawi inayojengwa juu ya ukuaji shirikishi na maendeleo endelevu.”

7. **TUKITAMBUA** kwamba Afrika ni makazi ya zaidi ya robo ya bioanuwai ya dunia, ikiwa na misitu mikubwa, savana, maeneo ya misitu ya asili, maeneo oevu, mifumoikolojia ya maji baridi na ya baharini, ambayo ndiyo msingi wa kilimo, uvuvi, utalii, uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na maisha ya mamilioni ya watu;

8. **TUKITHIBITISHA** kwamba bioanuwai ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Afrika na rasilimali ya kimkakati kwa maendeleo ya kiuchumi na kupunguza umaskini;

9. **TUKITAMBUA** umuhimu wa kulinda mifumoikolojia tajiri na yenye uanuwai ya Afrika katika mazingira ya shinikizo linaloongezeka la kimazingira, tunakubaliana kuufanya Mkutano wa Afrika wa Bioanuwai kila baada ya miaka minne;

10. **TUKITAMBUA** mchango muhimu wa maeneo ya uhifadhi yanayovuka mipaka ya nchi barani Afrika kama vielelezo vya kulinda bioanuwai kwa kiwango kikubwa, huku yakikuza ujumuishaji wa kikanda.

11. **TUKIREJELEA** Mpango Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Bioanuwai wa Afrika, Mpango wa Usimamizi Endelevu wa Misitu Barani Afrika, Mkakati wa Afrika wa Kupambana na Uvunaji Haramu na Biashara Haramu ya Wanyamapori na Mimea Asilia Barani Afrika, Mpangomkakati wa Kulinda Mazingira wa Umoja wa Afrika na Mpango wa Utekelezaji wa Miaka Kumi: Urejeshaji wa Mifumoikolojia na Maisha ya watu, pamoja na Uhimilivu (2024–2034);

12. **TUKIKARIBISHA** kupitishwa kwa Mfumo wa Kimataifa wa Bioanuwai wa *Kunming–Montreal* na Mfuko wa Mpango wa Kimataifa wa Bioanuwai pamoja na mikataba mingine ya kimataifa inayohusiana, ikiwamo makubaliano muhimu ya kihistoria kuhusu Uhifadhi na Matumizi Endelevu ya Bioanuwai ya Baharini katika Maeneo Yaliyo Nje ya Mamlaka ya Kitaifa chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria ya Bahari, na tunakaribisha kuanzishwa kwa Makundi ya Afrika ya Wajadiliano kuhusu masuala yanayohusiana na bioanuwai pamoja na mifumo mingine ya uratibu kwa ajili ya kuchangia katika kuunda matokeo ya kimazingira ya kimataifa kupitia misimamo ya pamoja.

13. **TUKITAMBUA** mchango wa Mkutano wa Mawaziri wa Afrika kuhusu Mazingira katika kutoa mwelekeo wa kimkakati na kisera kuhusu vipaumbele vya mazingira, ikiwamo vile vinavyohusiana na bioanuwai;

14. **TUKIELEZEA MASIKITIKO YETU MAKUBWA** kwamba bioanuwai tajiri ya Afrika iko katika hatari kubwa, jambo linalodhoofisha usalama wa chakula, afya, matarajio ya kiuchumi na uhimilivu;

15. **TUKISISITIZA** kwamba upotevu wa bioanuwai, mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa ardhi, jangwa na uchafuzi wa mazingira ni migogoro inayohusiana na kushabihiana, inayozidisha hatari kwa maendeleo ya Afrika;

16. **TUKISISITIZA** zaidi nafasi muhimu ya ufadhili unaoongozwa na Afrika kupitia taasisi za kifedha za bara lenyewe, na kuhimiza Nchi Wanachama kuharakisha kuridhia mikataba yao ya uanzishwaji. Kuimarisha taasisi hizi kutaboresha uwezo wao wa kutafuta rasilimali na kufadhili masuala ya bioanuwai barani Afrika, na hivyo kusukuma mbele malengo ya maendeleo na uendelevu ya bara;

17. **TUKITAMBUA** mchango wa mbinu ya Afya Jumuishi katika kulinda bioanuwai na kuhakikisha afya na ustawi wa binadamu;

18. **TUKITAMBUA** kwamba, licha ya kuwapo kwa juhudi na mifumo muhimu barani Afrika kuhusu bioanuwai, utekelezaji wake si madhubuti wala wenye ufanisi, hali inayosababisha kuendelea kwa upotevu wa bioanuwai.

19. **TUKISIKITISHWA** kwamba ufadhili wa bioanuwai haukidhi mahitaji ya Afrika na tukitambua umuhimu kwamba ubunifu na ongezeko la upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo vya ndani na vya kimataifa ni muhimu sana katika kutekeleza malengo yetu ya bioanuwai;

20. **TUKISISITIZA** kwamba watu ni kitovu cha shughuli za bioanuwai na tukitambua maarifa ya asili, ulinzi na mbinu endelevu za jamii za wenyeji, pamoja na mchango usiopingika wa wanawake na vijana katika kulinda bioanuwai ya Afrika;

21. **TUKISISITIZA** kwamba uhifadhi wa bioanuwai, matumizi endelevu ya vipengele vyake, na usambazaji wa haki na usawa wa manufaa ya asili hutoa fursa kubwa kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi barani Afrika.

22. **TUMEAZIMIA** kuchukua hatua madhubuti, kwa umoja na dharura, ili kuangamiza upotevu wa bioanuwai na kuhakikisha kwamba manufaa ya urithi wa asili wa Afrika yanadumishwa kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

23. **TUKITAMBUA** kwamba sauti ya pamoja ya Afrika kuhusu bioanuwai lazima ianzishwe kwenye thamani za pamoja, uangalizi wa kimaadili, na kanuni ya haki ya kiikolojia, na tukirejea wajibu wetu wa pamoja wa kulinda urithi wa asili wa bara kama msingi wa kimaadili wa ujio mpya wa Afrika.

**HIVYO TANAAZIMIA NA KUDHAMIRIA KAMA IFUATAVYO:**

24. Kuimarisha usimamizi wa bioanuwai katika ngazi zote barani Afrika, kuhakikisha uwazi, mshikamano na uwajibikaji katika taasisi zote, ikiwamo kuhuisha na kuwianisha sera, sheria na taasisi ili kutekeleza Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Bioanuwai wa Umoja wa Afrika, Mkakati wa Afrika wa Kupambana na Uvunaji Haramu na Biashara Haramu ya Wanyamapori na Mimea Asilia, Mkakati wa Uchumi wa Kijani wa Baharini wa Afrika, Ajenda ya Hatua ya Bara la Afrika ya Kurejesha Mifumoikolojia kwa Kuongeza Uhimilivu, na Mfumo wa Kimataifa wa Bioanuwai wa *Kunming–Montreal* kwa ufanisi;

25. Kuhimiza Nchi Wanachama zote kuhuisha na kutekeleza Mikakati yao ya Kitaifa ya Bioanuwai na Mipango ya Utekelezaji kwa kuwinisha na Mpango wa Kimataifa wa Bioanuwai wa Kunming–Montreal, na kujumuisha mikakati hii katika mipango ya kitaifa ya maendeleo, sera za sekta na bajeti.

26. Kujumuisha masuala ya bioanuwai katika kilimo, uvuvi, misitu, madini, nishati, miundombinu, uzalishaji na usindikaji, utalii, bioteknolojia na sekta nyinginezo, ili malengo ya uhifadhi na maendeleo yaende sambamba na kuimarishana;

27. Kukuza haki ya kiikolojia na usawa katika mgawanyo wa manufaa ya bioanuwai, kuhakikisha kwamba jamii za wenyeji na Watu wa Asili wanapata fidia stahiki kwa gharama za uhifadhi, huduma za mifumoikolojia, na kupoteza upatikanaji wa maliasili zinazotokana na sera za kimazingira za kimataifa;

28. Kuimarisha uratibu wa taasisi kupitia mbinu za serikali nzima kwa ajili ya utekelezaji unaoeleweka wa ahadi za bioanuwai kwa kuanzisha au kuimarisha kamati za mawaziri za kikanda katika ngazi ya kitaifa ili kusimamia ujumuishaji wa sera na utekelezaji wake.

29. Kuiomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kwa kushirikiana na washirika, kuimarisha uratibu wa kikanda, ikiwamo kupitia kuanzishwa kwa Mfumo wa Uratibu wa Bioanuwai wa Afrika, ili kukuza mshikamano wa jitihada katika Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda pamoja na miradi yao;

30. Kuhimiza Nchi Wanachama ambazo bado hazijafanya hivyo, kuridhia na kutekeleza kwa ufanisi Mkataba wa Afrika wa mwaka 2003 uliorekebishwa kuhusu Uhifadhi wa Asili na Maliasili pamoja na mikataba na protokali ya kimataifa na kikanda inayohusiana na bioanuwai;

31. Kuhimiza Nchi Wanachama zote ambazo bado hazijafanya hivyo, kuridhia Makubaliano chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria ya Bahari kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya bioanuwai ya baharini katika maeneo yaliyo nje ya mamlaka ya kitaifa, na kwa pamoja kutafuta utambulisho wa maeneo ya baharini yaliyo na ubora wa juu na yaliyosimamiwa kwa ufanisi.

32. Kusisitiza umuhimu wa kuendeleza mifumo ya uwajibikaji ili kutekeleza kikamilifu dhamira ya kusitisha na kuzuia nyuma ukataji miti na uharibifu wa ardhi ifikapo mwaka 2030, kama ilivyoainishwa katika Tamko la Addis Ababa lililopitishwa katika Kikao cha 19 cha Kawaida cha Mkutano wa Mawaziri wa Afrika wanaoshughulikia Mazingira, hatua itakayochochea maendeleo ya kimataifa na kukuza usawa zaidi katika viwango vya ulinzi wa misitu.

33. Kurekebisha na kuhuisha sheria na sera za kitaifa na kikanda zinazohusiana na bioanuwai ili kushughulikia changamoto za sasa, kuunda mazingira yanayounga mkono ukuaji wa uchumi wa kijani, na kuimarisha uwezo wa kutimiza, kutekeleza na kusimamia sheria na sera hizi.

34. Kuhakikisha mbinu ya ushiriki wa jamii nzima na ushiriki kamili na wa ufanisi wa jamii za wenyeji, asasi za kiraia, wanawake na vijana katika maamuzi na hatua zinazohusiana na bioanuwai;

35. Kushirikiana ili kuhakikisha kuwa spishi zote za wanyamapori zilizo hatarini kutokana na matumizi ya moja kwa moja yasiyo endelevu zinatambuliwa, zinafuatiliwa, zinalindwa ipasavyo chini ya Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira, pamoja na sheria za kitaifa, na kurejeshwa kupitia hatua madhubuti za uokoaji na urejeshaji.

36. Kuimarisha ushirikiano kati ya jamii na mshikamano wa kikanda kupitia jukwaa la ushiriki linalounganisha wanasayansi, walinzi wa asili wa jadi, vijana, na watunga sera, kuhakikisha kwamba maarifa ya bioanuwai ya Afrika yanasambazwa, kulindwa na kutumika kwa ustawi wa pamoja.

37. Kuimarisha na kupanua maeneo ya uhifadhi yanayovuka mipaka na maeneo yaliyolindwa, na hivyo kuchangia katika utekelezaji wa ahadi ya kimataifa ya kulinda asilimia 30 ya sayari kufikia mwaka 2030 kama ilivyowekwa katika Lengo la 3 la Mpango wa Kimataifa wa Bioanuwai wa Kunming-Montreal, kama miradi ya mfano ya kulinda mifumoikolojia na spishi zinazoshirikiana barani Afrika;

38. Kuwekeza katika kutumia kikamilifu uwezo wa bioanuwai na maarifa ya jadi kusukuma ukuaji endelevu wa uchumi, utofauti, na uhimilivu barani Afrika ikiwamo fursa za uchumi zinazotegemea asili, biashara endelevu ya bioanuwai na viwanda vya bioanuwai, vinavyotumiwa kwa haki kwa walinzi wa rasilimali ili kufungua masoko ya kikanda na ya kimataifa kwa bidhaa zinazotokana na bioanuwai na kuongeza ushindani wa Afrika katika uchumi wa dunia wa bioanuwai;

39. Kutoa wito kwa Nchi Wanachama kuandaa mikakati ya uchumi unaotegemea bioanuwai na mipango ya utekelezaji ili kutumia kikamilifu kwa njia endelevu uwezo wa kiuchumi wa mtaji wa asili wa Afrika, na kuomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika na washirika wake kukusanya rasilimali za kifedha kwa ajili ya mpango huu;

40. Kujumuisha thamani ya bioanuwai katika michakato ya hesabu na mipango ya kitaifa ya maendeleo ili kufanya mchango wa asili uonekane katika maamuzi yetu ya kiuchumi na kuvutia uwekezaji na ufadhili wa maendeleo kwa ajili ya uhifadhi wa bioanuwai;

41. Kuimarisha uwezo wa data na taarifa ili kuongoza usimamizi na mifumo ya upatikanaji wa fedha na bioanuwai barani Afrika;

42. Kuimarisha na kuwezesha mtandao wa Vituo vya Kikanda vya Kitaalamu (TRCs) kama uti wa mgongo wa miundombinu ya maarifa ya bioanuwai barani Afrika na

kujumuisha TRC katika utawala wa kikanda ili kukuza uhusiano kati ya sayansi na sera.

43. Kupanua mbinu zinazotegemea mifumoikolojia na urejeshaji wa mifumo ikolojia ili kuchangia kupunguza mabadiliko ya tabianchi huku bioanuwai ikilindwa.

44. Kukuza mshikamano mkubwa katika utekelezaji wa Mkataba wa Bioanuwai, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Jangwa na mikataba mingine inayohusiana na mazingira katika ngazi ya kitaifa, kuhakikisha kwamba upatikanaji wa fedha za tabianchi na mipango ya uhimili yenye gharama nafuu, ili kufikia malengo ya bioanuwai na tabianchi kwa wakati mmoja.

45. Kuboresha na kuimarisha usimamizi wa maeneo oevu kama chombo cha kulinda bioanuwai kwa wingi.

46. Kuongeza kwa kiasi kikubwa ufadhili wa ndani na kutafuta ufadhili wa kimataifa kwa ajili ya bioanuwai na kutamani kutenga angalau asilimia 1 ya Pato la Taifa (GDP) kwa ajili ya kuelekea bioanuwai, kama uwekezaji katika uchumi wetu na ustawi wa watu;

47. Kusisitiza uongozi wa Afrika katika kuunda ajenda ya kimataifa ya bioanuwai na kudai uwakilishi wa haki katika vyombo vya kimataifa vya maamuzi vinavyohusiana na mazingira na rasilimali za asili. Afrika haiwezi tena kuwa tu kipengele cha kufanyiwa maamuzi bali iwe mdau mkuu wa utawala wa bioanuwai.

48. Kuunga mkono Ajenda na Tamko la Wanyamapori kwa ajili ya Hatua za Tabianchi na kuhamasisha dunia nzima kuunga mkono Afrika na rasilimali za wanyamapori wa Afrika;

49. Kuandaa na kutekeleza mipango ya kitaifa ya ufadhili wa bioanuwai ili kufunika pengo la ufadhili;

50. Kukuza fursa za bioanuwai kwa kuvutia uwekezaji binafsi na kuhamasisha biashara ya kawaida ili kuhakikisha uendelevu wa bioanuwai ya Afrika;

51. Kuhimiza Nchi Wanachama kutekeleza Mpango wa Uhusiano wa Maeneo Yaliyo Hifadhiwa ya Afrika wa dola bilioni 1.2 kwa mwaka na kukusanya rasilimali za ziada kwa ajili ya mifumo mingine ya mifumoikolojia.

52. Kuhimiza washirika wa maendeleo wa kimkakati kutekeleza ahadi zao za kutoa angalau dola bilioni 30 kwa mwaka kufikia mwaka 2030 kwa ufadhili wa bioanuwai kwa nchi zinazoendelea kama ilivyokubaliwa katika Mfumo wa Kimataifa wa

Bioanuwai wa Kunming-Montreal, na kuomba kuanzishwa kwa mifumo ya uwajibikaji kufuatilia utekelezaji wa ahadi za kimataifa kufikia mwaka 2027;

53. Kuhimiza Mfuko wa Mazingira wa Ulimwengu, Mfuko wa Mpango wa Kimataifa wa Bioanuwai na mifumo mingine ya ufadhili ya kimataifa ikiwamo Mfuko wa Bioanuwai wa Kunming, Mfuko wa Cali na Mfuko wa Kijani wa Tabianchi, kuipa kipaumbele upatikanaji wa haki kwa nchi za Afrika, na kualika taasisi za uhisani, sekta binafsi, na benki za maendeleo za kimataifa kuongeza kwa kiasi kikubwa na kurahisisha upatikanaji wa ufadhili kwa jitihada za usimamizi wa bioanuwai barani Afrika;

54. Kuomba kuanzishwa kwa majukwaa ya Afrika kwa ajili ya kushirikishana mbinu bora na bunifu za kifedha, kama vile mikopo ya bioanuwai, dhamana za kijani na za buluu, na malipo kwa huduma za mifumoikolojia.

55. Kuhimiza kuanzishwa kwa Mfuko wa Bioanuwai wa Afrika ili utumike kama mfumo maalumu, wa haki na unaopatikana kwa urahisi wa ufadhili wa bioanuwai barani Afrika, na kuomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuandaa mbinu za kuendesha Mfuko huu;

56. Kualika Benki ya Maendeleo ya Afrika, taasisi za kifedha za kikanda za Afrika na Nchi Wanachama kuunda mipango ya ziada ya ufadhili, ikiwamo ufadhili mchanganyiko kama vile mikopo na fidia za bioanuwai, dhamana za kijani na za bluu, na mifumo ya malipo kwa huduma za mifumo ikolojia inayochangia mtaji wa umma na binafsi.

57. Kusisitiza wito wa Afrika kwa ajili ya mageuzi ya mifumo na mifumo ya fedha ya kimataifa ili kutoa fursa bora za nchi zinazoendelea za kupata ufadhili unaohusiana na bioanuwai ili kukidhi mahitaji yao;

58. Kuzungumza kwa sauti moja ili kutetea vipaumbele vyetu vya pamoja katika majukwaa ya kimataifa ya bioanuwai kwa kuimarisha uratibu wa kikanda na uongozi katika shughuli za kimataifa za mazingira, kuimarisha Makundi ya Afrika ya Waendesha majadiliano katika majadiliano yanayohusiana na bioanuwai, na kushirikisha jamii za wenyeji, wanawake, vijana, asasi za kiraia, taasisi za elimu na sekta binafsi;

59. Kukuza ushirikiano kati ya sekta mbalimbali kati ya serikali, asasi kiraia na sekta binafsi, ili kuhamasisha mbinu bunifu na uwekezaji unaochangia kwa njia chanya kwenye mazingira asili unaosaidia mabadiliko ya uchumi endelevu huku ukihifadhi bioanuwai na kuimarisha uhimilivu wa mifumo ikolojia kote barani, kwa mujibu wa Tamko la Gaborone kuhusu Uendelevu Barani Afrika.

60. Kujumuisha elimu ya bioanuwai katika mitaala ya kitaifa na programu za uraia, kukuza ufahamu wa kiikolojia wa Kiafrika unaothamini mshikamano na asili, kujitegemea, na usimamizi wa rasilimali kama maadili muhimu kwa ustawi endelevu.

61. Kuhimiza kujengea uwezo, ushirikiano wa kitaalamu na kisayansi na uhawilishaji wa teknolojia, ikiwamo kuondoa vikwazo vya kupata teknolojia zinazofaa kwa ajili ya ufuatiliaji wa bioanuwai, usimamizi na matumizi endelevu, pamoja na maendeleo ya uchumi unaotegemea maliasili;

62. Kuongeza uwekezaji ili kufanikisha kuziba pengo la kisayansi, kiteknolojia na kiubunifu ili taasisi na kampuni za Afrika ziwe na vifaa na uwezo wa kutumia zana za kisasa za bioanuwai ikiwamo teknolojia za kidijitali kwa ajili ya utafiti na maendeleo;

63. Kuipa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kwa kushirikiana na Nchi Wanachama, Jumuia za Kiuchumi za Kikanda, mashirika ya Umoja wa Mataifa na washirika husika, jukumu la kufuatilia na kurahisisha utekelezaji wa ahadi zilizotolewa katika Azimio hili.

64. Kuomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Uchumi ya Afrika (ECA) na Mpango wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa (UNEP), kuandaa ripoti ya kila miaka minne kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa azimio hili, kwa ajili ya kuwasilishwa katika kila Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika kuhusu Bioanuwai.

65. Kutambua kwamba bioanuwai ni kiini cha uhuru wa kiikolojia na kiuchumi wa Afrika, ukiunganisha nguvu zetu kujenga bara la kijani, safi, na lenye uhimilivu kufikia mwaka 2063.

66. Kutahadharisha kwamba Azimio la Gaborone kuhusu Mkutano wa Kwanza wa Bioanuwai wa Afrika litumike kama jiwe la msingi la mpango wa pamoja ya Afrika ya kurejesha uwiano kati ya binadamu na mazingira, kutumia bioanuwai kwa ustawi wa pamoja, na kuhimiza haki ya Afrika ya kuamua hatima yake ya mazingira, huku ahadi zake zikitumika kama msingi wa mpango wa Afrika wa kutumia bioanuwai kwa ustawi wa bara.

***(Limeipitishwa Gaborone, Botswana, tarehe 5 Novemba 2025 na Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika)***.

## TAMKO LA MKUTANO WA LUANDA WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI KUHUSU UFADHILI KWA AJILI YA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU YA AFRIKA

**SISI** Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tulikutana tarehe 15 Februari, 2026 katika Mkutano wetu wa 39 wa Kawaida mjini Addis Ababa, Ethiopia;

**TUNAPITISHA** Tamko lililoambatanishwa la MKUTANO WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI KUHUSU UFADHILI WA LUANDA KWA AJILI YA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU YA AFRIKA uliofanyika tarehe 30 Oktoba 2025 mjini Luanda, Jamhuri ya Angola

# TAMKO LA LUANDA KUHUSU UFADHILI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU YA AFRIKA

**SISI,** Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, mbele ya Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, Wakuu na Wawakilishi wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD), Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs), Taasisi za Fedha, sekta binafsi, na washirika,, tulikutana katika Mkutano wa 3 wa Ufadhili wa Maendeleo ya Miundombinu ya Afrika, Mkutano wa Luanda wa Ufadhili wa Miundombinu (LFS) unaofanyika Luanda, Jamhuri ya Angola, chini ya kaulimbiu "MTAJI, KORIDO, BIASHARA: Kuwekeza katika miundombinu kwa AfCFTA na ustawi wa pamoja";

**HIVYO**;

1. **TUNAMPONGEZA** Mheshimiwa João Manuel Gonçalves Lourenço, Rais wa Jamhuri ya Angola na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, kwa uongozi wake usioyumba na kujitolea kwake kwa maendeleo ya miundombinu barani Afrika, na **TUNATOA** shukrani zetu za dhati kwa Serikali na watu wa Angola kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano huu kwa ukarimu;

2. **TUNAWASHUKURU** wajumbe wa Taasisi za Programu ya Maendeleo ya Miundombinu barani Afrika (PIDA), zinazojumuisha AUC, AUDA-NEPAD, RECs, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), na Tume ya Uchumi ya Afrika (UNECA), kwa juhudi zao za pamoja katika kuongoza utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya kikanda na kuendeleza PIDA, Soko Moja la Umeme Afrika (AfSEM), Mpango Mkuu wa Mifumo ya Umeme wa Bara (CMP), Soko la Usafiri wa Anga Moja la Afrika (SAATM), Mkakati wa Mabadiliko ya Kidijitali (DTS) na Mtandao Jumuishi wa Reli Afrika (AIRN), miongoni mwa mengine.

3. **TUNATAMBUA** uongozi na msaada wa AfDB, Kundi la Benki ya Dunia (WBG), na Muungano wa Taasisi za Fedha za Afrika (AAMFI), unaojumuisha Shirika la Fedha la Afrika (AFC), Benki ya Uagizaji na Usafirishaji Nje ya Afrika (Afreximbank), Kundi la Benki ya Biashara na Maendeleo (TDB Group), Shirika la Bima ya Afrika (Africa Re), Bima ya Maendeleo ya Biashara na Uwekezaji ya Afrika (ATIDI), Benki ya Maendeleo Endelevu (SHAFDB), na ZEP-RE (PTA Reinsurance Co.), pamoja na Chama cha Hifadhi ya Jamii Afrika (ASSA), na washirika wengine wote wa kimataifa, wa pande mbili, wa kitaalamu, na wa kifedha kwa kujitolea kwao kwa ajenda hii ya mageuzi ya miundombinu;

4. **KWA KUONGOZWA** na maono ya Ajenda 2063 na **KWA KUTAMBUA** kwamba miundombinu thabiti na ya kiwango cha dunia ndiyo uti wa mgongo wa mchakato wa ujumuishaji na ukuaji wa viwanda wa Afrika, Mpango wa Utekelezaji wa Kipaumbele cha PIDA 2 (PIDA-PAP 2) unatumika kama mpango wa bara la Afrika wa kuendeleza mageuzi haya

5. **TUNAPONGEZA** kasi kubwa iliyopigwa tangu Mkutano wa Pili wa Ufadhili wa Dakar (2023) na Mkutano wa Nishati wa Afrika wa Dar Es Salaam (2025), na **TUNAREJELEA** ahadi za kisiasa na ahadi zilizotolewa katika Mikutano hii husika kuelekea kuendeleza miundombinu ya bara, mpito wa nishati, na ajenda ya maendeleo endelevu;

6. **TUNAELEZEA MASIKITIKO** yetu kwamba licha ya maendeleo yanayoonekana, mapengo makubwa ya ufadhili na miundombinu yanaendelea kote barani, ikisisitiza hitaji la haraka la kuharakisha juhudi katika kuhamasisha ufadhili na kuongeza utekelezaji wa miundombinu endelevu, jumuishi, na thabiti barani Afrika;

7. **TUNASIKITISHWA ZAIDI** kuhusu vikwazo vya kimuundo vya utekelezaji wa miradi, haswa, kushindwa kwa soko katika kufadhili maandalizi ya mradi kwa hatua za awali, ambapo husababisha uhaba sugu wa ufadhili wa miradi, na kuzuia uwekezaji;

8. **TUNAZINGATIA** kazi muhimu inayofanywa na AUC na AUDA-NEPAD katika kuendeleza Programu ya Kuharakisha Maendeleo ya Viwanda Afrika (PAIDA), inayolenga kuboresha matumizi yenye tija ya uwekezaji wa miundombinu na nishati ili kuharakisha utekelezaji wa AfCFTA.

**SISI, WAKUU WA NCHI NA SERIKALI ZA UMOJA WA AFRIKA, TULIOPO NA TULIOWAKILISHWA, HAPA;**

9. **TUNADHAMIRIA** kufanya mageuzi muhimu ya sera, udhibiti, na taasisi yanayohitajika ili kutekeleza **Ajenda ya 5%,** kwa ajili ya **uhamasishaji wa kimkakati wa rasilimali za ndani za Afrika, ikiwa ni pamoja na mali za hifadhi ya jamii, utajiri wa uhuru, na mifuko ya bima**, ili kupata ufadhili wa muda mrefu na endelevu kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu barani, kulingana na Uamuzi Assembly/AU/DEC.665-689(XXX) wa 28/29 Januari 2018 wakati wa Mkutano Mkuu wa 30 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali;

10. **TUNADHAMIRIA ZAIDI** katika kuendeleza mabadiliko ya kimuundo ya usanifu wa ufadhili wa Afrika ili kushughulikia pengo linaloendelea katika ufadhili wa miradi ya mapema na yenye hatari kubwa, kwa lengo la kuanzisha mradi ya miundombinu inayoweza kufadhiliwa katika bara zima;

11. **KUIDHINISHA** miradi 38 inayoweza kufadhiliwa katika LFS hii **NA KUPONGEZA** ahadi ya taasisi za fedha na washirika wa maendeleo ya kuunga mkono miradi 13 ya PIDA PAP2, inayowakilisha uhamasishaji wa uwekezaji wa pamoja wa dola bilioni 18, kama matokeo ya moja kwa moja ya Mkutano huu.

12. **KUZIHIMIZA** benki za maendeleo za kimataifa (MDBs), taasisi za fedha za maendeleo (DFIs), na washirika wa kimataifa kurahisisha masharti ya ufadhili, ikiwa ni pamoja na kuchunguza mifumo ya urekebishaji wa deni na kuelekeza upya Haki Maalum za Kutoa Pesa (SDRs), ili kujenga uwezo mkubwa wa kifedha kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu.

13. **TUNADHIMARIA** kufufua Mpango wa Marais Vinara wa Miundombinu (PICI), kushughulikia vikwazo vya mipakani, kuharakisha makubaliano ya kikanda, na kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya kimataifa unafanyika kwa wakati.

14. **TUNASISITIZA MSAADA** kwa Mkakati wa Kanda wa Uchumi Jumuishi kama mkakati mkuu wa kuendeleza viwanda na maendeleo ya mnyororo wa thamani wa kikanda chini ya PAIDA na AfCFTA, na **TUNASISITIZA** hitaji la kuweka kipaumbele kwa majukwaa kamili ambayo yanaunganisha vifaa bora, mifumo ya nishati inayoaminika, na muunganisho wa kasi wa kidijitali na Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZs) na maeneo ya viwanda;

15. **TUNADHAMIRIA** kuharakisha utendaji kazi wa mipango mikuu jumuishi ya kisekta na:

(a) **KUTEKELEZA** AfSEM na CMP kama hati za kuimarisha usalama wa nishati na kupanua ufikiaji wa nishati kwa wote; na zaidi kuahidi kuongeza msaada kwa mpango wa Mission 300 na Mpango wa Nishati Mbadala wa Afrika (AREI) ili kuendesha mpito wa nishati wa haki.

(b) **KWA KUONGOZWA NA** Mkakati wa Mabadiliko ya Kidijitali kwa Afrika (DTS), tunajitolea kuziba pengo la miundombinu ya kidijitali na ujuzi unaohakikisha upatikanaji wa intaneti kwa wote na salama, kuharakisha uanzishwaji wa vituo vya kubadilishana intaneti na vituo vya data.

16. **TUNADHAMIRIA** kuendeleza matumizi ya busara ya Akili Mnemba katika miundombinu na usafiri kwa kukuza ubunifi na uwekezaji, kukuza ushirikiano wa umma na binafsi, kuhakikisha utawala shirikishi na unaojumuisha wote, kuimarisha usalama na uendelevu, na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kujenga uwezo kulingana na kanuni za kimataifa.

17. **TUNASISITIZA** ahadi yetu ya kupanua na kuboresha miundombinu na huduma za usafiri, huku tukiendeleza mpito wa haki hadi uhamaji endelevu, usiotumia kaboni nyingi na hasa kujitolea kuharakisha kukamilika kwa Barabara Kuu kati ya nchi za Afrika, maendeleo ya AIRN, uhamasishaji wa Ufadhili wa Maendeleo ya Mpango Mkuu wa Miundombinu ya Usafiri wa Anga wa Bara ikiwa ni pamoja na usanifu wa anga usio na kikwazo chini ya SAATM, na kuimarisha usafiri endelevu wa mijini, maendeleo ya baharini, utawala wa usafiri wa barabarani, na usalama barabarani, kote barani.

18. **TUNADHAMIRIA** kuingiza teknolojia na ubunifu katika mzunguko mzima wa maisha wa miundombinu na **KUWEKA KIPAUMBELE** kwenye usawa wa kijinsia na ushirikishwaji wa kijamii katika mnyororo wa thamani wa miundombinu, kuhakikisha kwamba uwekezaji unachochea upatikanaji wa fursa katika ajira na ujasiriamali kwa raia wote.

**HIVYO**:

I. **TUNAIOMBA** AUC, kwa kushirikiana na AUDA-NEPAD, AfDB, AAMFI na Taasisi zingine za Ufadhili, na RECs, kutengeneza mwongozo wa utekelezaji wa ahadi zilizotolewa katika LFS zitakazowasilishwa kwa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika.

II. **TUNAIOMBA** AUC na AUDA-NEPAD, kwa kushirikiana na AfDB, AAMFI, na RECs, kuharakisha maendeleo ya Mtandao wa Barabara Kuu katika ya nchi za Afrika kupitia Programu za Uwekezaji wa Kikanda za Muda wa Kati hadi wa Muda Mrefu na kuharakisha utekelezaji wa Mpango Mkuu wa AIRN kwa kuzingatia viwango vya ushirikiano na muundo wa miradi ya kipaumbele ya kanda kwa ajili ya ufadhili.

III. **TUNATOA WITO** kwa AUC na AUDA-NEPAD kuharakisha uundaji wa PAIDA, kuhakikisha ulinganifu na AfCFTA, Mpango wa Rais Kinara wa Miundombinu (PICI) na mifumo ya PIDA, kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa na Vyombo vya Sera katika Mkutano Mkuu ujao wa Kawaida wa AU.

IV. **TUNATOA WITO** kwa Taasisi za AUDA-NEPAD na PIDA kuchukua hatua zinazohitajika ili kuimarisha taasisi za maandalizi ya miundombinu zilizopo, ikiwa ni pamoja na SDM na NEPAD-IPPF, na **KUKARIBISHA** ushirikiano wenye tija na uamuzi kati ya AUDA-NEPAD na AAMFI, na maendeleo yaliyopatikana katika kuchagua miradi 13 inayoweza kufadhiliwa na PIDA PAP2 kwa ajili ya uwekezaji.

V. **TUNATOA WITO ZAIDI** wa kuanzishwa mara moja kwa Kituo cha Ufadhili wa Mradi wa AAMFI (Miundombinu) kama utaratibu muhimu wa bara, ambao unaiweka Afrika katika uhuru mkubwa wa kifedha na mabadiliko ya muda mrefu, na **KUIELEKEZA** AUDA-NEPAD na AAMFI ili kuharakisha kuanzishwa kwake.

VI. **TUNAIOMBA** AUC na AUDA-NEPAD kuanzisha utaratibu wa ufuatiliaji na utoaji taarifa ili kufuatilia utekelezaji wa Tamko hili, na ahadi zilizotolewa hapa, na kuripoti kwa Mkutano Mkuu wa AU.

VII. **TUNAWAHIMIZA** washirika wetu wa pande nyingi, pande mbili, na sekta binafsi kuoanisha msaada wao wa kifedha na kitaalamu na vipaumbele vilivyoainishwa katika Mkutano huu.

VIII. **TUNAIOMBA** AUC iwezeshe uwasilishaji wa Tamko hili la Luanda kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa.

**LILIPITISHWA** na Wakuu wa Nchi na Serikali katika Mkutano wa 3 wa Ufadhili wa Maendeleo ya Miundombinu ya Afrika mjini Luanda, Jamhuri ya Angola**, tarehe 30 Oktoba 2025**.

**Limeandaliwa tarehe 30 Oktoba 2025, Luanda, Jamhuri ya Angola**

## TAMKO KUHUSU
## MIPANGO MUHIMU YA BARA YA BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA (AfDB)

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAPOKEA KWA SHUKRANI** Ripoti ya Mhe. Dkt. Sidi Ould Tah, Rais wa Kundi la Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB);

2. **UNAMPONGEZA Mhe.** Dkt. Sidi Ould Tah kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, kielelezo cha imani iliyoonyeshwa na wanahisa wa AfDB katika uwezo wake wa kuiongoza taasisi hiyo katika kuendeleza ajenda ya mageuzi na utangamano ya Afrika;

3. **UNAREJELEA** uamuzi Assembly/AU/Dec. 817(XXXV) uliopitishwa wakati wa Mkutano wa 35 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu AfDB kuhamasisha ufadhili kwa ajili kuharakisha ufufuaji wa uchumi wa Afrika, maendeleo na ujumuishaji wa Afrika;

4. **UNAKARIBISHA** urejeshaji wa kihistoria wa Mfuko wa Maendeleo ya Afrika (ADF-17) kwa takriban dola bilioni 11, na **UNAPONGEZA** ahadi zilizoongezeka za Afrika kwa dola takriban milioni 283, ongezeko la mara nane zaidi ya mizunguko ya awali ya urejeshaji na ishara ya wazi kwamba Afrika inazidi kuwa tayari kufadhili vipaumbele vyake vya maendeleo;

5. **UNAKARIBISHA ZAIDI** mwelekeo wa kimkakati wa Rais wa AfDB unaozingatia Vipaumbele Vinne vya Kimkakati (*Cardinal Points*) ikiwa ni pamoja na lengo jipya la Benki kuhusu: (i) upatikanaji ulioboreshwa wa mtaji na utafutaji wa rasilimali za fedha za Afrika; (ii) kurekebisha na kuimarisha mifumo na taasisi za fedha; (iii) kutumia mabadiliko ya idadi ya watu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi; na (iv) kujenga miundombinu inayostahimili mabadiliko ya tabianchi na ongezeko kubwa la thamani;

6. **PIA UNAZINGATIA** Muundo Mpya wa Kifedha wa Afrika (NAFA), unaozingatia Vipaumbele Vinne vya Kimkakati vya AfDB, kama mpango mkubwa wa kuimarisha uhuru wa kifedha wa Afrika na kupunguza udhaifu wa mishtuko ya fedha ya nje, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha na kuzidisha mtaji wa Afrika, kuweka dhamana kimkakati, na kutumia vyaraka zinazolengwa kimkakati ili kutumia rasilimali za masharti nafuu na kuingiza uwekezaji katika sekta binafsi kwa kiwango kikubwa;

7. **UNATAMBUA** azma ya AfDB, kupitia NAFA, ya kuimarisha na kurasimisha ushirikiano wa kimkakati na Umoja wa Afrika, taasisi za fedha za maendeleo ya bara na kikanda za Afrika, benki za kikanda, mifuko ya pensheni, na wawekezaji wengine wa Afrika na kimataifa, ikiwa ni pamoja na kukusanya rasilimali

zinazohitajika ili kuendeleza na kupanua vituo vya viwanda vya Afrika na minyororo ya thamani;

8. **UNAMUOMBA** Rais wa Kundi la AfDB kuwasilisha taarifa mpya kuhusu maendeleo yaliyopatikana kuelekea utekelezaji wa azimio hili, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa NAFA na ushirikiano na mipango inayohusiana, kwa Mkutano ujao wa Uratibu wa Nusu Mwaka (MYCM) wa Umoja wa Afrika mwaka 2026.

# MATAMKO MATATU (3) YA KUAMBATANISHWA KWENYE YA UAMUZI Assembly/AU/Dec.942(XXXIX)

# TAMKO LA ALGIERS

## KUHUSU UHALIFU WA UKOLONI BARANI AFRIKA:
## *"KUELEKEA KUREKEBISHA DHULUMA ZA KIHISTORIA KUPITIA KUTANGAZA UKOLONI KAMA UHALIFUI"*
## (ALGIERS, NOVEMBA 30 - DESEMBA 1, 2025)

Sisi, Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika (AU), Wakuu wa Ujumbe, Wawakilishi wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika ikiwamo Bunge la Afrika , Mwakilishi wa eneo la CARICOM, wanataluma, wataalamu, wanasheria na wanahistoria, tumekutana mjini Algiers tarehe 30 Novemba na 1 Desemba 2025, katika mpango wa Mkutano wa Kimataifa kuhusu Uhalifu wa Ukoloni Barani Afrika (humu umerejelewa kama "Mkutano wa Algiers"), kwa mwaliko wa Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, kwa ushirikiano na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, na kwa mujibu wa uamuzi Assembly/AU/Dec.903(XXXVIII) wa Februari 2025;

Tukisisitiza kwamba Mkutano wa Algiers unawakilisha hatua muhimu ya kisiasa katika jitihada za Afrika za kutafuta haki, utambuzi wa kihistoria, fidia, na uhuru wa kumbukumbu katika kukabiliana na uhalifu mtambuka wa ukoloni, ukiendana kikamilifu na kaulimbiu ya Umoja wa Afrika ya mwaka 2025 inayolenga upatikanaji wa haki na fidia kwa Waafrika na watu wa asili ya Afrika, na kuthibitisha kuwa kaulimbiu hiyo inapaswa kuongezewa muda wa utekelezaji kwa mpango wa miaka kumi unaojumuisha kipindi cha 2026–2035;

Tukirejelea maamuzi yote ya Umoja wa Afrika, ukiwamo uamuzi wa Baraza la Wakuu wa Nchi na Serikali Assembly/AU/Dec.884(XXXVII) wa Februari 2025, uliotangaza kaulimbiu ya mwaka 2025 kuwa *"Haki kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Kiafrika Kupitia Fidia"*; Uamuzi wa Baraza la Wakuu wa Nchi na Serikali Assembly/AU/Dec.934(XXXVIII) wa Februari 2025, kuhusu uainishaji wa utumwa, uhamisho wa kulazimishwa, na ukoloni kuwa uhalifu dhidi ya ubinadamu na mauaji ya kimbari dhidi ya watu wa Afrika; pamoja na Azimio la Addis Ababa kuhusu Ushirikiano wa Mabara kwa ajili ya Haki ya Fidia (tarehe 7 Septemba 2025) lililopitishwa na Mkutano wa Pili wa Afrika–Karibi tarehe 7 Septemba 2025; Azimio la Abuja la 1993**;** Azimio la Durban na Mpango wa Utekelezaji (2001)**;** na Tamko la Accra la Novemba 2023 kuhusu kuanzishwa kwa jukwaa la pamoja kwa ajili ya haki na fidia kwa Waafrika;

Tukirejelea na kuheshimu kujitolea kwa watu wote wa Afrika waliopigana kwa mshikamano ili kurejesha uhuru na mamlaka ya nchi za Afrika, na kurejesha ukweli na haki;

Kwa kuzingatia kwamba hakuna fidia inayoweza kuponya kikamilifu mateso yaliyosababishwa, wala kurejesha mwelekeo wa maisha ya kibinadamu, kisiasa,

kiuchumi na kiutamaduni uliokatizwa; lakini kwamba mchakato huu unatokana na wajibu wa haki, kumbukumbu na utu, usiotenganishwa na uthibitisho wa mamlaka ya watu wa bara hil;

Tukisisitiza dhamira yetu ya pamoja kwa misingi ya umoja wa Afrika, haki, usawa, uhuru na kujitawala, ambayo ilitokana moja kwa moja na mapambano dhidi ya utawala wa kikoloni na kurejeshwa kwa mamlaka ya rasilimali za kiuchumi, kiutamaduni na maliasili za Afrika; pamoja na utu kwa Waafrika na watu wenye asili ya Kiafrika; na katika kuendeleza haki za binadamu, amani na heshima kwa uhai, mamlaka, ukamilifu wa kimamlaka na uhuru wa Nchi Wanachama, pamoja na umoja, uhusiano, mshikamano wa ndani na ushirikiano miongoni mwa nchi na watu wa Afrika kwa mujibu wa Sheria ya Msingi ya Umoja wa Afrika na Mkataba wa Umoja wa Mataifa; na tukisisitiza kwamba misingi hii inaendelea kuongoza juhudi za bara hili katika kulinda mamlaka yake dhidi ya aina zote za kuingiliwa, uingiliaji na shinikizo la nje;

Tukitambua mapambano ya kishujaa ya watu wa Afrika, harakati za ukombozi, wanataaluma, wanawake na vijana, pamoja na diaspora wa Afrika duniani, ambao walibadilisha mateso ya pamoja kuwa mshikamano na upinzani, na ambao kujitolea kwao kunabaki kuwa msingi wa harakati za kupata uhuru, utu, na haki kwenye bara hili;

Tukitambua nafasi ya kihistoria na yenye kuamua nafasi ya wanawake wa Afrika katika mapambano ya ukombozi wa bara hili, ambao dhamira, ujasiri na kujitolea kwao kulichangia kwa kiasi kikubwa kuibuka kwa harakati za kitaifa na kupata uhuru;

Tukitambua hoja kwamba maeneo kadhaa duniani bado yako chini ya utawala wa kikoloni, kinyume na msingi ya sheria za kimataifa, na tukithibitisha mshikamano wetu usiobadilika na watu wanaoendelea kupigania uhuru wao na kujitawala, ikiwamo watu wa Palestina wanaoteseka kila siku kutokana na maovu ya ukoloni;

Tukitambua kwamba kurekebisha ukosefu wa haki wa kihistoria ni muhimu ili kufanikisha malengo ya Ajenda ya mwaka 2063, "Afrika Tunayotaka," ikiwamo maendeleo ya pamoja, ustawi wa kijamii unaojumuisha wote, na bara lililo na amani na umoja;

Hivyo basi, tunapitisha **"Tamko la Algiers"** kama tamko la pamoja la Afrika katika kurejesha ukweli wa kihistoria, kuendeleza haki, na kuendeleza hoja ya fidia:

**<u>Kuhusu kumbukumbu, historia ya pamoja, ukweli, na wajibu wa kimaadili:</u>**

Tunatambua, kwa huzuni kubwa, kwamba watu wote wa Afrika waliteseka, chini ya utawala wa kikoloni, kutokana na uvunjaji wa haki zao msingi, kuharibiwa kwa tamaduni zao, lugha, utambulisho, na wizi wa urithi wao wa kushikika na usioshikika;

Uzoefu huu wa pamoja unaunda urithi unaounganisha Wafrika katika jitihada zao za pamoja za kufikia ukweli, haki, fidia, na kuondolewa kabisa kwa mabaki yote ya udhalimu wa kikoloni wa zamani;

Tunasisitiza kwamba watu wote wa Afrika wanabaki wakiwekeza kwa dhati katika kuhifadhi kumbukumbu zao za kitaifa, kuheshimu mashahidi wao na matendo ya kujitolea yaliyofanywa kufanikisha uhuru wao, jambo ambalo ni haki ya kimsingi na kamili, ya kujenga na kuwasilisha simulizi zao za kihistoria, kulingana na uzoefu wao wa maisha, heshima yao, na matarajio yao;

Tunatoa wito kwa makoloni ya zamani kutekeleza kikamilifu majukumu yao ya kihistoria kupitia kutambua kwa uwazi na kwa umma ukatili uliofanywa;

Tunakubaliana kuimarisha jitihada katika utafiti, kumbukumbu, na urithishaji wa kizazi hadi kizazi ili kuhakikisha uhalisi wa kumbukumbu za pamoja;

Tunapendekeza kuundwa kwa kumbukumbu za kidijitali za Afrika, mapitio ya mtaala wa elimu, na uanzishaji wa kumbukumbu, makumbusho, na siku za kumbukizi;

Tunakubaliana kufanya kazi kuelekea urejeshaji wa mali za kitamaduni, kumbukumbu, na mabaki ya binadamu yanayoshikiliwa kinyume cha sheria na nchi za kikoloni;

## <u>Kuhusu Aina za Makosa ya Kikoloni</u>

Tunasisitiza kwamba ukoloni, utumwa, kuhamishwa kwa nguvu, na ubaguzi wa rangi vinaunda uhalifu dhidi ya binadamu na aina za mauaji ya kimbari, ambavyo vimeleta madhara ya mfumo kwa watu wa Afrika. Matendo haya yanawakilisha ukiukaji mkubwa zaidi unaotambulika chini ya sheria za kimataifa na sheria za kibinadamu za kimataifa na hayazuiliki kwa muda;

Tumejizatiti kukuza utambuzi wa kimataifa wa makosa ya kikoloni na kufanya kazi kuelekea ufafanuzi wake kama uhalifu wazi ndani ya vyombo na mifumo ya sheria za kimataifa;

Tunaomba mahakama za Kiafrika, za kikanda, na za kimataifa, pamoja na vyombo husika vya sheria za kimataifa, ikiwa ni pamoja na Umoja wa Mataifa (UN), Baraza la Haki za Binadamu, Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ), Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC), na vyombo vya kikanda vya Kiafrika kama Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, kufanya uchambuzi wa kina wa kisheria wa ukatili wa mfumo unaohusiana na ukoloni, kwa lengo la kuanzisha uhusiano wake wa moja kwa moja na makundi yanayotambulika ya uhalifu dhidi ya binadamu na vipengele vinavyounda uhalifu wa mauaji ya kimbari;

Tunaunga mkono uanzishaji na kuimarishwa kwa mifumo ya kisheria katika ngazi ya kitaifa, kikanda, kibara, na kimataifa inayolenga kuanzisha uhalifu wa ukoloni ndani ya sheria za kimataifa kupitia uhifadhi wa kumbukumbu, upatikanaji wake, na urejeshaji kamili, na kuhakikisha uwajibikaji wa kisheria kwa makosa ya kikoloni pamoja na matokeo yake ya kudumu;

Tunawaomba taasisi za kielimu za Nchi Wanachama wa AU kuendeleza sheria za mfano, kuandaa mkataba, na uchambuzi wa kifasihi unaounga mkono utambuzi, uhalifu, na kuendesha kesi za makosa ya kikoloni;

Tunakaribisha uanzishaji wa mifumo mipya ya AU kuhusu fidia, Kamati ya Wataalam wa AU kuhusu Fidia (AUCER) na Kikundi cha Marejeo cha Wataalam wa Sheria wa AU kuhusu Fidia (AULER), na tunapendekeza kuimarishwa kwake;

Tunaunga mkono uundaji wa Kamati ya Afrika ya Kumbukumbu na Ukweli wa Kihistoria, ambayo itakuwa na jukumu la kuratibu mbinu za kihistoria, kusimamia ukusanyaji wa kumbukumbu, kuratibu vituo vya utafiti vya Kiafrika, na kutoa uchambuzi na mapendekezo kwa bara;

**Kuhusu Athari kwa Binadamu na Haki kwa vizazi**

Tunalaani aina zote za ukoloni, ambazo ziliunda mfumo wa kiutawala, unyonyaji, na kufutwa kwa utambulisho, uliojikita katika ukoloni wa kijeshi, ukatili wa kimbari, kuhamishwa kwa nguvu, kupoteza ardhi, wizi wa rasilimali, majaribio ya nyuklia na mazingira, na kufutwa kwa urithi wa kiutamaduni, lugha, utambulisho, na kiimani, pamoja na utengenezaji wa simulizi bandia ulioanzishwa kwa lengo la kupinga ukweli, heshima, na upinzani wa watu wa Kiafrika;

Tunadai kutambuliwa kwa athari hizi kubwa za kibinadamu, ambazo zimeleta madhara ya kudumu ya kisaikolojia kwa jamii na watu wa Kiafrika na ambazo zinaendelea kuonekana hadi leo kupitia aina mpya za ubaguzi, ubaguzi wa rangi wa mfumo, na maneno ya chuki;

Tunapendekeza upanuzi wa juhudi za kitaifa na bara za kumbukumbu, ikiwa ni pamoja na makumbusho, masanamu, maeneo ya kumbukumbu, siku za kumbukizi, na mageuzi ya kielimu;

**Kuhusu Athari kwa Mazingira**

Tunakumbuka kwamba ukoloni ulisababisha uharibifu mkubwa wa mazingira, unaohusiana na unyonyaji wa maliasili kwa wingi, jambo lililosababisha madhara ya muda mrefu ya kiikolojia na kiafya;

Tunakemea majaribio ya nyuklia yaliyofanywa kwenye bara la Afrika, ambayo yalisababisha uharibifu mkubwa wa kiafya, kimazingira, kijamii na kiuchumi unaoendelea kuathiri watu wa Afrika;

Tunasisitiza haja ya kuanzishwa kwa tathmini ya kibara kuhusu athari za kiikolojia na mageuzi ya tabianchi yanayohusiana na ukoloni, pamoja na mahitaji ya urejeshwaji wa maeneo yaliyoathirika na majaribio ya nyuklia, kemikali, na viwanda;

Tunaunga mkono uanzishaji wa Jukwaa la Afrika la Haki za Mazingira, lenye jukumu la kubaini maeneo yaliyoathirika, kutathmini uharibifu, kusaidia Nchi husika, na kutoa mapendekezo ya bara kwa ajili ya urejeshwaji na fidia;

Tunayahimiza mataifa yaliyo na wajibu kihistoria kwa uharibifu wa mazingira uliosababisha mageuzi ya tabianchi, hususan mamlaka za kikoloni, kutekeleza wajibu wao wa kimaadili na kisiasa, tukiwataka kutoa msaada wa kifedha, kiteknolojia, na kitaasisi kwa jitihada za bara la Afrika za kuzoea na kupunguza madhara;

Tunapendekeza kuongezwa kwa ushirikiano wa washirika wa kimataifa kusaidia juhudi za Afrika, kwa usawa, fidia, na haki ya maendeleo endelevu;

**Kuhusu Elimu, Uzalishaji wa Maarifa, Lugha za Kiafrika, na Uhifadhi wa Kumbukumbu**:

Tunasisitiza haja ya dharura ya kufanya mageuzi katika mifumo ya elimu barani Afrika ili kuunganisha kikamilifu historia ya kabla ya ukoloni, kipindi cha ukoloni, na baada ya ukoloni, na kuwezesha kizazi cha vijana kuwa na ufahamu wa kihistoria ulio sahihi na wa kina;

Tunasisitiza haja ya haraka ya kuboresha mitaala ya elimu ili iakisi ukweli wa kihistoria, itambue na kuheshimu harakati za upinzani wa Waafrika, na kukuza utambuzi na mshikamano wa Uafrika;

Tunaunga mkono uandaliwaji wa Mpango wa Afrika wa Urithishaji wa Kumbukumbu ya Kihistoria, kukuza lugha za Kiafrika, kuendeleza kazi za kiutamaduni na kisanaa zinazozingatia kumbukumbu na historia ya Afrika, pamoja na kuandaa maudhui ya elimu na vyombo vya habari yanayoelezea upinzani wa Waafrika;

Tunazihimiza vyuo vikuu na taasisi za kitaaluma barani Afrika kuanzisha programu za mafunzo na shahada ikiwa ni pamoja na Astashahada ya Juu ya Taifa (HND), Shahada ya Kwanza na Shahada ya Uzamili ambazo mitaala yake inajengwa juu ya kumbukumbu ya kihistoria, ukweli, haki, na haki ya fidia;

Tunatoa wito wa kuanzishwa na kutekelezwa kwa jukwaa la bara zima kwa ajili ya watafiti na wanafunzi wa Afrika wanaojihusisha na historia ya ukoloni, litakalotoa fursa ya kupata vitabu, vyanzo vya kumbukumbu za kihistoria, nyaraka, na ufadhili wa masomo;

Tunaunga mkono kampeni za uhamasishaji wa umma na mitaala ya kitaifa ya shule inayobainisha kwa uwazi uhalisia wa uhalifu wa kikoloni na athari zake zinazoendelea hadi leo;

**Kuhusu Fidia za Kiutamaduni na Urejeshwaji wa Urithi wa Afrika:**

Tunakumbuka kuwa utawala wa kikoloni uliambatana na uporaji wa kimfumo na uharibifu wa urithi wa kiutamaduni, kiakili na kiimani wa Afrika;

Tunasisitiza haki ya watu wa Afrika ya kurejeshewa bila masharti rasilimali zao za kiutamaduni, ikiwamo mabaki ya sanaa, miswada, nyaraka, vitu vitakatifu na mabaki ya mababu yaliyochukuliwa wakati wa utawala wa kikoloni;

Tunadai kurejeshwa kwa mali zote za kiutamaduni za Afrika kwa mujibu wa Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu urejeshwaji wa rasilimali za urithi, pamoja na Sheria ya Mfano ya Umoja wa Afrika kuhusu Ulinzi wa Mali na Urithi wa Kiutamaduni;

Tunatoa wito kwa mamlaka za kikoloni kushirikiana kikamilifu na bila masharti katika urejeshwaji wa rasilimali hizo kwa nchi zake za asili;

Tunaihimiza Kamisheni ya Umoja wa Afrika na washirika wa kimataifa kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ya urejeshwaji, na kuunga mkono mifumo endelevu ya kurejesha urithi wa Afrika;

Tunatoa wito kwa Umoja wa Afrika kuharakisha uanzishwaji wa Makumbusho Makuu ya Afrika kama taasisi ya bara zima iliyopewa dhamana ya kuhifadhi urithi wa Afrika na kuandika historia ya athari na urithi wa ukoloni;

**Kuhusu Masuala ya Kijamii na Kiuchumi**:

Tunatambua kuwa utawala wa kikoloni ulisababisha upotoshaji wa muda mrefu wa mifumo ya kiuchumi kupitia unyonyaji wa nguvu kazi ya Waafrika, ardhi na rasilimali zao, hali iliyozaa maendeleo duni ya kimfumo na ukosefu mkubwa wa usawa wa kimuundo ambao unaendelea hadi leo;

Tunabainisha kuwa athari za kiuchumi za ukoloni zinaendelea kujitokeza katika sura nyingine, hususan kupitia baadhi ya sera za ukoloni mamboleo kama vile udhibiti wa rasilimali muhimu na mifumo ya kifedha, mikataba isiyo ya haki ya kibiashara, utegemezi wa kiteknolojia, mzigo wa madeni, misaada ya maendeleo yenye masharti, pamoja na kuingiliwa kwa sera za kiuchumi kunakopunguza mamlaka na uhuru wa nchi za Afrika;

Tunasisitiza umuhimu wa kufanya tathmini ya bara zima kuhusu athari za kiuchumi za ukoloni kwa lengo la kuandaa mkakati wa fidia unaozingatia haki, ikiwamo, miongoni mwa mambo mengine, fidia ya mali zilizoporwa, kufutiwa madeni, na ufadhili wa maendeleo wenye usawa;

Tunasisitiza haja ya kufanya mageuzi katika utawala wa uchumi wa dunia ili kuvunja urithi wa kikoloni uliokita mizizi ndani ya taasisi za kifedha za kimataifa na mifumo ya biashara ya kimataifa;

Tunaunga mkono utekelezaji wa mikakati ya pamoja ya kisheria, kidiplomasia na kiuchumi ili kuendeleza ajenda ya fidia na kukuza uhuru wa kiuchumi na ujenzi wa viwanda barani Afrika.

**<u>Kuhusu Utetezi wa Kimataifa na Ushirikiano kati ya Afrika na CARICOM</u>**

Tunasisitiza kuwa Waafrika wanaoishi ughaibuni (diaspora) pia wamekuwa waathirika wa uhalifu wa kikoloni na wanaendelea kukabiliwa na ubaguzi unaotokana na mifumo ya kibaguzi ya kikoloni;

Tunasisitiza mshikamano wetu na nchi za CARICOM katika juhudi zao za kudai fidia, na tunatoa wito wa utekelezaji kamili wa Azimio la Addis Ababa kuhusu Ushirikiano wa Mabara katika Kurejesha Haki (tarehe 7 Septemba 2025).

Tunahimiza Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, nchi za Karibe, na diaspora kuendesha kwa pamoja na kwa uratibu mikakati ya utetezi na kisheria ili kufanikisha haki ya marejesho;

Tunalaani vikali utukuzaji au uhalalishaji wa watu waliohusika na uhalifu wa kikoloni, utumwa, na vurugu za kibaguzi;

Tunalaani bila shaka aina zote za ukoloni mamboleo, ikiwamo kuingiliwa kwa masuala ya kisiasa, unyonyaji wa kiuchumi, na kihramu kwa majeshi ya kigeni kusikofuata sheria au mamluki katika ardhi ya Afrika;

**<u>Kuhusu Fidia za Kimuundo katika Utawala wa Dunia</u>:**

Tunalaani miundo ya utawala wa dunia ambayo inaendelea kuakisi ukosefu wa usawa wa nguvu uliorithiwa kutoka kipindi cha ukoloni, na tunatoa wito wa kurekebisha ukosefu huu wa usawa wa kimuundo ili kufanikisha urejeshaji wa haki;

**Masharti ya Mengine**:

Tunapendekeza kwamba suala la kuchagua tarehe ya Siku ya Kumbukizi ya Waathirika na Mashujaa wa Biashara ya Watumwa, Ukoloni, na Ubaguzi wa rangi lipelekwe kwa Kundi la Mabalozi wa Afrika huko Addis Ababa, ili watoe pendekezo la pamoja. Tarehe itakayokubaliwa itawasilishwa kisha kwa Baraza Kuu kwa ajili ya uthibitisho, na baadaye kwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kwa ajili ya kuidhinishwa rasmi;

Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika kwa msaada wake, uongozi wake katika kubuni, kuratibu, na kuendeleza ajenda ya bara zima kuhusu haki ya fidia, kama ilivyoamuliwa na Mkutano wa AU, na kwa kuanzisha mifumo maalum ya kutekeleza Kaulimbiu ya AU ya Mwaka 2025;

Tunapitisha Azimio la Algiers kuhusu Uhalifu wa Kikoloni Barani Afrika liidhinishwe na Wakuu wa Nchi katika Mkutano wa Kawaida wa 39 wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU Februari 2026, kama hatua ya kwanza ya bara zima kuelekea kurasimisha uhalifu wa kikoloni wa aina zote na kufanikisha haki ya marejesho;

Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Abdelmadjid Tebboune, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, kwa juhudi zake za kuandaa Mkutano wa Algiers kuhusu Uhalifu wa Kikoloni Barani Afrika, na tunaishukuru kwa dhati Serikali na watu wa Algeria kwa ukarimu wake na rasilimali walizowekeza kuhakikisha mafanikio ya tukio hili kuu;

Azimio la Algiers ni hatua muhimu kuelekea kutambua uhalifu wa kikoloni na linatoa njia halisi ya kuipa Afrika nyenzo za kudumu za kumbukumbu, ukweli, haki, na fidia, kwa ajili ya mustakabali wa haki, maendeleo, na heshima kwa vizazi vijavyo.

**Limepitishwa mjini Algiers, Algeria, Tarehe 1 Desemba 2025**

# TAMKO LA KONGAMANO LA TISA LA UMAJUMUI WA AFRIKA LA LOMÉ

**SISI,** wawakilishi wa Mataifa ya Kiafrika yanayoshiriki, nchi zenye jamii za watu wa asili ya Afrika, mashirika na vyama vya Waafrika wanaoishi nje ya nchi zao katika Amerika, Ulaya na Asia, taasisi za kikanda, asasi za kiraia, wanawake na vijana, wanataaluma na mashirika ya kimataifa, tulikusanyika katika jiji la Lomé kuanzia tarehe **8 hadi 12 Desemba, 2025**, kwenye Kongamano la 9 la Umajumui wa Afrika, lililokuwa na mada: **"Kuhuisha Umajumui wa Afrika na Nafasi ya Afrika katika mageuzi ya taasisi za kimataifa: kutafuta rasilimali na kuwa na njia mpya za utekelezaji"**;

**TUNAREJELEA** misingi ya kihistoria na desturi za umajumui wa Afrika, harakati za kudai uhuru, utu na haki kwa watu wa Afrika na wenye asili ya Kiafrika, pamoja na jukumu muhimu la kupambana dhidi ya madhila ya ukoloni na mapambano mapya kwa ajili ya kuleta mageuzi ya mfumo kwenye taasisi za kimataifa, urejeshaji wa mali za kitamaduni na haki ya kufidiwa kwa maovu ya zamani;

**TUNATIWA MOYO** na hamasa mpya ya umajumui wa Afrika katika karne ya 21, unaotetewa na wasomi wanasiasa, watu na wawakilishi wa makundi mbalimbali ya kijamii na kitaaluma;

**TUNAZINGATIA** kwamba mfumo wa mahusiano katika ngazi ya kimataifa unaotokana na Vita vya Pili vya Dunia unaendeleza utegemezi wa kisiasa, kiuchumi, kijeshi, na kifedha kwa kuifanya Afrika iendelee kudumazwa na watu waliokuwa wakoloni wake hapo awali;

**TUNASISITIZA** kuhusu umuhimu wa kuwa na mfumo wa kidunia ulio wa haki zaidi, usawa, na uwakilishi, uliojengwa katika kuheshimu uhuru wa nchi kujitawala, haki ya kijamii, usawa, amani, na ustawi wa pamoja;

**TUNAZINGATIA** Ajenda ya Umoja wa Afrika ya 2063 kama mwelekeo wa kuwa na Afrika jumuishi, yenye ustawi, na amani, inayotokana na umajumui wa Afrika, utawala bora, haki, kuthamini maarifa ya asili, na mchango mkubwa wa vijana na wanawake;

**TUNAREJELEA** maamuzi muhimu ya Umoja wa Afrika, hasa Uamuzi wa Mkutano Mkuu /AU/Dec.807(XXXIV) lililotamka **muongo wa 2021–2031 kama "Muongo wa kurejea Asili za Waafrika na waafrika walioko Ughaibuni"**; Uamuzi wa Mkutano Mkuu AU/Dec.848(XXXVI) unaohusu Kongamano la 9 la Umajumui wa Afrika la Togo; na Uamuzi wa Mkutano Mkuu AU/Dec.913(XXXVIII) ulioahirisha utekelezaji wake hadi 2025, kwani usingeweza kufanyika mwaka 2024;

**TUNAREJELEA PIA** kuhusu kaulimbiu ya Umoja wa Afrika ya 2025 mahususi kwa ajili ya haki ya fidia kwa maovu yaliyotokea "**Haki ya Fidia kwa Waafrika na Watu wenye Asili ya Afrika**";

**Tunatambua kwamba**, ili kukabiliana na changamoto za karne ya 21, Afrika haiwezi kufanikisha peke yake bila mchango wa watu wa asili ya Afrika walioko duniani kote, ambao mchango wao ni muhimu katika kupigania haki, uhuru wa kujitawala, kujitegemea, na kufanya mabadiliko katika mifumo ya taasisi za kimataifa;

**TUNASISITIZA** kwamba mapambano ya mageuzi ya taasisi za kimataifa yanatakiwa yasukumwe na umajumui wa Afrika ukiongozwa na Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Karibi (CARICOM), Jumuiya ya Amerika Kusini na Karibi (CELAC) pamoja na makundi mbalimbali ya watu duniani;

**TUNAENDELEZA** uhuishwaji wa mipango ya Umoja wa Mataifa ya kuunga mkono jitihada za watu wa Afrika, hasa Miongo ya Kimataifa ya Watu wa Asili ya Afrika (2015-2024; 2025-2034), ambayo lengo lake ni kuchangia katika kutengeneza mazingira na kulinda haki za binadamu, kisiasa, na kiuchumi za Afrika na watu wake;

**TUNATAMBUA** kuwa mikutano sita ya awali ya ya Kongamano la 9 la Umajumui wa Afrika ilifanyika katika kanda sita za Afrika, ikiwa ni pamoja na ughaibuni;

**AMBAPO** mikutano sita muhimu ya awali ifuatayo iliyoandaliwa, ni sehemu muhimu ya maamuzi ya Kongamano la 9 la Umajumui wa Afrika: Desemba 4 na 5, 2023, nchini Afrika Kusini ukiwa na mada kuhusu "Umajumui wa Afrika, Sayansi, Maarifa, na Teknolojia"; Machi 14 na 15, 2024 ulifanyika nchini Mali ukihusu "Umajumui wa Afrika, Watu wa Asili ya Afrika, na Maendeleo"; Aprili 18, 2024 ulifanyika Moroko ukihusu "Umajumui wa Afrika na Uhamiaji"; Mei 24, 2024 ulifanyika Kongo ukiwa na mada ya "Umajumui wa Afrika na uchumi na kuinika kwa Afrika"; Julai 6, 2024, ulifanyika Tanzania ukihusu "Umajumui wa Afrika, Utamaduni, Elimu, na Utambulisho wa Afrika"; na Agosti 29 hadi 31, 2024 ulifanyika Bahia, Brazili ukiwa na mada kuhusu "Umajumui wa Afrika, Kumbukumbu, Urejeshaji, Fidia, na Ujenzi Mpya";

**TUNASIKITISHWA** na athari za kudumu za ukoloni, ikiwa ni pamoja na kuingiliwa, mifumo isiyofaa ya kiuchumi, ukosefu wa usawa wa mifumo, na ubaguzi wa rangi na kimfumo, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa usawa kidijitali;

**TUNASISITIZA** umuhimu wa kuhuisha nafasi ya Afrika na walioko ughaibuni ndani ya mfumo wa taasisi za kimataifa, kwa mujibu wa maono ya **Makubaliano ya Ezulwini** na **Azimio la Sirte**, ambayo tanasisitiza haki sawa ya uwakilishi kwa bara la Afrika katika vyombo vya maamuzi vya taasisi za kimataifa;

**TUNASISITIZA** nafasi ya wanawake, vijana, wasomi, wanaharakati, tamaduni za Kiafrika, falsafa ya Ubuntu, na mifumo mingine mipya ya kiasili katika kujenga Umajumui wa Afrika ambayo ni jumuishi, na ya kiukombozi;

**TUNAAZIMIA** kuunganisha nguvu zetu ili kuchangia katika kutengeneza ulimwengu mpya, tukileta pamoja maadili ya Kiafrika ya mshikamano, ubinadamu, uhimilivu, uvumbuzi, na utu;

**TUNAKUBALIANA**, kwa kuzingatia nguzo za kongamano la 9 la Umajumui wa Afrika, kuhusu yafuatayo:

## I. KUHUSU MAONO MAPYA YA UMAJUMUI WA AFRIKA KATIKA KARNE YA 21

1. **KUSISITIZA kuwa** Umajumui wa Afrika ni mfumo wa kimkakati wa kuleta umoja, mazungumzo, na mapambano ya kulinda uhuru wa kujitawala na ukombozi wa Waafrika, watu wa asili ya Kiafrika, na jamii za watu wenye asili ya Afrika duniani kote.
2. **KUHUISHA** maono mapya ya Umajumui wa Afrika katika karne ya 21 ya kwamba lazima yajikite katika tunu za asili za Kiafrika na katika falsafa ya Ubuntu inayohimiza kuhitajiana, kushikamana, na kujali ubinadamu katika maendeleo na mahusiano ya kimataifa.
3. **KUTOA WITO** kwa nchi za Afrika na mataifa yenye watu wa asili ya Kiafrika kuunda umoja uliojengwa katika Umajumui wa Afrika kwa ajili ya kuwa na mapambano ya pamoja ya kudai fidia na mageuzi ya taasisi za kimataifa, na kutengeneza mifumo ya kudumu ya uratibu wa umajumui wa Afrika na kuondoa ukoloni katika sekta za umma, kwa kuwaenzi waasisi wa umajumui wa Afrika.
4. **KUWAALIKA** waafrika na wenye asili ya Kiafrika, pamoja na jamii na taasisi zinazowakilisha katika kujenga umoja wa umajumui wa Afrika wa kutetea maslahi yao kwa pamoja, kusisitiza nafasi yao muhimu na thabiti katika majukwaa ya kimataifa kwa kuzingatia usawa, ujumuishi na uwakilishi zaidi.
5. **KUSISITIZA** kwamba zama mpya za umajumui wa Afrika zinapaswa ziambatane na mshikamano wa kimkakati ulioimarishwa, uongozi wenye maono, na ushiriki mkubwa wa vizazi vipya, ili kuiwezesha Afrika na wale walioko ughaibuni kushughulikia kwa pamoja migogoro mingi inayowaathiri wengi duniani—kama vile afya, mabadiliko ya tabianchi, usalama na kiuchumi—ambayo hakuna serikali au jamii inayoweza kukabiliana nayo peke yake.
6. **KUSISITIZA** kwamba Afrika na waafrika wa ughaibuni wanaunda umoja kwa ajili ya kupigania hatima yao, kuongeza ushawishi wao wa kisiasa, kitamaduni, na kiuchumi kwa dunia nzima, na kutoa wito wa kuimarishwa kwa uhusiano wa kudumu wa kimataifa unaojengwa katika mshikamano, historia ya pamoja, na majadiliano kwa ajili ya mustakabali wa pamoja wa pande zote mbili.
7. **KUKUMBUSHA** umuhimu wa Afrika na watu wa asili ya Kiafrika kuzungumza kwa sauti thabiti na moja katika mijadala ya kimataifa, ili kuleta mabadiliko ya maamuzi yanayohusu mustakabali wa watu na kuhimiza uwepo wa mfumo wa dunia unaozingatia haki, usawa, utu wa binadamu, na kutambua michango ya waafrika katika ustaarabu wa ulimwengu.

## II. KUHUSU FIDIA, HAKI YA KUFIDIWA NA MAPAMBANO DHIDI YA UBAGUZI

8. **KUSISITIZA** kutambuliwa kwa maovu ya kihistoria—utumwa, biashara ya utumwa ya Atlantiki, kufukuzwa, ukoloni, mauaji ya kimbari, ubaguzi wa rangi, na uporaji mkubwa wa rasilimali—ni mambo ya msingi ya kutambuliwa kwa haki ya fidia, na kutoa wito wa kupitishwa kwa msimamo wa pamoja wa Kiafrika unaodai msamaha rasmi, utambuzi rasmi wa maovu haya, na kuanzishwa kwa michakato ya fidia kulingana na maamuzi ya Umoja wa Afrika na vifungu vya sheria za kimataifa.

9. **KUUNGA** mkono maamuzi yaliyotolewa kwenye Kongamano la 9 la Umajumui wa Afrika kuhusu mipango ya pamoja ya Umoja wa Afrika na CARICOM juu ya haki ya kurejesha mali zilizoporwa, na kutoa wito wa kuimarishwa kwa ushirikiano kati ya mataifa ya Afrika, mataifa yenye watu wa asili ya Kiafrika, na taasisi za kikanda zinazohusika katika mchakato huu.

10. **KUSISITIZA** umuhimu wa Azimio la Durban na Programu ya Utekelezaji (2001), haswa katika muktadha wa maadhimisho yake ya miaka 25, kama mfumo wa kimataifa wa kupambana na ubaguzi wa rangi, na kutoa wito kwa Mataifa, taasisi, na wadau muhimu ili kuhakikisha utakelezwa kikamilifu, haswa kupitia elimu, kuweka sawa historia ya kweli ya Afrika, mageuzi ya sera, na kuondoa mifumo ya ubaguzi, ikiwa ni pamoja na aina zake za nyakati hizi kama vile ubaguzi wa rangi.

11. **KUTOA WITO** wa kuanzishwa kwa Makumbusho ya umajumui wa Afrika kuhusu urejeshwaji wa mali zilizoporwa na kupamabana na dhidi ya Ubaguzi wa Rangi - yakiwa na jukumu la kutunza taarifa za matukio ya kihistoria na ya sasa, kufuatilia ahadi zilizotolewa na Mataifa, na kusaidia kutafuta fedha, utetezi, na elimu.

12. **KUTOA WITO** kwa nchi za Kiafrika, jamii za watu wenye asili ya kiafrika, wapenda haki na taasisi husika katika kuungana dhidi ya maovu ya zamani na sasa ya ubaguzi wa rangi, ili kuunga mkono urejeshaji wa mali za kitamaduni zilizoporwa kutoka Afrika, na kuhimiza mageuzi ya kimfumo yanayozingatia heshima, usawa, na haki za msingi za Waafrika na watu wa asili ya Kiafrika duniani kote.

13. **KUTOA WITO** kwa Umoja wa Afrika, mataifa ya Afrika, na mataifa yenye jamii za watu wa asili ya Kiafrika wawasilishe maombi rasmi kwa Umoja wa Mataifa na mashirika yake juu ya haja ya kurekebisha ramani ya bara la Afrika isiyo na uhalisia, hasa ile inayoonyeshwa kwenye Mercator, ni kitendo cha kutambua kuwa haki na fidia ni muhimu kwa ajili ya kuipa Afrika hadhi inayostahili katika ramani ya dunia.

## III. KUHUSU MAGEUZI KATIKA TAASISI ZA KIMATAIFA

14. **KUSISITIZA kuhusu** hitaji la kufanya mageuzi makubwa na ya haraka ndani ya taasisi za kimataifa kwa ajili ya kutekeleza haki ya fidia na usawa ili iakisi hali halisi ya

dunia pana na kurekebisha makosa ya ukosefu wa usawa uliorithiwa kutoka kwenye mifumo ya taasisi za kimataifa iliyoundwa baada ya vita, ambayo imeitenga kabisa Afrika na watu wa asili ya Afrika.

15. **KUSISITIZA** kuhusu ushirikiano wa watu wa Afrika na wale wenye asili ya Kiafrika katika kutekeleza kikamilifu Makubaliano ya Ezulwini na Azimio la Sirte, yanayosisitiza kuhusu uwepo wa nafasi mbili za kudumu kwa Afrika ndani ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ili kuwa na uwakilishi unaolingana na idadi ya watu, kijiografia, na kihistoria ya bara.

16. **KUTOA WITO** kwa mataifa, waafrika na jamii za watu wenye asili ya Kiafrika kuimarisha mifumo ya majadiliano ya kisiasa na kidiplomasia, haswa kwa kuanzisha nafasi ya kudumu ya utaratibu wa pmahusiano ya taasisi mbalimbali kabla ya kuingia kwenye majadiliano ya ngazi kubwa ya kimataifa na kutetea maslahi ya kimkakati ya bara.
17. **KUHIMIZA** uanzishwaji wa ushirikiano wa maeneo ya kanda mbalimbali—hasa ya Afro-Caribbean, Afro-Latin, na Kusini-Kusini—pamoja na kuimarisha majadiliano na makundi mbalimbali kama vile BRICS na G20, ili kuongeza ushawishi wa pamoja wa Afrika na wale walioko ughaibuni katika michakato ya kufanya maamuzi duniani.

18. **KUZIOMBA** taasisi za kimataifa zichukue hatua madhubuti za kuondoa ubaguzi wa rangi unaoendelea, ikiwa ni pamoja na mifumo mipya ya ubaguzi wa rangi, na kuhimiza ushiriki wa taasisi za kimataifa unaozingatia usawa wa nchi huru, uwazi, na ushiriki jumuishi wa watu.

## IV. KUHUSU KUONDOA ATHARI ZA UKOLONI KATIKA FIKRA NA KUJITAMBUA

19. **KUSISITIZA** kuwa kuondoa athari za ukoloni wa fikra ni jambo muhimu la kumwamsha mwafrika aweze kujitambua, kwa kuwa na elimu ya kina na ya asili inayotokana na maarifa, lugha, falsafa, na urithi wa Kiafrika, ili kujenga upya hali ya kujithamini kwa mtu binafsi na kujitambua kwa pamoja na kufungua uwezo wa asili wa kiubunifu, kiakili, na kiroho wa waafrika na watu wa asili ya Kiafrika.

20. **KUHAMASISHA** ushirikiano wa mataifa ya Afrika, Umoja wa Afrika, CARICOM, CELAC, na taasisi za elimu na utamaduni katika kukuza uhuru wa kifikra na kitamaduni unaotegemea epistemolojia za Kiafrika—hasa Maat, Maaya, Ubuntu, na Ummah—kusaidia tafiti kuhusu athari za kisaikolojia za utumwa na ukoloni, na kuongeza nafasi za kutengeneza, kutumia sanaa na majadiliano ya utambulisho.

21. **KUOMBA** serikali, vyuo vikuu, vyombo vya habari na taasisi za kitamaduni za ndani ya Afrika na kutoka katika nchi zenye jamii za watu wa asili ya kiafrika kuandaa njenzo za mawasiliano na kuzalisha maarifa kwa kuweka kipaumbele cha fikra za kiafrika,

kusahihisha hadithi potofu za kikoloni, na kuhuisha nafasi ya ustaarabu wa Kiafrika katika historia ya dunia, na hivyo kutunza kumbukumbu ya kudumu na ya thamani.

## V. KUHUSU KUJITEGEMEA KIMAENDELEO NA AFRIKA HALISI NA JUKUMU LA KIMKAKATI LA WATU WALIOKO UGHAIBUNI

22. **KUTOA WITO** kwa mataifa ya Afrika, pamoja na watu na jamii zenye asili ya Kiafrika, kujenga mfumo wa kujitegemea kimaendeleo unaotokana na kuweka kipaumbele cha kutumia rasilimali za ndani, kuimarisha mfumo huru wa kifedha wa Kiafrika, kuongeza akiba inayotokana na mapato ya ndani na ya waafrika wa ughaibuni kwa ajili ya kufadhili maendeleo kwa kuendana na Ajenda ya 2063.

23. **KUHIMIZA** udhibiti wa pamoja na huru wa rasilimali za kimkakati za bara la Afrika, kuongeza kasi ya usindikaji wa malighafi za ndani, na kuwa na nyenzo za umajumui wa Afrika—mfumo wa udhibiti wa rasilimali za bara la Afrika, kodi za pamoja kwa bara nzima la Afrika, taasisi za upimaji wa mwenendeno wa uchumi wa Afrika, na soko la mtaji kwa ajili ya kuendeleza malighafi za Afrika—ili kusaidia mabadiliko ya kimfumo, kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa Afrika, na kupunguza athari za utegemezi wa misaada ya nje.

24. **KUHAMASISHA** matumizi ya maarifa ya Kiafrika na ya walioko ughaibuni kwa ajili ya kutumia vipaji, kusaidia kuibuka kwa viwanda ndani ya Afrika, kuimarisha ujasiriamali na upatikanaji wa huduma za kibenki kwa jamii za watu wa asili ya Afrika, na kuelekea uanzishwa wa sarafu ya pamoja ya Afrika na benki ya maendeleo ya Afrika mahususi kwa ajili ya miradi ya nishati, viwanda, na miundombinu.

25. **KUTOA WITO** wa kuimarishwa kwa ushirikiano kati ya Kusini na Kusini, ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa viunganishi vya masuala ya kiuchumi, kielimu, kisayansi, na kitamaduni na nchi za Karibi, Amerika, Bahari ya Hindi, na Ulaya ambapo kuna idadi kubwa ya watu wa asili ya Kiafrika, na kuendeleza harakati za kupigania uhuru wa watu kutembea, kutoa maoni na kufungamanisha kikamilifu jitihada za kiuchumi kati ya Afrika na watu wa ughaibuni ili kuwa na mfumo kamili wa kiuchumi na kuwaunganisha wana majumui wa Afrika.

## VI. KUHUSU UTAMADUNI, UTAMBULISHO NA ELIMU

26. **KUSISITIZA** kuhusu umuhimu wa kuchukua hatua za haraka za kuondoa athari za ukoloni katika mifumo ya elimu ya Kiafrika kwa kupitisha mitaala yenye taswira ya umajumui wa Afrika inayotokana na dhana na elimu ya Kiafrika, ili kuifanya elimu hiyo iwe nyenzo ya ukombozi, uhuru wa kifikra, na umoja.

27. **KUBAINISHA** jukumu la msingi la utamaduni wa Kiafrika, utambulisho, na maarifa katika ujenzi wa umajumui wa Afrika wa nyakati za sasa, kwa kukuza lugha za

Kiafrika, maarifa ya asili, na vielelezo vya sanaa kwa ajili ya kuleta mshikamano, kujithamini kwa pamoja, na kuendeleza historia wa waafrika na watu wa asili ya Afrika.

28. **KUYAHIMIZA** mataifa na nchi zenye watu wa asili ya kiafrika kufanya mageuzi kamili ya mifumo yao ya elimu, kuunganisha historia ya Kiafrika, maarifa ya umajumui wa Afrika, maadili ya Maat, Maaya, na Ubuntu, pamoja na michango ya wanawake, vijana, na walioko ughaibuni, ili elimu hiyo iwe kichocheo cha ukombozi, ubunifu, na uhuru wa kifikra.

29. **KUTOA WITO** wa kuimarishwa kwa ushirikiano wa kielimu na kitamaduni kati ya Afrika na waafrika walioko ughaibuni, ikiwa ni pamoja na kubadilishana wanataaluma, kuanzisha vigoda vya kitaaluma katika umajumui wa Afrika, kuanzisha makavazi ya kidijitali, kuendeleza weledi katika tasnia za kitamaduni, na utekelezaji wa mipango ya mfumo wa elimu ya umajumui wa Afrika, ikiwa ni pamoja na miradi ya vyuo vikuu au majukwaa ya mtandaoni ya umajumui wa Afrika mahususi kwa ajili ya kuwa vitovu vya maarifa, uvumbuzi, na majadiliano ya kitamaduni.

## VII. KUHUSU NAFASI YA KIHISTORIA NA YA SASA YA WANAWAKE KATIKA MAPAMBANO YA UMAJUMUI WA AFRIKA NA UHURU

30. **KUWAENZI** wanawake wa Afrika na walioishi ughaibuni ambao walipambana vya kutosha dhidi ya utumwa, ukoloni, ubaguzi wa rangi, na aina zote za ukandamizaji, na kusisitiza umuhimu wa kuongeza jitihada za kufanya utafiti, kuweka na kuhifadhi kumbukumbu zao ili kutambua kikamilifu mchango wao katika historia ya umajumui na uhuru wa Afrika.

31. **KUHIMIZA** ushiriki mkubwa wa wanawake mashuhuri katika programu za elimu, vyombo vya habari, taasisi za kitamaduni, na taasisi za umma, ili kuthamini urithi wao, kuhamasisha vizazi vya sasa na vijavyo, na kuimarisha utamaduni jumuishi wa umajumui wa Afrika unajikita katika ukweli wa kihistoria.

32. **KUHIMIZA** ujumuishwaji wa wanawake na vijana kikamilifu katika michakato ya kufanya maamuzi ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, na kitamaduni kama sharti muhimu la kuhuisha fikra za kiafrika, na kutoa wito kwa serikali, taasisi za kikanda, na asasi za kiraia kutoa nafasi za uongozi kwa wanawake katika ngazi zote za kiutawala.

## VIII. KUHUSU MAAMUZI, UFUATILIAJI, URATIBU NA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA KONGAMANO LA 9 LA UMAJUMUI WA AFRIKA

33. **KUSISITIZA** umuhimu wa kuwa na utaratibu jumuishi na wa uwakilishi wa ufuatiliaji, unaohusisha Umoja wa Afrika, mataifa ya Afrika, jamii za watu wenye asili ya kiafrika, na nchi zenye makundi watu wengi wenye mafungamano na Afrika, ili kuwa na

mwendelezo, mshikamano, na utekelezaji wa mapendekezo ya Kongamano la 9 la Umajumui wa Afrika.

34. **KUIPA** Jamhuri ya Togo, jukumu la kuwa nchi mwenyeji na mwandaaji mwenza wa Kongamano, nia ya kuratibu, kwa ushirikiano na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, mataifa ya Afrika na nchi zenye wakazi wenye asili ya Kiafrika, pamoja na taasisi za waafrika walioko ughaibuni, ufuatiliaji wa utekelezaji wa ahadi na maamuzi ya Kongamano la 9 la Umajumui wa Afrika.

35. **KUAMUA** kuhusu kuanzishwa kwa Kamati inayohusika na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo na maamuzi ya Kongamano la 9 la Umajumui wa Afrika.

36. **KUUNGA** mkono jitihada za kuanzishwa kwa Siku ya Afrika kwa ajili ya kumbukumbu ya waliohamishwa na kuathiriwa na utumwa na ukoloni, na kutoa wito kwa mataifa ya Afrika, Umoja wa Afrika, CARICOM na nchi wanachama wake, Jamii za watu walioko Amerika ya Kusini na Karibi (CELAC), pamoja na majukwaa mengine yote na ya waafrika wanaoishi ughaibuni katika mabara yote, kushauriana kwa haraka iwezekanavyo ili kubaini tarehe halisi ya kuadhimisha Siku hii.

37. **KUIOMBA** Jamhuri ya Togo iwasilishe kwa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ombi la kutambua azimio la kuanzishwa kwa Siku ya Kimataifa ya Fidia na Urejeshaji wa mali za kitamaduni zilizoporwa Afrika.

38. **KUAMUA** kuandaa Kongamano la Umajumui wa Afrika kila baada ya miaka mitano (5) na kuanzisha ofisi ya kudumu ya Kongamano la Umajumui wa Afrika ambapo uamuzi kuhusu nchi na/au taasisi mwenyeji utafanyika baada ya mashauriano miongoni mwa Mataifa na wadau mbalimbali.

39. **KUAMUA** kuwasilisha rasmi Azimio hili kwa Mkutano Mkuu wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kwa ajili ya kupitiwa na kuzingatiwa na vyombo, mifumo, na michakato sahihi ya Umoja huo, pamoja na washirika wa kikanda na kimataifa wanaohusika katika kutangaza malengo ya Umajumui wa Afrika.

40. **KUTOA WITO** kwa mataifa ya Afrika na yenye jamii na watu wenye asili ya Kiafrika wa kuchukua mapendekezo ya Kongamano la 9 la Umajumui wa Afrika na kuyaingiza katika sera zao za kitaifa, kikanda, na kidiplomasia.

**Limetolewa Lomé, tarehe 12 Desemba 2025**

# TAMKO LA MKUTANO WA PILI WA AFRIKA–CARICOM

## TAMKO LA ADDIS ABABA KUHUSU "USHIRIKIANO WA BARA KATIKA KUTAFUTA HAKI YA FIDIA KWA WAAFRIKA NA WATU WA ASILI YA AFRIKA KUPITIA MALIPO YA FIDIA" ADDIS ABABA, JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA SHIRIKISHO LA ETHIOPIA, TAREHE 7 SEPTEMBA 2025

**1.** **Sisi**, **Wakuu wa Nchi na Serikali za Umoja wa Afrika na CARICOM**, tumekutana Addis Ababa, Ethiopia, tarehe 7 Septemba 2025, katika Mkutano wa Pili wa Afrika–CARICOM, uliofanyika chini ya kaulimbiu: "Ushirikiano wa bara katika Kutafuta Haki ya Fidia kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Afrika kupitia Malipo ya Fidia",

***2.*** **TUNAELEZA** shukrani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Abiy Ahmed Ali, Waziri Mkuu, pamoja na Serikali na wananchi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia kwa kuandaa Mkutano huo, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Afrika na CARICOM,

### <u>MISINGI YETU MIKUU YA MAREJELEO KWA AJILI YA HAKI YA FIDIA</u>

3. **TUKIREJELEA** Uamuzi (Assembly, AU/Dec.847), uliounga mkono pendekezo la Serikali ya Ghana la kuandaa kwa pamoja, kwa kushirikiana na wadau husika, Mkutano wa Kimataifa kuhusu *"Kujenga Umoja wa Pamoja wa Kusukuma Mbele Ajenda ya Haki na Malipo ya Fidia kwa Waafrika"*; pamoja na Uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika, Assembly/AU/Dec.884(XXXVII) wa Februari 2024 ulioteua Kaulimbiu ya Mwaka wa Umoja wa Afrika kwa mwaka 2025 kuwa *"Haki kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Afrika Kupitia Malipo ya Fidia"*; na Uamuzi wa Assembly/AU/Dec.903(XXXVIII) kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka 2025: "Haki kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Afrika Kupitia Malipo ya Fidia*"*– doc. EX.CL/1569(xlvi),

4. **TUKISISITIZA** chimbuko la kina la Uafrika la Umoja wa Afrika na mtangulizi wake, Jumuiya ya Umoja wa Afrika, linalojumuisha uhusiano wa kihistoria, kiutamaduni na undugu unaounganisha Bara la Afrika na Diaspora ya Waafrika; na unasisitiza misingi ya kujitawala na mamlaka ya nchi iliyoongoza harakati za ukombozi, pamoja na heshima ya uhuru wa nchi na mipaka kieneo, kutoingilia masuala ya ndani ya nchi nyingine, ujirani mwema kama misingi ya Sheria ya Kuanzishwa ya Umoja wa Afrika na Mkataba wa Umoja wa Mataifa,

5. **TUKISISITIZA** Mkutano wa Kwanza wa Afrika kuhusu Malipo ya Fidia uliofanyika Abuja mwezi Aprili 1993, unaojulikana kama "Azimio la Abuja la Malipo ya Fidia la mwaka 1993", ambao uliitaka jumuiya ya kimataifa kutambua deni la kipekee na lisilo kifani la kimaadili linalodaiwa kwa watu wa Afrika,

6. **PIA, TUKIREJELEA** Tamko na Mpango wa Utekelezaji wa Durban wa mwaka 2001 kuhusu athari za Ubaguzi wa Rangi, Ubaguzi wa Kikabila, Chuki dhidi ya Wageni, na Mienendo Mingine ya Kutovumiliana inayohusiana, ambao uliweka mwongozo wa kina na wa maono mapana unaoakisi dhamira ya dunia kukabiliana na janga la ubaguzi wa rangi katika aina na maudhui yake yote.

7. **TUKIZINGATIA** kwamba Tamko la Accra kuhusu kaulimbiu "Kusukuma Mbele Haki: Malipo ya Fidia na Uponyaji wa Maumivu ya Ubaguzi wa Rangi" lililotolewa Agosti 2022, lilizitaka nchi za Afrika, raia wake na viongozi wa kisiasa kusimamia na kutekeleza madai ya fidia kamili kutoka kwa mataifa, taasisi na serikali zinazohusika, kutokana na athari hasi zilizosababishwa na biashara ya utumwa ya Afrika, utumwa wa mali, ukoloni, ubaguzi wa rangi na mauaji ya kimbari, kwa Waafrika na watu wa asili ya Afrika,

8. **TUKIREJELEA** Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa namba 62/122 kuhusu kumbukumbu ya kudumu na ukumbusho wa waathirika wa utumwa na biashara ya watumwa ya kuvuka Atlantiki, pamoja na Tamko la Accra kuhusu Malipo ya Fidia, matokeo ya Mkutano wa Kimataifa kuhusu Malipo ya Fidia uliofanyika Accra, Ghana, kuanzia tarehe 14 hadi 17 Novemba 2023,

9. **TUKITAMBUA** kwamba Jumuiya ya Karibe (CARICOM) mwaka 2013 iliunda Tume ya CARICOM ya Malipo ya Fidia, chini ya uangalizi wa Wakuu wa Serikali, kama utaratibu wa kikanda wa kusukuma mbele ajenda ya malipo ya fidia,

10. **VILEVILE TUKITAMBUA** kwamba CARICOM mwaka 2014 iliandaa Mpango wa Hoja Kumi wa Haki ya Fidia kama mfumo wa kujadiliana kuhusu makubaliano ya kina ya fidia kwa ajili ya kurekebisha madhara yaliyosababishwa kwa karne nyingi, kwa kuzingatia mkabala wa maendeleo ya pamoja; mpango huo unataka kuwepo kwa ombi rasmi la kuomba radhi, programu za kurejea barani Afrika kwa hiari na uraia, programu ya maendeleo ya watu wa asili, urekebishaji wa mifumo ya afya ya umma na elimu, uanzishaji wa taasisi za kiutamaduni, urejeshaji wa mali za kiutamaduni, kuunganisha upya utamaduni na uponyaji wa kisaikolojia, maendeleo kupitia teknolojia, kufutwa kwa madeni na fidia ya kifedha; na mpango huo umetajwa sana na unaheshimiwa kwa kiwango kikubwa kimataifa,

11. **TUKIREJELEA** maamuzi ya Mkutano wa Tathmini wa Kati wa Mkutano wa Thelathini na Tano wa Wakuu wa Serikali wa CARICOM uliofanyika Septemba 2023, uliolenga kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Afrika katika kusukuma mbele mipango ya pamoja ya fidia, ikiwamo kudhamini kwa pamoja azimio la fidia katika Umoja wa Mataifa na kuitisha mkutano wa kimataifa wa fidia; pamoja na uamuzi ya Mkutano wa Kawaida wa Arubaini na Saba wa Baraza Kuu uliofanyika Julai 2024, uliokubaliana kuanzisha kikosikazi cha pamoja cha wataalamu na Umoja wa Afrika, na kuimarisha maadhimisho ya Siku ya Afrika–CARICOM tarehe 7

Septemba katika Nchi Wanachama wa CARICOM na Umoja wa Afrika,

12. **TUKITAMBUA** wito unaoongezeka kimataifa kutoka kwa asasi za kiraia, taasisi za kitaaluma, mashirika binafsi, na serikali barani Afrika na katika Diaspora kuhusu haja ya majadiliano na hatua za utekelezaji za haki ya fidia, ikiwamo utambuzi wa hadharani wa uwajibikaji na wale waliohusika kusababisha madhara kutokana na matendo ya kihistoria ya zamani.

## MASUALA MUHIMU YA KUSHUGHULIKIA HAKI YA FIDIA

13. **TUNASISITIZA** kwamba, katika muktadha wa madai ya haki ya fidia, kuna haja ya kushughulikia ukosefu wa usawa unaotambulika katika mifumo ya sasa isiyo ya haki ya kiuchumi na siasa ya kimataifa, jambo linalohitaji mageuzi ya mfumo wa fedha na biashara wa dunia, pamoja na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, huku tukitambua Mpango wa Bridgetown 2.0; katika muktadha huohuo wa haki ya fidia,

14. **TUNATAMBUA** haja ya kushughulikia matokeo ya biashara ya utumwa kwa Waafrika, utumwa wa mali, ukoloni na ubaguzi wa rangi uliotekelezwa na tawala za kikoloni, pamoja na athari zake zote ambazo zimechangia, zimejitokeza au zimeendelea katika sura mbalimbali, zikiwamo bila kusahau mzigo usio wa haki wa madeni ya uhuru wa taifa, mzunguko haramu wa fedha, au hasara na uharibifu pamoja na majanga ya kimazingira yaliyosababishwa na majaribio ya nyuklia.

15. Hivyo**, TUNASISITIZA** kwamba uwajibikaji na utoaji wa suluhu, fidia, malipo ya fidia, urejeshwaji wa haki na haki ya fidia kwa uhalifu wa kihistoria ikiwamo biashara ya utumwa kwa Waafrika pamoja na ukoloni, mauaji ya kimbari na ubaguzi wa rangi ni wajibu wa msingi chini ya sheria ya kimataifa,

16. **TUNASISITIZA** sharti la msingi la kupambana na ubaguzi wa rangi wa kimfumo, na kusukuma mbele haki za binadamu, utu na uponyaji wa Waafrika na watu wa asili ya Afrika.

## MALENGO – MATOKEO YA HAKI YA FIDIA

17. **TUNASISITIZA** kwamba malipo ya fidia na utoaji wa haki ya fidia kwa Afrika na Diaspora ya Afrika ni mojawapo ya nguzo za maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi barani Afrika na katika sehemu husika za Diaspora ya Afrika katika *Global South,* na ni chachu ya utekelezaji wa Ajenda ya Umoja wa Afrika 2063;

18. **TUNASISITIZA** umuhimu wa msingi wa kutambua haja ya kulinda utamaduni, urithi na heshima ya bara, tukihimiza kupitia kuandaa Nafasi ya Pamoja kuhusu Urejeshaji wa Mali na Urithi wa Kiutamaduni na Mpango wa Utekelezaji wa Mazungumzo kwa ajili ya kurudisha mali za kiutamaduni zilizoporwa kinyemela,

urejeshaji kamili wa makabidhiano ya kifedha, kidini, kumbukumbu za kihistoria, makaburi ya watu na vitu vingine vya kiutamaduni vilivyoporwa kutoka Afrika;

19. **TUNATAMBUA** Majadiliano ya Kikanda kuhusu Urejeshaji wa Mali na Urithi wa Kiutamaduni yaliyofanyika Novemba 2021 na jitihada za Umoja wa Afrika zilizolenga kurudisha vitu vilivyoporwa, ikiwamo vya kidini na ya kiutamaduni;

20. **TUNALENGA** kurejesha hasara za kijamii na kiuchumi zilizopatikana kwa nchi za Afrika na jamii zake, pamoja na nchi na jamii za watu wa asili ya Afrika katika diaspora;

21. **TUNASISITIZA** kwamba ni hatua muhimu kuelekea kutafuta haki na uponyaji kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Afrika, kuhakikisha uwajibikaji kutoka kwa tawala za kikoloni zilizopita na nchi nyingine pamoja na taasisi zinazohusika kwa uhalifu mkubwa uliofanywa dhidi ya Waafrika na diaspora ya kimataifa ya Kiafrika wakati wa kipindi cha biashara ya utumwa kwa Waafrika , utumwa wa mali, ukoloni, ubaguzi wa rangi, mauaji ya kimbari na ukoloni mamboleo, ikiwamo lakini si tu kuhamishwa kwa nguvu, mauaji ya wengi, kufungwa kiholela, mateso, wizi wa maliasili, kutekeleza mifumo ya kiuchumi isiyo ya haki, kukandamiza harakati za ukombozi, na majaribio ya nyuklia, yote yaliyosababisha majanga ya kibinadamu na ya mazingira.

## <u>MATOKEO KWA AJILI YA KUFIKIA MALENGO YA HAKI YA FIDIA</u>

22. **TUNAKARIBISHA** KWA DHATI uamuzi wa Baraza Kuu la Umoja wa Afrika ulioutaka utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka kuendelezwa zaidi ya mwaka 2025 na kupendekeza kuanzishwa kwa Muongo wa Umoja wa Afrika wa 2026–2036 kwa ajili ya Haki kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Afrika Kupitia Malipo ya Fidia**.**

23. **TUTAFANYA KAZI PAMOJA** kuelekea kuimarisha utetezi wa nafasi ya pamoja kuhusu malipo ya fidia barani Afrika na Karibe, tukijumuisha ndani yake Mpango wa Hatua za Haki ya Fidia tukizingatia Mpango wa Hoja Kumi za CARICOM kuhusu Haki ya Fidia; na kuunda msimammo wa pamoja na Diaspora kwa kiwango cha kimataifa, utakaochangia kuimarisha harakati za bara na za kimataifa za malipo ya fidia, kwa lengo la kudumisha kasi yake na kuhakikisha uendelevu wake, na kuunda msimamo wa pamoja imara ndani ya mfumo wa Ushirikiano wa bara, katika kutafuta malipo ya fidia na haki ya fidia kimataifa.

**24.** **TUNAUNGA MKONO** uteuzi wa malipo ya fidia kwa biashara ya Utumwa ya Kuvuka Atlantiki kwa Waafrika, utumwa wa mali, ukoloni na ubaguzi wa rangi, kuwa Kipaumbele Kikuu na Mradi wa Umoja wa Afrika**;**

25. **TUNAIUNGA MKONO** Mpango wa Jamhuri ya Togo kuhusu utambuzi wa utumwa, kuhamishwa kwa nguvu na ukoloni kama uhalifu dhidi ya binadamu na

mauaji ya kimbari dhidi ya watu wa Afrika, pamoja na kuandaa Mkutano wa Tisa ya Pan -Afrika huko Lomé, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Afrika;

26. **TUNAIDHINISHA KIKAMILIFU** kuanzishwa kwa Siku ya Afrika kwa heshima ya mashujaa wa Afrika na waathirika wa biashara ya utumwa Afrika, utumwa wa mali, ukoloni na ubaguzi wa rangi na TUNAKARIBISHA ombi la Aljeria la kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kimataifa wa Uhalifu wa Ukoloni, kwa ushirikiano na Kamisheni ya Umoja wa Afrika.

**HATI NA MIKAKATI YA KUSUKUMA MBELE MALENGO NA MATOKEO YA HAKI YA FIDIA**

**27.** **TUNAMSHUKURU,** na kutambua jitihada za Mheshimiwa John Mahama, Rais wa Jamhuri ya Ghana, kama Kiongozi wa Umoja wa Afrika katika kusukuma mbele ajenda ya haki na malipo ya fidia kwa Waafrika**;**

28. **TUNATOA SHUKRANI** kwa Mheshimiwa Mia Amor Motley, Waziri Mkuu wa Barbados na Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Waziri Mkuu kuhusu Malipo ya Fidia, kwa mchango muhimu na wa thamani wa CARICOM na utetezi bila kuchoka katika kufuatilia malipo ya fidia kwa Afrika na diaspora ya Afrika, na hivyo kuhamasisha harakati za kimataifa za haki ya fidia;

29. **TUNAAHIDI** kutekeleza Utaratibu wa Pamoja wa Afrika–Karibe kuhusu Haki ya Fidia**,** kama ilivyoelezwa katika Uamuzi namba 847 wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika na kuungwa mkono na Mkutano wa Tathmini wa Kati ya Vipind vya Mkutano wa Thelathini na Tano wa Wakuu wa Serikali wa CARICOM uliofanyika Septemba 2023;

30. **TUNAUNGA MKONO** utekelezaji kamili wa Tume ya Wataalamu wa Umoja wa Afrika kuhusu Malipo ya Fidia, kwa ajili ya kuandaa Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu Malipo ya Fidia**,** na kujumuisha Mpango wa Hatua za Haki ya Fidia wa Afrika**,** pamoja na Kundi la Marejeleo la Wataalamu wa Sheria la Umoja wa Afrika**;**

31. **TUNAIDHINISHA** kuanzishwa kwa Mfuko wa Kimataifa wa Malipo ya Fidia ulioko barani Afrika, utakaoshirikiana na Umoja wa Afrika na CARICOM, kusukuma mbele kampeni ya Umoja wa Afrika kuhusu malipo ya fidia, na kufadhiliwa hasa na nchi, falme, mashirika binafsi, familia, raia na taasisi nyingine za mataifa ya kikoloni yaliyohusika katika uhalifu wa biashara ya utumwa kwa Waafrika, utumwa wa mali, ukoloni na wizi wa maliasili.

32. **TUNASISITIZA** msaada wetu madhubuti katika mchakato unaoendelea barani Afrika unaolenga urejeshaji kikamilifu wa rasilimali za kidini na kiutamaduni, kumbukumbu za kihistoria na mabaki ya binadamu ya Kiafrika zilizoporwa;

33. **TUNAHIMIZA** Nchi Wanachama zinazoshiriki kutoa jitihada za kuwa wenyeji wa Mkutano wa Kila Mwaka wa Malipo ya Fidia, kwa kubadilishana kati ya Bara la Afrika na CARICOM;

34. **TUTAJITAHIDI** kupanua Mfumo huu wa Ushirikiano wa bara unaojumuisha Afrika na CARICOM ili pia ujumuishe Diaspora ya Afrika katika Amerika ya Kusini, Amerika Kaskazini, Ulaya, na sehemu nyingine za dunia, kwa lengo la kuunda msimamo wa pamoja imara kati yao katika kutafuta malipo ya fidia na haki ya fidia kimataifa.

35. **TUNAUNGANA** na Haiti katika kumbukumbu ya miaka mia mbili ya kutozwa kwa deni kubwa na Ufaransa kwa Haiti kama malipo ya uhuru, na TUNAKARIBISHA kuanzishwa kwa kamati ya pamoja ya kuzingatia urejeshaji wa deni la uhuru wa Haiti.

**USHIRIKIANO WA KIDUNIA NA KIMATAIFA**

36. **TUNATOA WITO** wa kuimarisha ushirikiano na mfumo wa Umoja wa Mataifa, ikiwamo Jukwaa la Kudumu la Umoja wa Mataifa la Watu wa Asili ya Afrika, Kikundikazi cha Wataalamu wa Watu wa Asili ya Afrika, Kamati ya Kuondoa Ubaguzi (CARICOM), na UNESCO, katika kutekeleza tamko hili; ikiwa ni pamoja na kutoa msaada wa kiufundi kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya madai, kupitisha azimio na kuunda mfumo wa kisheria na mpango wa urejeshaji na malipo ya fidia;

37. **TUNAHIMIZA** kuanzishwa kwa Programu ya Ushirika wa Malipo ya Fidia kusaidia kujenga uwezo wa wasomi, wataalamu wa sheria, na wanaharakati kutoka Afrika na Karibe kushirikiana katika utafiti na utetezi wa haki ya fidia, na tunawasihi wadau wa sekta binafsi wenye uhusiano wa kihistoria na utumwa wa kuvuka Atlantiki na ukoloni kushiriki na kuchangia katika Mfuko wa Malipo ya Fidia kupitia ahadi za hiari.

**HATUA INAYOFUATA**

38. Tunatambua umuhimu wa ufuatiliaji na tathmini yenye ufanisi katika kuhakikisha utekelezaji wa mafanikio wa ahadi zetu kama ilivyoelezwa katika azimio hili, na tunaamua kuanzisha mfumo thabiti wa ufuatiliaji na tathmini ili kufuatilia maendeleo, kubaini changamoto na kutoa taarifa ya maamuzi.

39. **TUNAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Sekretariati ya CARICOM kuwasilisha Ripoti ya Pamoja ya Maendeleo katika Mkutano ujao wa Afrika–CARICOM, na kuiomba kuwasilisha nyaraka ya mpangomkakati na mpango wa utekelezaji wenye muda wa ukomo, na kutokana na haya, **TUNAAMUA** kushughulikia jambo hili kikamilifu.

**AFRICAN UNION** **UNION AFRICAINE**

**الاتحاد الأفريقي** **UNIÃO AFRICANA**

**UMOJA WA AFRIKA** **UNIÓN AFRICANA**

**Addis Ababa, ETHIOPIA P. O. Box 3243 Telephone : 5517 700 Fax : 251-11-5517844**
**website : www.au.int**

**Rev 2**

# TAARIFA
## YA MKUTANO WA PILI WA AFRIKA NA JUMUIYA YA MATAIFA YA KARIBIANI (CARICOM)
**Addis Ababa, Ethiopia**

**7 Septemba 2025**

1. Wakuu wa Nchi na Serikali wa nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) na ya Jumuiya ya Mataifa ya Karibiani (CARICOM) walikutana kwa Mkutano wa Pili wa kihistoria wa Afrika na CARICOM mnamo tarehe 7 Septemba 2025, ulioandaliwa na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Sekretarieti ya Jumuiya ya Karibea (CARICOM) huko Addis Ababa, Ethiopia. Mkutano huo uliongozwa kwa pamoja na Waziri Mkuu wa St. Kitts na Nevis, na Mwenyekiti mpya wa Mkutano wa Wakuu wa Serikali wa CARICOM, Mheshimiwa Dkt. Terrence Drew, na Rais wa Jamhuri ya Angola, na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, Mheshimiwa João Manuel Gonçalves Lourenço.

2. Mkutano huo ulihudhuriwa na Wakuu wa Nchi/Serikali na Wakuu wa Jumbe wafuatao:

   Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika: **Algeria, Angola, Benin, Botswana, Burundi, Cabo Verde, Cameroon, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Comoros, Kongo , Côte d' Ivoire, Djibouti, Misri, Eritrea, Eswatini, Ethiopia, Equatorial Guinea, Gabon, Gambia, Ghana, Guinea Bissau, Kenya, Lesotho, Lesotho, Malawi, Liberia, Liberia Mauritius, Morocco, Msumbiji, Namibia, Nigeria, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Sahrawi, Senegal, Seychelles, Sierra Leone, Somalia, Afrika Kusini, Sudan Kusini, Tanzania, Togo, Tunisia, Uganda, Zambia na Zimbabwe.**

   Jumuiya ya Mataifa ya Karibiaani (CARICOM)**: Antigua na Barbuda, Barbados, Bahamas, Belize, Bermuda, Dominika, Grenada, Haiti, Jamaika, Saint Vincent na Grenadini, Saint Kitts na Nevis, Surinam, Trinidad na Tobago**

3. Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Wakuu wa Mashirika ya Kikanda na Kimataifa wafuatao: Mheshimiwa Mahmoud Ali Youssouf, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Mheshimiwa Dkt. Carla Natalie Barnett, Katibu Mkuu wa CARICOM, Mheshimiwa Bw. Parfait Onanga-Anyanga, Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Mkuu wa Ofisi ya Umoja wa Mataifa katika Umoja wa Afrika, pamoja na wakuu na wawakilishi kutoka Mashirika na vyombo Maalum vya Umoja wa Mataifa [Umoja wa Kimataifa wa Mawasiliano (ITU), Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) na UN Women], Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Vyombo vya Umoja wa Afrika na Mashirika na Taasisi Maalum ikiwa ni pamoja na Afreximbank, Jumuiya ya Mataifa ya Karibiani (CARICOM), Tume ya Fidia ya CARICOM, Shirika la Mataifa ya Afrika, Karibiani na Pasifiki, pamoja na Shirika la *International Federation of Red Cross and Red Crescent Societies (IFRC)* na Kituo cha Dunia cha Historia, Urithi na Elimu ya Weusi (GBHHEC).

4. Mkutano huo, ambao ulifanyika chini ya kaulimbiu "Ushirikiano wa Bara katika Kutafuta Haki ya Fidia kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Afrika kupitia Fidia", ulithibitisha tena uhusiano mkubwa wa historia ya pamoja na mshikamano wa kitamaduni unaowaunganisha watu wa Afrika na Jumuiya ya Mataifa ya Karibiani na Diaspora kwa ujumla. Ulikuwa wakati muhimu katika kuimarisha ushirikiano mpana na wenye nguvu kati ya maeneo hayo, na hivyo kujitolea kubadili matarajio ya pamoja kuwa matokeo yanayoonekana kwa manufaa ya pande zote mbili ya watu wao.

5. Kwa kutambua ushirikiano mkubwa wa Umoja wa Afrika na Diaspora ya Afrika, Mkutano huo ulikaribisha maadhimisho ya Siku ya Nne ya CARICOM-Afrika mnamo tarehe 7 Septemba 2025, kama ushuhuda wa vifungo vya kudumu.

6. Mkutano huo pia ulifanyika katika wakati muhimu katika uhusiano kati ya Afrika na CARICOM ambapo Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (kwa uamuzi Assembly/AU/Dec.884 (XXXVII)) uliteua kaulimbiu ya AU ya Mwaka ya 2025 kuwa; *"Haki kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Afrika Kupitia Fidia". Uamuzi huo* unatoa wito zaidi wa kuanzishwa kwa Mfumo wa Ushirikiano wa baina ya mabara unaohusisha AU, CARICOM na Diaspora ya Afrika katika Amerika ya Kilatini, Amerika ya Kaskazini, Ulaya na kwingineko duniani, ili kujenga umoja imara miongoni mwao katika kutafuta fidia na haki ya fidia katika ngazi ya kimataifa; na ulikumbuka kwamba katika Uamuzi wa Wakuu wa Mkutano Mkuu (Assembly/AU/Dec.847(XXXVI), ulitoa wito wa kuanzishwa kwa Mfumo wa Pamoja wa Karibiani na Afrika kuhusu Haki ya Fidia, kulingana na azimio la Mkutano wa Kimataifa wa Diaspora ya Afrika uliofanyika Afrika Kusini mwaka 2012.

**Ushirikiano wa Kihistoria na Dira ya umajumui wa Afrika**

7. Wakuu wa Nchi na Serikali walisisitiza kujitolea kwao kwa roho na dira ya umajumui wa Afrika, iliyotetewa na mababu wa Afrika na Mataifa ya Karibiani katika mkutano

wa kwanza wa umajumui wa Afrika wa 1900. Wakuu hao walithibitisha kujitoa kwa viongozi wa Afrika na mataifa ya Karibiani katika kuimarisha vifungo vya umoja na mshikamano kati ya watu wote wenye asili ya Afrika na kuendeleza ajenda ya pamoja kwa ajili ya utaratibu wa kimataifa wa haki na jumuishi zaidi.

8. Mkutano huo ulikumbuka zaidi Azimio la Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika wakati wa Mkutano wa Kawaida wa Thelathini na Tatu wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU, uliofanyika mjini Addis Ababa, Ethiopia kuanzia tarehe 9-10 Februari 2020, ambao ulitoa wito wa ushirikiano wa karibu kati ya Umoja wa Afrika, Diaspora ya Afrika, na Watu wa Asili ya Afrika walio katika Mataifa ya Karibiani.

9. Pia walikumbuka Kikao cha Thelathini na Moja cha Mkutano wa Wakuu wa Serikali wa CARICOM, uliofanyika Bridgetown, Barbados kuanzia tarehe 18-19 Februari 2020, ambacho kilithibitisha ushirikiano unaokua kati ya Nchi Wanachama wa CARICOM na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika.

10. Mkutano huo ulikumbuka Mkutano wa kwanza wa Afrika na CARICOM, ulioandaliwa na Jamhuri ya Kenya, na ulifanyika kwa njia ya mtandao mnamo tarehe 7 Septemba 2021. Wakati wa tukio hili muhimu, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU) na CARICOM waliahidi kukuza mazungumzo zaidi na kuendeleza ushirikiano katika maeneo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na biashara, afya, ushirikiano wa watu, vyombo vya habari, na mabadiliko ya tabianchi.

11. Mkutano huo ulibaini ushirikiano wa hivi karibuni wa ngazi ya juu kati ya Umoja wa Afrika na Nchi Wanachama wa CARICOM katika Mkutano wa Karibiani wa Moroko uliofanyika Julai 2007 kuhusu Ushirikiano wa Nchi zenye uchumi wa chini, na katika Mkutano wa Arobaini na Tano wa Mkutano wa Wakuu wa Serikali wa CARICOM huko Trinidad na Tobago mnamo Julai 2023, Mkutano wa Kwanza wa Mawaziri wa CARICOM-Afrika Kusini mnamo Machi 2024, na katika Mkutano wa Kawaida wa Thelathini na Nane wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika uliofanyika mnamo Februari 2025 mjini Addis Ababa.

12. Mkutano huu wa kwanza wa ana kwa ana uliitishwa kufuatia ahadi zilizotolewa na Viongozi wa AU na CARICOM katika Mkutano wa kwanza wa CARICOM na Afrika na majadiliano zaidi na Mhe. Abiy Ahmed Ali, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia, na Mheshimiwa Mia Amor Mottley, Waziri Mkuu wa Barbados ~~,~~ pembeni ya Mkutano wa Kawaida cha Thelathini na Nane wa Umoja wa Afrika uliofanyika Februari 2025 huko Addis Ababa.

13. Mkutano huo pia ulifanyika kwa mujibu wa maamuzi ya Mkutano wa Kawaida wa 47 wa Baraza Kuu la Umoja wa Afrika (EX.CL/Dec.1310-1322 (XLVII)), kilichofanyika kuanzia tarehe 10 hadi 11 Julai 2025, huko Malabo, Equatorial Guinea kuhusu kuwa uandaaji wa Mkutano wa Pili wa Afrika-CARICOM huko Addis Ababa, Ethiopia mnamo tarehe 7 Septemba 2025.

14. Mkutano huo ulitambua uwezo mkubwa uliopo katika uhusiano ulioimarishwa kati ya Afrika na CARICOM. Eneo la ardhi **lililounganishwa**, nafasi ya baharini, na idadi ya watu, pamoja na maliasili, mali za kiufundi, kitamaduni na kiakili za bara la Afrika na eneo la Karibeani, na maeneo yao ya kijiografia ya kimkakati, vinatoa fursa kubwa za maendeleo ya haraka, yanayojizalisha na yanayojiendeleza.

**Kuimarisha Uhusiano na Ushirikiano wa Kitaasisi**

15. Wakikaribisha utiaji saini wa Mkataba wa Makubaliano (MoU) mnamo Septemba 26, 2024 kati ya Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Mataifa ya Karibiani kuhusu Kuongeza Ushiriki na Uhusiano na Watu wa Asili ya Afrika, Wakuu wa Nchi na Serikali waliahidi katika utekelezaji wake ili kukuza ushirikiano katika maeneo yaliyokubaliwa. Hizi ni pamoja na biashara na uwekezaji, uhusiano ulioboreshwa wa usafiri wa anga na baharini, ujasiriamali, elimu, utafiti na maendeleo ya kisayansi, uhamishaji wa maarifa, utalii, tasnia za kitamaduni na ubunifu, urithi, mwingiliano wa watu, usaidizi na mshikamano katika kutatua migogoro ya kulinda amani na migogoro mingine ya kijiografia na kisiasa. Mkutano huo ulielezea kuunga mkono Muongo wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa kwa Watu wa Asili ya Afrika, (2025-2034) na uliutambua kama mfumo na chombo muhimu kinachotumika katika ushirikiano wa Afrika na CARICOM kwa ajili ya kukuza ushirikiano katika maeneo yaliyotajwa hapo juu. Mkutano huo pia ulikaribisha mikutano ya awali iliyofanyika kati ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Sekretarieti ya CARICOM, na ulitoa wito wa mashauriano ya mara kwa mara na mikutano ya mapitio, na kuamuru kuanzishwa kwa mifumo zaidi maalum ya ushiriki, ikiwa ni pamoja na Kamati Ndogo za Pamoja, ili kutekeleza kwa ufanisi MoU na kupitia mara kwa mara maendeleo katika maeneo yaliyokubaliwa ya ushirikiano.

**Biashara na Ushirikiano**

16. Mkutano huo ulitambua kwamba, licha ya historia ya pamoja na uhusiano wa kina wa kitamaduni, mauzo ya nje ya nchi mbili kati ya maeneo hayo kwa sasa yanachangia chini ya 3% ya jumla ya biashara yao. Waligundua kuwa katika muongo mmoja uliopita, kiwango cha mauzo ya nje hakijazidi 6%. Kwa kuzingatia hali hii, Wakuu wa Nchi na Serikali walisisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano katika biashara na maendeleo. Zaidi ya hayo, walitoa wito wa uwekezaji zaidi katika sekta zinazoibuka, ikiwa ni pamoja na fedha, mawasiliano, na teknolojia.

17. Mkutano huo, huku ukitambua Diaspora ya Afrika kama eneo lenye nguvu na mojawapo ya chanzo kikubwa cha uwekezaji kwa Afrika, uliamua kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji wa Diaspora ya Afrika zaidi ya pesa zinazotumwa kwa miradi yenye athari kubwa na endelevu katika Afrika na CARICOM, ikiwa ni pamoja na biashara mpya, mali isiyohamishika, miundombinu, na mipango ya uhamishaji wa teknolojia. Hii itatumia maarifa yao muhimu, ujuzi, na mtaji kupitia uwekezaji wa

kimaadili na ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi, na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi na kuunda fursa za ajira kama nguzo ya msingi ya Ushirikiano wa Kibara kwa ajili ya Haki ya Fidia na kuimarisha malengo ya utangamano wa kiuchumi ya mikataba ya biashara na uwekezaji ya bara.

18. Wakuu wa Nchi na Serikali walithibitisha tena ahadi yao katika kuimarisha ufadhili wa biashara ndani ya kanda, na kuhamasisha rasilimali kupitia kukuza uwekezaji na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi. Walisisitiza ushirikiano unaokua kati ya Nchi Wanachama wa CARICOM na Benki ya Afreximbank kama ulio muhimu kwa ajili ya kuimarisha uhusiano huu ili kusaidia ubia na miradi ya maendeleo ya kiuchumi. Katika suala hilo, Mkataba wa Ushirikiano wa CARICOM na Afreximbank, kuanzishwa kwa ofisi ya Karibeani ya Afreximbank huko Barbados, pamoja na uandaaji wa Mkutano wa Mwaka wa Thelathini na Moja wa Afreximbank (AAM) huko Nassau, Bahamas mnamo 2024, vilitambuliwa kama hatua muhimu. Utekelezaji endelevu wa Jukwaa la Biashara na Uwekezaji la AfriCaribbean (ACTIF) la kila mwaka, kufuatia jukwaa lake la uzinduzi huko Barbados mnamo 2022, na toleo lake la nne huko Grenada mnamo 2025 pia uliangaziwa. Katika suala hili, walihimiza ushiriki wa AfCFTA katika kuandaa jukwaa hilo huku wakipendekeza kwamba lifanyike kila baada ya miaka miwili kwa kubadilishana kati ya AU na CARICOM.

19. Walikaribisha uandaaji wa Algeria wa Toleo la 4 la Maonyesho ya Biashara ya Ndani ya Afrika (IATF) 2025, kuanzia tarehe 4-10 Septemba 2025 na walitambua, kwa shukrani, ushiriki wa nchi Wanachama wa Karibiani katika tukio hili muhimu, lililoandaliwa kwa ushirikiano wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC), AfCFTA na Afreximbank. Wakuu wa Nchi na Serikali walithibitisha tena ahadi yao ya kuimarisha ufadhili wa biashara ndani ya kanda, na kuhamasisha rasilimali kupitia kukuza uwekezaji na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi.

20. Mkutano huo uliahidi zaidi katika maendeleo ya muunganisho wa baharini na anga. Kwa lengo hili, kulikuwa na azimio jipya la kuanzisha Mkataba wa Huduma za Anga za Kimataifa, kuhitimisha makubaliano ya kukomesha ushuru maradufu, kurahisisha taratibu za visa, na kuanzisha safari za ndege kati ya Afrika na Karibeani.

21. Mkutano huo uliahidi zaidi kuendeleza ushirikiano wa nchi zenye uchumi mdogo za Kusini mwa Dunia na kujenga uwezo katika afya kupitia Ushirikiano wa Maendeleo ya Afya kwa Afrika na Karibiani ( HeDPAC ), Idara ya Afya, Masuala ya Kibinadamu na Maendeleo ya Jamii ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika (HHS-AUC) na Vituo vya Afrika vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (Africa CDC), hasa kukuza uwezo wa kikanda wa kuzalisha dawa, vifaa tiba, na chanjo, na kuimarisha nguvu kazi ya afya katika Karibiani na Afrika. Pia waliahidi kuendeleza MADA NA ushirikiano katika utafiti na maendeleo ya kisayansi, hasa katika sayansi ya chakula, kilimo, na nishati mbadala, kupitia sekta za umma na binafsi. Wakuu wa Nchi na Serikali walionyesha nia yao ya kushirikiana katika kuendeleza afya na ustawi wa raia wao, kama ilivyoainishwa chini ya SDG 3, na Ajenda 2063.

**Ubunifu wa Kiteknolojia na Akili Bandia**

22. Mkutano huo ulitambua uwezo wa mabadiliko wa teknolojia ya kidijitali na uvumbuzi kama vichocheo vya kuharakisha maendeleo endelevu, kuongeza tija, na kushughulikia changamoto ngumu katika maeneo yote mawili. Wakuu wa Nchi na Serikali walijitolea kuendeleza ushirikiano katika utafiti na maendeleo, uvumbuzi pamoja na utawala unaowajibika na uenezaji jumuishi na wa kimaadili wa teknolojia zinazoibuka, hasa Akili Bandia (AI). Ushirikiano huu utajumuisha kukuza uelewa na ujuzi wa kidijitali katika sekta binafsi, na miongoni mwa raia; uhamishaji wa teknolojia ili kuhimiza ujasiriamali na ufafanuzi wa suluhisho za kidijitali za pamoja; ubia na uwekezaji katika uchumi wa kidijitali ili kuendeleza fursa katika biashara ya mtandaoni na huduma za kidijitali; na ushirikiano mkubwa katika majukwaa muhimu ya kimataifa ili kuimarisha sauti ya Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Mataifa ya Karibiani na ya Kusini mwa Dunia katika kuunda kanuni za kimataifa za kidijitali.

23. Kwa kutambua nguvu ya ubadilishanaji wa kitamaduni, ushirikiano wa kisayansi na muunganiko, viongozi waliahidi kuimarisha uhusiano wa mawasiliano, sanaa, elimu, sayansi na habari kati ya Afrika na Karibiani. Mipango hiyo italenga kukuza ushirikiano mkubwa wa vyombo vya habari, kukuza tasnia za kitamaduni na ubunifu na muunganisho wa kitamaduni, kuwezesha ubadilishanaji wa kisayansi na programu zingine za kielimu, na kutumia teknolojia za kidijitali ili kuunganisha umbali wa kijiografia na kuimarisha uelewa wa pande zote.

**Ushirikishwaji na Uwezeshaji wa Vijana**

24. Kwa kutambua jukumu muhimu la vijana kama vichocheo vya maendeleo endelevu, uvumbuzi, na mshikamano wa kikanda, Wakuu wa Nchi na Serikali walithibitisha tena ahadi yao ya kuwawezesha vijana wenye asili ya Afrika na Karibiani. Walikubaliana kukuza ushirikishaji wa kina wa vijana kupitia ubadilishanaji wa elimu, mipango ya ujasiriamali, vituo vya uvumbuzi, ukuzaji wa ujuzi wa kidijitali, na programu za uongozi.

25. Mkutano huo ulisisitiza umuhimu wa kuunda majukwaa yaliyopangwa kwa ajili ya sauti za vijana katika michakato ya kuunda sera katika ngazi za kitaifa na kikanda. Pia walihimiza ushirikiano kati ya mashirika ya vijana ya Afrika na Karibiani ili kukuza utambulisho wa pamoja, ubadilishanaji wa kitamaduni, na hatua za pamoja katika kuendeleza malengo ya Umajumui wa Afrika na haki ya fidia.

**Changamoto za Maendeleo Endelevu**

26. Wakuu wa Nchi na Serikali walitambua udhaifu wa kipekee wa Nchi zinazoendelea ikiwa ni pamoja na Nchi Zinazoendelea za visiwa Vidogo, za Pwani, nchi zisizo na bandari na nchi zenye maendeleo duni za bara la Afrika na Jumuiya ya Mataifa ya

Karibiani. Mkutano huo ulitambua udhaifu unaoendelea wa kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na changamoto zinazohusiana na mseto wa kiuchumi, mzigo mkubwa wa madeni, na ufikiaji mdogo wa ufadhili wa kutosha wa maendeleo wenye masharti nafuu kama kichocheo kikuu cha hatua za pamoja na zilizoratibiwa na utetezi wa pamoja katika ngazi ya kimataifa kwa ajili ya utaratibu wa kimataifa wenye usawa na endelevu zaidi.

27. Wakuu wa Nchi na Serikali walipongeza kazi ya Mpango wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa Afrika (AAI), Mpango wa Nishati Mbadala wa Afrika (AREI), Mpango wa Kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwenye Kilimo cha Afrika (AAA) na Tume za Tabianchi za Afrika (Tume ya Mabadiliko ya Tabianchi ya Bonde la Kongo, Tume ya Tabianchi ya Ukanda wa Sahel na Tume ya Tabianchi ya Nchi za Visiwa vya Afrika) katika kuratibu utekelezaji wa mwitikio wa Afrika kwa Mabadiliko ya Tabianchi.

**Changamoto za Amani na Usalama**

28. Wakuu wa Nchi na Serikali walisisitiza haja ya haraka ya usaidizi thabiti wa kushughulikia mgogoro wa pande nyingi nchini Haiti, na kutetea mtaji mkubwa wa Mfuko wa Dhamana wa Umoja wa Mataifa ulioanzishwa kwa ajili ya Misheni ya Usaidizi wa Usalama wa Kimataifa (MSS) inayoongozwa na Kenya. Waliwasihi wadau wa kimataifa kutimiza ahadi zao za kutoa rasilimali zinazohitajika, ikiwa ni pamoja na msaada wa kifedha, vifaa na kiufundi pamoja na ujenzi wa uwezo kwa ajili ya utekelezaji wa sheria na walisisitiza umuhimu wa kuhakikisha ufanisi wa Misheni hiyo katika kusaidia Polisi ya Taifa ya Haiti kurejesha usalama na kukuza mazingira yanayofaa kwa ajili ya kufanya uchaguzi huru na wa haki. Mkutano huo ulitambua jukumu muhimu la CARICOM na Serikali ya Kenya na usimamizi wake usioyumba na kujitoa kwa Misheni ya MSS nchini Haiti.

29. Mkutani huo ulisisitiza umuhimu wa kuimarisha na kukuza ushirikiano wa usalama wa nchi za Kusini mwa Dunia ili kushughulikia uhalifu uliopangwa wa kimataifa na ahadi ya kuanzisha ushirikiano wa pamoja wa utekelezaji wa sheria, mifumo ya kubadilishana intelijensia, na ujenzi wa uwezo na kubadilishana wataalamu wa masuala mbalimbali.

30. Wakuu wa Nchi na Serikali walisisitiza haja muhimu ya kuondoa migogoro katika maeneo na kuunda mazingira yanayofaa kwa ukuaji, utangamano, na maendeleo na utangamano wa jamii zetu, wakikumbuka Azimio la CARICOM kuhusu Vita dhidi ya biashara ya silaha na Uhalifu na Vurugu kama Suala la Afya ya Umma na la Kusitisha Mapigano barani Afrika ifikapo Mwaka 2030, na kuimarisha Muundo wa Usalama na Amani wa Afrika.

31. Zaidi ya hayo, Wakuu wa Nchi na Serikali walionesha wasiwasi mkubwa kuhusu hali ya usalama inayobadilika na vitisho vingi kwenye amani, usalama, na utulivu katika

Bara la Afrika, na ndani ya ukanda wa CARICOM, na kusisitiza jukumu la msingi la UNSC katika kudumisha amani na usalama wa kimataifa. Walibainisha kwa wasiwasi changamoto za kifedha zinazoendelea zinazokabiliwa na PSO zinazoongozwa na AU na ukanda wa CARICOM, ambazo zinaathiri vibaya utekelezaji mzuri wa jukumu lao la usalama. Walisisitiza umuhimu wa ufadhili wa kutosha, unaotabirika na endelevu kwa ajili ya Operesheni za Usaidizi wa Amani (PSOs) zinazoongozwa na AU, ikiwa ni pamoja na matumizi ya michango iliyotathminiwa ya UN, kulingana na azimio 2719 (2023) la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) na Mkakati wa Usalama wa CARICOM na programu zingine za usalama. Walisisitiza jukumu la msingi la Umoja wa Mataifa katika kufadhili amani na usalama wa kimataifa.

32. Wakuu wa Nchi na Serikali walielezea uungaji mkono wao kwenye kujitoa kwa Umoja wa Afrika katika kupambana na ugaidi na itikadi kali, walilaani shughuli za askari mamluki na wapiganaji wa kigeni, pamoja na uingiliaji wa nje kwenye mambo ya ndani ya nchi za Afrika.

**Usimamizi wa Uchumi wa Dunia na Fedha za Maendeleo**

33. Wakuu wa Nchi na Serikali walisisitiza umuhimu mkubwa wa ushirikiano imara wa pande nyingi ili kushughulikia changamoto za pamoja za kimataifa na kukuza utaratibu wa kimataifa wenye usawa zaidi. Walisisitiza haja ya dharura ya mageuzi kamili ya muundo wa fedha wa kimataifa, wakitambua kwamba mfumo wa sasa hautoshi kukidhi mahitaji ya kipekee ya maendeleo na udhaifu wa mataifa ya Afrika na Karibiani.

34. Mkutano huo ulitoa wito wa ujumuishaji mkubwa na uwakilishi wenye usawa zaidi katika taasisi za fedha za kimataifa ili kuhakikisha usambazaji wa rasilimali na michakato ya kufanya maamuzi kwa haki. Mkazo mkubwa uliwekwa katika kufikia uendelevu wa deni kwa nchi zinazoendelea, hasa katika kukabiliana na ongezeko la majanga ya kimataifa.

35. Mkutano huo ulitambua kwamba mzigo mkubwa wa deni huzuia uwekezaji muhimu katika vipaumbele vya maendeleo ya kitaifa. Kwa lengo hili, walitetea mifumo bunifu ya fedha za maendeleo, pamoja na kuchunguza njia mpya za uwekezaji wa sekta binafsi ili kusaidia kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika. Mkutano huo pia ulikaribisha kupitishwa kwa Makubaliano ya Sevilla (*Compromiso de Sevilla*) kutoka Mkutano wa 4 wa Kimataifa kuhusu Ufadhili wa Maendeleo, ambayo yanaangazia pamoja na mambo mengine haja ya kupunguza pengo la ufadhili wa SDGs na kurekebisha muundo wa fedha wa kimataifa ili kuunda mfumo jumuishi na wa usawa wa utawala wa uchumi wa kimataifa.

36. Mkutano huo uliangazia jukumu la taasisi kama vile Afreximbank, Benki ya Maendeleo ya Karibiani, Benki ya Maendeleo ya Afrika, na Mfuko wa Maendeleo wa CARICOM katika kukusanya rasilimali na kuimarisha ushirikiano wa nchi za Kusini mwa Dunia kama mfano wa mipango ya siku zijazo.

37. Mkutano huo ulirudia wito wake wa kuondolewa kwa vikwazo na vizuizi vya vya adhabu na vya upande mmoja dhidi ya nchi ya Zimbabwe, Eritrea, Sudan Kusini na Cuba ili kuziruhusu kutekeleza matarajio yao ya maendeleo.

**Mageuzi ya Umoja wa Mataifa**

38. Wakitambua haja ya dharura ya mageuzi kamili ya mfumo wa Umoja wa Mataifa, hasa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Wakuu wa Nchi na Serikali walisisitiza kwamba mageuzi kama hayo ni muhimu ili kuhakikisha mfumo wa pande nyingi wenye usawa, jumuishi na wa uwakilishi zaidi, unaowezesha Umoja wa Mataifa kutimiza vyema jukumu lake la kudumisha amani na usalama wa kimataifa. Kwa lengo hili, waliidhinisha uwakilishi kamili wa Afrika katika Baraza la Usalama, ingawa si chini ya viti viwili vya Kudumu vyenye haki zote za uanachama wa Kudumu ikiwa ni pamoja na haki ya kupiga kura ya turufu mradi tu ipo, na viti vitano visivyo vya kudumu, sambamba na Msimamo wa Pamoja wa Afrika kama ilivyoainishwa katika Makubaliano ya Ezulwini na Azimio la Sirte, pamoja na kiti kubadilishana kwa zamu katika Baraza la Usalama la Nchi Zinazoendelea za Visiwa Vidogo (SIDS) katika maeneo yote ambayo yana SIDS katika Baraza la Usalama. Waliamua kuimarisha zaidi ushirikiano kati ya wanachama wa Afrika (A3) wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) na wenzao wa Karibiani kuelekea kufikia malengo ya pamoja kuhusu kudumisha amani na usalama wa kimataifa.

39. Wakuu wa Nchi na Serikali walisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya Afrika na CARICOM kwa ajili ya maendeleo endelevu na mageuzi ya utaratibu wa kiuchumi na kisiasa wa kimataifa. Viongozi waliahidi kuchukua hatua za pamoja juu ya changamoto kubwa za kimataifa, ikiwa ni pamoja na uwepo wa chakula na afya ya umma. Walitoa wito wa usambazaji wa haki zaidi wa rasilimali za kimataifa ili kuwezesha kufikia Ajenda 2030, Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika.

**Mabadiliko ya Tabianchi na Hatua za Pamoja**

40. Mkutano huo ulisisitiza uharaka wa pamoja kwa mataifa ya Afrika na Karibiani kushughulikia athari zinazoongezeka za mabadiliko ya tabianchi, ukitambua

uwezekano wao wa kupata matukio mabaya ya hali ya hewa na changamoto zingine zinazosababishwa na tabianchi. Walikubaliana kuimarisha uratibu na kukuza sauti yao ya pamoja katika jukwaa la kimataifa, na kutetea upatikanaji bora wa ufadhili wa tabianchi. Hii ni pamoja na kutafuta upatikanaji mkubwa wa fedha za masharti nafuu na usaidizi wa ruzuku, kuelewa kwamba nchi zilizoendelea zitatoa rasilimali za fedha ili kusaidia nchi zinazoendelea kwa kuzingatia kupunguza na kukabiliana na hali hiyo katika kuendeleza majukumu yao yaliyopo chini ya Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) na kupitia Mfuko wa Hasara na Uharibifu wenye rasilimali za kutosha. Viongozi hao walisisitiza kwamba kuimarisha ustahimilivu wa tabianchi ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya maeneo yote mawili. Zaidi ya hayo, mkutano huo ulitoa wito wa juhudi za kimataifa zilizoimarishwa ili kuzuia ongezeko la wastani wa hali ya joto duniani hadi chini ya 2°C juu ya viwango vya kabla ya viwanda, na kufanya juhudi za kupunguza ongezeko la hali ya joto hadi l.5°C juu ya viwango vya kabla ya viwanda, ukitambua kwamba hii ingepunguza hatari na athari za mabadiliko ya tabianchi.

41. Afrika na CARICOM zilithibitisha tena kujitolea kwao kwa pamoja kwa hatua za haraka na zenye malengo makubwa za tabianchi, wakitambua jukumu kuu la misitu na bayoanuwai katika kudumisha maisha, riziki, na utulivu wa sayari. Kanda zote mbili, zikiwa ni makao ya baadhi ya misitu muhimu zaidi ya kitropiki duniani, mifumo ikolojia tajiri, na spishi za kipekee, ambazo hufanya kazi kama vitu vinavyofyonza kwa wingi hewa ya kaboni na kinga dhidi ya athari za mabadiliko ya tabia nchi, ziliahidi kuendeleza mipango ya pamoja ya ulinzi, usimamizi endelevu, na urejesho wa mali hizi asilia, zikiongozwa na kanuni za haki ya tabianchi, usawa, na haki za Watu wa Asili na jamii za wenyeji. Zilikubaliana kufanya kazi pamoja ili kuimarisha uchumi unaotegemea misitu, kupambana na upotevu wa bayoanuwai, na kutetea ufadhili wa haki na unaotabirika wa tabianchi, ikiwa ni pamoja na kupitia mbinu za kimahakama na mifumo inayotegemea soko, uhamishaji wa teknolojia, na ujenzi wa uwezo ili kulinda urithi wao wa asili wa pamoja kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

42. Afrika na CARICOM walisisitiza wasiwasi wao kwamba viwango vya juu na vinavyoongezeka kwa kasi vya uchafuzi wa plastiki vinawakilisha na kusababisha tatizo kubwa la kimazingira kwa kiwango cha kimataifa, na hivyo kuathiri vibaya masuala ya kimazingira, kijamii na kiuchumi ya maendeleo endelevu katika maeneo yote mawili.

43. Viongozi hao walithibitisha tena ahadi yao ya kuendelea kuunga mkono agizo lililowekwa katika Azimio la UNEA 5/14, ambalo liliamua kwamba Kamati ya

Majadiliano ya Serikali Mbalimbali itaunda chombo cha kisheria cha kimataifa kuhusu uchafuzi wa plastiki, ikiwa ni pamoja na mazingira ya baharini.

44. Walisisitiza haja ya dharura ya chombo cha kisheria cha kimataifa kinachoshughulikia mzunguko mzima wa plastiki, ndani ya muktadha wa kukuza mzunguko na maendeleo endelevu, kwa kuzingatia hali na uwezo wa kitaifa na kwa ajili ya utoaji wa rasilimali mpya, za ziada, za kutosha, zinazotabirika, endelevu na za wakati unaofaa na upatikanaji wa teknolojia kwa nchi zote zinazoendelea.

**Haki ya Fidia**

45. Wakuu wa Nchi na Serikali walirudia wito wao usioyumba wa haki ya fidia kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Afrika. Walisisitiza kwamba urithi wa kudumu wa biashara ya watumwa wa Waafrika ya kuvuka Atlantiki na utumwa ni uhalifu mkubwa dhidi ya ubinadamu, ambao unahitaji fidia na maendeleo. Kwa lengo hili, Mkutano ulikubali kupitisha "Azimio la Addis Ababa kuhusu Ushirikiano wa Bara katika Kutafuta Haki ya Fidia kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Afrika Kupitia Fidia."

**Hitimisho**

46. Wakuu wa Nchi na Serikali waliahidi kutekeleza kwa kadri iwezekanavyo ahadi za Taarifa hii ili kuimarisha uhusiano kati ya Afrika na CARICOM. Kwa hiyo watafanya kazi ili kuimarisha uhusiano wa kitaasisi kati ya Sekretarieti ya AUC na Sekretarieti ya CARICOM, walionesha nia yao ya kuendelea kuchunguza njia za ziada za ushirikiano, ikiwa ni pamoja na kuzingatia kuanzisha ofisi ya uwakilishi ya AU huko Georgetown, Guyana, makao makuu ya CARICOM na idhini kwa Nchi zote Wanachama wake, na ofisi ya CARICOM huko Addis Ababa katika makao makuu ya Umoja wa Afrika. Zaidi ya hayo, walithibitisha tena azimio lao la kufanya Mkutano huo mara kwa mara, huku wakibadilishana katika kuandaa kati ya Afrika na Karibiani.

47. Wakuu wa Nchi na Serikali walitoa shukrani zao za dhati kwa Serikali na watu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia kwa ukarimu wao na mipango yao bora. Shukrani pia zilitolewa kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, na Sekretarieti ya CARICOM kwa usaidizi wao muhimu wa ushirikiano katika kuandaa Mkutano huo.

48. Mkutano wa Pili wa CARICOM na AU ulimalizika kwa hisia mpya ya kusudi na azimio thabiti la kuunda ushirikiano mzuri, kutetea maslahi ya Afrika na Diaspora ya

Afrika na Mataifa ya Karibiani na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika mustakabali wa kimataifa wenye haki zaidi, ustawi, na endelevu.

49. Wakuu wa Nchi na Serikali walitoa wito wa Mkutano wa tatu wa Afrika na CARICOM kufanyika tarehe 7 Septemba 2028, katika Nchi Mwanachama wa CARICOM.

# MAAZIMIO

# AZIMIO KUHUSU ATHARI ZA VIKWAZO NA HATUA ZA NGUVU DHIDI YA NCHI WANACHAMA WA UMOJA WA AFRIKA

**SISI, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika**, tulikutana tarehe 14 na 15 Februari 2026, katika Mkutano wetu wa kawaida wa 39 Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mjini Addis Ababa, Ethiopia;

**TUKIREJELEA** madhumuni na kanuni za Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika, pamoja na masuala mengine, kuthibitisha uhuru, ulinzi wa mipaka na uhuru wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, pamoja na kujitolea kukuza maendeleo endelevu katika ngazi za kiuchumi, kijamii na kitamaduni, kwa bara lililounganishwa na lenye ustawi;

**TUKITHIBITISHA** tena Azimio la Kanuni za Sheria ya Kimataifa kuhusu Uhusiano wa Kirafiki na Ushirikiano miongoni mwa Nchi kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa, ambao unatamka, pamoja na mambo mengine, kwamba hakuna Nchi inayoweza kutumia au kuhimiza matumizi ya hatua za kiuchumi, kisiasa au aina nyingine yoyote ya nguvu Nchi nyingine ili kupata kutoka kwayo utiifu wa utekelezaji wa haki zake za uhuru;

**TUNASISITIZA** kwamba hatua na sheria za nguvu za upande mmoja ni kinyume na sheria za kimataifa, sheria ya kimataifa ya masuala ya kibinadamu, Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika, Mkataba wa Umoja wa Mataifa na kanuni zinazosimamia uhusiano wa amani miongoni mwa Mataifa;

**TUKIREJELEA** matamko ya Maazimio ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA) 80/209 (18 Desemba 2025), 80/120 (18 Desemba 2025), 79/193 (16 Juni 2025—kutangaza tarehe 4 Desemba kama Siku ya Kimataifa dhidi ya Hatua za Nguvu za Upande Mmoja), 79/167 (17 Desemba 2024), 78/135 na 78/202 (19 Desemba 2023), na 76/161 (16 Desemba 2021); na Maazimio 58/3 ya Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa (UNHRC) 58/3 (3 Aprili 2025), 55/7 (3 Aprili 2024), 54/15 (11 Oktoba 2023), 52/13 (3 Aprili 2023), 49/6 (31 Machi 2022), 46/5 (23 Machi 2021), 43/15 (22 Juni 2020), 40/3 (21 Machi 2019), 37/21 (23 Machi 2018), 36/10 (28 Septemba 2017), 30/2 (1 Oktoba 2015), 27/21 (26 Septemba 2014), 24/14 (27 Septemba 2013), na Uamuzi 18/120 (30 Septemba 2011); kutoa wito kwa Mataifa kutotambua hatua za kiuchumi za nguvu za upande mmoja, na kutotambua au kutumia hatua au sheria kama hizo zinazowekwa na Nchi yoyote kuvuka mipaka ya nchi, ambazo ni kinyume na kanuni zinazotambulika za sheria ya kimataifa na kusisitiza kwamba hatua na sheria za nguvu za upande mmoja ni kinyume na sheria ya kimataifa, sheria ya kimataifa ya masuala ya kibinadamu, Mkataba, desturi na kanuni zinazosimamia uhusiano wa amani miongoni mwa Mataifa;

**TUKIZINGATIA** Ripoti ya Mjumbe Maalum kuhusu athari za hatua za nguvu za upande mmoja katika kufurahia haki za binadamu, iliyochapishwa mwezi Agosti 2025 (A/HRC/60/36);

**TUNAKIRI** kwamba vikwazo vya kijamii na kiuchumi na hatua za nguvu ni vikwazo vinavyozuia utekelezaji wa Ajenda ya Umoja wa Afrika 2063 na Ajenda ya Umoja wa Mataifa 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

**TUNAELEZEA** wasiwasi wetu mkubwa kuhusu athari za vikwazo na hatua za nguvu za upande mmoja juu ya haki ya maendeleo, na kukuza uhusiano mzuri wa kimataifa, biashara, uwekezaji, ushirikiano, pamoja na amani, usalama na utulivu;
Tunasisitiza kwamba hatua hizi zina athari kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi na maendeleo ya kitaifa kwa ujumla na kuibua wasiwasi wa kibinadamu na migogoro katika Mataifa yanayolengwa;

**TUKISHTUSHWA** na viwango tofauti na gharama zisizo sawa za kibinadamu za hatua za nguvu, na vikwazo vya upande mmoja na athari zake kwa raia, hususani wanawake na watoto, wa Mataifa yanayolengwa;

TUKISIKITISHWA SANA na athari za vikwazo na hatua za nguvu za upande mmoja juu ya maendeleo ya baada ya migogoro, ujenzi mpya, ujenzi wa amani na kwa Kaulimbiu ya Mwaka ya Umoja wa Afrika ya 2026: **"Kuhakikisha Upatikanaji Endelevu wa Maji na Mifumo Salama ya Usafi wa Mazingira Ili Kufikia Malengo ya Ajenda 2063**";

1. **TUNALAANI VIKALI** kuendelea kutumika na kutekelezwa kwa hatua za upande mmoja na baadhi ya nchi kama zana za shinikizo, ikiwa ni pamoja na shinikizo la kisiasa na kiuchumi, dhidi ya nchi yoyote, hasa dhidi ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, kwa lengo la kuzuia nchi hizi kutumia haki yao ya uhuru na kujitawala;

2. **TUNAYATAKA** Mataifa yote kuacha kuchukua hatua za nguvu, tunatoa wito kwa Nchi hizo kutotumia hatua hizo kwa kuwa ni kinyume na Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika, Mkataba wa Umoja wa Mataifa, desturi na kanuni zinazosimamia uhusiano wa amani miongoni mwa mataifa katika ngazi zote na kuzuia ukuaji kamili na maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya mataifa lakini yakiathiri utumikaji wa haki za binadamu.

3. **TUNAPINGA VIKALI** hatua kutoka nje ambazo zinatishia uhuru wa Mataifa.

4. **TUNATOA** WITO kwa Mataifa yote kutotambua hatua hizi wala kuzitumia, na kuchukua hatua zinazofaa, ili kukabiliana na matumizi ya nje ya nchi au athari za hatua za nguvu za upande mmoja.

5. **TUNAIHIMIZA** Serikali ya Marekani kuondoa vikwazo vya muda mrefu vilivyowekwa kwa Serikali na Watu wa Zimbabwe, ili kurahisisha ufufuaji wa kijamii na kiuchumi wa nchi hiyo. Tunatoa wito kwa Serikali ya Uingereza na Ireland Kaskazini kuondoa vikwazo vyote vilivyowekwa kwa Zimbabwe ambavyo ilirithi ilipojiondoa kutoka Umoja wa Ulaya tarehe 31 Januari 2020 na vikwazo vyote vya

ziada ambavyo ilivichukua yenyewe. Tunatambua hatua zilizochukuliwa, miongoni mwa mambo mengine, mazungumzo ya kisiasa na ushirikiano wa kiwango cha juu kati ya Zimbabwe na Umoja wa Ulaya kuelekea kuondolewa kwa vikwazo. Zaidi ya hayo, tunauhimiza Umoja wa Ulaya kuchukua hatua zinazohitajika ili kuhakikisha kwamba vikwazo vyote vilivyobaki vinakomeshwa.

6. **TUNATOA WITO** kwa Marekani, Nchi na Taasisi zingine kuondoa hatua zote za nguvu za upande mmoja zilizowekwa kwa Serikali, Viongozi na Watu wa Jamhuri ya Sudan Kusini kwani hazina tija kwa juhudi za kukuza maendeleo, ujenzi mpya na ujenzi wa amani baada ya migogoro, na kutoa wito kwa Umoja wa Mataifa kuondoa Vikwazo vya Silaha visivyo vya haki vilivyowekwa kwa Sudan Kusini, na vikwazo vingine vyote na hatua za nguvu kutoka kwa vyombo vingine ili kuiwezesha nchi kuharakisha utekelezaji wa mageuzi ya Usalama kulingana na Mkataba Ulioboreshwa katika Maazimio ya Mgogoro katika Jamhuri ya Sudan Kusini (R-ARCSS) uliosainiwa mwaka wa 2018.

7. **TUNAUTAKA** Umoja wa Ulaya na Marekani kuondoa vikwazo vya nguvu vilivyowekwa dhidi ya Nchi ya Eritrea;

8. **TUNALIAGIZA** Jopo la Watu Wenye Busara, kushawishi tena nchi hizo ambazo zimeweka vikwazo haramu vya kiuchumi na vingine dhidi ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, ili viondolewe mara moja na bila masharti;

9. **TUNATHIBITISHA TENA** mshikamano wetu na Watu wa Zimbabwe, Sudan Kusini na Nchi ya Eritrea katika kutumia haki yao ya uhuru ili kuamua hatima yao wenyewe.

**AZIMIO LA KUONDOA VIKWAZO VYA KIUCHUMI, KIBIASHARA NA KIFEDHA VILIVYOWEKWA NA MAREKANI KWA JAMHURI YA CUBA**

**Mkutano Mkuu**,

1. **UNAELEZEA** wasiwasi mkubwa kuhusu vikwazo vya kiuchumi, kibiashara na kifedha vinavyoendelea isivyo halali vilivyowekwa kwa Serikali na watu wa Cuba;

2. **UNATHIBITISHA** tena uungaji mkono wake kamili kwa azimio la UNGA "Umuhimu wa kukomesha vikwazo vya kiuchumi, kibiashara na kifedha vilivyowekwa na Marekani dhidi ya Cuba";

3. **UNASIKITISHWA** na kuzorota kwa uhusiano wa pande mbili kati ya Cuba na Marekani na kwa mara nyingine tena, unaitaka Serikali ya Marekani kuondoa vikwazo vya kiuchumi, kibiashara na kifedha vilivyodumu kwa muda mrefu na visivyo msingi vilivyowekwa dhidi ya watu wa Cuba;

4. **UNASIKITISHWA PIA** na hatua zilizotekelezwa na Serikali ya Marekani tangu tarehe 9 Novemba 2017, ambazo zinaimarisha vikwazo na **UNASIKITISHWA SANA** na kupanuka kwa vikwazo hivyo nje ya mipaka, ikiwa ni pamoja na utekelezaji kamili wa Sura ya III ya Sheria ya Helms-Burton (kulingana na aya ya 426 ya Azimio la Mawaziri la G-77 la 2025, ambalo linadumisha msimamo ule ule (uliokubaliwa mwaka 2024);

5. **UNASIKITISHWA** kwa kiasi kikubwa na kujumuishwa kiholela kwa Cuba katika orodha ya nchi zinazodaiwa kufadhili ugaidi, ambayo imezidisha zaidi vikwazo vya kifedha kwa Cuba vinavyotokana na vikwazo hivyo; hivyo, unatoa wito wa kuondolewa kwa Cuba kutoka kwenye orodha hiyo;

6. **UNATAMBUA** kwamba athari za vikwazo hivyo imeongezeka na hata kuwa ya kikatili zaidi katika muktadha wa sasa, wakati Cuba inakabiliwa na athari za kiuchumi na kijamii za janga la UVIKO-19 na majanga ya asili;

7. **UNATAMBUA PIA** kwamba vikwazo hivyo ni kikwazo kikuu cha utekelezaji wa Cuba wa Ajenda ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu ya 2030 na unaonyesha wasiwasi huu kutokana na umuhimu ambao Umoja wa Afrika unaupa kwa mafanikio ya malengo ya Ajenda hiyo;

8. **PIA UNATHIBITISHA TENA** mshikamano wake na watu wa Cuba.